

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 21 Julai, 2012

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe.Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Ifuatayo Iliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwatachia Ramadhani Karim Waislamu wote waliojaliwa kuanza Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani *Inshallah* Mwenyezi Mungu azikubali saumu zetu na azikubali toba zetu.

Naomba sasa kuwasilisha Mezani Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa Fedha, 2012/2013.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa 2012/2013
Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge na mimi nichukue fursa hii kuwatachia kila la heri wale wote ambao wanaanza mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani tunawatachia kila la heri kama ambavyo tumekwisha ambiana na sisi Bungeni hapa maandalizi yote yamekamilika.

Kila siku ambazo tutakuwa tukifanya kazi jioni tutamaliza kwa muda ule ambao Mheshimiwa wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu alitoa hoja jana na tukakubaliana na kutakuwa na futari katika kantini yetu ya Bunge kila siku jioni, sasa uchangiaji unaendelea naomba mchangiaji wetu wa kwanza awe Mheshimiwa Martha Mlata. (*Makofii*)

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niwatakie heri Waislamu wote Tanzania kwa mwezi huu Mtukufu. Pamoja na salamu hizo za heri naomba pia niseme kwamba kuna karatasi ilikuja mezani kwako jana na ninaamini bahasha ile ilikataa kufunguka kwa hiyo naomba niseme kilichokuwemo ni kwamba kwa niaba ya Watanzania wote na wapenzi wote wa Yanga napenda kuipongeza Yanga kwa ushindi mkubwa

iliyojipatia jana, baada ya salamu hizo na wewe nikutakie heri pia kwa mchezo wa Simba leo. (Makofi/Kicheko)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa leo ni mjadala wa Kilimo, Chakula na Ushirika. (Makofi/Kicheko)

MHE . MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu hizo ninaomba sasa niingie kwenye hoja iliyoko mbele yetu sitakuwa nimetenda haki kwa kutoa pole kwa Watanzania wote kwa janga kubwa ambalo limetupata Watanzania wote tuwe na subira tumwombe Mwenyezi Mungu na kuwaombea heri wale wote walionusurika na wale wote waliopatwa na misiba.

Lakini pia nitoe pole kwa Mama mzazi wa Yohana ambaye alifariki katika vurugu za kisiasa kwa sababu anatoka kwenye kijiji ninachotoka na ni jirani yangu na ni kijana ambaye alikuwa mwalimu wa kwaya yangu kwa hiyo, ninaomba nitoe pole hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Serikali na hasa kwa Waziri Mkuu baada ya mimi kuleta hoja ya mgogoro wa zao la alizeti Singida, Serikali illingilia katni na mgogoro huo sasa umekwisha. Hali sasa hivi ni shwari na wafanya biashara pamoja na wakulima na wote ambaeo ni wadau wa zao hilo wanaendelea na shughuli zao kama kawaida.

Ombi langu ni kwamba tunaomba Serikali iwe makini kuwatendea haki watu ambaeo wanajitoa kwa dhati kujikwamua kutoka kwenye hali ngumu ya maisha hasa wakulima ninaomba wakulima hawa na wafanyabiashara wote na wadau wote wa zao hili wasipatiwe bughudha, pamoja na kwamba zao hili la alizeti ndilo linaloongoza katika Mkoa wangu wa Singida kwa biashara na kwa kipato lakini bado Serikali hajjaweka mikakati mizuri kwa kutoa pembejeo kwa sababu hata mbegu zinazopelekwa kule ambazo zinatumika sasa hivi ni aina mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini ninaamini kuna mbegu zingine kuna kituo cha kuzalisha mbegu Pambaa ambacho ni cha Serikali. Ninaomba Serikali izidi kupeleka zana za kilimo kule ili waweze kuzalisha mbegu nydingi zaidi za kuweza kutosheleza katika Mkoa wa Singida na hata Mikoa jirani kwa sababu mbegu inayotoka pale Mpambaa ina ubora zaidi kuliko wanayoitumia wananchi wa Mkoa wa Singida.

Pamoja na kumaliza mgogoro wa zao la alizeti Singida, bado kuna mgogoro mkubwa sana wa zao la mahindi katika Mkoa wa Singida. Historia ya zao la mahindi katika Mkoa wa Singida mimi nimeikuta ni zao ambalo kwetu sisi ni chakula na Mkoa wa Singida una zone tatu.

Kuna zone ambazo zinaweza kulima zao la mahindi, zao la mtama, pamoja na uwele na mazao mengine Iakini cha kushangaza Serikali ninaomba ilete majibu hapa ni takwimu zippi, ni wataalamu gani walioenda Mkoani Singida wakapima udongo wa Mkoa wa Singida na kusema kwamba zao la mahindi haliwezi kustawi na kulimwa Mkoani Singida. (Makofi)

Kwa hali kama hiyo wananchi wamekuwa kwenye hali tete wakizuiwa kulima zao la mahindi hata takwimu zinazopatikana kwenye Mkoa wa Singida kwa zao la mahindi iwe pato au iwe takwimu tu kuwa Mkoa umezalisha kiasi gani hazingizi na wala haziletwi kwenye RCC eti kwa sababu zao lile halitakiwi kulimwa Mkoani Singida. Ninaomba Mheshimiwa Waziri anakapokuja kujibu hoja zetu anieleze ni wataalamu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalamu walitumia nini kuona kuwa Mkoa ule haufai kulima zao la mahindi. Ninaomba kama hataleta mimi nitaomba nitoe shilingi ili kuonyesha kuwa wakulima wa zao la mahindi katika Mkoa wa Singida hawaungi Mkono Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la mahindi lilletewa pembejeo Iakini pembejeo zile zikakataliwa eti kwa sababu zao hilo halitakiwi kulimwa Mkoani Singida. Ni kweli kuwa Mkoa wa Singida kuna maeneo ambayo yanastawisha mtama, uwele, ufuta na mazao mengine.

Hivi mtu anapojitoa kulima ni Serikali gani ambayo inamzuia mtu na kukataa takwimu ambazo ni wazi kabisa na ni sahihi kabisa na ni sahihi kabisa zao lile hata mwaka huu vijana wengi na wakulima wengi wametoka kwenye umasikini kutokana na zao la mahindi. Ni zao la pili katika

Mkoa wa Singida kwa biashara leo hii wakulima wanapigwa *stop* na Serikali. Mimi ninaishangaa sana Serikali ninaomba Waziri utakapoleta majibu yako ulete majibu fasaha na uniambie takwimu zake zikoje, pato lake likoje kwa sababu mimi binafsi nimeshindwa kupata takwimu ya zao hili kutokana na kwamba hata wataalamu wanaogopa kutoa takwimu na kuzungumzia zao hili kwa sababu watapata *demotion* kwa kuzungumzia na kusimamia zao hili.

Ninaomba sana Serikali ije Mkoa wa Singida itusaidie kutatua mgogoro huu. Katika masuala ya umwagiliaji kuna *scheme* nydingi ambazo zimejengwa Mkoani Singida lakini *scheme* zile mimi bado mdogo leo ni Mbunge na ni Mbunge kwa kipindi cha mara ya pili ziko palepale tunapitisha Bajeti hapa ooh tutaleta kuna hela zimewekwa hivi hii Bajeti ambayo tunasomewa hapa sasa hivi kwanza mimi nilikuwa nataka kusema hii Bajeti ina ujumbe gani.

Waziri amesoma anataka kutueleza nini kwenye hotuba yake hii aliyoitoa, maana mimi sielewi naomba ujumbe kamili juu ya hotuba hii kwamba ujumbe wake ni nini maana hata fedha zilizotengwa humu mimi naona ni kama kiini macho na ndiyo maana hata miradi au *schemes* zilizoko Mkoa wa Singida hazitekelezeki kwa sababu ya viini macho vilivyomo kwenye Bajeti husika kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi inawezekanaje kweli wewe na Mke wako na familia yako mnapanga Bajeti kila mtoto unamwambia lete mahitaji yako halafu unamwambia Bajeti inakuwa ni 100,000 halafu unamwambia kuwa mimi nina 20,000 halafu unawaambia kuwa 80,000 nitakwenda kuomba kwa Mlata, nitakwenda kuomba kwa Mheshimiwa Joseph Selasini na mahali pengine, unajuaje kama utapata hizo hela?

Hiyo ni Bajeti gani, kwa nini tunaletewa Bajeti ya kusubiri kupewa hela kwa watu mimi ninaomba pale tunapoweka kipaumbele kwenye jambo fulani fedha za kusubiri kupewa tusiziingize kwenye Bajeti tujue moja kwa moja kwamba hela zetu za ndani ndizo zitakazoweza kukomboa jambo letu tuliloliweka kwenye kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa kweli hapa niliposimama ninashindwa kuunga mkono hoja hii kwa sababu sina hakika Mwangeza kuna miundombinu ambayo ilishawekwa mpaka ina chakaa inasubiri mvua inyeshe ndiyo yale maji yapite hakuna mabwawa. Ukienda Kata ya Msingi kule vilevile naambiwa Mwanga kutakuwa sijui na mradi wa matone, matone gani kama mlishindwa kuendeleza miradi iliypangwa miaka mingi hayo matone mtayaletaje mimi kwa kweli ninashindwa kuunga mkono hoja. Hapa juzi nimeuliza kuhusu suala la kilimo cha vitunguu nikaambiya ohltutawachimbieni mabwawa hapa hata sioni na kuwezesha watu sijui mashine, sijui kitu gani hazipo sasa mimi nitaungaje mkono hoja wakati watu walishapokea kwa furaha kabisa nilikuwa ninaomba sana Serikali tuwe makini katika kuweka Bajeti kwenye vipaumbele tusitegemee fedha za kuomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia watendaji wetu hebu tutende haki kama fedha zimetolewa basi mtoe fedha ambazo zinakwenda kukidhi ule mradi, tusiwe tuna dokoadokoa halafu tunaacha tunawadanganya wananchi. (*Makofii*)

Wakulima wa Mkoa wa Singida na Mikoa hii kama ya Dodoma Mikoa ambayo ni kame mnakaa mnapiga marufuku kulima mazao eti hayastawi kwenye ukame mnapigaje marufuku badala ya kusaidia zao, badala ya kusaidia wakulima chimbeni mabwawa wekeni miundombinu tuvune maji yanayomwagika kwa wakati mmoja mvua ikienda zake tunabaki na maji yetu badala ya kuwasaidia watu mnaanza kuwapiga marufuku mimi nashindwa kuelewa. (*Makofii*)

Nilikuwa ninaomba pia pembejeo kwenye zao la mtama pamoja na mazao mengine kama uweli mimi naomba tupatiwe pembejeo hizi ili wale watu wanaolima mtama, wanaolima uweli na wao waweze kupata pembejeo.

Mimi kwa kweli nitashindwa kabisa kuunga mkono hoja lakini nilikuwa ninaomba pia kuweza kuwawezesha wakulima waweze kupata mikopo. Kuna watu ni masikini wakulima bado wanatumia jembe la mkono, halafu unamwambia eti unazuia njaa, unazuia njaa gani umemwacha mtu analima kwa mkono kwa nini usimpelekee pembejeo za kujikwamua kulima

eneo kubwa usidhani hii Mikoa inayopata njaa ni kwa sababu eti wameshindwa kulimwa ni jembe la mkono tangu miaka nenda rudi jembe la mkono trekta zimefungiwa tu kwenye magodauni why? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana mimi siungi mkono hoja. (Makof)

MHE. ABDUL J . MAROMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Kilimo lakini nianze kusema kwa masikitiko makubwa sana.

Masikitiko makubwa ni kwamba siungi mkono hoja hii na siungi mkono nina sababu Mwaka 2006 aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa alitisha Bodi za Mazao yote katika nchi yetu ili kuweza kuwahamasisha Bodi hizo wakishirikiana na viongozi wa Serikali kuzalisha mazao mara mbili zaidi ya kile ambacho Mwaka 2006 walikuwa wakizalisha. Mko wetu wa Pwani tuliiwa na Mikoa yote inayolima zao la korosho tukahamasishwa kuweza kulima korosho kwa wingi zaidi. Kwa bahati nzuri kuanzia mwaka 2007 ruzuku ya Serikali ikawekwa kwenye pembejeo na baada ya hapo uzalishaji wa zao la korosho uliongezeka sana.

Mko wetu wa Pwani kwa wakati ule tulikuwa tunazalisha wastani wa tani 5 hadi 6 lakini kwa sasa Mko wa Pwani unazalisha zaidi ya tani 15,000 tani ambazo ni nyangi, ambazo zinahitaji hata Serikali kuwa- encourage hawa wakulima waweze kulima zaidi ili waweze kutuingizia fedha za kigeni kutokana na uuzaji wake nje ya nchi. Lakini mwaka jana yalitokea matatizo makubwa sana katika ununuaji wa korosho na mwaka huu uzalishaji wa korosho umezidi kuongezeka kuanzia mwaka jana hadi sasa korosho za Mko wa Pwani zilizonunuliwa ni chache sana Serikali iliingilia kati na baada ya kuingilia kati kwa bahati nzuri tuliletewa mnunuzi kutoka Marekani alikuwa ni Mzungu, tuliambiwa kabisa kuwa mnunuzi huyo ndio atanunua korosho za Mko wa Pwani lakini kwa bahati mbaya yule mnunuzi toka walivyoingia mkataba mwezi wa tano mwaka huu mpaka hivi sasa hata tani moja ya korosho haijanunuliwa katika Mko wetu wa Pwani.

Sasa kinachoendelea ni nini? Kinachoendelea ni kwamba korosho zile zipo kwenye magodauni ya Serikali baada ya kukaa kwenye magodauni ya Serikali Benki ambazo zimekopesha Vyama vya Ushirika ili viweze kununua korosho hizo *interest rate* zinazidi kuongezeka. Walikuwa wanalipia *interest rate* ya 15% kuanzia mwezi wa kumi mwaka jana mpaka hivi sasa kila Chama cha Msingi kinalipia *interest rate* ya 15% ya fedha ambazo zimekopa wamekopa mwezi wa kumi mwaka jana lakini mpaka leo korosho hizi hazijanunuliwa kwa maana nyingine ni kwamba *interest rate* inazidi kuongezeka anayeongezewa *interest rate* ni yule mlimaji ambaye tayari yeye amepeleka mazao yake pale akitegemea kuwa Serikali au yale mazao yatauzwa, lakini mazao hayauzwi kwa hiyo, kadri tunavyoendelea kukaa kimya, kadri mazao haya yanapoendelea kubakia kwenye maghala maana yake ni kwamba *interest rate* inazidi kuongezeka. La pili, itakapofika mwezi wa kumi mwaka huu *interest rate* hii itaongozeka hadi kufikia 21% kwa sababu ya *penalt* hii *interest rate* ipo *within* mwaka mmoja lakini itakapokuwa imeongezeka kufikia mwezi wa kumi maana yake *interest rate* itakuwa 21% sasa inapokuwa 21% nani anayepata au anayeonewa zaidi.

Nieleze ukweli wakulima wa zao la korosho wanaonewa sana kutokana na hili ambalo linalojitokeza wenzenetu wa Mikoa ya Kusini tayari wao kwa kupitia Serikali yetu wameweza kulipwa fedha zote Wizara ya Kilimo imeshindwa kutatua tatizo la Mko wa Pwani, lazima niseme ukweli kuwa Wizara ya Kilimo imeshindwa wameshakaa vikao zaidi ya 10 kujadili namna gani hizi korosho zinazawa na ahadi nyangi zimetolewa lakini hakuna kinachoendelea matokeo yake zile korosho zimebakia tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili niunge mkono Bajeti hii ninamwomba Waziri Mkuu leo atoe tamko, kama alilolitoa kwa Mko wa Mtwara na Lindi kwa Serikali kuingilia kati. Ninaomba Waziri Mkuu alilingilia kati suala hili la korosho za Mko wa Pwani ziweze kununuliwa zote, kwa sababu Wizara ya Kilimo yenye imeshindwa kutoa majibu. Hata kwenye kitabu hiki walichokitoa hapa hakuna maelezo yejote kuhusiana na korosho za Mko wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni jambo la kwanza ambalo naiomba sana Serikali ilizingitie na iwaonee huruma watu wa Mko wa Pwani. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo jingine naiomba Serikali kwa sababu waliosababisha hii *interest rate* kuendelea kuwepo ni Serikali, ili hao wakulima waweze kupata pesa zao zote zikiwa zimekamilika, *interest rate* ichukuliwe na Serikali wasipewe hawa wakulima. Serikali ijingize moja kwa moja kuchukua *interest rate* na wakulima mara baada ya kuza korosho zao fedha zote wapewe wao, Serikali ilipe kwa sbaabu mwenye matatizo siyo Mkulima, mkulima amekuwa *encourage* aweze kulima kwa wingi na amelima, lakini Serikali imeshindwa kumsaidia mkulima. Naomba sana Serikali iweze kujibu. Hasa namwomba Waziri Mkuu atupatie majibu hapa leo kwa sababu Wizara ya kilimo imeshindwa kutoa majibu kwa watu wa Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nirudie tena kwamba katika Bajeti ya Waziri Mkuu sikuiunga mkono hotuba ile, na sikuiunga mkono kwa sababu kulkulla na suala ambalo mpaka leo linaendelea. Utu wa mgongo wa Taifa letu ni kilimo na kilimo katika nchi yetu ndicho tunachokitegemea. Nchi hii haiwezi kuendelea kwa kutumia wafugaji hata siku moja. Lakini Mkoa wa Pwani hasa Wilaya ya Rufiji nimesema tumevamiwa sana na wafugaji. Kauli ya Serikali bado hajatolewa kwamba katika Bonde la mto Rufiji ambalo ndilo linalofaa sana kwa kilimo. Wenzetu wa Wizara ya Kilimo ukurasa wa 86 wameelezea kwamba sasa hivi Bonde la mto Rufiji hekta laki moja na tano elfu. Hekta laki moja na tano elfu hazipatikani Kilombero, zinapatikana Rufiji ndio kwenye hekta hizo na zinaweza kupatikana zaidi ya hekta laki moja na tano elfu huko Rufiji. Sasa unaposema kwamba sisi tunataka kupima hekta laki moja na tano elfu, hivi hekta hizi mmezitoa wapi? Mtaenda kuzitoa kwa wafugaji wale ambaao tayari wamevamia lile bonde au mtakwenda kultoa maeneo mengine? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ielete hatua ambayo Wizara ya Kilimo inachukua, tena haikueleza ni lini hizo hekta laki moja na elfu tano zitaanza kupimwa haikuelezwu imeachwa wazi tu. Watueleze hizi hekta wanazipata wapi. Wakishazipata hizo hekta katika Bonde la Mto Rufiji ndipo mimi nitawenza kuziunga mkono. Lakini ninamwomba Waziri Mkuu tena kuingilia kati suala la kilimo katika Wilaya ya Rufiji. Mifugo imeenea katika Bonde lote la Mto Rufiji, kilimo katika Wilaya ya Rufiji kimekuwa duni sasa hivi. Tulikuwa tunajitegemea sisi kwa asilimia mia moja. Lakini kuanzia walivyoingia ng'ombe kwenye Bonde la mto Rufiji tunajitegemea si zaidi ya asilimia 20. Mwaka huu kumetokea na kunaendelea kutokea njaa kali kutokana na kuwepo kwa mifugo. Kila unapolima mazao yako ng'ombe wanakula tu. Ninaombwa Serikali itoe kauli ni nini inachokifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tena ingekuwa vizuri zaidi Wizara zote zinazohusika, Wizara mtambuka ziende zikaangalie hali halisi tuseonekane kwamba sisi ni wabaya, nendeni mkaangalie hali halisi ya Wilaya ya Rufiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, lakini siungi mkono hoja mpaka nitakopata maelezo. Nashukuru. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mhehsimiwa Jabir Marombwa, Mheshimiwa Suzan Lyimo atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Henry Shekifu.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii nyeti ili nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa sababu ni Wizara ambayo inahusisha zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania. Nichukue fursa hii kuwapongeza wakulima wote wa Tanzania kwa kazi kubwa sana wanayoifanya pamoja na kuwa katika mazingira magumu hasa ikizingatiwa kwamba hawapati mbolea kwa wakati, lakini vile vile tunatambua kwamba mazao yao hayana masoko, vile hakuna miundombinu ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema tukaipatia kipaumbele Wizara hii ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanaishi bila njaa. Mwaka 2003 na mwaka 2006 Wakuu wa Nchi za Afrika walikutana Abuja na Maputo kwa lengo la kuhakikisha kwamba chakula katika Afrika kinaboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ninukuu malengo ya Mkutano ule ambaao ulikuwa unajulikana kama *Comprehensive Africa Agriculture Development Programme*. Moja, ilikuwa ni

kuongeza pato la kilimo kufikia asilimia sita mwaka 2013 katika nchi za Afrika. Lakini la pili, ilikuwa ni kutenga asilimia 10 ya Bajeti ya nchi hizi kwa ajili ya Wizara ya Kilimo na mwisho, ilikuwa ni kuipatia mbolea ya ruzuku nchi hizo kutokana na ardhi kutokuwa na rutuba ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoongea hapa ninaomba Waziri atuambie ni kwa kiasi gani malengo hayo yametekelezwa hasa ikizingatiwa kwamba Tanzania iliridhia makubaliano hayo na vile vile nikiangalia katika Bajeti ya Wizara hii, kwa kuwa, lengo ilikuwa ni kuhakikisha kwamba Bajeti ya Wizara hii inakuwa asilimia kumi, lakini mpaka sasa hivi kwa mwaka huu peke yake Wizara hii imetengewa Bajeti asilimia 1.5 ya Bajeti ya Taifa.

Wizara hii imepata shilingi billioni 237 tu wakati ilitakiwa kama kweli tuna lengo na kwa sababu nchi iliridhia ina maana Wizara hii peke yake ilipaswa kupata shilingi 1.5 billioni lakini imepata asilimia 1.5. Hii ni aibu kwa kweli hatutakii nchi hii mema na ndiyo sababu kunaendelea kuwa na matukio mengi kwa sababu wananchi wana njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu wa Kenya aliyahi kusema *a hungry man is an angry man*. Ina maana kwamba mtu mwenye njaa ni mtu mwenye hasira. Ndiyo sababu tunaona matukio mengi ya uvunjifu wa amani kwa sababu watu wana njaa, watu wameamua kufanya mambo kwa sababu wana njaa, kama akili haifanyikazi vizuri kutokana na njaa ni lazima utafanya mambo ya ajabu. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali ihakikishe inawekeza kwenye kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nauliza swali kuhusiana na *green revolution*, tunataka kufanya mabadiliko ya kilimo, tunataka kufanya mabadiliko ya kijani, lakini hatuwezi kuyafanya kwa mwendo tunaokwenda nao sasa hivi. Wakati Naibu Waziri akijibu swali langu alisema kuanzia mwaka 2006 mpaka mwaka 2011 tumeweza kuongeza hekari za umwagiliaji 81,000 tu. Hii ina maana kwamba kwa mwaka mmoja Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeweza kuongeza ekari 13,500. Wakati nchi hii ina ekari zaidi ya milioni 29 za kilimo cha umwagiliaji. Ina maana kwamba kwa miaka 2120 ndiyo tutaweza kumaliza tatizo la umwagiliaji. Hii ni aibu, ninaomba kwa sababu Serikali inakuwa na mpango mkakati kwa miaka mitano, watuambie wakati wanaenda kumalizia kipindi chao na kukabidhi kwa Serikali nyingine watakuwa wamekamilisha kiwango gani cha umwagiliaji katika nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakin vile vile nilitaka kujua, katika hizi *scheme* za umwagiliaji ambazo tumekuwa tukizisikia miaka nenda miaka rudi, ni kwa kiasi gani wameweza kukamilisha walau *scheme* moja tu, watuambie kwa sababu hata kwenye kitabu cha maendeleo sioni ni kwa kiasi gani wanaweza kukamilisha. Kwa hiyo ninaomba sana Waziri na Serikali kwa ujumla tusicheze na kilimo kwa sababu kilimo ndicho kinachotoa ajira kwa vijana, ndicho kinachotoa ajira kwa akina mama na nchicho ambacho kinawenza kutulisha Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende kwenye Mkoa wangu wa Kilimanjaro, sisi wakazi wa Kilimanjaro tulizoea kilimo cha kahawa, kilimo cha kahawa ndicho ambacho kimewasomesha watoto wengi wa Kilimanjaro, lakin sasa hivi zao la Kahawa limeshuka sana na ilifiki kipindi wakulima wakaamua kukata kahawa zao kutokana na soko la dunia. Lakini inashangaza pamoja na kwamba soko la dunia limepanda kilo moja naambiwa imefika mpaka shilingi elfu kumi na mbili lakin Mtanzania au Mkulima wa kahawa Kilimanjaro bado anauza kahawa yake kwa shilingi 4500.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, bado extension officers hawafiki katika mashamba yale ili kuweza kuwaeleza wakulima wale ni kitu gani kinaendelea kuwasaidia katika kilimo bora cha kahawa, mbaya zaidi hata mbolea haifiki kwa wakati na ninapozungumza hivi tunatatizo kubwa sana la ukame Mkoa wa Kilimanjaro kwa mara ya kwanza, wakulima wamefanya kazi yao kubwa sana ya Kilimo, wamepoteza muda wao na pesa kwa ajili ya kutayarisha mashamba kulima lakin hatuna mazao kabisa mwaka huu mahindi yote yamekauka, ninaomba Serikali ihakikishe kwamba inasaldia wakulima wa kilimanjaro hasa wanaolima katika mabonde kule Uchira na maeneo mengine waweze kusaidiwa kupata chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala zima la mbolea. Ni jambo ambalo haliniinngii akilini tukitambua kwamba tuna kiwanda cha mbolea pale Minjingu, kiwanda

ambacho kinatengeneza mbolea sawa sawa na inayotoka nje ya kupandia, na inayouzwa kwa shilingi 32,000 tu kwa mfuko, lakini tunaendelea kukumbatia soko la nje, tunaleta mbolea kutoka nje kwa gharama kubwa sana, matokeo yake ni kwamba sasa hivi tunavyoongea kiwanda kile kimefungwa kwa sababu mbolea nyigi ambayo haina soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli tunaitakia mema nchi, na tunataka kuzalisha ndani, ni kwanini bado Serikali inaendelea kuleta mbolea kutoka nje tena kwa bei kubwa sana lakini haifiki kwa wakati, wakati tunacho kiwanda chetu pale Mijingu ambacho siyo tu hakizalishi lakini wale wananchi wanaoishi maeneo yale sasa hivi hawafanyi shughuli yeoyote.

Ninaomba Serikali ihakikishe inanunua mbolea ile ili wananchi waipate kwa wakati, lakini vile vile iendelee kutoa hamasa na morali kwa watu wetu wa ndani ili waweze kuwekeza katika kilimo. Hii inapelekea kuamini kwamba labda Serikali au watendaji wakuu wa Serikali wana mkono wao ndiyo sababu hawataki tununue mbolea kwa wakati.

NAIBU SPIKA: Samahani Mheshimiwa Suzan Lyimo, Naona Mheshimiwa Ally Kessy, amesimama.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa mzungumzaji nikitumia kifungu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suzan Lyimo ukae ili upokee taarifa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68 (8), kueleza kwamba Kilimo ndiyo Utu wa mgongo wa vijana wengi nchini Tanzania, hii siyo kweli. Vijana wengi wanaauza maji, wanaauza sidiria, wanaauza vichupi barabarani, ni wazee pekee ndiyo wakulima na akina mama. Ni kusingizia vijana, vijana wengi hawafanyi kazi ya kilimo katika nchi hii. wanaauza chupi, wanaauza maji na sidiria. (*Kicheko/Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suzan Lyimo unaipokea taarifa?

MHE. SUZAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba Mheshimiwa Ally Kessy Mohamed, ameliona hilo na hiyo ni kwa sababu ya sera mbovu za CCM ambazo zinafanya vijana waache kufanyakazi za msingi wanakuja kufanya kazi za kuuza hivyo alivyovisema. Kwa hiyo, ninaamini kungekuwa na mipango mizuri ya Serikali vijana hawa wangekaa vijijini walime ili waweze kulilettea pato Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo nilitaka kulizungumzia nadhani muda wangu unakaribia kwisha ni suala zima la maonesho. Kumekuwa na maonesho mengi ya Wakulima lakini kinachoshangaza maonesho haya yanafanyiwa mijini wakati wakulima wapo vijijini, ninaomba sana tuende sasa katika ngazi ya Tarafa, maonesho yawe yanafanyika kule ili wakulima waone ni mbinu gani wanaweza kuzitumia.

Lakini jambo la mwisho ni kwamba najua sana kumekuwa na mpango mkakati wa *Public Private Partnership (PPP)* hapa nchini, na wote tunatambua kwamba wakulima wana mashamba lakini hawana utalaam, lakini natambua kwamba tuna SUMA JKT na watalaam wengine ambao wangeweza kuingia ubia na wakulima, wao wapeleke utalaam pamoja na matrepta na wakulima waweze kuwapatia mashamba yale ili sasa wawe na ubia wa pamoja na ninaamini kwa hili Serikali ingeweza kupata kilimo bora na wakulima wangeweza kupata kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la viwanda vya kusindika, nimeona katika hotuba ya Waziri ameelleza kwa kirefu, lakini bado wakulima wetu wana matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi hoja mkono. (*Makof*)

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mungu lakini nikushukuru na wewe pia kwa kunipa nafasi hii asubuhi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kutoa pole kwa wahanga wa meli kule Zanzibar, pia niwatakie wenzetu wa dini ya Kiislamu mfungo mwema wa mwezi mtukufu na tatu niipongeze Serikali kwa kukubali kuwalipa wananchi wetu hasa wafanyakazi wa mashamba ya mkonge kule Tanga ambao wamelipwa haki zao walizokuwa wanafanyakazi hapo zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya muda mimi nitajielekeza katika mambo machache. Kwanza naunga mkono juhudzi za Serikali kuanzishwa kwa *commodity exchange*, ni njia moja ya kitalaamu ambayo itatusaidia ninaamini hivyo. Pia nasisitiza uanzishwaji na uendelezaji wa Bodi ya mazao mchanganyiko ambayo kwa kweli tunatamka tu lakini hatujaipa umuhimu unaotakiwa.

Nawahakikishia kwamba mazao mchanganyiko kwa sasa katika soko ndiyo yaliyo na bei nzuri na yanaweza kutupatia fedha nyingi na yatapunguza pia tatizo kubwa la chakula hapa nchini na mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nzungumzie kwa kifupi sana suala la mbolea hasa mbolea ya Mijingu. Mimi nilikuwa Mkoa wa Manyara najua uchungu wa Waziri Mkuu kwa kiwanda hiki kuendelea, tulishirikiana nae nikiwa Mkuu wa Mkoo kuhakikisha kwamba mbolea inazalishwa ya kutosha hapa nchini, kwa bahati mbaya mpaka leo sijaona mkakati kweli wa kuhakikisha kwamba kiwanda hiki, mbolea kidogo inayozalishwa inasambazwa kikamilifu na Serikali inasaidia katika kuhamasisha wananchi watumie mbolea hii inayozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyozungumza wenzangu hatuhitaji kusisitiza mapenzi ya Mungu kwetu, kiwanda kile ukifika hata wewe mwenyewe utaona ajabu, Mungu kautuletea mbolea ile ni kuchimba tu na kusaga. Nashauri Wizara isimamie uanzishwaji wa kiwanda cha *Urea* ili tupate mbolea ambayo inakubalika kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya ya utangulizi, nimwombe Waziri Mkuu aendelee na juhudzi, mbolea iliyopo iuzwe na awashikilie watendaji. Tatizo letu ni kwamba watendaji wanapewa maelekezo na hawayafuatilii. Naomba Serikali ichukue jukumu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika eneo ambalo linanihusu sana, katika ukurasa wa 28. Serikali imetamka vizuri kuhusu uzalishaji wa mazao ya bustani.

Mimi natoka Wilaya ya Lushoto, kwa wale wote wenye kujua historia wanaelewa wazi kwamba Wilaya hii ni katika Wilaya za mwanzo na Wilaya ambazo zinaishi kwa ajili ya shughuli za bustani na mazao ya kawaida ya mbogamboga na matunda. Lakini kwa bahati mbaya katika Wilaya zilizosahaulika, Lushoto ni moja ya Wilaya hizo. Hasa katika suala la kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunalima sana kahawa kwa ajili ya uhaba wa ardhi mashamba yote hayo ya kahawa yakawa yamekufa. Kwa sasa tunalima chai lakini ni eneo dogo sana linalolima chai. Wananchi wengi hasa vijana wanahangaika kwa kilimo cha mazao ya bustani ambayo ni matunda pamoja na mboga mboga.

Lakini hakuna mpango wowote hata ukiangalia humu ndani ambao unatamkwa, zaidi ya kusema kwamba *Horticultural Association* itaaniszha vikundi vyta kununua mazao. Kuanzisha vikundi vyta kununua mazao ni jambo moja, lakini pia kutafuta masoko na kuwa na uwezo wa kuweka matunda hayo au mboga mboga hizo katika *package* nzuri inayokubalika nje ni jambo jingine. Hili linahitaji uwekezaji mkubwa ambao mwananchi au mkulima mdogo hana uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu hasa vijana uwezo wao ni mdogo, hakuna mpango wowote wa kuwawezesha hata kununua viwatilifu, pembejeo zinazoweza kuyafanya mazao haya yanunulike kwenye soko la dunia. Ndugu zangu ni rahisi kutamka ku-export matunda au mboga mboga.

Lakini zinahitaji uwekezaji mkubwa sana katika ukuzaji wa mboga mboga, katika ukuzaji wa mazao haya lazima kununua viwatilifu, lazima kununua pembejeo ili kuanzia pale shambani mkulima anapoanza zao liwe na *quality*. Maana katika ushindani wa dunia ya leo huwezi ukapeleka ma-pears ambayo yana alama 1000 katika pears hilo hata ukaulize Ulaya watakushangaa. Huwezi ukalilima hilo bila kutumia dawa za kutosha na kulilima kwa kutumia mbolea halisi ili litoke na sura inayokubalika.

Ndizi lazima uchague aina ya ndizi. Maua yametamkwa hapa wenzetu wa Kenya wana *export* ya maua 1.3 billion dollars. Sisi tuko kwenye 300,000 ni hela iko nje nje, tukiwekeza na kuwawutia watu na kuwapa motisha watalima lakini leo utakuta wakulima hawa wa mboga mboga na matunda wanahangaika wenyewe hawana msaada wowote wa Serikali. Mimi ningeomba Waziri sina tabia ya kutounga mkono Serikali yangu. Ninajua kasungura haka ni kadogo sana lakini lazima tugawane wote kwa haki.

Naomba busara zitumike katika kugawa ili kila mtu apate kidogo kidogo. Sisi wakulima wa matunda na mboga mboga na sisi tupate haki. Kwa leo Lushoto kumekauka hakuna maji. Mimi nilitigemea hata suala la umwagiliaji lingeangaliwa kule Waziri anaweza kujibu kwamba inawezekana liko katika utaratibu ule wa *ASDP*.

Lakini ni ukweli kwamba tunapeleka maombi, hayajapata majibu. Sasa sisi twende wapi, maji yanakauka, matunda ya ardhisi tuko wengi kule milimani. Ni kweli mtatuambia tuhamie maeneo mengine, sasa hivi watu ni wajanja. Maeneo mengine utahamia wapi? (*Makof*)

Sawa mnaweza kutuandalia, lakini kumhamisha mwananchi kutoka Lushoto aende akakae Handeni, Kilindi siyo kazi rahisi ilikwisha tamkwa tangu wakati wa ukoloni mazoea ya baridi kule ni tofauti na huku kwenye ukame.

Kwa hiyo, tunahitaji kuwasaidia wananchi waweze kuendesha kilimo chenye tija. Kilimo chenye tija ni kile ambacho kinahitaji matumizi bora ya pembejeo. Pembejeo ni ghali, Mbunge mmoja ananiambia nienda Kaliua, siwezi kwenda kukaa jangwani kule ni mtani wangu huyu Mheshimiwa Kapuya. (*Makof*)

Kwa hiyo, mimi niombe sana Wizara kama iliyotamka na madhumuni ya kuhakikisha kwamba kilimo cha mboga mboga na matunda kinapewa umuhimu wa kwanza. Sasa tuone matendo vijana walioko kule wasaidiwe mitaji midogo midogo wanunulie pembejeo. Tusaidiwe uwezekano wa kujenga mabwawa ambayo yatasaidia kumwagilia mwaka mzima.

Sasa hili tusipoliona nasema kwa kweli mwaka ujao kidogo nitakuwa mkali. Nitakuwa sina tabia na naomba sana hiyo tabia iondoke ili Serikali yetu mapato ni madogo hatuwezi kila mmoja akaridhishwa katika upande wake. Lakini tugawane sungura huyu kwa haki, kila mtu apate.

Katika kupata ni kuoneana huruma matunda na mboga mboga ndio yatakayosaidia vijana wanatoroka vijijini kwa sababu unalima kabeji huwezi kupiga dawa, unalima nyanya huwezi kuipiga dawa kwa vyovyote itakufa. Vijana hawa hawana mitaji wanatoroka wanakwenda mjini kwenda kuuza pini, kwenda kuuza vitu vya ajabu ajabu sana. Sasa tuhakikishe tunawavutia kule vijijini kwa kuwapa mitaji pamoja na mambo ambayo tunaweza kuwafanya ili wakubali kukaa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sipendi nipigiwe kengele ya pili, nimwombe Waziri Mkuu asisitize sana katika mambo niliyoyasema mbolea ya minjingu itumike, nina uchungu sana kile kiwanda kimepanuliwa kwa juhudini nyingi. Lakini kwa sasa hivi kama vile tumefanya mchezo mbolea tunahitaji nchini wananchi wanalamika mbolea imejaa. Suala la usindikaji wa mazao ni moja ya mambo ambayo yatasaidia sana vijana wapate ajira. Hili lipewe kipaumbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, umwagiliaji na mabwawa kama walivyosema wengine juhudini za umwagiliaji zimeendelea sana. Kwa mfano, tuna *scheme* ya kitivo kule Lushoto. *Scheme* za Mombo, lakini ukiangalia kweli tathimini ya ongezeko la mazao ni ndogo sana. Baada ya

kusema hivyo naunga mkono hoja, nashukuru sana nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofî*)

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote na mimi naomba niungane na wenzangu kutoa pole nyingi sana kwa maafa yaliyotokea ya ajali ya meli hivi majuzi kule Zanzibar.

Aidha, naomba kwanza ni-declare *interest* kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho, Tanzania ambaye niliteuliwa tarehe 8 Agosti, 2011 - mwaka jana. Hata mwaka haujatimia bado tangu niteuliwe. (*Makofî*)

Vile vile nianze kwa kukumbushia methali moja iliyosemwa hata jana ingawaje ilitaka kuleta tafrani kwamba akili ni nywele kila mmoja ana zake. Mimi ningependa kuelezea hayo ambayo nitapenda kuelezea hapo baadaye wala siyo tusi hili la kusema kwamba hata nywele zetu hazilingani. Wengine wana nywele chache, wengine nyingi, wengine nyeupe wengine nyeusi hiyo ndio methali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja. Ninaomba nimpongeze sana Waziri kwa hotuba yake. Lakini nitilie mkazo kwa mambo mawili viwanda nya korosho. Katika maeneo ya korosho viwanda vipo ila vilibinafsishwa. Waliouziwa tena kwa bei chee hawavitumii. Matokea yake ni mabaya sana. Haya matatizo yanayofikirwa kwamba ni ya Bodi, siyo ya Bodi.

Sasa hivi tunauza korosho zetu karibu zote nje ya nchi, badala ya kubangua hapa nchini tumepeleka soko India huko ndiko wanakopata watu kazi na vitu vyote vinavyotokana na korosho. Korosho siyo ile mbegu ya kutafuna peke yake, lakini lile ganda ni mali zaidi kuliko hata korosho yenewe hapo baadaye.

Kwa hiyo, tunapeleka nje. Kwa hiyo, tunaomba ile kadhiya ya viwanda hivi hebu ifanyiwe kazi. Tunaomba viwanda hivyo na vikirudishwa vikafanyiwa mikakati mizuri tutabangua korosho zetu zote. Kwa kweli mimi ninaomba sana jambo hili lifanyike. (*Makofî*)

Lakini wakati huo tunafanya hivyo kuna suala la uuzaji wa korosho zenyewe. Mimi naomba ule mkakati aliousema Waziri wa *Commodity Exchange* tafadhalii mimi nadhani tumeanza siku nyingi sana kuzungumza hebu tulimalize hili jambo. Hiyo ndio dawa ya mauzo ya korosho. Kwa sasa hivi hakuna zao ambalo kweli kidogo halilendi vizuri katika mauzo kama korosho. Kwa hiyo, haya mambo mawili ndio yatakayoweza kufufua hili zao la korosho na wakulima wakapata faida ya maendeleo ya korosho zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ukurasa wa 19 alisema kati ya mwezi Oktoba mwaka jana na Januari mwaka huu, Bodi ilipata shilingi bilioni 2 kwa ajili ya shughuli za kuendeleza tasnia ya korosho nchini. Labda niweke sawa kwamba kutokana na fedha za *export levy* zilipatikana zaidi ya bilioni 15 katika hizo bilioni 15 bodi ilipewa hizo bilioni 2 kwa ajili ya kuendesha shughuli za kusimamia tasnia hii.

Kwa hiyo, hazikuwa kwa ajili ya kuendeleza hiyo tasnia ni kusimamia. Hizi bilioni 13 zilizobaki Waziri bila shaka katika maelezo yake ataaeleza zimekwenda kwa wadau mbalimbali ambao wana kazi ya kusimamia tasnia yote pamoja na bodi. Kwa hiyo, ni vizuri kuweka maneno vizuri kuliko kuyaweka jumla jumla kwamba basi bilioni mbili za tasnia hazikufanya kazi hiyo siyo sahihi. Naomba hilo la kwanza kulisahihisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, vile vile mimi najua kwamba katika hizi ofisi zetu kuna watu wanaendewa halafu kazi yao kuchomoa karatasi kuwapa wasiohusika. Lakini wangewaambia maneno ya ukweli siyo kuchukua tu karatasi halafu unakuja kuyatoa hapa unaonekana hukusema ukweli. Mimi sipendi kusema lakini nataka niseme hili moja ambalo lilisemwa hapa ambalo ni kwa masikitiko kabisa kwamba eti Mke wa Mheshimiwa Mudhihir alilingia kwenye Bodi akalipwa.

Mimi nasema mtu aliyeandika hivi, kwanza hamfahamu Mheshimiwa Mudhihir. Kama angemfahamu angejua tatizo la Mzee Mudhihir. Mheshimiwa Mudhihir alikuwa ni Mbunge hapa,

alipopata ajali akiwa Mbunge, hata hapa Bungeni alikuwa na msaidizi wake, alikuwa anasaidiwa. Sasa kule kwenye Bodi yeye ni Makamu Mwenyekiti, huwezi kumwambia njoo kwenye Bodi kutoka Dar es Salaam peke yake kwa hali aliyo nayo, amepewa msaidizi wa kumsaidia. Sasa yeye kachagua kusaidiwa na mkewe. Nongwa iko wapi?

Ndugu zangu hili kama mngeuliza tungewaambia kwa nini, wala hakuingia kwenye Bodi wala haingii. Humo ndani tuna Wabunge wenzetu pia walemaru hawaingii na wasaidizi wao wanakaa nje. Kwa hiyo, huyo mama anakaa pale nje anamngojea mzee yule anapotoka mle ndani kama ana shida yake anamsindikiza anamsaidia anarudi.

Ndugu zangu haya maneno yaliyoandikwa hapa myasahihishe si kweli kwamba anaingia kwenye kikao yeye si mjambe wa kikao. Anakaa nje ya ukumbi wa Mkutano, anamsaidia Mheshimiwa Mudhihir. Yule kwa kuwa tu ni mkewe ndio maana mnaandika. Lakini ni msaidizi wake kwa hii shughuli maalum ya kuwa mjambe wa Bodi. Naomba tuyarekebishe haya maneno.

Sio vema kuandika vitu ambavyo kwa kuwa mmevisikia ni kweli amelipwa wala sikatai, lakini sio kwa sababu yeye ni mjambe, kwa kuwa yeye ni msaidizi wa mjambe ambaye ana ulemavu maalum unaotakiwa awe na msaidizi. Kwa hiyo, nilitaka nieleze hilo. (*Makof*)

Kuhusu Mheshimiwa Jerome kwa bahati mbaya hayuko humu leo ndani lakini angeeleza inaonekana amelipwa mara mbili siku moja. Nataka niseme hivi, ile siku alilipwa kweli siku moja lakini alifanya kazi nydingine kabla ya pale. Tumekwenda katika orodha yote ya shughuli alizofanya aliiwtwa.

WABUNGE FULANI: Ahaa!

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Ndio sasa mnakaidi nini mkaguzi yupo atakwenda kukagua yatakuja hapa. Sasa nasema msiandike mambo kwa kusikia wala kwa kupewa. Guna ufanyeje lakini mseme maneno ya ukweli. (*Makof*)

Kuhusu kwamba wakulima hawakusaidiwa, nataka niseme katika mwaka ambao wakulima wamesaidiwa ni mwaka huu. Tulipotangaza bei ya dira ilikuwa shilingi 1200 kwa kilo moja ya korosho. Mnada wa kwanza tulipata shilingi 2200 tukaona mambo ni mazuri sana mkulima atafaidika.

Lakini kwa sababu zisizojulikana kwa ajili ya *curtail* ya ununuzi wa korosho bei ile mara inakuwa kubwa, mara watu hawataki kununua wakagoma wanunu. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiongozwa na Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete iliamua kwamba wakulima wote wa korosho watalipwa bei ya shilisngi 1200 na Serikali ikatoa *guarantee*.

Kila Chama cha Ushirika kilitakiwa kuchukua fedha za kulipa mkulima ili apate shilingi zake 1200. Sasa kilitokea nini kwa vyama vingine pengine hilo ndio kazi inayofanyika sasa kujua fedha zilikwenda wapi ama hawakuchukua. Lakini Serikali ilitoa *guarantee* na mimi naishukuru sana Serikali bila hivyo ingekuwa ni mgogoro mkubwa sana.

Baada ya Serikali kutoa *guarantee* ndipo hata wale waliokuwa wanagoma kununua korosho wakaanza kujitokeza na wengine kinyemela kuja kununua zile zile korosho. Lakini dawa ya zao la korosho ni kubangua.

Kwa kweli hata tukisema tunataka kuanza tena kujenga viwanda, viwanda viwo zaidi ya 10. Naomba sana kazi hii ya kuangalia hivi viwanda vinafanya kazi gani hebu tuimalize mapema ili kadhia hii iishe tafadhalini sana. Naomba sana Serikali yangu ifanye hii kazi.

Lakini naomba nikipongeze Chama Kikuu cha Ushirika cha Newala Tandahimba, *TANECU* wao walikwahkenda *TIB* kwenda kukopa fedha za kujenga kiwanda, nafikiri shughuli karibu zinaanza za kujenga mpaka mwakani watakuwa wanaanza kubangua korosho zao na pengine vyama vyote vya msingi kama kweli Serikali inataka kuwaachia hawa walionunua hivi viwanda wabaki na yale magofu lakini mimi ningombia pia Vyama vya Ushirika vifanye hivyo *TANECU*

wameonyesha njia na mimi nina hakika mwakani kwa korosho za Chama kile zote zitanunuliwa na wananchi wenyewe watabangua.

Hili ni nzuri kwa sababu anayebangua ni Chama kile kile cha Ushirika ambacho ndicho ni mzalishaji. Kwa hiyo, hata fedha zitakazopatikana korosho zilizobanguliwa zitarudi tena kwa mkulima kuliko hivi sasa. Kwa kweli mkulima wa korosho akishauza korosho yake hakuna kitu kinarudi tena kwake isipokuwa ile ya mauzo tu hela zote za korosho, korosho jamani ina hela kubwa sana wanaoenda kuiuza kuna fedha nyingi sana.

Kwa hiyo, hizi haki yake ingekuwa inarudi angala sehemu kwa mkulima. Kwa hiyo, mimi naviomba vyama vyaya ushirika viwe na ubanguaji. Nashukuru sana na naunga mkono hoja hii. ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Nitoe matangazo kidogo halafu tutaendelea na Mheshimiwa Magdalena Sakaya na wengine.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 10 wa Mheshimiwa Moshi Kakoso, ambaa ni Wabunge ambaa ni wajumbe wa Shirikisho la Vyama vyaya Ushirika wakiongozwa na Ndugu Hassan wa Kasuvi Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tabora. Karibuni sana wageni wetu kutoka Shirikisho la Vyama vyaya Ushirika. Wageni 5 wa Mheshimiwa Paul Lwanji, wakiongozwa na Ndugu Charles Mzilo Mwenyekiti wa CCM wa Kata ya Ipande. Karibuni sana Ndugu zangu kutoka kule Ipande, karibuni hapa Bungeni. (*Makof*)

Mwenyekiti wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko Dkt. James Wanyancha amefuatana na mjambe wa Bodi Ndugu Godwin Mkanwa karibuni sana. Mheshimiwa Dkt. Wanyancha alikuwa Mbunge mwenzetu na Mheshimiwa Godwin Mkanwa alikuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa mpaka majuzi hapa. (*Makof*)

Kuna walimu wawili na mwanafunzi mmoja kutoka shule ya Canon Dayosisi ya *Central Tanganyika Dodoma*. Karibuni sana. Waheshimiwa Wabunge, Shule ya *Canon* iko hapa karibu sana na jengo la Bunge hapa. Karibuni sana hapa Dodoma. Ahsanteni sana. Naomba tuendelee baada ya Mama Anna Abdallah, kumaliza sasa nimwite Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kidogo kwenye hoja ambayo iko mbele yetu. Lakini pia niungane na Wabunge wenzangu na Watanzania wote kuomboleza na kutoa pole kwa msiba mzito uliotupata wa kupoteza ndugu zetu katika ajali ya meli iliyotokea, Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuwa na maendeleo ya kilimo Tanzania na kuondoa umaskini kwa Watanzania kwa kuendelea kutenga kiasi cha fedha kinachotengwa kila mwaka kwenye Wizara muhimu kama hii.

Ukisoma maombi ya fedha zilizoombwaa, ukisoma fedha ambayo imetengwa na Serikali inasikitisha. Fedha ambayo imeombwa na Wizara hii mwaka huu shilingi bilioni 237.62 katи ya hizo bilioni 170.3 ni fedha za *administration*. Shilingi bilioni 67.2 ni fedha kwa ajili ya maendeleo.

Kati ya hizo shilingi bilioni 67 bilioni 52 ni fedha tunazotegemewa kutoka nje. Tunawezaje kuendeleza kilimo kwa asilimia zaidi ya robo tatu kutegemea ufadhili? Hela ya ndani iliyotengwa ni bilioni 14.9 tu.

Hivi mimi nikawa najiuliza hii bilioni 14.9 ambayo ndio tuna uhakika nayo ndio fedha yetu ya ndani ya nchi inaweza kufanya nini Tanzania nzima Mikoa yote tuliyonayo kuendeleza kilimo itajenga *scheme* za maji Mikoa yote, itaweka mbolea ya ruzuku, itatoa huduma za ugani, itajenga viwanda vyaya kusindika, bilioni 14.9 tuliyotenga inaweza kusaidia kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kwa sababu Serikali inafahamu. Fedha ya ufadhili ina changamoto zake na tumekuwa tunaziona ndiyo maana kila Mbunge anayesimama hapa

anasema *scheme* haziendelei, zipo za miaka tangia 2008, 2006, 2007 haziendelei kwa sababu pesa tunayotenga ni kidogo.

Hatutaweza kuwa na kilimo kwanza kweli kama Serikali itafika mahali tuone kwamba *at least*, angalau nusu ya pesa ya kilimo inatoka ndani ya nchi. Hili ni tatizo kubwa sana na kweli njaa itaendelea kuwepo, kina mama wataendelea kuteseka, vijana wataendelea kutoka Vijiji kuhamia Mijini kwa sababu kilimo hakina tija Vijiji na matatizo bado yataendelea kuwepo katika nchi yetu kwa sababu hatutengi fedha ya kutoshakuinua kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha kama hii ambayo imetengwa hata ukiangalia vyuo vyetu nya utafiti, karibia vyote viko hoi, havifanyi kazi kwa sababu hawawezeshwi na hatuwezi kuwa na kilimo bora, kilimo ambacho ni cha kisasa kama hatuna tafiti za uhakika. Vyuo vyetu nya utafiti viko hoi, havina pesa, haviwezeshwi kiutendaji, vinafanya kazi chini ya viwango kwa sababu hakuna fedha ya kufanya kazi. Tunacho chuo kimoja tu Tanzania nzima ambacho kipo Kibaha ambapo kinafanya kazi ya kutafiti magonjwa mbalimbali ya mazao hapa nchini.

Chuo hiki, ndiyo chuo pekee kinazalisha wadudu ambao ni *friendly* kwa ajili ya wakulima na kuwasambaza kwa wakulima na kwenda kufuatilia ustawi wao kwenye mashamba. Chuo hiki ni miaka mingi hakijawezeshwa, chuo hiki kimefanya kazi muda mrefu na kimeweza kutatua changamoto, kimesaidia katika mambo mengi, ndiyo chuo ambacho kimeweza kuibua magonjwa ya utitiri wa mihogo, magugu maji, funza wa mabua, magonjwa ya kebichi, funza weupe na mengine mengi.

Lakini magonjwa mengi haya ambayo yameibuliwa na chuo hiki yalitoka nje ya nchi kwa muda karibu miaka kumi chuo hiki Serikali imekisahau kabisa, kina changamoto nyngi kweli kweli. Sasa kama tuna chuo kikubwa kiasi hiki na ni kimoja Tanzania nzima na tunakaa hatukiangalii, hivi kweli kwenye kilimo tunakwendaje? (*Makof*)

Ukiangalia changamoto kubwa za Watanzania kuna madudu yanayoingia kila kukikicha, Watanzania wengi wakulima wanasumbuliwa na magonjwa ya mazao yao na hatuwezi kuyaondoa kama hatuwezeshi vyuo nya utafiti. Tukiangalia mazao mengi yanayozalishwa Tanzania, mazao ya mbogamboga yanashindwa kwenda kupata masoko mazuri ndani na nje kwa sababu ya kushambuliwa na wadudu. Tukiangalia leo Tanzania, tunalima nyanya nzuri, haziwezi kupata soko nje la kutosha.

Tunalima maembe, hayaendi nje kwa sababu ya magonjwa, tunalima mihogo haziwezi kupata soko zuri nje kwa sababu ya magonjwa. Chuo kama hiki ndiyo ambacho kinaweza kusaidia kupambana na magonjwa kama haya, tuweze kuwa na mazao mazuri yaliyo kwenye viwango, tupate soko zuri ndani na nje kwa sababu shida kubwa ya wakulima wa Tanzania ni kutokupata masoko mazuri. (*Makof*)

Lakini Serikali imetulia, kipo Kibaha hapa Pwani. Imetulia, tuna wataalamu wazuri pale wamekaa kwenye benchi hawana cha kufanya. Wana changamoto nyngi, wanahitaji kutoa elimu, mimi bahati nzuri pia ni mtaalamu wa kilimo na mifugo sio *insecticide*, siyo viuatilifu vyote ambavyo vinafaa kwa kila mmea, wadudu wengine ambao wako ndani ya mimea ni kama kinga kwa ajili ya ile mimea, lakini wakulima wanapoenda kutumia *insecticide* au viwatilifu, vinakwenda kuuwa wale wadudu ambao ni *friendly* kwa ajili ya wakulima.

Kwa hiyo, matokeo yake mmea unakua hauna kinga, mdudu ye yeyote anapokuja anaingia kirahisi pale. Sasa chuo kama hiki, wataalamu wa chuo kile, walitakiwa wazunguke nchi nzima kutoa elimu kwa wakulima, wadau mbalimbali, Wabunge kwa sababu ndiyo wasimamizi wakuu wa shughuli za maendeleo, Madiwani, hawawezeshwi, wako pale hawana cha kufanya. Hawana maabara ambayo inaweza kufanya kazi za kitaalamu vizuri ikaweza kufanya kazi kwa ufanisi hawana. Hawana elimu ya kutosha, hawawezi kutoa elimu ya kutosha na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri chuo cha Kibaha akitambue, Serikali iweke uzito wa kutosha, itoe kipaumbele chuo hiki kiweze kufanya kazi kwa utafiti kusaidia wakulima wa Tanzania hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na chuo hiki pia niombe Serikali tuwe makini sana kufuatilia mazao yanayoingia ndani kutoka nje ya nchi kwa sababu magonjwa mengi yanaingia kupitia mipakani. Serikali ihakikishe kwa kupitia Wizara hii ya kilimo inakuwa na ukaguzi makini unafanyika kabla ya mmea wa aina ye yote kuingia ndani ya nchi.

Tumekuwa tunasafiri mara nyngi, huwezi kuingia hata na jani, kijani au mbegu kwenye nchi za wenzetu lakini nchi yetu inaonekana kuna udhaifi mkubwa, tunaiomba Serikali ihakikishe kwamba mipakani, viwanja vya ndege, maeneo yote ambapo kuna usafiri wa aina mbalimbali wahakikishe kwamba kabla ya chochote kuingia ndani ya nchi yetu kinachunguzwa ili kuweza kuepuka na magonjwa haya ambayo yanashambulia mimea yetu, mazao na inakuwa ni hasara kwa wakulima na pia tunashindwa kuwa na mazao ambayo ni mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye madalali wa mazao. Inasikitisha sana, wakulima wetu pamoja na kuwa wanalima na wanazalisha madalali wamekuwa wanawalalia na kuwaonea sana wakulima na Serikali imeshindwa kuliona hili, ni kwanini Serikali imeshindwa kuweka vipimo maalum kwa ajili ya mazao ya wakulima Vijiini?

Mwaka 2009 nilikuwepo hapa, Mheshimiwa Mama Nagu alikuja Bungeni akatuambia Serikali imekataza lumbesa Vijiini, akasema Serikali inaleta mizani, wakulima watumie mizani kwa ajili ya kuza mazao yao. Cha kusikitisha baada ya miezi miwili, akaja na tamko lingine Serikali imesitisha mpango ule kwa sababu mizani hazijapatikana. Sasa mimi najiuliza swali, 2009, 2010, 2011, 2012 kweli mizani hazijapatikana? Kwa nini wakulima waendelee kuonewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Vijiini, tena hapa wanapouza viazi hapa karibu na Kongwa hapa, hapa Kibaigwa, gunia moja, wanachukua magunia mawili ya viazi, gunia moja hata watu watatu hawawezi kubeba. Sasa yule mkulima kapata haki yake pale?

Huu ni wizi naiomba Serikali ihakikishe inakuja na mizani za kuwasaidia wakulima. Wafanyabiashara wanakwenda Vijiini na viloba vya debe kumi, wakulima wanadanganyika, lakini Serikali imenyamaza kimya, hatuwezi kumwondoa mkulima kwenye umasikini kwa kuendelea kuacha aonewe kiasi hiki. (*Makof*)

Muda unakwenda haraka, lakini niende kwa haraka. Nataka niseme suala la tumbaku kwa Mkao wa Tabora na Mikoa mingine. Kwa kweli, wengi wameongea hapa Bungeni, lakini nashindwa kuelewa kwa nini kila mwaka ushauri tunaotoa sisi Wabunge haufanyiwi kazi? Tumekuwa tunasema kwamba WETKO ambayo inasimama kati ya makampuni na vyama vya ushiriki ni wezi, hakuna kazi wanayoifanya pale WETKO, kwa nini kampuni isiende *straight* kwenye vyama vya ushirika ambavyo vinaunganisha wananchi, kwanini WETKO hapa katikati ana kazi gani pale?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine la wale ma-classifiers. *Classifiers* ni rushwa ya ajabu inayotembea, wapo wakulima wanauzu tumbaku mpaka shilingi 200 kwa kilo kwa sababu kashindwa kutoa.....

*(Hapa Kengele illilia kuashiria kumalizika
muda wa mzungumzaji)*

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Kwanza niwape pole sana Watanzania wenzetu waliopata ajali kule Zanzibar, lakini pia niwatakie Waislamu wote waliobahatika kufunga mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Ramadhani Kareem na wale amba kwa bahati mbaya hawakufunga basi *Inshaalah* Mwenyezi Mungu pia awabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza, kuna mchangiaji mmoja hapa ndani ya Bunge alisema kwamba Sera mbovu za CCM ndiyo zinafanya vijana wengi wanazurura kuza maji. Inawezekana upeo wake wa kutambua matatizo ya ajira duniani ni mdogo. Leo Marekani na mimi mwaka jana tu nilikuwa huko kuna tatizo la ajira hakuna CCM inayotawala pale, Uingereza

kuna tatizo la ajira kwa vijana, hakuna CCM inayotawala pale Ufaransa na nchi nyingine zote duniani, hakuna CCM inayotawala pale. Tusitumie tatizo la ajira kama kigezo cha kujitafutia umaarufu ndani ya Bunge na ndani ya Tanzania hii. Niko tayari kupokea taarifa ya mtu yeoyote kama mtu makini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la chakula. Hali ya chakula kwa kweli si nzuri sana katika maeneo mengi kutokana na kutokuwepo na mvua ya kutosha mwaka jana. Kwa hiyo, ningeomba Wizara itizame jambo hili hata kwenye Jimbo langu la Wilaya ya Kondoa tatizo la chakula liko kwenye baadhi ya maeneo. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia jana Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kwenye ukurasa wa 96 alisema "*Kilimo ni biashara inayoweza kuleta utajiri na maendeleo kama zilivyo biashara nyingine kwa kuwa kilimo kinaajiri asilimia 75 ya Watanzania, kina nafasi kubwa ya kupunguza umaskini katika nchi yetu*". Mwisho wa kunukuu. Tunapozungumza kilimo ni biashara, lazima tuhakikishe kwamba kweli kile kinacholima kama ni cha biashara, kinapata soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shahidi pia hata katika Jimbo lako, vijana wengi na Watanzania wengi ni wakulima wazuri hasa wa zao la alizeti, lakini soko la alizeti limekuwa finyu na hii inasababishwa sana na baadhi ya makampuni yanayoagiza *crude oil* ya alizeti kutoka nje ya nchi.

Mimi hili nitaendelea kulisemea leo, kesho na hata mille. Sina tatizo lolote na watu kuagiza mafuta ya kula kutoka nje *crude oil*, lakini hata kwenye alizeti? Ningeomba sana kwenye alizeti Serikali iangalie jambo hili na wapo wanasema hakuna *crude oil* ya alizeti kutoka nje si kweli. Yapo makampuni yanayoingiza *crude oil* ya alizeti. (*Makof*)

Wakulima wa Singida, Dodoma, Manyara, Tabora, Iringa sasa hivi wanalima alizeti kwa wingi sana. Ebu tuangalie ni jinsi gani tuzuie *crude oil* kutoka nje ama tuongeze VAT yake iwe kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, alizeti inaweza kulisha nchi hii kwa asilimia 7 ya mafuta bado ni kidogo, lakini nina hakika tukipiga marufuku *crude oil*, alizeti kutoka nje, wakulima wetu watapata soko la uhakika sana. (*Makof*)

Sisi kwenye Mkoa wa Dodoma kwenye kikao tume- *declare* kwamba alizeti ndiyo zao la biashara la Mkoa huu. Lakini tukiendelea kuachia *crude oil* ya alizeti kutoka nje kwa watu wanaosema eti hakuna *crude oil* kutoka nje kuna *pam* tu, tuache *pam* ije, lakini alizeti kama tunaiingiza tusinginze *crude oil* lakini vile vile ikiwezekana tupige marufuku uingizaji wa *crude oil* ya alizeti kutoka nje, itatusaidia sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nje kwenye umwagiliaji. Kwenye Jimbo langu pale mwaka jana tulitengewa milioni 700 kwa ajili ya umwagiliaji pale Kidoka, lakini tumechimba visima viwili pale mwaka jana, hakuna kitu kinachoendelea. Sasa hata hizo milioni 700 haziwezi kuchimba visima viwili.

Kwa hiyo, ningeopmba Mheshimiwa Waziri ebu jaribu kufuatilia jambo hili. Umetenga 700 million, umechimba visima viwili vya milioni 90, hizi nyingine zinafanya kazi gani hakuna kitu kinachoendelea pale. Naomba sana jambo hili mliangalie kwa makini.

Kwenye Jimbo langu kule Mrijo, Jangalo, Itolwa ni wakulima wazuri sana. Tunalima pale kwenye eneo la sikia ambako ni mpakani kati ya Kiteto na Chemba, zamani Kondoa. Warangi wa Kilima wale watani zangu wa masai, mazao hayajavunwa wanaingiza ng'ombe.

Kila siku jambo hili linazungumzwa leo, kesho, kesho kutwa na wakulima hawa wanafuata taratibu zote, wanakwenda kwenye Vijiji pale, wanajijandikisha tunataka kulima hapa, lakini watani zangu pale wanakwenda wanachukua ng'ombe wanaingiza kwenye mashamba kabla watu hawajavuna.

Lazima watakuwa hawana chakula. Matokeo yake wakati mwingine wanajaribu hata kushukua sheria mikononi lilishawahi kutokea hata huko nyuma. Lakini tunajaribu kuwashamasisha wasichukue sheria mikononi kama iliyotokea miaka minne, mitano iliyopita. Naomba sana Wizara ya Kilimo iangalie jambo hili, iangalie tatizo lilioko pale Kondoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye mbolea. Wengi wamezungumzia kiwanda cha Minjingu, mimi naamini kabisa kwamba tunaagiza mbolea nyingi sana kutoka nje wakati kiwanda cha Minjingu pale kina mbolea ya kutosha na ni ajira kubwa sana kwa watu walioko pale kwa sababu eneo lile hakuna kitu kinaweza kustawi, eneo lile ni kame lakini mbolea ile, kiwanda kile ndiyo kinatumika kama sehemu kubwa ya ajira kwa wananchi wa eneo lile. (*Makof*)

Naomba sana Serikali iangalie kwa namna gani ambavyo inaweza kuboresha suala la Minjingu ili mbolea ya Minjingu iweze kutumika nchini badala ya kuagiza kiwango kikubwa cha mbolea kutoka nje. (*Makof*)

Lakini nadhani kama tukitumia gesi iliyopo, tunaweza kutengeneza kiwanda cha *yurea*, ukichukua *yurea* ile na kiwanda kingine hiki cha Minjingu, Tanzania inaweza kujitosheleza kwa mbolea badala ya kuagiza kiwango kikubwa cha mbolea kutoka nje, gesi tunayo ya kutosha sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwenye suala la matrektta. Matrektta yalipoingia hapa nchini ya mikopo haya, mimi kwangu karibu vikundi 26 vilikopa, bei ikaja ikashuka. Sina hakika Serikali kama mtatusaidia na sisi vikundi vile vilivyokopa wakati ule bei ikiwa juu, walipe sasa kwa bei ya sasa, lakini pia kwenye vipuri vya matrektta tulipitisha kwenye Bunge kama sikosei mwaka jana hapa, kwamba vipuri vya matrektta visitozwe kodi, lakini bado VAT inatoza kodi ya vipuri vya matrektta.

Kwa hiyo, naomba sana bado *TRA* wanatoza kodi ile, naomba sana Serikali ebu angalieni jambo hili. Lakini pia leo unapomwambia mkulima yuko tayari kukopa trekta wakati ardhi yake hajathaminiwa, inakuwa vigumu kweli.

Kwa hiyo, ningeomba Serikali kwenye jambo hili iangalie ni namna gani Wizara ya Ardhi itahusishwa na Wizara ya Kilimo ili wakulima hawa waweze kukopa matrektta yale kwa urahisi zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja na nikumbushe tu kwamba matatizo ya ajira duniani sio ya CCM bali ni ya dunia nzima. Ahsante sana. (*Makof*)

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema na fadhila zake nyingi, nikushukuru nawe kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Nianze pia kwa kutoa salaam za rambirambi kwa ndugu na jamaa wote ambao wamepoteza ndugu zao katika ajali ya meli iliyotokea hivi karibuni kule Unguja na niwatakie kheri pia wale wote wenye kutekeleza lbada ya kufunga. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa nijielekeze katika hoja. Nianze na Maafisa Ugani. Ni kweli kwamba idadi ya vyuo vimeongezeka kutoka vyuo vinane hadi vyuo kumi na nne. Ni dhahiri pia wahitimu wameongezeka, lakini tatizo la Maafisa Ugani bado ni kubwa katika nchi yetu na kinachosikitisha zaidi ni kwamba wahitimu hawa ambao wangeweza kuja kuwasaidia sana wakulima wetu wakibadili kilimo chao kuwa ni kilimo cha kisasa na kilimo bora hawana ajira.

Wamekaa, wamehitimu, walikuwa wanatarajia kwamba elimu walioipata, wangeweza kwenda kuwasaidia wazazi wao na ndugu zao na Watanzania wenzao Vijijini, lakini hawana ajira.

Jambo hili, nafikiri Serikali sasa imefika wakati wa kuacha ubabaishaji. Waangalie suala la kuwasaidia wakulima Vijijini kwa kuwapeleke Maafisa Ugani. Niwaombe waangalie hawa vijana ambao hawajaajiriwa, waweze kuajiriwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la kilimo cha umwagiliaji. Katika nchi yetu kilimo kimekuwa kikitegemea mvua, mvua ambazo zimekuwa hazina uhakika. Wakati mwininge zinakuja mapema sana au zinakuja kwa kuchelewa, zinakuja nyngi au zinakuja kidogo na zimekuwa hazitabiriki na mara kadhaa maeneo mengi yamekumbwa na ukame, kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Kwa hiyo, matarajio kwa watu makini na kwa Serikali makini, ni lazima iwekeze sasa nguvu zake zote katika kilimo cha umwagiliaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana kwamba, jambo hili, halipewi umuhimu unaostahili, halisimamiwi ipasavyo na hakuna jitihada zozote za kuhakikisha kwamba, miradi hii ya umwagiliaji inakamilika kwa wakati. Kumekuwepo na mradi wa umwagiliaji kule Ugala, katika Kijiji cha Ugala, mpaka sasa mradi huu haujakamilika, ungeweza kumwagilia zaidi ya hekta 3000, ambazo zingeweza kusaidia sana kuongeza chakula. Ni kwa nini na kwa sababu gani mradi huu haujakamilika? Mimi sifahamu, nitapenda Wizara itueleze mradi huu unakamilika lini?

Mheshimiwa naibu Spika, lakini pia kuna mradi wa Mwamkulu, ambao tayari banio limekamilika, mifereji hajatengenezwa. Yenyewe pia ingeweza kusaidia sana. Kuna mradi wa Kakese, nao haujaanza. Nigombe tu Serikali, kwamba, kwa hali tuliyonayo katika nchi yetu sasa hivi ya kutokuwa na mvua zenye kutabirika, miradi hii ipewe kipaumbele, fedha zielekezwe huko, ziweze kukamilika kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Mwamkulu pia, una adha nyngine. Nitaitaka Serikali, itoe maamuzi ya haraka, ili kuhakikisha kwamba, wakulima katika eneo la Mwamkulu, wanawenza kufanya kazi zao vizuri, kwa kujiamini, na kwa kuongeza na kuwekeza katika kilimo. Eneo ambalo ni zuri kwa ajili ya kuzalisha chakula, linagombaniwa sasa na Hifadhi ya *Ubende Wildlife Management Area*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatukatai kuwepo kwa hizi *WMA*, lakini pia tuangalie pale ambapo zinawabughudhi wananchi, zinapunguza eneo la kilimo, basi tutazame kwamba, kilimo kinapewa umuhimu kwanza, kabla ya jambo lingine lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro huu nao, ningependa na kuisihi sana Serikali, ihakikisha kwamba, wameumaliza, ili wananchi wa Kata ya Kakese, ambayo iko katika Jimbo la Mpanda Mjini sasa na kwa namna yoyote haipakani na Hifadhi yoyote ya Taifa wala Pori lolote la akiba, waweze kuondolewa katika hiyo *WMA*, ili waweze kuendeleza kazi zao mahsus za kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Pembejeo ni adha, ni kero kwa wakulima wadogo wadogo. Toka umeanzishwa Mfuko huu, haujawasaidia sana wakulima wadogo wadogo wa Vijiini kwa sababu, umekuwa na usumbufu na urasimu usiokuwa na mfano, lakini tatizo kubwa ni kwamba, Mfuko huu mtaji wake unapungua mwaka hadi mwaka. Umuhimu wa wananchi sasa kukopa unafahamika, lakini fedha hakuna na hazitoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tu kushauri kwamba, kwa sababu, Mfuko huu una *chain ambayo*, inafika mpaka kwa mkulima mdogo kuitia Ofisi za Kilimo za Wilaya, basi ndio lingekuwa eneo la kuwasaidia wakulima wadogo wadogo maskini na wakulima wa kati na wakulima wakubwa, wakatumia dirisha hilo ambalo lipo katika benki ya *TIB* kwa sababu, wana uwezo wa kufika Dar-es-Salaam. Mfuko wa Pembejeo, ubakie mahsus kwa ajili ya wakulima maskini wadogo wadogo ambao wametapaka katika nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana, katika Taarifa ya Kamati, ukurasa wa 11, imetoa mapendekezo kadhaa kwa ajili ya kuwasaidia wawekezaji. Lakini kwa masikitiko, nasikitika sana kwamba, Kamati hii, imewesahau kabisa yale walijowatuma wapiga kura wao, wakulima maskini, hakuna hata kurasa moja ambayo Kamati, imetoa mapendekezo ni namna gani wakulima maskini katika nchi hii waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi, tunaonekana kwamba, akili zetu wote zimechotwa na uwekezaji. Hakuna njia ambayo tunafikiria isipokuwa ni kuwasaidia wawekezaji. Tunaanzia kwenye Kamati zetu mpaka kwenye Wizara na mpaka Serikali nzima. Sipangi uwekezaji, uwekezaji tunaweza kwendanao, lakini tutakuwa ni watu ambao hatujawatendea haki kabisa wananchi

waliotuchagua kwa sababu, hatuna mkakati wowote mahsus wa kumsaidia Mkulima mdogo mdogo, ambaye kwa miaka 50 kutoka uhuru amekuwa akililisha Taifa hili kwa juhud na maarifa yake bila kusaidiwa kwa namna yoyote. Ni lazima tuwe na mpango maalum sasa wa kuwawezesha wakulima wetu wadogo wadogo. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumewatendea haki wakulima maskini wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kuzungumzia kwa ujumla kuhusu mazao ya biashara. Taarifa zinaonesha Mazao ya biashara, yanapungua katika uzalishaji, tatizo ni nini? Ni lazima tupate suluhisho la kuangalia ni kwa nini mazao *traditional* yale ya biashara yanashuka katika uzalishaji? Tutafute mbinu bora ambazo zinaweza kuchochea, kuongeza tija na uzalishaji katika mazao ya msingi ya biashara, kwa maana ya kahawa, katani, korosho, pamba na kadhalika. Kila eneo lina matatizo lukuki, ni vyema sasa Wizara hii, ikajipanga kwa kadiri itakavyoweza kupunguza matatizo katika maeneo hayo hasa Bodi zinazosimamia mazao haya makuu ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la tumbaku na lenyewe lina matatizo lukuki. Ameyazungumzia kwa muhtasari Mheshimiwa Sakaya, naungana mkono na yeze kwamba, zao hili lina matatizo mengi, ni lazima tuangalie kwa makini ni namna gani tunaweza kuwasaidia wakulima wa tumbaku. Tuna tatizo la kutokuwa na *classifiers* wa kutosha, masoko yanachelewa, malipo ya wakulima hawapati kwa wakati, mkulima anaanza shughuli za kilimo cha tumbaku kuanzia mwezi wa Tisa na mpaka mwezi wa Tisa mwaka unaofuata, hajalipwa fedha. Hii inasikitisha, inawakatisha tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe tu wenzetu katika Bodi ya Tumbaku na Chama Kikuu cha *APEX* ya Tumbaku, wajipange vizuri. Wajipange vizuri, waangalie njia bora ya kuweza kuwasaidia wakulima wa tumbaku. Kuwasaidia wakulima wa tumbaku, ni lazima kuwepo na soko la uhakika. Makampuni yaliyopo yanashindwa kununua tumbaku yote inayozalishwa. Tumbaku ya ziada imeandaliwa mkakati gani, ili isijitokeze kama ilivyojitokeza msimu uliopita wa kutokuwa na uhakika wa kuuza tumbaku yao, wakulima ambao tayari walikuwa wameshashughulikia kwa kipindi kirefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Arfi, nakushukuru sana kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, nimekuwa nikipata vikaratasi vinavyonitaka nifafanue endapo baadhi ya mavazi ya leo ni sawa au si sawa. Nimetazama Mwongozo wetu hapa, ambao ni Kanuni, nikumbushie tu Kanuni ya 146 (b) na hasa Kanuni 146 (b) lakini ya (ii) ndogo ya Kirumi, "Vazi la Kimwambao litakuwa ni kanzu rasmi, koti, baraghashia, makubazi na viatu." Au kwa vile leo tunaanza mfungo, leo ni siku maalum kwa hiyo, tuvumiliane. Msiniletee tena vikaratasi, Waheshimiwa. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Mheshimiwa Kamani, atakayefuata ni Mheshimiwa Modestus Kilufi. Mheshimiwa Kamani!

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kumpongeza Waziri na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kuandaa Mpango huu wa uwekezaji katika Sekta ya Kilimo. Lakini zaidi nimpongeze Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa kufanikisha upatikanaji wa dola milioni 897 kwa ajili ya kuboresha kilimo katika nchi hii kuanzia mwaka ujao, mwaka 2013. Eneo moja muhimu lililotajwa ni pamoa na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nitoe angalizo mapema kabisa kwamba, fedha hii itakapokuja, safari hii sasa iangaliwe sehemu nyingine ya nchi hii, hususan Kanda ya Ziwa.

Nalisema hili kwa sababu, katika bajeti ya mwaka huu wa fedha, fedha nyingi za kilimo imeelekezwa kusaidia sana mpango wa *SAGCOT* wa Kusini mwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo jema tu na vizuri tuwe na vipaumbele, lakini niseme vile vile kwamba, Kanda ya Ziwa, tumechoka kuwa watu wa kutegemea msaada wa chakula kila mwaka, ni pamoja na Kanda ya Kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanda hizo zina mito, zina Ziwa, lakini kwa sababu ya ukame ambao unajirudia kila mwaka, ambao sio uchaguzi wetu tunakuwa na hali ya njaa kila mwaka. Ningombwa sana, maeneo kwa mfano, Jimbo la Busega, tuna Bonde la Lwangwe, ambalo linahitaji kuwekewa bwawa na Bonde lote la Busega, liweze kumwagiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri mwaka huu nimesikia juzi tu Serikali, imetangaza tenda kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la Lutubiga, naomba kazi hii ikamilike, ili kilimo cha umwagiliaji kiweze kuanza. Lakini vile vile tuna mwambao wa zaidi ya kilomita 120, katika Kata za Kiloleli, Mwamanyili, Kabita, Kalemela na Lamadi. Tuna Bonde kubwa la Mto Duma na Mto Simiyu katika Kata za Ngasamo, Malili, Badugu na Nyaluhande, zijengewe miundombinu ya umwagiliaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za Misri, Sudan, Zimbabwe, kimsingi ni kame zaidi kuliko Tanzania. Lakini kwa sababu, wameweza kukinga maji, sasa hivi watu hawa hawana shida na wanasafirisha hata chakula nje ya nchi. Ni kwa nini sisi tuendelee kuwa wategemezi wa chakula pamoja na kuwa na ziwa kubwa katika Bara la Afrika? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri sana Mwanza, ndio Kituo Kikuu cha Umwagiliaji cha Kanda ya Ziwa. Lakini kile kituo ukifika, utafikiri ni kwa mtu binafsi. Ofisi ziko duni, hawana miundombinu, watendaji wako wazuri waliosomea na Mkurugenzi wa Umwagiliaji wa Wizara ni Msomi, Injinjina, kwa nini tunakuwa wategemezi? Kwa nini kilimo hiki cha umwagiliaji kisiwezeshe, kiweze kuwezesha nchi yetu kujikomboa katika hili? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu Kanda ya Ziwa, tumekuwa na vilio vya mazao. Tumekuwa na kilio cha zao la pamba, tumekuwa na kilio cha samaki, sasa watu wanalia alizeti nayo inachakachuliwa, bei haitaki kuwekwa wazi, ili watu waweze kuuza mazao yao. Lakini mimi ni Katibu wa Wabunge wa Majimbo yanayolima pamba, tumekuwa na majadiliano mafuru, tumejadiliana na Waziri, tumejadiliana na Waziri Mkuu, tumejadiliana na Mheshimiwa Rais, lakini bei hajjaweza kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mjumbe mmoja aliyezungumza hapa muda mchache uliopita alisema, korosho iliwekewa *guarantee*, wakulima wakalipwa vizuri; kwa nini, pamba isiongezewe na Serikali hiyo pesa ndogo, wakulima wakapata 1,000/= kwa kilo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wetu wa mahesabu wameshakokotoa, wameonesha ilivyo gharama kubwa kuzalisha zao la pamba, kuna tatizo gani? Naona hapa Serikali, inachezea moto. Watu 16,000,000 kuwafanya wawe wategemezi ni hatari kubwa sana. Ni muhimu sana kwa usalama wa Taifa letu, ni muhimu sana kwa ustawi wa wananchi wanaolima zao la pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali, ikafikirie tena licha ya majadiliano tuliyoyafanya, watafute kila namna bei iweze kufikia 1,000/=, ili tuondokane na matatizo. Haya ni matatizo ya mwaka huu, lakini nashukuru kwamba, Serikali, imekubali kuboresha viwanda vya nyuzi kwa maana ya kuweka *zero rating* katika kodi; hilo ni jambo jema, lakini bado mapato hayo au matokeo ya maamuzi hayo, hayajawafikia wakulima kwa wakati huu. Ni muhimu tu, tuwasaidie bei ifike 1,000/. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo lingine katika zao la pamba, hili dude hili, Bodi ya Pamba, ambayo ina wajibu wa kusimamia, imepigwiwa kelele sana na Wabunge wengi kwa sababu ya utendaji wake wa kazi. Lakini tatizo pale sio Bodi, tatizo ni Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba, watu wanazungukazunguka kusema ukweli, tatizo ni Mkurugenzi. Huyu amekuwa ni *Dictator* wa ajabu, sijui amepewa Mamlaka ya kiasi gani? Hata Mwenyekiti wa Bodi, ndugu yetu

hana Limbu, tutamhukumu, tunamsulubu bure, Mkurugenzi hawesi kuguswa hata na Bodi yenye; huyu mtu Mkurugenzi huyu amekuwa na Mamlaka ya ajabu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa anatoa maamuzi, ameweka *conditions* nyingi sana hata kwa wanunuzi. Sasa hivi bei iko chini, lakini bado amewawekeea *conditions* nyingi sana wanunuzi wa pamba ili washindwe kuingia kwenye soko. Anaanza kuteuwa wanunuzi wachache tu, anataka makampuni 10 tu ya matajiri wakubwa, wale Watanzania wengine wadogo wadogo wasiweze kunyanyuka, huyu ni mtu wa aina gani huyu? Rais, amefanya kazi kubwa sana kwenda kutafuta wawekezaji wa kusaidia zao la pamba, lakini huyu, Mkurugenzi amekuwa *Dictator* wa hali ya hatari, anaua zao la pamba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza kuwahamasisha vile vile kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi haya, wananchi wetu, tuanze kulima mazao mbadala. Nahamasisha Busega, tuanze kulima zao la alizeti ili tuepukane na matatizo ya bei inayobadilika kila wakati. Nashukuru, kwamba, Wizara, Watendaji, waliahidi kwamba, watasaidia pembejeo katika mbegu za alizeti. Naomba watekeleze hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lakini nashukuru vile vile nimepata wadau wa maendeleo, *MSK Group of Companies*, ambao wana nia ya kuwekeza katika zao la alizeti. Wameahidi kuja kutoa mafunzo kwa Madiwani, kutoa mafunzo kwa Watendaji wa Kata na Vijiji ili waweze kusaidia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana makundi ya wakulima ambayo yameshajitokeza kuwa makundi ya mfano wa kilimo cha alizeti, wawe tayari wataalam hawa watakapokuja. Vile vile nishukuru kwamba, Mkuu wetu wa Wilaya, ambaye ni kijana mpya mchapakazi, Mzindakaya, yuko mbele sana katika kusaidia zao hili la alizeti. Naomba tuendelee kushirikiana vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la pembejeo. Matumizi ya pembejeo katika nchi hii bado yako chini. Lakini kinachoumiza zaidi ni kwamba, hata mbolea ambayo tunaizalisha sisi wenye; hapa nchini, hatuitumii. Imesikitisha sana, Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, walipotembelea Minjingu, wamekuta mbolea imerundikana kiwandani, ma-godown yamejaa, wafanyakazi wamesimamishwa kazi, kiwanda hakiwezi kusambaza mbolea hii. Tatizo ni kwa sababu kuna mbolea kutoka nje inayoingizwa, inapewa ruzuku, wakati mbolea ya nchi yetu imesimama, imerundikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sisi Watanzania, kwa akili ya kawaida ni watu wa aina gani? Tunakaribisha Rais, Mawaziri, wanazunguka nchi za nje kukaribisha wawekezaji, watu wamekuja wamewekeza, halafu tunawashindanisha na watu wa nje; hivi tunakwenda wapi? Tunajimaliza wenye; Kuna nini hapa katika hii mbolea inayotoka nje? Mheshimiwa Waziri, hebu aangalie Watendaji wake, kuna nini hapo? Ajira zilizosimama sasa, hawa watu wanaishije na familia zao? Mbolea hii imeshapimwa, wataalam wa Kilimo walishaipima na kuona kwamba, inafaa. Kwa nini sasa haitumiki? Uhujumu huu! Tunaomba sana Serikali, iliangalie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kuna watu wanaitwa *Pass*. Hawa *Pass* ni akinanani? Hili dude *Pass* ni nini? Hawa *Pass*, wanakwamisha mikopo ya matrektu na zana za kilimo kwa wananchi wetu. Huyu *Pass* amewekwa na nani? Wananchi wangu wameunda vikundi vizuri kabisa nya Ushirika nya *SACCOS*, vimeombia kwa miaka miwili, naomba liangalie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli, orodha ni ndefu sana, lakini na umuhimu wa hii Wizara, sote tunaufahamu. Naomba tumalizie kwa wachangiaji wawili wa mwisho, Mheshimiwa Kilufi na Mheshimiwa Salum Baruan, watufungie uchangiaji wetu.

Mheshimiwa Kilufi!

MHE. MODESTUS D. KILIFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, kwa niaba ya wananchi wa Mbarali naomba nichangie hii Wizara muhimu ambayo inatoa ajira kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Wizara hii haionyeshi kabisa kwamba, Serikali ina dhamira ya kuendeleza Kilimo Kwanza kama ambavyo imekuwa ikitamkwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuweka bajeti ya shilingi bilioni 67 kutoka shilingi bilioni mia moja na zaidi kipindi kilichopita ni kuonesha ni jinsi gani ambavyo Wizara hii tunaizungumza kwa maneno kuliko kwa vitendo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina uhakika kabisa kwamba kama kilimo kingezingatiwa, vijana wetu wengi ambao wapo mitaani wangeweza kupata ajira. Niliiwahi kutoa mapendekezo Bungeni kwamba hivi kuna ubaya gani kama Serikali ingeanzisha *centres* za kilimo tukaweka wataalam wetu wanaomaliza vyuo vikuu, wakasimamia na miundombinu ikaboreshwa ili vijana wetu wakapata ajira hata kwa kukopeshwa kwamba utorialipa baada ya mavuno, wapewe ardhi iliyoandalika ili vijana wetu waweze kupata ajira lakini nalo bado naona halijazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea tena kusisitiza kwamba, kuwepo na *centres* za kilimo ambazo patakuwepo na wataalam, kutakuwepo na vifaa vya kilimo vinavyoweza kumudu kulima eneo kubwa ili vijana wetu wanaozurura ambao tunasema wanazurura wanahangaika basi waelekezwe kwenda huko wakapewe ardhi ili waweze kulima na ili Taifa liweze kupata tija kutockana na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, nirudi Mbarali. Mbarali tuna eneo la hekta milioni 1,600,000 kwa Wilaya nzima lakini tuna eneo linalofaa kwa kilimo la hekta 77,076. Lakini eneo ambalo linalimwa kwa sasa hivi ni hekta 37 tu ina maana bado tuna eneo lingine kubwa ambalo linafaa kwa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana Serikali kwa kuiweka Wilaya ya Mbarali kuwa Wilaya ya mfano kwa kilimo cha umwagiliaji. Wilaya ya Mbarali ina *scheme* 30 zilizoboreshwa kushirikiana na Serikali na vile vile tuna *scheme* 50 ambazo wananchi wanahangaika wanahitaji msaada wa Serikali ili ziweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kwa sababu gani? Katika mwaka huu wa fedha tumeomba fedha kwa ajili ya *scheme* ya Mbuyuni shilingi milioni 445,600,000 na tumeomba shilingi milioni 390 kwa *scheme* ya Gwiri, tumeomba shilingi milioni 800 kwa *scheme* ya Igomero, tumeomba shilingi milioni 787 kwa *scheme* ya Ruanyo kwa maana ya ujenzi wa bwawa la Ruanyo ambalo tunaamini likikamilika litatoa ajira nyingi kwa Watanzania watakaotumia maji hayo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tumeomba shilingi milioni 469 kwa ajili ya *scheme* ya Madibira, tumeomba pia shilingi milioni 775 kwa ajili ya *scheme* ya Majengo, tumeomba shilingi milioni 579 kwa ajili ya *scheme* ya Mashara, tumeomba pia shilingi milioni 768 kwa ajili ya *scheme* ya Mpungammoja, tumeomba shilingi milioni 763 kwa ajili ya *scheme* ya Mwendamititu, tumeomba shilingi milioni 391 kwa ajili ya *scheme* ya Njalalila na shilingi milioni 117 kwa ajili ya *scheme* ya Uturo. Jumla ya fedha ambazo tumeomba ni bilioni sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbarali tuna uwezo wa kulisha mchele kwa maana ya mpunga kwa asilimia kubwa katika nchi hii na bahati nzuri sana ardhi ya Mbarali inatoa Mpunga ambao una ladha yaani Mchele wake una ladha. Nilikuwa naongea na baadhi ya wafanyakishara na ndugu zangu Wabunge hapa, wengi wamekuwa wakinuliza kwamba mchele wa Mbarali vipi? Nadhani lije lori moja zima ili Waheshimiwa Wabunge muweze kuona mchele wa Mbarali jinsi ambavyo unanoga, unatoa harufu nzuri kabla hata hujaanza kuupika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naamini kabisa ndugu zangu mtuunge mkono watu wa Mbarali ili *schemes* ziweze kupewa fedha ambazo tunazionbea, tukipata fedha hizi nina uhakika Mbarali Tanzania tutapata mchele ambao ni bora. Ardhi ile imebarikiwa kwani iko chini

ya Bonde la Ufa, mbegu ile ile kalime eneo lingine, mchele wake ni tofauti. Kwa hiyo, naomba mwendelee kuwaunga mkono wananchi wa Mbarali ili tuweze kuendeleza kilimo hiki ili Watanzania wengi wanufaikie na kilimo hiki cha umwagiliaji.

Ndugu zangu wale ambao hamjaona kilimo cha umwagiliaji, naomba mje Mbarali muone, tuna vinu vingi vinavyokoboa mpunga karibu kila siku Semi 15 zinasafirisha mchele kwenda Dar es Salaam na maeneo mbalimbali ya nchi hii na wafanyabiashara wengi hasa ndugu zangu wa Pemba na Zanzibar wapo Mbarali wamejaa wanafanya biashara ya mchele. Kwa hiyo, Ndugu zangu nawaomba fedha hizi ambazo tumeomba tupewe ili tuweze kuendeleza kilimo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa Mbarali hawana amani sawasawa, hawana amani sawasawa baada ya mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha *National Park* na wakulima wa Mbarali. Eneo lile ambalo wananchi walihamishwa walishalipwa haki zao wakaondoka, sasa ukatokea mkanganyiko hapa katikati kwamba kuna eneo lingine tena linachukuliwa. Lakini namshukuru Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye kampeni alitamka kwamba hakutakuwa na ongezeko lingine tena la Kijiji wala Kitongoji, wananchi wakafurahi!

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikaa na Kamati ya Maliasili na Utalii yaani *TANAPA* Taifa au Maliasili kwa ujumla. Katika kutatua migogoro tulikubaliana, naomba hili lizingatiwe. Tulikubaliana kwamba kuondoa mgogoro wa Mbarali na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ananisikiliza, tulikubaliana kwamba, itumike ramani ile ya kwanza ambayo haina mgogoro na wananchi wa Mbarali, hili lilishapitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninachoshangaa, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu alipoleta Tume yake kuangalia ni wapi wananchi walikuwa wanataka na ni wapi Serikali ilitaka kuchukua, lile jambo likaeleweka. Tume ile tumezungumza nayo vizuri, lakini ninachoshangaa sasa ni kwamba kuna wanasiwa wamejitokeza wanakwenda kule wanawaambia wananchi tuishtaki Serikali, wanasema tuishtaki Serikali kwa sababu inanyang'anya ardhi ya wakulima.

Sasa Mheshimiwa Waziri, niliomba kwa maandishi kwamba naomba Serikali ikaainishe ile mipaka ili tuondoe ugomvi na wananchi, kwa makubaliano ya kutumia ramani ile ya kwanza ambayo haina mgogoro na wananchi kama tulivyokubaliana. Sasa hii Serikali imenigeuka lini tena? Mpaka kuna watu wamejitokeza sasa hivi ninavyozungumza wamefungua kesi Mahakamani ili kuishtaki Serikali eti kwa sababu inanyang'anya ardhi ya wakulima.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba hili lipate majibu ili wananchi waache kuhangaika kuichukia Serikali yao bila sababu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa Kapunga iliyokuwa *NAFCO* wana mgogoro na mwekezaji. Mgogoro ule upo wazi na si jambo la kukawiza kwenda kutatua ule mgogoro, lakini mpaka leo ninavyozungumza ule mgogoro bado haujamalizika na wale wananchi wanapiga kelele sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ya pale ya mwekezaji iliyokuwa *NAFCO* ni hekta 5500 inafahamika na ardhi ya wananchi ambayo ni makazi yao ni hekta 1070 inafahamika, ardhi ya *small holder* ni hekta 800 inafahamika, kigugumizi kipo wapi? Kwa nini jambo hili lisimalizike, wananchi wakakaa kwa amani? Kwa hiyo, naomba kama ni Wizara ya Ardhi basi ifanye haraka, kwani tatizo tulilonalo sisi ni kutokutatua migogoro haraka mpaka wananchi wanafika mahali wanashindwa kutuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili lifanyiwe haraka ili mgogoro umalizike kwani wananchi wale vile wile wana kesi ya kuchomewa mazao yao, kesi ile iko Mahakamani sivezi kuizungumzia lakini kuna kitu kinachokwamisha ushahidi kutoka Wizara ya Kilimo, hajapeleka. Sasa wale wananchi wanahangaika, wanakwenda Mahakamani wanarudishwa, wanakwenda tena wanarudishwa. Kwa hili la ushahidi pia naomba mpeleke kile kinachotakiwa ili jambo hili liishe mara moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kilufi na nakushukuru sana!

Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Barwany.

MHE. SALUM KHALFAN BARWANY: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya mwisho ili kuchangia Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kutoa mkono wa rambirambi kwa tukio la msiba wa ndugu zetu amba wamepoteza maisha katika ajali ya meli Zanzibar. Tunawaombea kila la kheri Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi na wale amba wamepatwa na misiba kwa ndugu zao basi katika kipindi hiki kizito cha msiba awape moyo wa subira na imani tukiamini kwamba kila mmoja wetu atarejea huko ambako ametoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kuwatakia shufaa Watanzania wote amba wataingia katika mfungo huu wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Mwenyezi Mungu awajaalie funga yao iwe nyepesi na Mwenyezi Mungu awakubalie funga yao hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangia katika suala zima la Wizara ya Kilimo. Kwanza katika nchi zetu hizi za Kusini mwa Afrika yaani SADC tulikubaliana kwamba katika bajeti zetu katika nchi hizi kila nchi itenye angalau 10% ya bajeti yake kwa ajili ya bajeti ya kilimo. Makubaliano ambayo yamedumu zaidi ya miaka mitano sasa hivi tangu mkataba huu usainiwe na nchi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mpaka leo bado zoezi hili halijakamilika na zaidi ya kushuhudia tu kwamba kila mwaka bajeti yetu katika eneo la kilimo inazidi kushuka. Hii inasababisha hali ya kilimo kuwa duni kwa kiasi kikubwa kiasi kwamba bajeti zetu hazikidhi kabisa haja ya mahitaji ya kusonga mbele katika kilimo chetu, tukiamini kwamba zaidi ya 80% ya Watanzania wapo vijijini na wao wanashughulika na kilimo. Hii ni kuonesha dhahiri kabisa kwamba bado Serikali hajawa na nia thabiti ya kuonesha kwamba tunaondokana na kilimo duni ambacho wananchi wetu huko vijijini wanakumbana nacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, ningetaka Serikali itueleze pamoja na makubaliano yale ambayo tulikubaliana tukatia saini katika nchi zile ni tatizo lipi ambalo linashindwa kufikia 10% ya bajeti zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nizungumzie suala la ushuru wa vifaa vya kilimo. Wenzangu walotangulia wamezungumza hapa, ni kweli kwamba hali ya Watanzania amba wanahuksika na kilimo hasa ni maskini wa kutupwa huko vijijini na hawamudu gharama za vifaa vya kilimo, hivyo Serikali ingeona umuhimu wa kuhakikisha kwamba vifaa hivyo vinawafikia wananchi kwa gharama naafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikubaliana katika Bunge liliopita kwamba vifaa vya kilimo viondolewe ushuru wake ikiwa ni pamoja na matairi, lakini tunashuhudia mpaka leo bado TRA wanaendelea kutoza ushuru katika vifaa hivyo. Hivyo, nia ambayo Serikali inayo inaonesha inasuasua kwa kiasi kikubwa, hivyo inatutia mashaka. Ni kweli kuna dhamira ya kweli ya kuendeleza kilimo katika nchi yetu au tunapiga blaablaa tu za kisiasa siku ziweze kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la mbolea ambalo Wabunge wengi pia wamelizungumza. Tunaagiza mbolea kwa gharama kubwa na mabilioni ya pesa, pesa zetu za kigeni katika nchi zinatumika katika kuagiza mbolea kutoka nchi za nje. Hii inatuathiri kwa kiasi kikubwa tukiangalia kwamba tuna mambo muhimu ya matumizi ya pesa hizi kwa ajili ya kuleta huduma nyingine katika nchi hii kama vile madawa katika hospitali ambayo sisi wenywewe hatuwezi kumudu kutengeneza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunaweza tukatengeneza Viwanda vya Mbolea katika nchi yetu na kupunguza gharama ya kuagiza mbolea kutoka nje. Leo tuna gesi ya kutosha kutoka

mikoa ya Kusini ambayo gesi ile tungeweza kuitumia kutengeneza Kiwanda cha Mbolea, lakini bado haioneshi mikakati imara ya kuhakikisha kwamba tunaweza tukatengeneza mbolea kupitia gesi ya kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo taarifa nilizonazo ni kwamba Serikali inatia saini mkataba wa uwekiwa wa bomba la gesi kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam na kutoka Songsongo Kilwa. Lakini niseme kitu kimoja tu ambacho kinanisikitisha, pamoja na kwamba mkataba huo ambao unatiwa saini tulisema mikataba ije Bungeni ili Wabunge tushuhudie, lakini hata bado Wabunge wa Mikoa ya Kusini hatuna taarifa juu ya jambo hili. Lakini si jambo bayaa pia taarifa tupate ili tunapochangia katika hoja hizi tuseme pia mahitaji ya gesi hiyo ni nini kama vile kujenga Kiwanda cha Mbolea katika Mikoa ya Kusini ili kiweze kuleta tija na kuongeza uzalishaji wa chakula katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala zima la mashamba ya mkonge. Suala la mashamba ya mkonge tumelizungumza muda mrefu sana, lakini bado mashamba mengi yametekelawa katika nchi hii hususani katika Mikoa ya Kusini. Lakini tumeambiwa na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kwamba kuliundwa *Taskforce* kutembelea katika mashamba na kutoa report. Kwa taarifa tulizonazo ni kwamba hiyo Tume imetumwa muda mrefu katika mikoa mbalimbali ambapo mkonge unalimwa na tunaambiwa mpaka sasa bado Tume hiyo haijakamilisha taarifa zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanahitaji mashamba hayo kwa ajili ya kilimo na pia ifahamike kwamba mashamba hayo yalichukuliwa wakati ule, ni maeneo ambayo yalikuwa katika rutuba nzuri, wawekezaji wa kikoloni waliyachukua mashamba hayo wakayadhibiti na wakawa wanayatumia kwa kilimo, bado tunakwenda katika mpango wa Kilimo Kwanza na wananchi bado hawana mashamba ya kutosha kwa ajili ya kilimo hicho.

Mheshimiwa Waziri tungemwomba aharakishe zoezi lake na atuletee taarifa Bungeni, hatua gani mpaka sasa Serikali imechukua kuhusiana na mashamba hayo ya mkonge ambayo tayari wananchi wanayasubiri? Tunafahamu kwamba ni utaratibu wa kisheria, lakini inafika mahali kwamba Serikali lazima pia iwe na maamuzi magumu na ihakikishe kwamba mashamba hayo yanarudi kwa wananchi ili waweze kuyatumia kwa ajili ya shughuli zao za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la umwagiliaji. Nchi nyngi sasa zimeshajitoa katika kilimo cha kutegemea mvua, nchi nyngi tu! Ni nchi chache kama Tanzania ambapo wananchi wake wanategemea kilimo cha kutegemea mvua. Kwa mujibu wa tabia za nchi hali ya mazingira ya nchi yetu imebadilika, Serikali sasa pamoja na kutuletea taarifa katika makabrasha na taarifa katika maandishi, inatakiwa zoezi rasmi lianz.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mito mingi, maziwa ya kutosha, maji yanatiririka katika bahari ya Hindi kila kukicha malita kwa malita ya maji yanapotea tu, basi Serikali ihakikishe kabisa sasa inakuja na mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba Watanzania sasa tunakwenda katika kilimo bora cha umwagiliaji ili wananchi wetu sasa waweze kuondokana na balaa hili la njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la ajira. Ajira zaidi ya 80% ya Watanzania sasa hivi wapo katika sekta ya kilimo na ndiko ajira inakopatikana. Kuna Mbunge mmoja amezungumza sasa hivi kwamba, suala la ajira siyo la Tanzania tu, lakini tunatofautiana katika viwango vya ajira katika nchi zetu. Leo huwezi kuchukua idadi ya watu wasiokuwa na kazi Marekani ukafananisha na idadi ya watu wasiokuwa na kazi katika Taifa letu, tunatofautiana! Leo Marekani unaweza kusema ni 2% ya Wamarekani ambao hawana kazi, lakini Tanzania ni asilimia ngapi ya Watanzania ambao hawana kazi?

MBUNGE FULANI: Si kweli!

MHE. SALUM K. BARWANY: Ni watu 120,000 tu ambao wameajiriwa katika sekta rasmi katika nchi hii na wakulima zaidi ya 80% wapo vijijini, bado kilimo chao ni duni...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Barwany namuona Mheshimiwa Waziri amesimama.

Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwa msemaji anayeendelea kuzungumza kwamba Marekani asilimia ya Waamerika ambao hawana kazi ni 8% na siyo 2% na kwa Waamerika tofauti na Tanzania mtu ambaye hana kazi ni kwamba hana kazi kabisa, lakini Tanzania mtu ambaye hana kazi yuko kwa Mjomba au kuna kazi nyingine ndogondogo anazofanya. Kwa hiyo, hiyo ndiyo tofauti.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa taarifa hiyo, Mheshimira Barwany unaipokea taarifa hiyo?

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Naibu Spika, naona wapiga kura wa Lindi wataamua kama taarifa hiyo ni rasmi au namna gani.

NAIBU SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Halima!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nilikuwa nampa taarifa nyingine kwamba Marekani wanapewa *Social Security Fund* na Serikali yao, yaani wanapewa fedha, lakini zaidi Tanzania tuna ukosefu wa ajira kwa 16% na katika 16% hiyo 60% ni vijana. Kwa hiyo, suala la ajira hapa kujadiliwa kwa mapana haliepukiki. Hiyo nilitaka nimpe taarifa juu ya taarifa na zama za kuishi kwa Wajomba zimepitwa na wakati, siku hizi kila mtu anabeba msalaba wake. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Barwany, endelea!

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Halima. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema sasa kama nchi tukajipanga kuhakikisha kwamba tunatengeneza ajira kwa wananchi wetu hususani wananchi ambao kwa vijijini wanategemea ajira ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, nasema siungi mkono hoja! (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Barwany.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Engeneer Chiza, Naibu Waziri, Mheshimiwa A. Malima, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuleta bajeti yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imekuwa na changamoto nyingi sana pamoja na kuwa Tanzania imeweka kipaumbele kwenye Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa sana ambayo wakulima wengi wanakuwa wakilalamika wakiwepo wakulima wa Mkoa wa Iringa hasa kuhusu ruzuku za mbolea na pembejeo kutofika kwa wakati hivyo kumkwamisha mkulima katika harakati zake za uzalishaji. Ni vizuri Serikali ingeshughulikia changamoto hii na kuona ni vipi tatizo hili linawezekutatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia kubwa sana ya wakulima wetu bado wanatumia jembe la mkono. Pamoja na kuwa Serikali imekuwa ikihimiza utuamiaji wa zana bora za kilimo kama matrekta na *powertiller*, tatizo kubwa ni masharti makubwa yaliyowekwa katika upatikanaji wa zana hizo. Pia sina uhakika kama Serikali imekuwa ikitoa elimu kwa watumiaji wa zana hizo jinsi ya kuzitunza na kuzifanya *service* wakati wa kuzitumia kwa sababu *powertiller* nyingi zimekuwa hazidumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri nyingi sana zina wataalam wa kilimo lakini wanakaa mijini badala ya kukaa vijijini au kwenda kutoa elimu mashambani ikiwa ni pamoja na

kuanzisha mashamba darasa ili wananchi (wakulima) waelimike zaidi kwa ajili ya kulima kilimo kilicho bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na miundombinu ya barabara zetu nchini kwetu kuwa mibovu inakwamisha wakulima wetu kusafirisha mazao kutoka mashambani kupeleka kwenye masoko mbalimbali. Pengeni sasa Serikali ingeangalia maeneo yale ya kiuchumi, zile barabara badala ya kumilikiwa na Halmashauri zipandishwe na kutunzwa na *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei za mazao (masoko), kutokana na utaratibu mbovu wa masoko, wakulima wanapata hasara kutokana na mazao yao kununuliwa kwa bei ndogo sana kwani gharama za uzalishaji ni kubwa sana kuliko bei wanazouza. Pia madalali wamekuwa wakiumiza sana wakulima kwa kulangua mazao yao na kuwarubuni kununua kwa bei ndogo na wao kupata faida kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyama vingi nya ushirika vimeshindwa kuwa na mikakati ya kumsaidia mkulima katika changmoto mbalimbali zinazomkabili ikiwepo ya upangaji wa bei za mazao na utafutaji wa masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sasa ingeweka mkakati mkubwa sana katika kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji ni muhimu sana kutokana na hali ya hewa kubadilika mara kwa mara. Pia miradi hii ingekuwa chini ya Wizara ya Kilimo kwa sababu Wizara ya TAMISEMI imekuwa ikitababisha miradi hii kusuasua hasa kutokana na kutokuwa na wataalam wa kutosha kwa mfano Halmashauri ya Iringa kuna miradi miwili ya *Mkoga Irrigation scheme* na *Kituiru Irrigation scheme*. Miradi hii imekuwa ni ya muda mrefu sana, haitengewi pesa mpaka kusababisha wananchi kukosa imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wakulima tungeomba ianzishwe mapema ili iweze kuwasaidia wakulima kulima kwa kilimo cha kisasa kwa kukopa mikopo katika benki hii na isiwe na masharti magumu pia itoze riba nafuu ili kuwasaidia wakulima wadogowadogo na wakubwa. Napenda Waziri atueleze maendeleo ya Benki hii mpaka sasa yamefikia wapi? Benki hii pia ingemsaidia mkulima kukopa zana za kilimo kama trekta na *powertiller*.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya wafugaji, Serikali iweke bayana mikakati itakayotumia kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji kugombea ardhi. Kumekuwa na migogoro mingi sana mpaka kusababisha umwagaji damu. Utafutwe ufumbuzi wa tatizo hili kwa mfano Iringa maeneo ya Idodi na Pawaga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inahitajika kuwa na mfuko rasmi wa kusaidia vyama nya ushirika kwa kuva vyama hivi havina mtaji hivyo kupelekea watu kushindwa kukopeshana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika baadhi ya Wilaya kumeanzishwa vyama nya mazao vyenye lengo la kununua mazao toka kwa wakulima ili kumsaidia mkulima kupata soko. Kwa kuwa malengo haya ya vyama hivi ni yenye kumsaidia mkulima, hata hivyo malengo haya hayafikiwi kwa kuva vyama havina mitaji, naishauri Serikali ivipatie mitaji vyama hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu zaidi haina budi kutolewa kwa wanachama na wananchi kwa ujumla ili kufahamu maana na faida za ushirika nchini. Serikali inahitajika kuongeza uwezo wa Maafisa Ushirika katika Wilaya nchini kwa kuwajengea uwezo na kuongeza fungu la matumizi ya kawaida (*OC*) ili wafanye kazi hizi kwa ufanisi. Pia ajira za Maafisa Utumishi hazina budi kuongezwa zaidi, hii ni sambamba na kutoa mafunzo kwa Wahasibu wa vyama nya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu wa awali na utendaji kazi wa sasa unaonesha umuhimu wa utengaji wa fedha kwenye Serikali za Mitaa mfano kutambua vipaumbele nya *DADP'S* kwa Wilaya tano zilizochaguliwa na zilifanikiwa kupata uchambuzi wa bajeti uliota gharama za moja kwa moja. Sehemu ya maendeleo na matumizi ya wazi huhusisha:-

- (a) Utekelezaji wa kilimo kama matrekta makubwa na madogo (*powertiller*).
- (b) Ruzuku za kilimo kama mbolea, mbegu, dawa za kilimo, chanjo, vyakula vya mifugo na kadhalika.
- (c) Malipo ya malazi nje ya kituo cha kazi, malipo ya muda wa kazi na malipo mengine ya wafanyakazi.
- (d) Nishati na madini.
- (e) Mahitaji ya ofisi na matumizi kama *computer* na kadhalika.
- (f) Mafuta ya dizeli, petrol na kadhalika.
- (g) Chakula na viburudisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba kiwango cha fedha hutumiwa kwa gharama ambazo si za moja kwa moja ambapo fedha za msaada zinazopelekwa kwenye maendeleo ya kilimo Wilayani hazitoshi kuleta mabadiliko kwenye sekta ya kilimo. Uchambuzi umeonyesha Mikoa yenye umasikini au ambayo ipo nyuma kimaendeleo hupokea bajeti asilimia 15.1 ya bajeti wakati Mikoa yenye umaskini hupata 44.3% na 40.4%, ingawa mgawanyo huo unaweza kuchochewa na umuhimu wa Mkoa husika na uwezo katika kilimo, lakini mgawanyo huo hauratibwi vizuri jambo ambalo huleta kutokuwepo kwa usawa mionganii mwa Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya kilimo bado haijaweza kufikia Azimio la Maputo la 2003 liliopendelekeza na Umoja wa Afrika ambalo liliopendelekeza kwamba asilimia 10 ya bajeti yote ya Taifa ilielekezwe kwenye kilimo. Naomba kutoa mapendelekezo yafuatayo:-

- (a) Mikoa iliyo nyuma kimaendeleo kupatiwa msaada kwa kiwango cha chini, inaanishiwa kwamba kama mipango haitawekwa wazi na kusimamiwa kwa umakini hakutakuwa na usawa na kuondoa umaskini hivyo Mikoa iliyo nyuma ipewe kipaumbele.
- (b) Kiwango cha uwekezaji kwa Tanzania hakitoshi kuleta mapinduzi ya kilimo kama ilivyopendelekeza na Azimio la Maputo (2003) la Umoja wa Afrika. Hivyo kiwango cha uwekezaji kilenge kuleta mapinduzi ya kilimo.
- (c) Serikali kupitia Benki ya Uwekezaji Tanzania (*TIB*) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo, iweke mfumo na taratibu ambazo zitahakikisha masharti ya dhamana hayawakwamishi wakulima wadogo kupata mikopo.
- (d) Ili kuongeza kasi ya kilimo, *LGA'S* zinapaswa kutenga kiasi kikubwa cha fedha kutoka kwenye vyanzo vyake ili kuchochea shughuli za kilimo.
- (e) Kuwepo na mfumo mmoja wa kuandaa bajeti na ufuatwe na Serikali zote za Mitaa ili kurahisisha ufuatilaji wa bajeti na taarifa za kina za mgawanyo wa bajeti kuanzia Serikali za Mitaa hadi Taifa ziwekwe wazi na zipatikane kwa wadau wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sekta ya kilimo itawekezwa ipasavyo, ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Sekta hii inaa jiri asilimia 77.5 ya Watanzania kwa kuchangia asilimia 4.2 tangu 2010 kutoka asilimia 3.2 ya mwaka uliotangulia, hivyo mchakato wa bajeti unatoa fursa muhimu ya kutathimini na kutoa ubora wa mipango ya kilimo kama inatekelezwa ipasavyo ili kufikia malengo yalikusudiwa.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Waziri na Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa hotuba nzuri ya bajeti. Napenda kupongeza kwa kutoa ushauri na maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Manyovu, Wilaya Mpya ya Buhigwe, tunayo mabonde mazuri ya kilimo cha umwagiliaji ambayo tunaiomba Wizara kuyatembelea na kufanya utafiti. Maeneo hayo ni Tarafa ya Muyama na Biharu hecta 700, Kilelema na Mugara hecta 800. Tunaiomba Wizara itusaidie tuzalishe mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Manyovu linalima vizuri zao la ndizi lakini ubora wa ndizi bado ni changamoto kubwa. Ombi letu ni kuiomba Wizara kuleta wataalamu ili kuelimisha wakulima wetu waweze kulima kisasa. Jimbo la Manyovu limepata masoko ya kimataifa yakatayojengwa na hivyo kuwa na umuhimu wa ndizi bora na kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pembejeo zinachelewa sana kufikia wakulima na ikiwezekana ruzuku izidi kuwekwa kwa kupunguza bei ya mbolea. Tunaishauri Wizara ijadili na wafadhili ili kulegeza masharti ya ufadhili huu ili mbolea ipatikane kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba wataalamu wa kilimo (wagani) wapangiwe kuja kufanya kazi Jimbo la Manyovu baada ya kupokea wagani watano tu katika Jimbo la Manyovu, Wilaya mpya ya Buhigwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya Mpya ya Buhigwe ipangiwe Afisa Kilimo mwenye taaluma inayoendana na mazao yanayolimwa Jimbo la Manyovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayoifanya.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara hii isirudie makosa ya mwaka jana ambapo Serikali ilizua wananchi kuuza mahindi nje ya nchi na hapohapo Serikali ikashindwa kununua hayo mahindi toka kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara inunue mahindi kwa wakulima wa Ludewa. Naomba wananchi wa Ludewa wapewe kipaumbele katika ununuzi huu wa mahindi.

MHE. ABDUL R. MTEKETA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kilimo katika Jimbo la Kilombero ni uti wa mgongo na kwa kuwa Mkoa wa Morogoro umeteuliwa kuwa moja ya ghala la Taifa nchini, napenda kusema kuwa nia ya Serikali isiwe ya maneno tu ila iwe ya vitendo. Nasema hivyo kwa sababu ugawaji wa pembejeo huchelewa sana na inapofikia hivyo pembejeo haleti ufanisi kamili. Je, Serikali ina mpango gani kutatua tatizo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya lloyo ya Sukari ya Kilombero sasa hivi imekabiliana na tatizo la kushindwa kupokea miwa ya *outgrowers*, inaonekana kuwa kiwanda ni kidogo. Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua kiwanda hicho ili kunusuru wakulima wa miwa wa nje wasipoteze kipato chao kwa sababu kampuni inashindwa kununua miwa ya wakulima hao?

MHE. MCH. DKT. GERTRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Kilimo Juu!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa hotuba nzuri yenye kukidhi. Pongezi kwa uhamasishaji na utekelezaji wa Kilimo Kwanza na usindikaji wa vyakula kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa utekelezaji wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima. Pongezi kwa udhibiti wa magonjwa ya mimea mbalimbali ili wakulima waweze kupata mavuno mengi. Pongezi kwa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga na kadhalika, kazi yenu ni njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mapendekezo yafuatayo:-

(i) Pamoja na jitihada na kazi nzuri, bajeti hiyo ni finyu mno kuweza kutekeleza azma ya Kilimo Kwanza.

(ii) Ucheleweshaji wa pembejeo unakosesha wakulima mavuno ya kutosha, inawakatisha tamaa.

(iii) Mfumo mbaya wa usambazaji wa mbolea.
(iv) Serikal ijenge viwanda vyta mbolea nchini.

(v) Mbegu bora zitumike nchini Tanzania sio za kutoka nje.

(vi) Mikopo iwfikie kwa wakati.

(vii) Migogoro kati ya wafugaji na wakulima. Serikali inapendelea wafugaji, hawachukuliwi hatua, wakulima tunapolalamika hatusikilizwi.

(viii) Migogoro kati ya wananchi na wawekezaji ni aibu, mikataba iwe na nguvu ya kumnyang'anya mwekezaji ardhi anaposhindwa kuiendeleza. Hiyo imeshawishi wananchi kuvamia ardhi isiyotumiwa na mwekezaji.

(ix) Serikai ilinde viwanda vyetu vyta sukari. Sukari isiponunuliwa hata wakulima wa nje wao wanaathirika kama Kilombero – Ilovo, wanalima 40% ya miwa na wakulima wadogo ni 60% ya miwa. Hivyo kama sukari hainunuliwi wananchi wanateseka, kama Mtibwa Sugar ni 50%, wakulima wa nje ni 50%. Hivyo ni dhahiri kiwanda kinawahitaji wakulima wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya kuendeleza kilimo hapa nchini. Pamoja na pongezi hizi, ninayo maoni na maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji – Manyoni. Ukurasa wa 19 wa bajeti umekiri kwamba kwa Mikoa na Wilaya kame (kama Singida na Manyoni) kilimo cha umwagiliaji ndilo jibu la kuondoa tatizo la njaa kila mwaka. Lakini bajeti hii haikuweka fedha za kutekeleza ujengaji wa skimu za umwagiliaji. Mwaka jana (2011/2012) skimu ya kijiji cha Chitalalo (Manyoni) ilifanyiwa upembuzi lakini fedha za kujengwa miundombinu hizikutengwa mwaka huu. Wizara itazame uwezekano wa skimu hii kuendelezwa kwa vile *design and soil test vilishafanyika*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa bwawa la Mbwasa la kilimo cha umwagiliaji. Eneo la Mbwasa lina bonde lilzungukwa na miinuko (*gorge*), kinachotakiwa ni kuziba mto tu ili kupata bwawa. Wataalam wa Wilaya na wa Bonde la Kati wametembelea eneo hili na kupitisha kwamba ni *site* nzuri kwa bwawa kubwa litakaloweza kutoa maji mengi ya kutosha kumwagilia mbuga yote ya Tarafa ya Kintinku hadi Bonde la Bahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko wa Tanzania/Japani *Food Counterfund* wameleta shilingi 200 milioni kuchangia mradi huu lakini wanasema zitumike katika ujenzi halisi na sio kwa upembuzi. Nilifika Wizarani kuongea na Mheshimiwa Waziri Chiza na pia niliandikia Wizara kuomba Serikai iweke fedha kwa ajili ya mradi huu amba ni mkubwa na gherama ni kubwa kiasi kwamba Halmashauri ya Wilaya haiwezi. Naomba Wizara iangalie namna ya kusaidia mradi huu uanze 2012/2013 hata kwa kugharamia upembuzi yakinifu na tathmini ya kimazingira, vinginevyo hata ule msaada wa mfuko wa chakula wa Tanzania/Japan wataondoa msaada wao kwani miaka miwili imepita, fedha hizo haianza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kupongeza Wizara hii kwa kazi nzuri na naunga mkono hoja hii.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba asilimia kubwa ya watu nchini ni wale walioko vijijini. Uchumi wetu umeripotiwa kupanda lakini maisha ya Watanzania walio wengi yaani walioko vijijini yanazidi kudidimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wengi nchini ni wakulima, ili Serikali iboreshe maisha yao, ni vema Serikali ikaangalia uwezekanao wa kuwawezesha na kuwadhamini ili wapate mikopo ya matrekt ya SUMAJKT. Wizara ya Kilimo ifanye makubaliano na SUMAJKT ili kila kijiji kikopeshwe trekta moja bila kuwataka kutoa malipo ya awali ya asilimia iliyowekwa. Endapo Serikali itawapa kila kijiji trekta moja wafanye utaratibu wa kila kijiji kulipia deni hilo baada ya kupata mavuno yao kila mwaka mpaka deni hilo limalizike.

Mheshimiwa Naibu Spika, sioni njia yoyote ya kuwaondoa kwenye umaskini Watanzania walio wengi ikizingatiwa kwamba wengi ni maskini na kipato chao hutegemea mazao yatokanayo na kilimo. Endapo Serikali itawasaidia wananchi kulima mashamba makubwa zaidi kwa kutumia trekta, hakika kutakuwa na ongezeko la chakula ambacho watatumia wenyewe na kuuza ziada ili wajipatie kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iweke *commitment* ili wananchi wawezeshwe kurahisisha shughuli za kilimo nchini zitakazowaletea maendeleo ya wananchi walio wengi. Hii ndiyo njia pekee ya kuleta maendeleo kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba hii kwa kuanza na kuishukuru Wizara ya Kilimo ambayo imekuwa ikiwakumbuka wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini kwa kutupatia fedha za kuendeleza miradi ya umwagiliaji iliyoko katika vijiji nya Rungwe Mpya na Titye. Naiomba Serikali hususani Wizara ya Kilimo iwapatie mikopo ya trekta na pembejeo ili waweze kuzalishsa chakula kwa wingi kitu ambacho kinaweza kusaidia chakula kwa mikoa ambayo haitakuwa na chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wakulima wa Jimbo langu ambao wamepakana na hifadhi na kwa kuzingatia kwamba hifadhi imezunguka Jimbo zima kwa kuanzia vijiji nya Makere, Kagerankanda, Mugombe, Zeze, Kigembe Kabhulanziwiri, Chekenya Kurugongo na kadhalika. Mheshimiwa Waziri atuhakikishie na kwamba yuko tayari kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ili kuweka mawazo ya pamoja ya kuhakikisha wakulima wa maeneo hayo hawasumbuliwi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali ifahamu Wilaya ya Kasulu ndio inayoongoza kwa kuzalisha mazao ya chakula, hivyo ni vyema wananchi wapewe fursa ya kuitumia ardhi ya kutosha kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nina imani kubwa na Wizara ya Kilimo, ninaamini tutawatetea Watanzania ili waondokana na umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kilimo cha kahawa, kwa sasa hivi katika Mkoa wa Kilimanjaro baada ya zao la kahawa kudorora, wakulima wengi baada ya kupata elimu ya kilimo cha kisasa, wamepata mwamko wa kulirudisha tena zao la kahawa. Lakini hapo nyuma wakulima wa kahawa walkuwa wakipata faida zao baada ya mauzo. Je, mtindo ule uliiishia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, *KNCU* ilifanya vizuri mpaka wakaweza kuwa na vitega uchumi, jambo la kusikitisha, uongozi uliopo wameanza kuuza mali za *KNCU* ambazo ni za wanachama kama nyumba bila ridhaa yao. Je, huu si ufisadi? Serikali inatoa tamko gani sababu mali hizi

zingekuwa ndio dhamana ya kukopa ili kuweza kuwa na kiwanda cha kisasa ili kuiongezea kahawa yetu *quality* na kuwaongezea wakulima faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la ndizi, zao hili ni kati ya mazao ambayo yanaweza kuliingizia Taifa fedha nyingi sana za kigeni lakini Serikali haijaweka umuhimu wa kutosha kwenye zao hili. Wakulima hawalimi kisasa, migomba huwa inapata magonjwa mara kwa mara. Zao hili lilitanikiwa sana kwa kutumia umwagiliaji wa asili, kutumia mifereji lakini kwa sababu ya ukame uliyoikumba Tanzania na dunia kwa ujumla, zao hili linakauka na kupotea. Je, Serikali kwa kupitia Wizara ya Maji na Kilimo, ipo tayari kushirkiana kuwepo na kilimo cha umwagiliaji Jimbo la Moshi Vijijini, kule Kibosho, Uru, Old Moshi Mashariki na Old Moshi Magharibi?

Mheshimiwa Naibu Spika, jimbo hilohilo la Moshi Vijijini, Kata ya Mabogini, Serikali ya Japan ilianzisha kilimo cha umwagiliaji, kilimo cha mpunga lakini tangu Wajapan waondoke kilimo kile kimesuasua. Je, Serikali ina mikakati gani ya kukiendeleza kilimo hicho cha mpunga? Badala ya kuanza sehemu mpya, tuimarishe sehemu zilizokuwa na kilimo cha umwagiliaji kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa mbegu bora, kama Taifa bado hapajakuwepo na msukumo wa kutosha kuzalisha mbegu zetu wenyewe hapa nchini kwa mfano mbegu kama za mahindi karibu zote zinatoka nje ya nchi ambazo zinakuwa ni za gharama kubwa sana na hii inapelekeea wafanyabiashara wa mbegu wasiokuwa waaminifu wanauza mbegu zisio na ubora. Kwa kuwa Jeshi la Magereza na la Kujenga Taifa wanazalisha mbegu lakini haizitoshelezi, Serikali iwayezeshe ili wazalishé mbegu za kutosha ili tuwezeshe upatikanaji wa mbegu hizi kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa benki ya kilimo, pamoja na Serikali kuonyesha nia nzuri ya kutenga fedha kwa ajili ya benki hii, sasa ni lini mchakato huu wa kuanzisha benki hii utaisha? Kama tujuavyo benki za kibashara zinatoza riba kubwa sana na kupelekeea wakulima kushindwa kukopa na kuishiwa kulima kilimo kisichokuwa na tija.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali, nampongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hotuba nzuri na uwasilishaji makini na kwa ufashaa. Pia nawapongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wa Wizara na watumishi wote kwa kuandaa hotuba nzuri yenye mwelekeo na matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa kusimamia kwa umakini na umahiri kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, pia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Kilimo (*ASDP*), umeendelea kuwa na mafanikio. Uingizaji wa matrekti mengi kupitia SUMA JKT, ni mradi mzuri wenyе taswira ya kuboresha kilimo. Uingizaji wa matrekti nchini mwanzo haukuratibiwa vyema kwa hivyo ikasababisha gharama kubwa ya ziada kupitia '*storage charges*' bandarini. Katika awamu zinazofuata, Wizara ilenge kudhibiti mianya mbalimbali ambayo inasababisha kuongeza gharama ya matrekti hayo kwa mnunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio mengi ya Kilimo Kwanza, katika Jimbo la Bagamoyo tuna changamoto nyingi, miradi yetu ni Chauru, *BIDP*, Kidogozero. Miradi yote hii haipati fedha za kutosha kujenga miundombinu ya umwagiliaji na kupanua eneo la kilimo. Mfano mwaka 2010/2011, Chauru ilitengewa shilingi 165 milioni lakini ikaishia kupelekewa shilingi 45 milioni tu! Kwa hali hii, kilimo kitaboreka vipi? Wizara ihakikishe kuwa miradi ya umwagiliaji nchini inapewa kipaumbele katika tengeo la bajeti na utoaji fedha katika mwaka mpya wa fedha 2012/2013. Wizara ihakikishe miradi ya umwagiliaji Bagamoyo inapata fedha zilizotengwa katika bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ABAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza kwa hotuba nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoo wa Dar es Salaam ulipatiwa mahindi kwa kupunguza ukali wa bei. Ni tani ngapi zilizotolewa katika Mkoo wa Dar es Salaam. Ni kampuni ngapi zilipewa mahindi hayo na kampuni zipi majina yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pamoja na pongezi hizi, ninayo machache ya kuchangia ili kuboresha hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Tayari Bunge letu lilishatunga Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko lakini mimi binafsi sijaona shughuli za bodi hii zikifanyika. Je, bodi hii imeshaundwa au bado? Kama imeundwa, je, kanuni zipo tayari na kama zipo tayari mbona hatuzioni zikitumika hasa kwa kuanza kununua mazao kwa vipimo halisi na kuachana na mazoea ya kununua na kuuza mazao ya wakulima kwa kutumia debe, gunia, ndoo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu umekuwa ni chanzo kikubwa cha kuwanyonya wakulima wetu wanyonge na kuwaneemesha wanunuuzi na hasa wanunuuzi wa kati (*middlemen*) mfano debe moja la maharage mazuri aina ya soya kutoka Karagwe yananunuliwa kati ya shilingi elfu tano na elfu kumi (Tshs.5000/= na 10,000/=) kwa debe moja au ndoo moja ambayo ina kilo karibu ishirini au kumi na tano na bei ya kilo moja ya maharage ni kati ya shilingi elfu mbili na elfu tatu. Unyonyaji huu ni sharti ukomeshwe kwa kuhakikisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko inafanya kazi yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mnyauko wa migomba limeukumba Mkoa wa Kagera ikiwemo Wilaya ya Karagwe. Serikali imekuwa ikieleza kuwa hakuna dawa ya kutibu ugonjwa huu. Je, hali hii itaendelea hivihivi hadi lini? Tunaiomba Serikali ijipange vizuri kuhusu tatizo hili moja kwa moja. Serikali ifanye tafiti mbalimbali na kujifunza nchi nyininge zimedhibiti kiasi gani ugonjwa huu mfano nchini Uganda na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vocha za mbolea, utaratibu unaotumika kusambaza mbolea kwa wakulima unawanufaisha wasambazaji tu na siyo wakulima kwani wakulima wanasainishwa vocha bila kupata mbolea na wakipewa, hawapewi kiwango husika. Serikali itafute njia sahihi ya usambazaji wa mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, soko la mazao mbalimbali, kwa kuwa nchi yetu imejaliwa ardhi nzuri, kubwa na yenyen rutuba na kwa kuwa wananchi wanazalisha chakula cha kutosha na kupata ziada mfano ni mahindi Rukwa, Ruvuma na Iringa, pia ndizi Wilaya ya Karagwe. Ni vema Serikali ikajipanga na kutafuta masoko ya mazao yetu nje ya nchi ili kilimo killiingizie Taifa fedha za kigeni na kuwanufaisha wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na ushirika lakini bado kuna malalamiko mengi toka kwa wakulima kuhusu ushirika kununua mazao yao kwa bei ndogo wakati bei ya soko la dunia liko juu. Mfano halisi ni bei ya kahawa inayotolewa na Vyama vya Ushirika vya KDCU (Karagwe) na KCU (Bukoba). Serikali iingilie katil hili illi kumnusuru mkulima wa Kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Karagwe tunapanga kuanzisha kilimo cha alizeti katika mwaka wa fedha 2012/2013. Kwa kuwa alizeti ni zao jipy kwa wananchi wa Karagwe, hivyo tunaomba Serikali itupatie mbegu bora za alizeti, elimu, wataalam wazuri na mashine za kukamulia alizeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

(a) Kwa nini Serikali hainunui mahindi mfano mwaka 2011/2012 haikununua mahindi ya Ludewa na kuwakopa wakulima?

(b) Kwa nini nchini hakuna Kiwanda cha Jembe la Mkono?

(c) Wizara ina mpango gani wa kufanya kilimo kiwe *mechanisation*, kutumia matrekta. Je, Ludewa na Makete wana matrekta mangapi Wilaya nzima?

(d) Kilimo cha umwagiliaji Serikali imefikia hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam haina shida ya njaa bali tatizo kubwa ni *inflation*. Rais wetu alitoa mahindi takribani tani 10,000 lakini hatujui mahindi haya yapo wapi na yameleta *impact* gani Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie bajeti ya Wizara hii kwa kutoa ushauri na kuomba ufanuzi wa Serikali katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ucheleweshaji na ubadhirifu katika utoaji wa pembejeo. Katika Jimbo la Mvomero, kuna tatizo la ucheleweshaji, uchache wa vocha na ubadhirifu wa pembejeo. Katika mwaka 2011/2013, pembejeo zinachelewa sana kuwafikia wakulima na pamoja na kucheleva pembejeo hizo kiasi kikubwa hazikuwafikia wakulima mpaka misimu wa kilimo ukaisha bila wakulima kupata pembejeo. Nashauri Serikali ifikishe pembejeo mapema kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ikumbukwe misimu ya kilimo katika Jimbo langu imetofautiana mathalani Tarafa ya Mgeta kilimo huanza Octoba na Novemba. Ni vema pembejeo zikapelekwa Septemba na upande wa Tarafa za Turiani, Mvomero na Mlali zikawakilishwa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa utoaji vocha umejaa ubadhirifu kwa mawakala wasio waaminifu kuwasainisha vocha wakulima na kutowapa pembejeo na wakati mwingine mawakala kutoa mbegu mbovu. Nashauri Serikali iboreshe mfumo wa utoaji pembejeo ili kumsaidia mkulima badala ya watu wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kiwanda cha Mtibwa Sugar, ni mnunuzi mkubwa wa miwa kutoka wakulima wa nje. Nimepiga kelele sana hapa Bungeni, nashukuru kwa sasa wakulima wanalipwa malipo haraka lakini maombi katika kiwanda hiki ni kuongeza bei ya miwa kwa wakulima, bado bei ni ndogo ukilinganisha na bei ya kiwanda cha Kilombero. Aidha, Serikali isaidie kusaidia *SACCOS* za wakulima wa miwa wapate fedha na wakulima wapate mikopo yenyeye riba nafuu. Kiwanda cha Mtibwa Kiangalie upya ajira ya wiki tatu si nzuri, warejeshe ajira ya msimu ya miezi sita badala ya uliopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, skimu za umwagiliaji. Niliwahi kuomba mapema hapa Bungeni kuhusu kutumia mabonde na mito iliyopo Mvomero katika kuboresha skimu za umwagiliaji katika kijiji cha Lukenge, Mkindo, Dakawa na bonde Mgongola. Nashukuru Serikali kwa kusikia ushauri wangu na mwaka 2011/2012, Serikali ilitenga fedha kijiji cha Mkenge hekta 1000 za umwagiliaji na Mkindo. Aidha, bajeti ya mwaka huu 2012/2013 skimu za umwagiliaji za Dakawa (hekta 3000) na Mgongola hekta 660 zitakazoghamariwa na *USAID*, nashauri kasi ya utekelezaji wa skimu hizi ziende kwa kasi. Naishukuru Serikali kwa skimu za Mkenge na Mkindo kuendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, uwezeshaji wa *SACCOS* kupata mikopo na matrekta. Naomba Serikali isaidie kuikopesha *SACCOS* ya Mkindo, imeshatimiza vigezo vyote lakini wamefuartilia *TIB* bado wanazungushwa, zipo *SACCOS* nyingi natolea mfano hiyo ambayo pamoja na kukidhi vigezo bado hawapatiwi mikopo. Naomba pamoja na kuziombea fedha *SACCOS* ya Mkindo, *TURISACCOS* na zingine Jimboni, ni vema Serikali ikatoa maelekezo ni jinsi gani *SACCOS* zinaweza kupata mikopo ya matrekta yanayokopeshwa na SUMAJKT. Endapo vikundi vya uzalishaji mali na *SACCOS* vitapata nyenzo kama trekta, vitamsaidia kumkomboa mkulima na pia nchi kuwa na chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. ZAKIA H. MEGHJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja ya Waziri na nampongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na viongozi mbalimbali wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote tumesema kilimo ndio uti wa mgongo wa nchi hii. Jambo hili ni sahihi lakini tunajuliza, je, utekelezaji wake ni sahihi? Tumekuwa na program mbalimbali katika sekta hii ikiwemo ya hivi karibuni ya *ASDP* na *SAGCOT*, tumekuwa na program nyingi zikizungumzia mambo hayohayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu kuweka bajeti kubwa kwenye miundombinu ya umwagiliaji. Hivi sasa asilimia ya umwagiliaji ni ndogo sana. Ijapokuwa hata *ASDP* ambayo ilianza miaka kadhaa iliyopita kwa mkopo wa Benki Kuu bado haikuweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kujitosheleza kwa chakula ni muhimu. Kuna usemi unasema '*a hungry man is an angry man*' huwezi kuwa na amani kama watu wana njaa. Kutegemea mvua haiwezi kutufikisha popote kwa sababu hakuna uhakika wa kupata mvua. Hivi sasa kuna uharibifu mkubwa wa mazingira na ndio unaotufanya tusiwe na mvua ya uhakika na mara nyine kuwa na mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, chakula na upatikanaji wake una uhusiano mkubwa na mfumuko wa bei. Asilimia kubwa ya mfumuko wa bei unatokana na chakula, pale ambapo chakula kinakuwa kidogo, bei inakuwa kubwa na kwa kuwa chakula ni kitu lazima kukipata, hali ya maisha inakuwa ngumu, ndio maana ni muhimu sasa tukaweka '*effort*' yetu katika kupanua na kuongeza maeneo ya umwagiliaji. Ni vizuri bajeti ya mwakani ikaonekana kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoagiza vitu kutoka nje, tunatumia fedha za kigeni. Pale ambapo tunaagiza chakula kutoka nje, chakula ambacho tuna maeneo na mabonde makubwa ya kuweza kuzalisha na pia pale ambapo tunaagiza vitu kama *juice* kutoka nchi za nje wakati hapa nchini tuna matunda mengi sana, ni kama hatuna mpango mkakati katika usindikaji wa matunda kama machungwa, nyanya na kadhalika. Huu ni wimbo wa siku zote kuwa tutafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kuwa na *link* kati ya kilimo na viwanda, hatutaweza kuongeza thamani katika mazao yetu na kwa hiyo kupata fedha zaidi na kuuza nje ya nchi. Kuna mpango kati ya Tanzania wa kushirikisha wawekezaji katika uzalishaji mkubwa kwenye mabonde yetu. Jambo hili ni zuri lakini tuwe na uhakika kuwa tunafaidika na jambo hili, wakati huohuo tunawaendeleza wakulima wadogowadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *biofuel* linazungumzwa duniani kote hivi sasa na upande wa Tanzania kuna wawekezaji katika baadhi ya maeneo ambapo walianza kupanda mazao kama *jetrofa* kwa ajili ya *biofuel*. Hivi sasa hakuna Sheria ya Uzalishaji wa *Biofuel* hapa Tanzania, ni muhimu kuwa uzalishaji wa aina hii ukasitishwa mpaka Sheria ya *Biofuel* ikaletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampongeza sana Waziri kwa hotuba nzuri na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa hapa ni suala la soko la mazao yetu kuanzia soko la mahindi, viazi kwenye Jimbo langu wananchi wanajitahidi kulima lakini soko linaukritimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeajiri Maafisa Ugani wengi lakini wanalima mashamba yao tu na hawajihusishi na kuwasaidia wananchi. Mimi nalima hekari 400 Wilayani kwangu kwa zaidi ya miaka 10 sijawahi kumuona Afisa Kilimo kutembelea shamba langu licha ya kila mwaka kijiji cha Mtungu chote kuongoza kwa uzalishaji wa mahindi katika Kata hiyo na sehemu kubwa ni kutoka shamba langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna usimamizi wa mbegu bora kulingana na eneo. Mbegu za mahindi, alizeti na mtama, mara za kutoka Kenya, mara wapi, sasa wananchi hawana msaada. Mwaka jana nimeuziwa mbegu za alizeti aina ya *Record* pale Makambako haikuota kabisa. Sasa hii ni hasara kubwa kwa wakulima, kwa nini mbegu zinazouzwa hazikaguliwi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji ni kizuri lakini kiwe cha kisasa zaidi ili kulinda rasilimali za maji. Watu wasilime kwenye vyanzo nya maji (vinyungu) na kilimo cha umwagiliaji kiwe cha matone badala ya kuelekeza mto mzima kwenye shamba kama yale ya Kapinga na Mbarali mpaka tunakosa maji ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunahitaji bajeti kubwa Wizara hii lakini viwepo vipaumbele:-

- (a) Kuzalisha chakula cha kutosha ili kupunguza mfumuko wa bei *Drip Irrigation*.
- (b) Kuzalisha mazao ya biashara ili kulingizia Taifa fedha za kigeni (pamba, kahawa, chai na kadhalika).
- (c) Kuzalisha mbegu bora ili wakulima walime kilimo chenye tija, suala la mbegu lisimamiwe vizuri.

MHE. ANGELAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri inayofanya pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kushauri Wizara iupitie upya mfumo unaotumika katika kusambaza mbolea na pembejeo pamoja na vocha za mbolea na pembejeo kwani wananchi wengine wamekuwa wakipewa vocha hizo wakati hawastahili lakini pia kuna watu ambaeo wamekuwa wakipatiwa vocha hizo na kuziwa tena kinyume cha utaratibu na mpango mzima. Hivyo basi ni vyema sasa utengenezwe mfumo wa *ki-electronic* utakaowezesha kufahamu nani amepata vocha na nani hajapata lakini pia itakapoingia kwenye milki ya mtu mwengine ili kuondoa kabisa ubadhirifu wa vocha hizo na pembejeo na mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kuligusia ni bodi mbalimbali za mazao. Ni muhimu sana uwakilishi katika bodi hizi uangaliwe kwa umakini mkubwa, wako wengine wanafanya biashara za mazao ambapo wao ni wawakilishi katika bodi hizo. Itakuwa vigumu sana mtu wa aina hii kuisimamia vyema bodi kwa sababu atakuwa na *conflict* kuhusiana na biashara zake, suala hili liangaliwe kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni suala zima la Kilimo Kwanza, wananchi wanaona tu program za Kilimo Kwanza na *SAGCOT* na hawaoni ni kwa nini Mikoa minginge kama Kilimanjaro, Mtwara, Lindi haimo katika *SAGCOT*? Ni nani anayekagua mradi wa *SAGCOT*? Ushiriki wa Serikali katika utendaji na uongozi wa *SAGCOT* ukoje? Ni nani anayekagua utendaji kazi wa *SAGCOT* na hesabu zake za mapato na matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu pia kuwafafanulia wananchi namna mtu anayetaka kujishughulisha na kilimo cha miwa kwa ajili ya uzalishaji wa sukari anatakiwa kufanya nini ili aweze kupata ardhi ya kilimo katika Mikoa iliyoainishwa katika mapango 2011 - 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya kuhamasisha na kutoa huduma muhimu za uzalishaji wa mazao muhimu kwa chakula na biashara kwa kuhakikisha kuwa:-

- (a) Ardhi inatengwa mahsusni katika kila eneo na Wilaya kwa uzalishaji wa mazao husika kwa chakula na biashara.

(b) Kuhamasisha na kuunda vikosi vya wananchi vya kuzalisha mazao haya katika makundi yanayojulikana na kutambulika rasmi katika maeneo haya.

(c) Kuwagawia ardhi hiyo kwa mmoja mmoja au vikundi huku makundi ya wanawake, vijana na wenyewe kuathirika na hali ya ulemavu, UKIMWI na matatizo mengine ya kijamii watengewe ardhi, fedha na mafunzo katika mkakati mahsusii.

(d) Kutoa mafunzo ya uzalishaji tangu kutayarisha mashamba hadi kuvuna na usindikaji.

(e) Kuwapatia pembejeo za kilimo na ufugaji, kuwapatia zana za uzalishaji kama matrekta na zana zingine husika kwa mikopo yenyewe masharti nafuu.

(f) Kuwawezesha kupata usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli zao kutoka kwa Maafisa Ugani muda wote wa uzalishaji.

(g) Kuwasaidia kupata taarifa za soko hususani bei, mahali kwenye uhitaji mkubwa wa mazao husika (*demand*) na kuwasaidia kuyafikia masoko hayo.

(h) Kuwasaidia wakulima, wafugaji wa nyama, samaki na nyuki kuanzisha viwanda vya usindikaji wa mazao hususani yale yanayoharibika kwa urahisi ili kuyaongezea thamani na kurefusha uhai wa matumizi yake kwa ajili ya biashara na matumizi ya baadaye.

(i) Kuwasaidia wakulima na wafugaji na wasindikaji kuanzisha vyama vya ushirika ili kuepuka kuza mazao yao kwa bei ndogo wakati wa uvunaji kwa sababu ya shida ya pesa ya kujikumu.

(j) Kuwasaidia kupata mafunzo ya ubora na viwango vya mazao ya biashara na biashara ya ukanda wa kimataifa kwa kufahamu viwango vinavyohitajika kukidhi soko la nje.

(k) Kufanya kazi kwa karibu na Wizara nyingine za Serikali kama Viwanda na Biashara, Maliasili na Utalii, Maji na Umwagiliaji, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Ardhi na Tume ya Mipango kwa kujenga *synergies* kwenye shughuli zinazoshabihiana.

(l) Kuboresha mafunzo ya ujasiriamali kwa wazalishaji wote wa sekta hii muhimu.

(m) Napenda kutoa angalizo juu ya kukimbilia masuala ya *GMO* kabla ya kuzingatia athari zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa Wizara hii ikishirikiana na Wizara tajwa hapa juu itaratibu vyema shughuli za uundwaji na usimamizi wa vikundi vya wazalishaji nchi nzima, mafunzo, usindikaji na masoko ya mazao katika kuhakikisha ukuaji wa tija, mali na ajira kwa wazalishaji hawa ambao ni zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wa Tanzania kufikia lengo la milenia ambalo litawezesha kufikiwa kwa malengo mengine yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

MHE. SLYVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo na chakula ndio msingi mkuu wa nchi yoyote, bila kilimo hamna chakula na hatimaye hamna uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunasema kuwa kilimo ni uti wa mgongo, ni mwajiri mkubwa wa Watanzania na hakika ni kweli lakini bado Serikali haijawa makini na kujali kama maneno haya yalivyo au yasemayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi leo kwa kiasi kikubwa bado Tanzania tunategemea kilimo cha mtu mmoja mmoja tena kwa ajili ya chakula na ziada kidogo. Mazao ya biashara nayo yanategemea mkulima mdogomdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ndicho pekee kitaweza kuchochaea uchumi wa nchi yetu kwa kasi kubwa na kiasi kikubwa tutapata chakula, hamna njaa, tutapata fedha za kigeni kusaidia kuondoa nakisi ya mlingano wa manunuzi na mauzo kwa fedha za kigeni (*balance of payment*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kufikia hayo ni lazima sasa tujikite katika kilimo cha kisasa lakini cha kibiashara (*commercial farming*). Pamoja na Kilimo Kwanza lakini wanaowezeshwa wengi wao hawana uwezo wa kutumia *tractors* hizi kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda umefika sasa wa kuhakikisha kilimo chetu hakitegemei mvua tu, tuna mito, maziwa ya kutosha, Serikali iwekeze kwenye miundombinu ya kilimo (umwagiliaji) kama tunavyowekeza kwenye barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itambue maeneo maalum ya kilimo, aina za mazao yanayostawi, imiliki maeneo haya na sasa iyatowe kwa wafanyabiashara wakubwa wa kilimo wenye uwezo wa kuwekeza vifaa vya kisasa vya ukulima (*Afromechanization*) kama matrektu makubwa ya kulima, kupanda na kuvunia. Kuwepo na masharti ya kusindika mazao yetu na kuyaongezea thamani. Tukifanya hivi sasa, mkulima mmoja anaweza hata kulisha Mikoa zaidi ya mmoja lakini pia kuzalisha ziada ya kuuza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutajenga miundombinu ya umwagiliaji kwa maeneo ya kilimo na tukachochaea usindikaji. Hii sasa itachochea wananchi wakulima wadogowadogo kulima na kuwauzia wakubwa na wasindikaji jambo ambalo kwanza litaleta soko zuri kwa wakulima hawa wadogo lakini kukuza ubora na thamani ya mazao yenye na kupata soko la dunia kirahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tukubali sasa kilimo cha kikabaila maana ulimwengu mzima sasa uchumi ni wa kibepari. Tukisukuma mbele *commercial farming*, Serikali itakuwa imezika njaa, imeboresha upatikanaji wa fedha za kigeni kwa mauzo ya mali iliyoindikwa itapunguza kuua bidhaa zilizotoka kwetu kama malighafi na kurudishwa kuuzwa kama mali zilizokamilika au za viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivi Serikali itaondokana na lawama za kila siku kuhusu pembejeo za kilimo maana wakulima watakuwa na uwezo na utaratibu wao wenye na kuandaa yote hayo Serikali itasimamia sera na kukusanya kodi na kutoa ruzuku kwa mujibu wa mahitaji ya kuchochaea kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Watanzania wengi na wakulima wamekataa tamaa na kilimo cha mvua na wengi hawalimi. Serikali iweke utaratibu kupitia Serikali za Mitaa na Vijiji kuhakikisha kuwa kila kaya inalima angalau chakula cha ziada ya kuuza. Hii itasaidia kwa hatua ya awali ya kupiga vita njaa na kuhakikisha uwepo wa chakula. Tanzania ni soko la kijamii na kapu la kijani (*green basket*) kwa Afrika Mashariki kama tukitekeleza haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuteuliwa tena na Mheshimiwa Rais kuwa Mawaziri na hususani kwenye Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Aidha, nimpongeze kipekee Mheshimiwa Chiza kwa kupanda cheo na kuwa Waziri kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kupitia kwa Wizara hii kwa kutenga shilingi 1.5 bilioni kwa ajili ya kununua ndege ya kunyonyuzia dawa ili kukabiliana na milipuko ya visumbufu vya mimea. Mkoaa wa Singida umekuwa ukisumbuliwa sana na *quelea quelea*, hatua hii ya kupata *aeroplane* ya kunyonyuzia ni mwafaka sana kuokoa mazao yanayostahimili ukame

kama vile mtama na uwete ili kukazia maagizo ya Serikali ya wananchi kulima mazao yanayostahimili ukame kama hatua ya kukabiliana na majanga ya njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ije na mpango kabambe wa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika Mikoa yenye upungufu wa mvua kama vile Singida, Dodoma na Shinyanga kulikosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale ambapo wananchi wameitikia vema wito wa Serikali wa kulima mazao yanayostahimili ukame lakini bado mazao yakaharibika na *quelea quelelea*, wanyamapori na hata ukame zaidi, Serikali ije na utaratibu wa fidia ya gharama halisi iliyotumika kuyalima na gharama halisi ya mazao yenye yaliyoharibiwa kwa ekari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha tumbaku mwaka huu kimesumbua sana wakulima wa Kata za Mgandu, Mitundu, Mwamagembe na Rungwa. Bei ilishuka ghafla wakati wakulima wanajiaanda kuuzo zao hili na kuzusha mgogoro baina ya wakulima na vyama nya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kutokana na tatizo hili, wakulima wengi walikopeshwa pembejeo waliambulia patupu baada ya kukatwa. Naiomba Serikali ifuatilie suala hili Manyoni na kwenye vyama nya msingi kuna ukubwa wa tatizo lenyewe na jinsi ya kuwafidia wakulima ambao wameachwa hawana kitu katika msimu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali badala ya kuruhusu kuuzo mahindi nje ya nchi kama nchi jirani za Kenya, Malawi na kadhalika uwekwe utaratibu wa kusaga mahindi na kuuzo unga badala ya mahindi ili kuongeza thamani ya zao hili na mengine ya nafaka na kuzalisha ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ije na mpango kabambe wa kuanzisha *scheme* kubwa za kilimo cha alizeti na zabibu ambazo zitaendeshwa na wakulima wadogo nchini chini ya usimamizi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo utaratibu wa kuwapima Maafisa Ugani kwa kila moja kuonyesha idadi ya wakulima alio wahudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. MANSOOR S. HIRAN: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba kuchangia hotuba ya Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichangie kuhusu pembejeo na zana za kilimo. Naomba kushauri Serikali pamoja na kupunguza bei za *tractor* wapunguze bei za majembe, *planters* na *harrow* ili mkulima apate nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni upimaji wa ardhi vijijini, nashauri Serikali ijipange kama mpango wa maji vijijini wa kila mwaka vijiji kumi vinapata maji basi na upimaji uende hivyo hivyo ili wananchi wapate hati miliki ili kuwasaidia kupata mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ni pamba, naishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, kitengo cha soko kutafuta soko la pamba kabla hajaanza kuchumwa na mwananchi ajue bei ambayo atapata kabla hajaanza kulima. Hotuba hii inasema mkulima anakula hasara ya shilingi $800-660=140/=$, hiyo hasara naomba Serikali kuwafidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne ni Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, nashauri Serikali iongeze *budget* ya mfuko huu kutoka shilingi bilioni 3.4 kufikia shilingi bilioni 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Benki ya Ardhi, nashauri Serikali kutenga maeneo ya ardhi kila Wilaya kwa ajili ya vijana ambao hawana ajira na pia hao vijana wapewa mtaji, wapewe msaada wa kuwatunza kwa mwaka wa kwanza mpaka hapo wakishaanza kuzalisha mazao yao basi unawaacha wanajitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, matrekta ya SUMA JKT. Haya matrekta nashauri yasambazwe kwenye Halmashauri ili yawe karibu na wakulima na pia yauzwe kwa mkopo wa asilimia 80%.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba ni mbolea. Naomba Serikali iendelee kuongeza idadi ya wakulima wanaopata ruzuku kwani itasaidia katika kuongeza tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, mbegu bora. Naishauri Serikali iongeze ufuatiliaji wa mbegu ndani ya nchi yetu kuliko kutegemea mbegu za kuagiza nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa ni kuhusu Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu. Naomba kushauri Serikali ifunge mkataba na kiwanda hicho na iagize kuwa mbolea yote inayozalishwa na kiwanda hicho inunuliwe na Wizara. Sasa hivi hiki kiwanda kimeacha uzalishaji kwa sababu hawana soko. Naishauri Serikali ithamini viwanda vya ndani na pia itafute mwekezaji awekeze kwenye kiwanda cha mbolea kwa sababu gesi asili tunayotele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi ni dawa. Naishauri Serikali iongeze bajeti na dawa zifike kwa muda mwafaka kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono bajeti ya Wizara ya Kilimo.

MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongezeni kwa hotuba nzuri pamoja na mipango mliyoiweka kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao. Katika Ibara ya 94 ya hotuba kuna taarifa ya udhibiti wa ndege aina ya kwelea kwelea kulikofanywa na Wizara katika maeneo kadha ikiwemo na Wilaya yetu ya Chamwino katika Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa Mheshimiwa Waziri hali halisi ilijojitokeza kwenye Wilaya yetu ya Chamwino ambayo imeathirika sana na uharibifu uliofanywa na ndege hao wa kwelea kwelea. Mwezi Februari na Machi, 2012 kulijitokeza makundi ya ndege waharibifu aina ya kwelea kwelea walivamia vijiji vya Chalinze, Wilunze, Majeleko na Chinangali vilivyo Tarafa ya Chilonwa. Pia Tarafa za Makang'wa, Mpwayungu katika Wilaya ya Chamwino vilivamiwa na ndege hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kusikitisha ni kuwa licha ya Wilaya na Kanda kutoa taarifa mapema na kukamilisha maandishi yote, Wizara ya Kilimo ilichelewa kutuma ndege ya kuwapulizia ndege hao waharibifu. Ndege ya kupuliza dawa illitetwa miezi miwili tangu taarifa zilipowasilishwa ofisi ya Kanda ambapo tayari uharibifu ulishafanyika kiasi cha kupoteza chakula karibu chote na hivyo kuleta upungufu wa chakula katika Wilaya ya Chamwino.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya uzalishaji wa mazao iliyofanywa na timu ya wataalamu na kiwilaya inaonyesha kuwa Wilaya inakabililiwa na upungufu wa tani 9573 za chakula katika msimu wa 2012/2013. Upungufu huu wa chakula kwa kiasi kikubwa umetokana na uharibifu wa kwelea kwelea katika zao la mtama. Naomba Wizara ichukue tahadhari mapema ya upungufu wa chakula Wilaya ya Chamwino.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirika, napongeza jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Wizara katika kuimarisha ushirika chini ya program kabambe ya mageuzi na *modernization* ya ushirika nchini. Lakini nimeshtushwa sana na upotoshaji unaoendelea kufanywa n hata Idara ya Ushirika yenye kwa kujaribu kuonyesha kuwa kuna vyama vya ushirika na wakati huohuo kuna *SACCOS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi vyama vya ushirika ni ujumla wa vyama vya ushirika vya aina zote zikiwemo na hizo *SACCOS*. Aya ya 20, ukurasa wa 11 inaonyesha ongezeko la vyama vya ushirika kutoka 9397 hadi 9769. Idadi ya *SACCOS* pia iliongezeka kutoka 5251 hadi 5424.

Nashindwa kuelewa hapa kinachokusudiwa kuelezwu ni kipi? Je, kwa ujumla kuna vyama vya ushirika zaidi ya 15,000? Naomba Wizara inayosimamia maendeleo ya vyama vya ushirika isijiingize kwenye upotoshaji unaoendelea kujengeka mionganii mwa jamii ya kutaka kutofautisha *SACCOS* na vyama vya ushirika vya aina nyingine ambavyo vyote kimsingi ni vyama vya ushirika.

MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuweza kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu kwa siku ya leo. Napenda pia kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri wa Kilimo, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kupanga mipango mizuri ya kukiendeleza kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani kwa wahisani kwa michango yao ya hali na mali ya kuharakisha maendeleo ya kilimo nchini kwetu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kilimo hakuna uhai wa binadamu, kwa hiyo, ombi la bajeti ya 2013/2014 kilimo kipewe kipaumbele cha kwanza. Kilimo kinaajiri zaidi ya watu asilimia 75. Kwa hiyo, bila ya kilimo hakuna uhai, hakuna lolote lile mijini na vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iweke wazi ni mfumo upi wa kusambaza pembejeo kwa wakulima kwa wakati. Naelewa lakini ni vyema wale viongozi wanaosimamia mfumo huo (wa usambazaji/kwa wakulima kwa kuhakiki) waelewe mapema na waanze kufanya kazi vizuri kuitia kwenye vocha kwa vikundi na kadhalika. Tamko la wazi lieleweke ili ucheleweshaji wananchi (kuhusu pembejeo) uendelee vizuri. Uhamasishaji wa mawakala na hasa yule wa Minjingu (kuleta mbolea) kwa wakati maana huu ndio msimu wa matayarisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi maalum kwa mbegu za ruzuku na hasa alizeti na mtama kwa Mkoa wa Iringa litiliwe maanani. Wananchi wa Iringa watafurahi sana kwa kupatiwa hasa mbegu hizi kwa njia ya ruzuku. Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ni nzuri, naamini kuitia Wizara hii, wananchi hawa watapewa mbegu hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na Wizara nzima kuitia Kilimo Kwanza, viwanda vya usindikaji vipewe kipaumbele na kusaidiana na Mikoa kwa jambo hili. Mazao mengi ili yapate thamani zaidi ni vizuri yasindikwe. Halmashauri/Wilaya/Mikoa, kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali wamejitatihidi. Naamini Wizara wakiongeza juhudhi, maendeleo yataongezwa katika usindikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji, msukumo wa hali ya juu uendelee kama Wizara ya Kilimo iliyotaja kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Kufuatana na hali ya mabadiliko ya tabianchi, kilimo cha umwagiliaji ni muhimu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchunguzi wa udongo (*soil analysis*) kwa matumizi ya mbolea ni muhimu sana. Ni vyema kama hotuba ya Waziri iliyotaja kwa kuwa na mipango ya vijana na hasa wanaomaliza mafunzo ya kilimo, SUA, kujajiri baada ya kuhitimu. Fedha zaidi ziongezwe kwa utafiti ili kukuza kilimo na utafiti ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri yote yaliyoainishwa ni vyema yatekelezwe kwani ni mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ahakikishe miradi yote ya umwagiliaji inafanya kazi ikiwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu yake mfano miradi ya umwagiliaji Wilayani Rungwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ahakikishe anamaliza tatizo sugu na mgogoro kati ya wakulima wadogo wa chai wa *RSTGA* wakishirikiana na *WATCO* dhidi ya mkulima mkubwa mwenye mashamba yake Wilayani Rungwe kwani inavuruga uwezo wa uzalishaji wa zao hilo. Waziri ni mgeni katika Wizara hii, wananchi wa Rungwe wana imani naye atamaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya *GMO* si mazuri hata kidogo kwa nchi changa. Kifaya ni mbaya na uharibifu wa mazingira ni mkubwa, tunalia na ukame, hivyo tusikubali kuharibiwa mazingira kwa njia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ya Waziri.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania iepuke matumizi ya mbegu za *GMO* kwa kuwa hata walaji wa nchi hizohizo zinazotumia aina hiyo ya mbegu hawapendi vyakula vinavyotokana na mbegu hizo. Sasa kwa nini sisi tutumie mbegu hizo? Ka nini hatuwezi kuendelea na mbegu za asilia na tuisitezze matumizi ya mbolea na kanuni zingine za kilimo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isaidie wakulima kupata masoko ya mazao yao, hakika wanataabika sana hasa wanapopata mazao mengi kama ilivyotokea mwaka huu hasa mahindi.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika miradi ya kilimo cha umwagilaji mabonde ya Luiche na Mkuti yaongezwe. Mkuti umetajwa kwa hekta 100 tu. Hii haitasaidia ukizingatia uwezo wa Mkoa wa Kigoma katika kilimo. Bonde la Luiche liwe ni mradi maalum wa kilimo cha mpunga ili kutatua tatizo la ajira kwa vijana wa Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 72 na 73 umezungumzia ubinafsishaji, tafadhalii namwomba Waziri arejee maelekezo ya Bunge kuititia Kamati ya *POAC* kuhusu viwanda vya korosho, uamuzi wa Bunge ni kurejesha viwanda hivi. Hotuba inapingana na maelekezo ya Bunge, viwanda ambavyo haviendeshwi virejeshwe Serikalini mara moja, pia viwanda vya iliyokuwa *NMC* Arusha na Dodoma wapewe Bodi ya Mazao Mchanganyiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *commodity exchange* lipewe msukumo maalum. Jambo hili linazungumzwa sana bila hatua yoyote kuchukuliwa. Timu iende Ethiopia tujifunze. Rais amekwishaagiza kuhusu jambo hili, kwa nini tunasuasua? *Commodity Exchange Corporation* kama ilivyo *DSE* ianzishwe haraka ipate *CEO* na bodi ili tuwe na mtu wa kumuuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 77 umezungumzia *social premium*, napenda kujua chama cha RUMAKU kule Kigoma kimefaidika namna gani na fedha hizi? Fedha hizi pia Kigoma walizihitaji ili kusaidia kujenga maghala ya kiwanda cha Kanyou. Napenda kupata maelezo kuhusu Mkoa wa Kigoma na hasa wakulima wa kahawa wa Kanyou wamefaidika vipi na mpango wa *social premium*?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti Serikali ilizungumzia sana mabonde maalum kwa ajili ya sukari (miwa) na mpunga. Nimesoma hotuba nzima sijaona mahali popote ambapo miradi hii ya Kilombero na Malagarasi ikitajwa. Napenda kupata maelezo kuhusu miradi hii na inasimamiwa na Wizara gani kama haipo kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshtushwa sana kwa namna ambavyo hivi sasa Serikali inashiriki katika suala la *GMO*. *GMO* ni maafa kwa nchi masikini. *GMO* inasababisha *dependency* ambapo daima tutaendelea kuwa koloni la makampuni ya Mashariki kwani kila mwaka tutakuwa tunaagiza mbegu kutoka makampuni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona ushiriki mkubwa wa Monsanto kwenye miradi ya kilimo hapa nchini. Monsanto ina historia mbaya sana kote duniani na hasa kwenye nchi maskini. Napenda kufahamu kama Taifa linayo *GMO policy*. Mimi binafsi ninapinga kabisa *GMO*, sipingi maendeleo ya sayansi, nappinga kufanya nchi yetu kuwa tegemezi kwa mabeberu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Kapunga Farm*, Kamati ya *POAC* ilitoa maelekezo ya kushughulikiwa kwa suala la kijiji cha Kapunga kule Mbalali ambapo Serikali iliua kijiji na wananchi wake. Miaka mitatu sasa imepita tangu maelekezo haya yatolewe na suala hili bado halijapata ufumbuzi. Waziri alipokuwa anajibu swali hapa Bungeni aliahidi kufuatilia suala hili ili kutekelezwa,

hadi sasa jambo hili halijafanyika. Naomba maelezo ya Serikali kuhusu hatma ya kijiji cha Kapunga na haki ya wananchi kulima na kujipatia riziki yao na kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mazao Mchanganyiko, bodi ipewe fedha ili kununua mahindi na kuanza kusaga katika kinu cha Iringa. Jumla ya shilingi 10 bilioni zinatakiwa ili bodi ianze kazi mara moja. Maeneo mengine kama Mwanza bodi iingie ubia na Watanzania wengine kwa kuanzisha kampuni tanzu na kuendesha miradi mikubwa, bodi isiuze maeneo haya bali iingie ubia ili kupata uzoefu.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula. Msimu uliopita wa kilimo, Jimbo la Bukene na Wilaya nzima ya Nzega lilipata mvua ndogo sana na kupelekea kuwepo kwa mavuno madogo sana ya mahindi na mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifanya ziara Jimboni kwangu miezi miwili iliyopita, kwa kweli hali ya chakula inatisha, hakuna kabisa mavuno ya mahindi wala mavuno ya mpunga. Mimi mjumbe wa Kamati ya Maafa ya Wilaya ya Nzega, mwaka jana hali pia ilikuwa si nzuri na tulioomba Serikali itupatie msaada wa mahindi ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya mahindi kulingana na hali halisi ilivyokuwa yalikuwa ni tani 21000 lakini hadi leo hii ni tani 7000 tu ndiyo Wilaya ya Nzega imepokea. Hali hii inapelekea baadhi ya familia kula mlo mmoja tu kwa siku kwa kukosa kabisa mahindi ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyo katika vijiji vingi vya Jimbo la Bukene ni ukosefu wa mahindi ya chakula na wakati huohuo wananchi hawana fedha za kununulia mahindi yanayouzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu ni kwamba Wizara ijandae mapema kwa maana ya kuhakikisha mahindi ya msaada yanawafikia wahusika kwa muda husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Engineer Christoper Kajoro Chiza kuwa Waziri wa Kilimo, ni mtu mwadilifu, mtaalamu na mchapakazi. Wizara ya Kilimo sasa imempata Waziri makini na mahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi bado naamini kwamba kilimo ndio ukombozi wa Mtanzania wa kawaida. Kama tunataka kuondokana na umaskini, sharti tuwe *very serious* na kuboresha kilimo. Kilimo cha jembe la mkono hakitufikishi popote. Kama tunataka kufikia ile nchi ya ahadi, *a medium income country*, ifikapo mwaka 2025 lazima tufanye *mechanization* ya kilimo. Tutumie zana za kisasa mfano matrektu na tutumie mbegu bora na tusambaze mbolea nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iongezwe bajeti ili mipango ya ASDP na DASIP iweze kuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya maendeleo ya kilimo. Trekta za *powertiller* ulikuwa ni ufisadi mfupi, trekta hizo hazifai kabisa. Wizara inaombwa iwe makini sana katika uagizaji kutoka nje wa zana za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ngara inahitaji kusaidiwa sana na Wizara ya kilimo. Wilaya ya Ngara bado ni maskini sana, kipato cha mwana Ngara kwa mwaka ni shilingi 170,000/= wakati wastani wa kipato kitaifa ni shilingi 800,000/=. Ngara haina zao la biashara la kuaminika, baadhi ya wananchi wameanza kufufua zao la kahawa, wananchi hao wanahitaji kusaidiwa na Serikali ili zao la kahawa liweze kuimashwa. Ngara mpaka sasa haimo kwenye orodha ya Wilaya zinazopata ruzuku ya pembejeo. Nilishamwandikia barua Mheshimiwa Waziri kuiweka Ngara katika orodha ya Wilaya zinazopata ruzuku ya pembejeo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri Ngara iwekwe kwenye orodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara itusaidie kuweka miundombinu katika mabonde mazuri ya Ngara ili tuweze kulima mpunga katika kupambana na umaskini uliokithiri. Ngara inayo mabonde mazuri sana yanayofaa kulimwa mpunga na miwa. Nchi ya jirani ya Rwanda inalima vizuri mpunga katika mabonde yake na sasa Rwanda inaiuzia mchele DRC Congo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa kilimo ni muhimu sana, mfano utafiti wa mbegu bora na kadhalika. Wataalamu wa utafiti wa kilimo ni watu muhimu sana lakini maslahi yao ni madogo sana. Wanaishi mbali na miji yenye huduma nyingi za kijamii. Kwa hiyo, wanahitaji kumotishwa kutokana na mazingira magumu wanayoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *extension services* hazipo, Maafisa Ugavi hawatoshi na wale wachache waliopo wanakaa maofisini lakini pia hawana vyombo vyaya usafiri kuwafikia wakulima. Wakulima wengi hawana uelewa wa kanuni za kilimo bora na za kisasa, wanahitaji kupewa elimu hiyo na Maafisa Ugavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ngara hakuna mashamba darasa kwa sababu *extension officers* hawako makini. Naomba Wizara ya Kilimo ikishirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kuiwezesha Ngara kuuza mazao yake ya maharage, mahindri, ndizi na mihogo katika nchi za Burundi na Rwanda kwa kufungua mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya mpakani, namalizia kwa kukuomba Mheshimiwa Waziri uwafikirie wananchi wa Ngara ambao ni maskini kuwapunguzia tena bei ya matrektu.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni uti wa mgongo na tunaamini kuwa asilimia 80 ya wananchi Tanzania ajira yao kuu ni kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia kilimo, tunazungumzia sekta iliyoshikilia maisha na uhai wa Taifa. Serikali imesema Kilimo Kwanza lakini wakulima wetu wamekuwa wa kwanza kuhangaika na Serikali yao haitoi *support* ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima hasa wa vijiji wamekuwa na shida ya mbolea hasa mbolea za ruzuku, wamekuwa wakinunua kwa bei ya juu sana na mbolea kutolewa kwa upendeleo mkubwa. Kumekuwa na suala la wakulima kunyang'anywa maeneo ya kulima, mashamba na baadhi ya watu wenye pesa kwa vigezo vyaya kutaka kuwekeza na visingizio vingine vingi. Naiomba Serikali kuhakikisha inawalinda wakulima wadogowadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee uwezeshaji wa wakulima na hasa kwa upande wa vitendea kazi. Serikali ilisema wakulima watapatiwa mikopo kwa masharti nafuu lakini mpaka sasa wakulima waliosaidiwa ni wachache sana tena wanaofahamiana lakini makundi mengi ya vijana wanahangaika na hawajui mahali pa kuanzia na wengi bado wanalima *locally* bila vitendea kazi vyaya kisasa, wengi wanalima kwa jembe la mkono na jembe la kutumia ng'ombe (maksai). Naiomba Serikali ni wakati sasa wa kufanya mageuzi kwenye kilimo sio Kilimo Kwanza kwa maneno bali iwe Kilimo Kwanza kwa vitendo, wakulima wapewe mikopo ya *tractor* na malighafi zote zinazohitajika katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa chakula, Watanzania wengi wanaumia kwa kula vyakula vilivyo na madhara. Naiomba Serikali kuititia *TFDA* kuzunguka na kukagua katika maeneo yote yanayotoa huduma za vyakula kama huduma kwa wananchi hasa mchele, maziwa, unga, nyama na kadhalika. Vinapotumika kwa wananchi baada ya muda unasikia chakula fulani kinaleta madhara huku wananchi tayari wanakuwa wametumia, tunaomba ukaguzi wa nguvu ufanyike. Napenda kuuuliza Serikali, je, Serikali ina mikakati gani ya kulinda afya za Watanzania kwa kuzuia chakula kibovu kisiingizwe nchini kutoka nje? Naomba majibu Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kuzungumzia ushirika (vyama vyaya ushirika), ushirika wa kilimo umekuwa wa kwanza kuwadhulamu na kuwanyonya wakulima katika vyama kwa wenyeviti wa vyama vyaya ushirika kuhujumu vyama na vyama baadhi vikifa bila faida kwa

wakulima. Tunaomba Serikali kusimamia vyama hivyo kwa kuwapa semina viongozi wa vyama namna ya kuendesha vyama bila tama, uonevu na unyanyasaji wa vitisho kwa wakulima tena bila kuingiza ubaguzi wa kisiasa katika vyama nya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza uongozi wa Wizara chini ya Waziri Eng. C. Chiza, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu wake, Wakurugenzi wa Idara mbalimbali na kadhalika. Baada ya pongozi hizi, nina mchango kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napongeza mradi wa majoribio (*pilot phase*) ya kuwezesha vijana kujajirji katika kilimo huko Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa kuwapa vijana hao seti za mashine na mafunzo ya usindikaji mhogo. Nashauri uwezekano huo uanzie kwenye uzalishaji wa kitaalam wa zao husika mpaka usindikaji, vijana wamilikishwe ardhi kisheria, walime na baadaye kuongeza thamani mazao yao. Hata hivyo, mradi usiishie kwa *pilot phase* tu upanuliwe kwenye maeneo mengine kwa mazao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni madawa ya mazao, kwa vile mazao kadhaa ya chakula sasa hushambuliwa sana na wadudu waharibifu, Serikali iondoe ushuru/kodi katika madawa hayo ili yauzwe kwa bei ambazo wakulima wanaweza kumudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji katika eneo la uwekezaji kwamba Serikali iwawajibishe wawekezaji kujenga viwanda vitakavyosindika mazao watakayowekeza kuyalima na sio kuwashimiza tu, kwa kujenga viwanda ajira zitapatikana na nchi itaongeza fedha za kigeni kwa kuuza mazao yaliyosindikwa – kuongeza thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili faida hizi zifikiwe ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa wananchi wa maeneo husika wanashiriki katika kuainisha maeneo ya uwekezaji, mikataba inayosaini inaeleweka kwa wananchi na kadhalika. Hii itasaidia kuepusha migogoro inayojitokeza kati ya wananchi na wawekezaji sehemu mbalimbali nchini kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kumbukumbu zangu, Mkoa wa Morogoro ulipangiwa kuwa Ghala la Chakula nchini hasa kwa zao la mpunga kwa jina maarufu la mpango wa FAMOGATA. Lakini sasa nataka ufanuzi mpango huu ndiyo uko kwenye mpango mpya wa SAGCOT au ndani ya Kilimo Kwanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, desturi ya kutumia majina tofautitofauti kwa dhana moja inawachanganya sana wananchi kwa vile kabla dhana moja haijaaelewaka vizuri, Serikali inabuni dhana nyngine. Mwisho wa yote wananchi wanachoshwa na maneno matamu bila kuona utekelezaji wake hivyo kuendelea kutuhoji wawakilishi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Kamati ya Kudumu kwa maoni yake kwamba matumizi ya teknolojia ya *GMO* bado inawatia hofu wananchi walio wengi nchini. Inakuwaje wakati nchi zilizoendelea kwa masuala ya sasa wanahimiza wananchi wao kula vyakula visivyo na kemikali wakati wa kuzalishwa kwake wakati sisi wa nchi zinazoendelea tunahimiza kuendeleza hicho kilimo kinachotumia aina ya kemikali na teknolojia kama hiyo ya *GMO*? Nashauri Serikali itenje fedha za kutosha kwa taasisi zetu za utafiti wa mbegu bora zinazomudu mazingira ya nchi yetu kuliko kuua mbegu hizo za asili kwa kukimbilia matumizi ya teknolojia ambazo hatimaye tutakuja kujilaumu kama nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja ila nahitaji ufanuzi wa sababu za msingi za Serikali kuhimiza matumizi ya *GMO*.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Kilimo Kwanza na utekelezaji wake kwa bajeti finyu ya maendeleo. Kwa kuzingatia umuhimu wa kilimo nchini na kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa lolote lile na kwa kuwa bila shibe au chakula hakuna maisha/uhai. Ni kwa namna gani sera hii inaweza kutekelezwa kwa bajeti yake ya maendeleo kuendelea kupungua mwaka hadi mwaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya mwaka jana, fedha za maendeleo ziliikuwa ni shilingi bilioni 105.94 na mwaka huu ni shilingi bilioni 67.260 ikiwa ni pungufu ya shilingi bilioni 38.68 (57.5%). Je, kwa namna hii ni kwa jinsi gani kilimo cha kisasa kitawezwa na hii sera ya Kilimo Kwanza ifikie malengo yake? Nashauri Serikali iongeze fedha kwenye shughuli za maendeleo ili kauli mbiu ya Kilimo Kwanza iwe na mashiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama wa chakula nchini na bajeti tegemezi. Nikinukuu hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni juu ya utafiti uliofanywa na Gabagambu (2011) Tanzania kwa Mikoa kumi ya Tanzania Bara (Arusha, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mwanza, Mtwara, Shinyanga, Singida na Tabora) umeonesha kwamba Tanzania haizingatii hali ya usalama wa chakula katika mgawanyo wa bajeti ya kilimo na hivyo kufanya Mikoa hii kukosa usalama wa chakula. Naishauri Serikali kutoa mgao sawa wa fedha za DADPS ili kuitendea haki Mikoa yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni kwa nini Serikali haikutenga fedha za ndani za usalama wa chakula na badala yake inategemea fedha za wafadhili kwa ajili ya shughuli hii nyeti ya utunzaji na usalama wa chakula? Kwa kutegemea fedha za wahisani, tuna uhakika gani wa fedha hizi kufika kwa wakati na kutolewa zote iwapo kutatokea m dororo wa uchumi au janga lolote kwa wahisani wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mara zote utegemezi hauleti mafanikio hasa katika Taifa huru kama Tanzania. Taifa linaloishi kwa kuombaomba chakula si Taifa huru na tutambue kuna msemo wa Kiswahili unaosema "adui yako muombee njaa", njaa ina madhara makubwa sana na hata husababisha hata uvunjifu wa amani na vita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba ya korosho na viwanda vyake. Korosho ni zao ambalo lina faida kubwa sana kama likipewa kipaumbele cha pekee. Faida za korosho ni nyingi kuanzia mti, tunda lake, ganda la korosho na korosho yenyewe. Wakulima wa korosho wamekuwa wakipiga kelele mara kwa mara na hata kusababisha mapigano kama tulivyoshuhudia siku zilizopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wamekuwa wakuiza korosho yao kwa bei ndogo sana isiyokidhi mahitaji yao na adha wanayoipata katika shughuli za kilimo hicho. Kama haitoshi, viwanda vya korosho vilivyobinafsishwa ili kubangua korosho, vimebadilisha matumizi yake na kuacha kazi ya kubangua korosho na kuwa maghala ya kuhifadhiya korosho ghafi. Ni kwa nini tuendelee kusafirisha korosho ghafi wakati walionunua viwanda wamebadilisha matumizi yake na wameachwa bila kuchukuliwa hata stahiki za kisheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya teknolojia ya uhandisi jeni (*genetic engineering*) na madhara yake makubwa. Teknolojia hii ambayo huzalisha *GMO* katika kilimo, ni teknolojia ambayo haifai katika mazingira ya nchi yetu. Pamoja na faida chache zilizoorodheshwa, tunatambua pia madhara makubwa sana kwa afya ya binadamu na uoto wa asili na uchafushaji wa mazao na mimea mingine pamoja na viumbi vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunajua haya ni matatizo makubwa ambayo kwa nchi kama Tanzania ambayo ni tegemezi kwa kila kitu, ni kwa nini tunaendelea kuishabikia teknolojia hii? Hii teknolojia haifai na ni bora iachwe zifatutwe njia zingine za kuendeleza kilimo cha kisasa kwani Tanzania ina ardhi kubwa na mabonde yenye rutuba ya kutosha kulisha wananchi wake mwaka mzima na kuuza ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha alizeti Mkoani Singida na faida zake. Mkoani wa Singida umebarikiwa sana kuwa na ardhi inayoruhusu kilimo cha zao la alizeti kwa kiwango

kikubwa sana. Tatizo liliopo ni vitendea kazi vya kufanikisha jambo hili kama zana za kilimo, matrekta, pembejeo na kadhalika, ni vizuri sasa Serikali ione umuhimu wa kuwapatia wakulima wa alizeti mikopo nafuu ya matrekta ili waweze kulima kisasa zaidi na kuzalisha kwa wingi. Wote tunatambua umuhimu wa mafuta ya alizeti maana ni mafuta ambayo hayana kemikali za sumu zinazosababisha magonjwa sugu kama kisukari, kansa na moyo au "High/Low Blood Pressure. Ni vizuri kwa Serikali kutilia mkazo zao hili ambalo licha ya kuwaongeza wananchi kipato na ajira, zao hili pia linachangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. UMMY A. MWALIMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii. Ni matumaini yangu na ni matumaini ya Watanzania wengi kuwa wataiongoza vema Wizara hii muhimu kwa maisha ya Watanzania wengi hasa walio vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri, nasikitika kusema kuwa nimeshindwa kuona mipango/mikakati yoyote inayolenga kusaidia ushiriki wa wanawake katika sekta hii muhimu inayogusa maisha ya wanawake wengi hasa walio vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO*), *IFAD* na *FAO* zinaonyesa kuwa karibia asilimia 54 ya wanawake Afrika Kusini mwa Sahara wanajishugulisha na kilimo. Kilimo ndio shughuli kuu ya kiuchumi kwa wanawake kutokana na ukweli kuwa asilimia 81 ya wanawake wapo katika sekta ya kilimo ukilinganisha na wanaume asilimia 73 katika maeneo ya vijijini, asilimia 98 ya wanawake wapo katika sekta hii ya kilimo. Hapa nchini kwetu Tanzania wanawake wanaojishugulisha na kilimo ni asilimia 81; kubwa kuliko wastani wa asilimia 55 katika nchi nyingine Kusini mwa Sahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hizi zinatukumbusha kuwa tunapozungumzia kilimo tunazungumzia wanawake. Kilimo ni wanawake na wanawake ni kilimo, wanawake wengi hasa vijijini ndio wanaotoa mchango mkubwa sana kwa ajili ya kuzalisha mazao ya chakula hasa chakula kwa ajili ya watoto na familia nzima. Wanawake hawa wanakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo kukosa ardhii ya kulima, pembejeo, mafunzo kuhusu kilimo endelevu, zana za kisasa za kilimo na mikopo nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata maelezo kuhusu mikakati na mipango mahsusiliyowekwa na Wizara kwa 2012/2013 kuhusu kusaidia/kuboresha shughuli za kilimo kwa wanawake hasa walio vijijini. Juhudi zozote za kuboresha na kuendeleza kilimo hapa nchini hazitaleta matunda bora kama wanawake ambaao ni nguvu kazi kubwa katika kilimo wataachwa nyuma katika mipango/mikakati ya nchi ya kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. PHILIP G. MTURANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hili, ndio sekta pekee yenye au ilio na uwezekano mkubwa wa kuajiri watu wengi sana. Asilimia 75 ya Watanzania wanategemea kuendesha maisha yao kutokana na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifike mahali Wizara hii iheshimiwe sana kwa maana ndiyo inayoshikilia roho ya nchi. Bajeti iliyotengewa Wizara hii ni ndogo sana haitoshi hata kwa kuhudumia nusu ya mahitaji ya kilimo kwa wakulima. Bila kutilia maanani kilimo, ajira ambazo Serikali imekuwa ikitinjilishi nazo itakuwa ndoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaisihi Serikali isikilize kilio cha wakulima wa pamba, iweke au kupanga bei ya pamba inayokidhi mahitaji ili nao wakulima hao wajione ni sehemu ya Watanzania wanaofaidi matunda ya jasho lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiuliza Serikali, ni lini itaufanyia uchunguzi uongozi wa Bodii ya Pamba ili kuondoa utata uliopo vinginevyo bodi hiyo ivunjwe kabisa na kuundwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha kisasa ni muhimu sana ili kuleta mapinduzi ya kilimo. Vocha za mbolea zifike maeneo husika kwa wakati pia kilimo cha umwagiliaji kitiliwe maanani kwa kutengeneza miundombinu ya kisasa ili kuwa na uhakika wa kuwa na chakula cha kutosha na cha akiba mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi wanayofanya ya kutumikia Taifa letu. Naomba kutoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, wakulima wa zao la Korosho wapewe uwezo wa kukopeshwa mashine ndogondogo za kubangua korosho. Hili litawezekana kwa kuwapatia elimu ya kujunga katika ushirika wa vikundi vidogovidogo na kuwa rahisi kukopeshwa. Mashine hizi zinaweza kutengenezwa kwa wingi (maelfu) kwa kutumia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitivo cha Uhandisi, Nyumbu – Kibaha, SIDO na kadhalika na wajibu wa Serikali ni kutoa/kuweka dhamana ya kupata mashine hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya kununua mazao kama vile korosho, kahawa, karanga na kadhalika itolewe kwa wakulima kuhusu utaratibu wa stakabadhi ghalani. Ni utaratibu mzuri kama utapata ushirikiano mzuri kutoka pande zote zinazohusika yaani wazalishaji na wanunuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la zao la pamba lipatiwe kipaumbele kwa sasa kwani meza ya mazungumzo huwezesha kupata suluhu ya haraka. Kwa mfano, Serikali kuweka/kutoa dhamana ya ununuzi wa zao la pamba kuititia Benki Kuu, au usimamizi mzuri wa soko huria na hasa Serikali kulinda haki/maslahi ya mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji kionekane kinafanyika kwa vitendo zaidi na tija iweze kuonekana kwa muda mfupi usiozidi miaka mitatu ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalamu wa kilimo vijiji wahimize wakulima kulima mazao asilia na yanayohimili ukame kama vile mihogo, viazi vy'a aina zote, mtama, uwele na kadhalika. Mazao yanayoendana na mila, desturi na utamaduni pia yapewe kipaumbele.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikichangia kwa maneno nilitamka kwamba siungi mkono hoja, nilitoa sababu ambazo ni pamoja na bei ya pamba na kero ya wakulima wa tumbaku Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande kero za zao la tumbaku, tatizo la *accessors* ni kubwa, wanadai hongo ya waziwazi. Ninaomba mtumishi mmoja anayeitwa Ngonyani, huyu amekuwa ni kero aondoshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia sielewi ni kwa nini Serikali ina-*subsidise* mbolea ya nje wakati hapa nchini tuna kiwanda cha Minjingu? Naomba majibu wakati Waziri akihitimisha hoja yake.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali/JKT iwakopeshe Halmashauri zote nchini zenye maeneo ya kilimo hayo matrekti ili wananchi walimiwe na hatimaye Halmashauri itarudisha huo mkopo JKT/Wizarani. Ahsante.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hotuba yake nzuri, nimpongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam K. Malima, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa utendaji mzuri katika Wizara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Kigoma vipo vyanzo vingi vya maji, ziwa, mito mikubwa ya Malagalasi, Ruchwe na mingine mingi midogo midogo. Hivyo ninaomba Serikali, ijielekeze katika Mkoa wa Kigoma kuweza kuweka miundombinu kwa kutumia fursa hiyo tuweze kuanzisha kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kigoma tunamshukuru Mheshimiwa Waziri C. Chiza kwa juhud zake za kuuhangainia Mkoa wetu hata miradi ya umwagiliaji iliyopo ni kwa ajili ya juhud zake, ikiwa ni pamoja na kuanzisha kilimo cha umwagiliaji cha mpunga, kahawa na sasa amehamasisha kilimo cha alizeti na wananchi wameitikia. Hivyo sasa naomba Serikali iandae utaratibu ili mbegu ya alizeti iweze kuwfikia wakulima kwa urahisi zaidi Mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba utaratibu wa ugawaji mbolea kwa njia ya vocha ubadilishwe, maana katika eneo hili wanaonufaika ni wafanyabiashara siyo wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia 100%.

MHE. RACHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika nikijikita katika mambo muhimu kadhaa ambayo nimeyaona na ningependa kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujikita katika uzalishaji wa zao la pamba na soko lake hivi sasa. Ni ukweli usiopingika wakulima wa zao la pamba ambao wengi wanatoka Kanda ya Ziwa wanategemea zao hili ili kukuza uchumi wao. Wakulima hawa wa pamba wamekuwa wakisomesha watoto wao, kununua chakula, kujenga nyumba kwa kutegemea zao la pamba. Hii leo wakulima hawa wanajuta kuendelea kulima pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu 2012, wakulima hawa wamelima pamba kwa wingi hasa Serikali ilipoleta kilimo cha mkataba, kilimo hiki kimefanya hata waliokuwa wanalima pamba kuingia katika mkumbo huo matokeo yake pamba iliyonunuliwa mwaka huu imepita yaani imezidi kiwango. Kilimo cha mkataba kimekuwa ni suluhisho kwa wakulima hawa wa pamba. Wamelima pamba nyingi sana wakitegemea bei ya pamba itakuwa nzuri lakini imekuwa ni kinyume chake. Sasa hivi wakulima hawa wanaiangalia pamba yao majumbani sababu bei ya Sh.660 iliyopangwa na wanunuzi inawatia hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima wa pamba kwa ekari moja inakadirisha kutumia Sh.395,800/= kwa bei ambayo imepitishwa sasa yaani Sh. 660/= kwa kilo ambapo kwa ekari moja mkulima atapata karibu Shilingi 360,000 tu. Hivyo anakuwa anapata hasara ya zaidi ya Sh. 30,000 na faida haitakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Pamba pamoja na Serikali imeshindwa kuwasaidia wakulima hawa waweze kuza pamba yao kwa bei ambayo itawapa faida na pengine kuongeza juhud za kilimo cha pamba msimu unaofuata. Wakulima hawa wameshindwa kuza pamba, matokeo yake hali zao za maisha zimekuwa duni huku watoto wakishindwa kulipiwa ada za shule. Naomba kuuliza Serikali kwa nini isiongeze bei ya pamba kutoka Sh.660 hadi Sh.1000 kwa kilo kwa kuchangia kiasi cha Sh. 340 kwa kila kilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima hawa wanapata tabu sana kipindi hiki kwani pamba ndio inayowafanya wawe na maisha mazuri, wale vizuri, wapeleke watoto wao shule, lakini kwa bei hii ya Sh.660/= ni kuwaonea na kuwanufaisha wafanyabiashara ambao ndio wanunuzi wakubwa wa pamba. Naomba Serikali iangalie kwa makini suala hili ili bei ya pamba iweze kufika Shilingi 1000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nampongeza Rais kwa kupunguza ushuru wa Halmashauri kwa zao la pamba kutoka 5% mpaka 2% pamoja na wanunuzi kutoka 10% mpaka 7%. Hili halitoshi bado bei itabakia pale pale ambayo ni sh. 660/=, naomba Serikali i-topup Sh. 340 kwa kilo ili mkulima wa pamba anufaikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii mwaka wa fedha 2011/2012, Waziri aliahidi ataweka juhudhi maalumu zitakazoelekeza katika kuhakikisha wakulima wanapata bei ya haki kuligana na nguvu ya soka. Sasa hapa Serikali iko wapi na kilimo hiki cha wakulima wa pamba?

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Waziri kuwa ishauriane na wadau wa mazao ili iangalie uwezekanao wa kuanzisha mifuko maalumu ya kufidia bei za mazao kwa wakulima pale inaposhuka (*price stabilisation funds*). Hii ingekuwepo tokea mwanzo wakulima wangeshakuwa wameuza pamba yao na pengine uzalishaji ungeongezeka maradufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2011/2012, Wizara ilisema itadahili na kufundisha vijana 3500 ngazi ya Stashahada na Astashahada kwa ajili ya kuongeza idadi ya Maafisa Ugani. Mwaka huu tena 2012/2013, Wizara inasema italipa idadi hiyo hiyo yaani 350 ngazi ya Stashahada na Astashahada. Nilitaka kujua pengine kupata mrejesho katika hili kwani kusomesha idadi kubwa ya wanafunzi kila mwaka kutaongeza pia ajira kwa vijana wengi, ni Mikoa gani ambayo imepatiwa Maafisa hawa? Je, mpaka sasa waliohitimu mafunzo hayo ya Stashahada na Astashahada ni wangapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo mengi katika vyuo vya utafiti hayaridhisha na hivyo kuhatarisha maisha ya watumiaji. Mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya mabweni mawilli ya Chuo cha Mbondo (Kigoma) ili kupokea wanafunzi 80 kuanzia Novemba – Desemba 2011. Mwaka huu wa fedha Wizara itakarabati majengo katika vyuo vya kilimo vya KATC – MOSHI na TUMBI – Tabora. Naipongeza Serikali kwa hatua hiyo na ujenzi wa mabweni Chuo cha Mbondo umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utekelezaji wa maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji ambao unazingatia Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010 na Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002. Bwawa la Masengwa (Shinyanga Vijijini) lipo katika hatua ya kuandaa zabuni, wasiwasi wangu maji ya kujazwa humo yatatoka wapi na ukizingatia Shinyanga miaka yote ni ukame?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri kuwepo na kilimo cha umwagiliaji katika nchi yetu lakini changamoto kubwa ni maji. Sasa kwa nini Serikali isilingie ubia na Halmashauri mfano kama Shinyanga kutoa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, maji haya yanetumika vizuri katika kilimo cha umwagiliaji na pengine kuongeza mabwawa mengine zaidi kwa sababu maji yapo Shinyanga tayari na hayataisha tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha, nikitegemea kupata majibu kutoka kwa Waziri.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti iliyotengwa kwa Wizara hii ni kidogo. Idadi ya Watanzania wanaotegemea kilimo nchini hapa ni kubwa sana ukilinganisha na bajeti. Eneo linalofaa kwa kilimo ni kubwa pia. Serikali izingatie namna gani iongeze fedha hasa katika miradi ambayo itasaidia wakulima wengi kuvuna chakula kwa wingi. Mfano Serikali ikamilishe na kukarabati mabwawa na malambo yaliyopo badala ya ya kuanzisha mapya. Serikali ianzishe mpango wa *drip irrigation* pale ambapo inafaa ili kusaidia maeneo yanayopata *impact* ya ukame (mfano Mikoa ya Kaskazini mwa Tanzania – Manyara, Arusha na Kilimanjaro).

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuajiri Maafisa Ugani zaidi ya 400. Wagani hawa watasaidia sana kuelimisha wakulima kuhusu kanuni bora za kilimo na kuwasaidia katika matatizo ya mifugo. Nashauri Serikali itoe agizo waandaliwe utaratibu wa ku-monitor performance zao katika maeneo waliyopo. Serikali iwatake wawe mara kwa mara wanatoa shamba darasa kwa wakulima na wawe na mashamba ya mfano ili wakulima hawa waige kwoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mbolea ya ruzuku limeendelea kuwa chanzo cha manung'unko kwa wananchi. Serikali iweke mpango mzuri wa kupeleka mbolea kwa wakulima mapema kabla ya msimu wa kilimo kuanza katika eneo husika. Kamati ya Kugawa Mbolea ya Wilaya ikisimamiwa na Mkuu wa Wilaya, pamoja na kugawa lakini itembelee maeneo mapema

kabla ya wakulima kupanda mbegu ili wafahamu pale ambapo watendaji wa vijiji wanadhulumu wananchi katika mgawo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakuu wa Idara ya Kilimo (*DALDOs*), wengi wao wanakaa ofisini badala ya kutembea vijiji kuona kilimo kinavyofanyika. Serikali itoe agizo kwao ili wapimwe kwa namna wanavyotekeleza sera ya kilimo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazotengwa kwa ajili ya kilimo (mfano kujenga mabwawa) zinachelewa sana wakati mchakato wa kupata mkandarasi unachukua muda mrefu. Nashauri Serikali ioneeri/makubaliano na Hazina/TAMISEMI ili fedha za kilimo zilipwe mapema katika Halmashauri ya Wilaya ili kilimo kiendelee badala ya kusubiri muda mrefu ambapo wakulima wanakuwa tayari wamekata tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa mpunga Mwaleni, Mkoani Kilimanjaro unavurugwa na matajiri wenye fedha za kununua *pump* na ku-*pump* maji kinyume na taratibu. Naomba Serikali imtakie *DALDO* wa Moshi vijiji/Mratibu wa kilimo alifuatilie tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Namshukuru Waziri Chiza kwa sababu alipokuwa Naibu Waziri wa Maji alifanya yafuatayo Vunjo:-

- (i) Kupeleka Japan andiko la Mfereji wa Mchomba Vunjo ili kuliombea fedha.
- (ii) Kutengeneza barabara ya Mawala Kahe ili kusafirisha mpunga wa wakulima kutoka mashambani.
- (iii) Skimu ya umwagiliaji ya Mawala Kahe.
- (iv) Kuendelea na ukarabari wa mfereji wa Mwanga Kimwangamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Rais Jakaya Kikwete na Waziri Mkuu kwa kujenga miundombinu katika Jimbo la Vunjo la kusaidia wakulima:-

- (i) Kujenga soko la Kimataifa Himo.
- (ii) Barabara ya Lami Marangu Mtoni, Kilema Kaskazini, Kirua Vunjo Magharibi hadi Kawawa, Himo Pofo – Kilema hospitali.
- (iii) Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya – Himo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, namshauri Waziri afanye yafuatayo:-

(i) Wakati wa mdororo wa uchumi wa mwaka 2008/2009, Serikali ilifidia wakulima wa pamba na wafugaji wa Kimasai. *KNCU* ilikuwa na hasara ya shilingi 1.3 bilioni. Nitashukuru kama nitaambiwa fidia kutoka Serikalini itafika lini *KNCU*?

(ii) Kwa kuwa *KNCU* imekuwa inamkata mkulima shilingi 40 – 50 kwa kilo kwa ajili ya kulipia ghamama za kusimamia kahawa na sasa nasikia Bodi ya Kahawa inakusudia kukata Sh.900 kwa kilo kwa ajili hiyo, Wizara itafanya nini ili kuingilia katika wakulima wasinyonywe?

- (iii) Naomba Wizara ipunguze ghamama za kuzalisha kahawa kwa kuimarisha *TACRI*.
- Kwa sababu inazalisha kahawa inayopambana na magonjwa sugu.
- Inazalisha kahawa inayozaa kwa muda mfupi.

(iv) Kuimarisha sera ya kumnufaisha mkulima. Badala ya kuza kahawa mbichi mkulima kuititia vyama vya ushirika ashughulikie kahawa yake kwa kuikoboa na kuikausha mwenyewe au kuititia chama chake cha ushirika ili apate bei nzuri.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya umwagilaji Kashagube, Nyanganga, Mgambozi na Konkwa. Hii ni miradi imekuwepo tangu mwaka 2007. Mradi kama ya Konkwa na Mgambazi tayari Serikali imepata kuwekeza lakini bado mradi kumaliziwa lakini katika bajeti hii hakuna hata senti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo mzima wa tumbaku katika uuzaaji umejaa rushwa katika *grading*. Inawalazimu wakulima kuhonga ili wapate *grade* stahiki. Naomba Mamlaka ya Tumbaku ichunguzwe. Kuna malalamiko mengi sana Kata za Nguruka, Mtogo, Mganza na Uvinza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninahitaji kujua mpango wa kutenga takriban ekari 95000 kwa kilimo cha miwa Mkoani Kigoma mradi ambaa ungeweza kuzalisha zaidi ya tani 1,000,000 kiasi ambacho ni zaidi ya mahitaji ya sukari nchini. Ningehitaji kujua suala hili limefikia wapi. Lakini zaidi napenda kushauri katika eneo hilo tutenge theluthi mbili kwa *out growers* kama ilivyo Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, agenda ya michikichi, napendekeza Serikali ianze mchakato wa kulifanya zao hili lipate msukumo kama ilivyo pamba, tumbaku na kahawa. Hili ni zao la kimkakati kwa sabuni, mafuta, vikapu na *products* zingine za michikichi. Naomba tujifunze *Malaysia* wanafaidika vipi na michikichi.

MHE. STEPHEN M. WASIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, natoa ushauri na maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfilisi wa Mara Coop Union. Mkoa wa Mara unazo *ginneries* tatu za Ushashi, Mugango na Kibara. Viwanda hivi vimekuwa chini ya Mfilisi kwa miaka zaidi ya 20, viwanda hivi ni mali ya wakulima. Mwaka 2010 Wizara iliandikisha chama kipywa cha wakulima wa *Mara Co-operative Union* (WAMACU), chama hiki hakijaanza kazi yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba WAMACU isaidiwe kusimama na viwanda vya Pamba virudishwe WAMACU ili viwe dhamana kwa chama kikuu ili turudishe ushirika. Vlikundi vya mkataba viandikishwe kwa vyama vya msingi ili kilimo cha mkataba kiwe baina ya wanunuvi na vyama vya msingi badala ya vikundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji, nashauri msaada wa fedha toka Serikali ya Marekani, zielekezwe katika umwagilaji maji nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yenyeye ukame kama vile Shinyanga, Dodoma, Singida, Mara na kadhalika ipewe fursa, ili wananchi wa maeneo hayo waweze kuzalisha chakula na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya umwagiliaji ya Nyatwali, Kisangwa na Mariwanda utekelezaji wake uharakishwe ili wananchi waanze kupata manufaa yanayotokana na miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuondoe ukiritimba katika ununuzi wa zao la pamba, ili wanunuvi wengi waruhusiwe ili kuongeza washindani.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

- (i) Nataka ufanuzi ni lini Serikali itamaliza tatizo la pembejeo kwa wakulima nchini?
- (ii) Ni lini mbegu bora za mazao ya chakula zitazalishwa nchini na kutosheleza wakulima?
- (iii) Ni lini Serikali itahamasishwa uwekezaji ili kujenga kiwanda cha mbolea kusaidia kupunguza bei ya mbolea?

(iv) Ni lini Serikali itatimiza nia yake ya kushirikiana na wakulima na vitengo husika kuwapatia wakulima masoko ya uhakika kwa mazao ya chakula baada ya kujitosheleza na chakula ndani ya nchi?

(v) Ni lini Serikali itaviwezesha vyama vya akiba na mikopo vijjjini viwe na nguvu kuwakopesha wananchi? Hata hivyo, ni kiasi gani benki ya wakulima na *TIB* inawafikia wakulima wa mazao ya chakula, liko tatizo wakulima wadogowadogo hawafaidiki na fedha hizi.

(vi) Ni lini sasa tatizo la sukari litatatuliwa kwa kutumia wakulima wadogowadogo na viwanda vidogovidogo? Jimbo la Peramiho tumeanza lakini mpaka sasa hatuna *support*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja iliyo mbele yetu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri kwa kuwasilisha hoja yake kwa umahiri. Nimpongeze pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Malima, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Wizara hii pamoja na watendaji wote wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Hongereni sana. Natamka kuwa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mimi kuunga mkono hoja hii, napedna nisajili mfadhaiko wangu kutohana na ukimya wa hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kuhusu bei ya pamba katika msimu wa 2012/2013. Ni mfadhaiko kwa sababu Wizara na kwa kweli Serikali nzima imeonyesha "*insensitivity*" ya hali ya juu kwa wakulima wa zao la pamba ambayo inategemewa na takribani watu millioni 16 hapa nchini. Waheshimiwa Wabunge wanaotoka kwenye maeneo yanayolima zao la pamba walishauri Serikali iangalie uwezekano wa kufidia bei ya pamba angalau ilingane na bei ya mwaka jana ili kuwapa wananchi wanaolima zao hili matumaini ya kuendelea kulima pamba. Inaonekana Serikali imeziba masikio yake kwa kilio cha wakulima pamba, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, nimeshangazwa pia na ukimya wa Serikali kuhusu mfumo wa ununuzi wa pamba. Wakati ambapo kuna m dororo wa bei ya pamba katika soko la dunia, nilitegemea kwamba Serikali ingetoa tamko la kuruhusu watu wote wenye fedha wanunue pamba kokote wanapotaka badala ya kung'ang'ania utaratibu uliopo wa kutoa leseni kwa wanunuzi wa pamba. Hata hii iwapo itachukuliwa italeta wanunuzi wengi na hivyo kuleta ushindani katika bei wanayotoa kwa wakulima. Nashauri Serikali itoe tamko kuhusu suala hili wakati Waziri wa Kilimo atakapokuwa anahitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo pia hili suala la Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Pamba, tarehe 30 Mei, 2012 Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika alkaririwa na vyombo vya habari kuwa amemsimamisha Mtendaji Mkuu ili kupisha uchunguzi kwa tuhuma zilizotolewa dhidi yake. Hainingii akilini kuwa mtu anasimamishwa na hapohapo anaendelea kubaki ofisini. Tuelewe ukweli kuhusu suala hili. Kama Mtendaji Mkuu amekuwa *cleared* na tuhuma zilizokuwa zinamkabili, Serikali itamke hivyo ili kuundoa mvutano usio wa lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuishauri Wizara ihakikishe kuwa tatizo sugu la mbegu ambazo hazioti na madawa ambayo hayaui wadudu linashughulikiwa kwa ukamilifu. Hata yote yanamwongezea hasara kubwa mkulima wa pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nashuri Muswada wa Sheria ya Kilimo cha Mikataba ucharakishwe kwa kupewa kipaumbele cha kwanza katika orodha ya Miswada inayopendekezwa kuandaliwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kama nilivyoanza kwa kusema naunga mkono hoja hii.

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuajiri Maafisa Ugani 4000 kwa ajili ya kutoa huduma kwa wakulima. Hii itasaidia sana kuendeleza kilimo bora na kuongeza uzalishaji katika nchi yetu. Hivyo naomba Wizara iwahudumie kwa kuwapatia vitendea kazi na usafiri ili waweze kuharakisha katika kufanya kazi zao na hasa sehemu zenye mazingira magumu. Pia wagani hawa wawezeshwe kwa kupatiwa *shortcourses* ili wawe bora katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kutumia *drip irrigation* katika kilimo (mazao na chakula) kwa kujenga malambo, makinga maji na kuchimba visima vingi sehemu za mashamba kwa wakulima kwani kilimo cha kutegemea mvua ambayo haitabiriki kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, itakuwa shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itilie mkazo kukarabati vyuo vya kilimo ili viwe na hadhi nzuri na wanafunzi wasome katika mazingira ya usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mbolea limekuwa tatizo kubwa kwa wakulima wetu hasa vijiji. Wakulima wengi wanalamika mbolea haipatikani kwa wakati hivyo inawafanya walime bila kutumia mbolea au mbolea inayotumika inakuwa kidogo kuliko inavyotakiwa. Nashauri Serikali iratibu vizuri ugawaji na usambazaji wa mbolea ili wakulima waondokane na matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo mbolea nydingi aina ya Minjingu ambayo wataalam wanasema ni nzuri kwa kilimo kwani imeshafanyiwa utafiti, imejaa kwenye maghala, hajifika kwa wakulima na pia wananchi wengi hawaifahamu ubora wake. Je, Serikali ina mpango gani wa matumizi ya mbolea hii na pia ni lini wakulima wataelimishwa ubora wake ili waweze kuitumia na kuondokana na dhana potofu kuwa mbolea hii si nzuri kwa matumzi ya kilimo, kwa kweli hii ni uharibifu wa mali na kutowatenda haki wakulima na wawekezaji katika sekta ya kilimo. Naomba majibu ya haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

MHE. ABDULSALAAM S. AMER: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuteuliwa kwao tena. Napenda kuwapongeza kwa kazi yao nzuri na yenye tija katika sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maendeleo, kuna changamoto za hapa na pale ambazo kwa uwezo wao najua na kuamini wataweza kuzitatuwa kwa pamoja na Naibu Waziri, pamoja na timu yote ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naongelea suala la pembejeo. Kwa kweli pamoja na juhudi za Wizara kufanya marekebisho kwa msimu huu yapo bado malalamiko mengi tu. Katika kijiji changu na Jimbo langu, baadhi ya maeneo mchezo mchafu umefanyika kwa kuwasainisha fomu zote tatu na kuwapa mbegu tu na kuwaambia kuwa wanawapa bure ila mbolea hawapewi. Katika kufuutilia, nimeambiwa kuwa kitabu kimeshafungwa na wanarudisha Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni mageti ya mazao. Katika Wilaya nydingi na hasa zilizopo Jimboni kwangu, wakulima wananyimwa au wanapunjwa bei ya mazao, ni kubwa kuanzia Sh.2000/= kwa gunia la viazi hadi 4000 kwa ujumla wa mazao yaye mahindi, maharage, mpunga na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, nikiwa mdau wa kilimo na pia mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Maji, Mifugo, natoa pongezi sana kwa bajeti ila pesa ni ndogo. Naomba ushirikiano wenu wa karibu katika kuleta mapinduzi ya kilimo.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri kwa uwasilishaji mzuri na umakini walioonesha katika utendaji wao yeye na Naibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kunukuu kauli ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ambayo alisema:- "Hatutafanikiwa kuendeleza kilimo, hatutapambana na umaskini na mtaendelea kunawiri, ninyi wa maofisini tu na kutembelea ma-balloon (magari) huku wakulima wakiendelea kuteseka."

Mheshimiwa Naibu Spika, mantiki ya usemi huu ni kuhakikisha kuwa jitihada zinaelekezwa katika kuinua kilimo, bajeti iliyotengwa ni lazima iongezeke kwa kuzingatia mahitaji halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pembejeo za mazao ya biashara kama korosho na pamba, ni lazima litiliwe mkazo kwa maana kuwa ucheleweshaji usio na lazima na imekuwa inajirudisha kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la soko pia limekuwa sugu hivyo nashauri Serikali iimarishe viwanda vya kuongeza ubora wa mazao kama korosho, pamba na tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa kwa mazao asili kama nazi, embe, machungwa na ndimu. Vizuizi ni vingi na mkulima anachoka kutoa mazao shambani kufika sokoni, lakini pia tunatoa misamaha kwa kuagiza *concentrate* hali ya kwa matunda yanaoza hapa nchini. Lazima tuimarishe viwanda vya ndani na kuzuia uagizaji huu wa *juice* kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia hotuba ya Waziri, pamoja na hotuba ya Kamati inaonyesha Serikali imeridhia kutumia *GMOs*, hii ni hatari sana kwa ustawi wa nchi yetu, ni kheri tukaangalia wenzetu nchi za Marekani, South Africa, China na kadhalika siku zote hata ukiangalia kwenye soko, bei ya *organic food* ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kumekuwa na upungufu mkubwa wa mchele. Serikali iondoe *excess duty* ya 75% ili kukabiliana na upungufu wa chakula kama nchi za jirani zilivyofanya Kenya, Uganda na Burundi. Mchele unachangia sana mfumuko wa bei hivyo jitihada za haraka zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja. Aldha, baada ya kuunga mkono hoja ilio mbele yetu naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usambazaji wa pembejeo, pamoja na kutokulipa kwa mawakala waliosambaza pembejeo. Serikali inao mtandao ulioenea nchi nzima lkifahamu misimu kwa nchi nzima, la kushangaza ni kwamba usambazaji wa pembejeo hauendi kwa wakati kwa kuzingatia kipindi ambacho wakulima wanakuwa wameuza mazao yao na hivyo kuwa na pesa za kuweza kumudu kulipia kwa kuchangia kiasi kile ambacho ni wajibu kwa mkulima. Ni ukweli usiopingika kwamba ukisambaza pembejeo kipindi ambacho mkulima hana pesa unamweka majaribuni kwani hawezi kulipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawakala walioshiriki zoezi la kusambaza pembejeo wanajutia kufanya kazi hii kwani zoezi limemwingiza katika umaskini mkubwa kwani walichukuwa pesa zenye riba na imechukua muda mrefu mpaka leo mawakala bado hawajalipwa kwa sababu ambazo hazieleweki. Namshauri Mheshimiwa Waziri aje na kauli ya lini mawakala watalipwa pesa zao ili wasiendelee kuwa maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya ushirika kutokufikia walengwa na *SCULT* kushindwa kulipa *SACCOS*. Elimu ya ushirika haitolewi kiasi cha kutosha na kama inatolewa basi inatolewa baadhi tu ya maeneo ya nchi yetu ya Tanzania. Jimboni kwangu na Wilaya mpya ya Kalambo, elimu haijafika na hivyo inakuwa ni vigumu sana pale unapomnyima mwananchi wa kawaida elimu ya ushirika lakini wakati huohuo unatarajia eti wananchi wajunge na vikundi pamoja na

SACCOS, hii si sawa hata kidogo. Hivyo naiomba Wizara ichukue juhudhi za makusudi za kuhakikisha elimu hii inawafikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza na kumatisha tamaa ni pale ambapo taasisi ya Serikali inaposhindwa kulipa au kurudisha amana iliyokuwa imewekwa ya kiasi cha shilingi milioni kumi (10m) ili kupata mkopo wa shilingi milioni thelathini (30m) na *SACCOS* ikatimiza masharti ya mkopo na kuweza kulipa pamoja na riba kwa kuchelewesha kulipa, cha ajabu pesa iliyowekwa kama amana ili kutimiza sharti la mkopo hadi leo hajjarudishwa na *SCULT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha miwa ili kuzalisha sukari, naipongeza Wizara kwa kuliona tatizo hili la upungufu wa sukari na kuamua kuongeza uzalishaji wa miwa ili tukabiliane na tatizo la upungufu wa sukari nchini. Naomba Wizara ihakikishe mbegu zinasambazwa hata Wilaya mpya ya Kalambo ambako tunalima miwa ambayo tunaambiwa si mizuri sana kwa uzalishaji wa sukari.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri kwa hotuba hii nzuri. Mimi naipongeza Serikali inavyojitahidi Watanzania waweze kuwa na kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa chakula nchini, naiomba Serikali ijipange kwenye Halmashauri zetu kwa kutafuta mbegu za mazao yote ili wananchi waweze kulima mazao mchanganyiko. Kuna mazao mengine yanastahimili ukame kwani tutapunguza sana suala la njaa, wananchi waelimishwe, ardhi tunayo, wataalam vijiji hakuna wa kutosha, hebu Serikali ifanye mkakati wa makusudi ili wananchi walilala waweze kuamshwa kwani bado tunaimba na kilimo mchanganyiko lakini uhamashishi uende sambamba na mbegu za mazao yanayostahimili ukame na matokeo tutayaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbolea ya Minjingu ikipigwa vita sana kwa kusema eti haifai, inachelewa kufanya kazi, mimi naomba Serikali itoe elimu juu ya mbolea ya Minjingu iweze kutumika kwani iko nydingi sana tena wataalam wanasesma inaweza kukaa ardhini ikiwa na nguvu kwa miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine hebu tuwaangalieni hawa waliopewa vibali vya kusambaza mbolea, ni kwa nini hawaji kuchukua mbolea hii na wakaweza kuwafikishia wananchi na baadaye hawa wananchi wakasema kuwa inafa au haifai?

Mheshimiwa Naibu Spika, zao mbadala la biashara ni minazi inayoitwa *Africa Toll*. Minazi hii inadumu zaidi ya miaka mia moja. Hili ni zao linalotoa mazao miezi mitatu, mitatu. Hebu Serikali ihamasishie wananchi walime zao hili ili waweze kujipatia kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

MHE. DKT. HAJI H. MPONDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali illiangalie kwa makini sana suala la kilimo cha mpunga na kuona namna gani inaweza kuwekeza zaidi katika bonde la Kilombero ambalo lina uwezo wa kulisha Watanzania na zao hili la mpunga ambalo huchangia kiasi kikubwa mfumuko wa bei ya chakula. Wizara waongeze bajeti katika vyanzo za mabanio manne katika Wilaya ya Ulanga, (mabanio ya Itete, Lupiro, Minepa na Musegese). Kama kweli Serikali ina malengo madhubuti katika kukabiliana na upungufu wa zao la mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri wakati akimalizia hoja yake, awaeleze wananchi wa Ulanga ugonjwa wa zao la mpunga ambao unazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka. Ugonjwa huu unaitwa "*Rice Yellow Mottle Virus*".

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wote kwa kufanikisha kuleta hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu ili nasi Waheshimiwa Wabunge tupate kutoa maoni yetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, madai ya wakulima wa korosho Pwani. Hadi sasa wakulima wa korosho Pwani hawajapata malipo yao ya pili na kipindi cha pili kwa ajili ya zao hili kimefika na wanaelezwa kuwa korosho bado zipo ghalani. Je, Serikali inawaeleza nini wakulima wanaodai pesa zao wakati msimu mwingine unakaribia na *sulphur* bado hawajapata?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali hii kweli ina dhamira ya dhati kumkomboa mkulima mnyonge wa Mkoa wa Pwani anayeishi Rufiji, Mkuranga na Kibaha kwa kuacha korosho zao zikioza katika maghala?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa *SAGCOT* na Kilimo Kwanza. Katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 2011/2012 ilionesa kuwa eneo la Bonde la Mto Rufiji liliopita Pwani nalo pia litatusika katika mpango huu wa *SAGCOT*. Katika bajeti hii ya Wizara ya Kilimo 2012/13 hakuna mpango wowote wa kilimo ambaa umeelekezwa katika Wilaya ya Rufiji kuititia Bonde la Mto Rufiji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika zao la mpunga. Je, mkakati ule wa kilimo cha umwagiliaji katika Wilaya ya Rufiji kuititia *SAGCOT* umeishia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona leo Mkoa wa Pwani tunaomba ama tuna upungufu wa chakula wakati tuna Bonde zuri la Mto Rufiji, Ruvu. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutumia ardhi yenye rutuba na mito yenye maji yanayoweza kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji kwa kuzalisha chakula kingi katika Mkoa wa Pwani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maneno yanazungumzwa kuwa Bonde la Mto Rufiji katika Wilaya ya Rufiji kuna mwekezaji wa zao la miwa kwa ajili ya sukari. Je, mchakato huu upo katika hatua gani? Namwomba Mheshimiwa Waziri anipatie majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa uteuzi wao na pia watendaji wote wa Wizara kwa kuwezesha kuandaa bajeti ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio ya Watanzania kwamba Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika itaendeshwa kwa dhana halisi ya "Kilimo Kwanza". Kwa msingi huo, Wizara ya Fedha itoe kipaumbele katika mfumo wa bajeti kuwezesha Kilimo Kwanza kwa vitendo licha ya kila Mbunge kutanguliza dhana ya "Maji Kwanza" kutokana na ukubwa wa tatizo la maji Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni Mpango wa Taifa wa Umwagiliaji (*National Irrigation Master Plan*). Mpango huu uliandaliwa muda mrefu na sina uhakika kama utatekelezwa kwa namna gani na ni kwa jinsi gani mapendekezo ya miradi mipya inaweza kuingizwa na kutekelezwa. Katika mpango huo Wilaya ya Muheza iliingiza miradi minne:-

- (i) Umwagiliaji mradi wa Bwala Misozwe.
- (ii) Umwagiliaji mradi wa Mashewa.
- (iii) Umwagiliaji mradi wa Potwe.
- (iv) Umwagiliaji mradi wa Mkizi/Pangani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi pekee unaotekeliza sasa kwa zaidi ya miaka mitano iliyopita ni "umwagiliaji mradi wa Bwawa Misozwe. Licha ya kuchelewa hivi sasa mradi kwa ujenzi wa bwawa na matoleo ya mabomba ya mifereji unakwenda vizuri na fedha zimetengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi umepewe hadhi rasmi wa kufikiwa kwa mbio za Mwenge tarehe 5 Julai, 2012. Maombi rasmi ya wanachama wa mradi huo wa umwagiliaji ni kama ifuatavyo:-

(i) Serikali itenye fedha kuwezesha ujenzi wa mifereji na skimu za umwagiliaji ikiwemo kusaidia kutifua ardhi na kuweka vipimo vya maeneo ya mpango wa mgao wa ardhi kwa wakulima. Wizara na sekta ya umwagiliaji Kanda ya Kaskazini isaidie Wilaya ya Muheza kuweka andiko la maombi ya fedha kwa kazi hiyo.

(ii) Serikali isaidie wanachama wa kikundi cha umwagiliaji kupata mbegu bora za mpunga kwa wakati ili kuanza kilimo mara baada ya ujenzi wa skimu.

(iii) Wizara isaidiane na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuwezesha upatikanaji wa mbegu bora za samaki kwa ajili ya bwawa hilo kubwa la maji lilojengwa.

(iv) Wizara isaidie kutoa ushauri juu ya uwezekano wa kusaidia familia chache zilizokuwa zinamiliki eneo hilo la zaidi ya hekta 100 kupata kifuta machozi kwa kuweza kuachia eneo hilo kwa wanachama zaidi ya 130 wa mradi huo. Baadhi ya wananchi waliopisha eneo la ujenzi wa bwawa walilipwa fidia na Serikali miaka ya 1970/1980. Wale wanaaoachia sasa hekta 100 za skimu hawajalipwa fidia yoyote. Wapo pia wananchi wachache nje ya eneo la skimu lakini karibu na bwawa ambapo kwa mazingira ya kuhifadhi bwawa hilo liliogharimu fedha nydingi, shilingi 1.2 bilioni. Ni lazima wananchi hao wahamishwe ili kuwezesha bwawa hilo kuwa endelevu. Tunaomba msaada na ushauri rasmi kutoka Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wadudu waharibifu wa machungwa na matunda hasa machungwa yameendelea kuwatesa wakulima wa machungwa Muheza. Jitihada za kupambana na janga hili zimechukua muda mrefu sana lakini bado uharibifu unaendelea. Nashauri sasa Wizara isaidie kwa dhati kabisa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kupambana na janga hili. Machungwa yanaiza na kusheheni wadudu ndani, kubadilisha rangi ya nje ya chungwa, kuwa na madoa na kukosa soko. Naomba Wizara iongeze jitihada za kutoa elimu na madawa kupambana na wadudu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa (*climatic change*) yanayoendelea duniani yanaathiri kilimo na chakula. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika iwe mdaa mkuu wa kufuatilia mabadiliko ya hali ya hewa duniani ili iweze kushauri wakulima juu ya mazao bora, muda wa kupanda, madawa ya kupambana na wadudu waharibifu na pia kubadili aina ya mazao ambayo wakulima wamekuwa na mazoea ya asili ya kuyalima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza hotuba nzuri, pamoa na mchango wangu kwa kuzungumza, naiomba Serikali iangalie suala la migogoro ya kilimo na wafugaji. Tatizo hili linearudisha nyuma maendeleo ya wakulima hasa wale wadogowadogo kwani mifugo inapokula mazao ya mkulima ambaye anatarajia avune ili aweze kula na kuza lakini mifugo ikishambulia mazao hayo, hakuna atakachopata, ni hasara tupu kwake na pia ndipo migogoro, mapigano na hata vifo hutoke. Naomba Serikali inipatie majibu ni viyi imejipanga ili kuwatengea maeneo wafugaji ambayo itakuwa na miundombinu yote stahili na kwenda kufuga huko. Naomba Serikali inipatie hiyo mipango mkakati ili kuinusuru jamii (ya wafugaji/kilimo) na kuweza kuijendezeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja.

MHE. LOLESEA J.M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa hotuba nzuri aliyowasilisha Bungeni. Nimpongeze pia Naibu Waziri kwa kazi nzuri. Bila kuwasahau watendaji wa Wizara ambaye ni Katibu Mkuu, Naibu wake na watumishi wote. Wizara ya Kilimo, ni Wizara nyeti sana na ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanajishughulisha na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali ni kutafuta namna ya kuwasaidia wakulima hasa wakulima wadogo wa vijiji. Serikali iwekeze katika kilimo cha umwagiliaji hasa Kanda ya Ziwa Victoria. Wilaya ya Geita, Sengerema, Chato zimezungukwa na maji ya Ziwa Victoria. Ninaomba wakati wa majumuisho Serikali injibu swali langu la kwamba ni lini Serikali itaananza rasmi kilimo cha umwagiliaji Geita na Kanda ya Ziwa kwa ujumla?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata nafasi ya kushiriki Mkutano wa Pili wa Wabunge kuhusu *Nile Basin Initiative*. Kupitia semina hiyo, nilijua mikakati iliyowekwa kwa ajili ya *Lake Victoria Basin*, hasa katika Jumuia ya Afrika Mashariki. Mipango iliyopo huko ni pamoja na kuanzisha kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa wa Mara, Mwanza na Geita. Niiombe Wizara kupitia fursa hii iangalie namna ya kuunga mkono mpango huu wa Jumuia ya "Afrika Mashariki. Mradi wa umwagiliaji Kanda ya Ziwa ni ukombozi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili linahusu kilimo cha pamba. Takribani zaidi ya miaka mitatu mfululizo kumekuwa na changamoto kubwa ya kushuka bei katika soko la dunia ambako kumesababisha pia kushuka kwa bei kwa mkulima. Hii ni hasara kubwa sana kwa mkulima, matokeo yake hatuvezi kupunguza umaskini kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ni vigumu kufikia malengo ya *millennium*. Kwa changamoto hizi ambazo zimekuwa za mara kwa mara, niishauri Serikali iwekeze katika viwanda. Viwanda vijengwe Mikoa hii inayolima pamba. Hii italeta neema kubwa kwa wananchi, pamba yote inayozalishwa itatumika katika viwanda vyetu. Si hili tu bali ajira kwa vijana wetu wasomi zitapatikana. Naomba Serikali iwekeze kwenye viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo mambo mawili muhimu, suala la kuanzisha *scheme* za umwagiliaji na viwanda, naomba Serikali iyachukulie kwa uzito mkubwa unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. TEREZYA L. HUVISA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri ya kuchochea maendeleo ya kilimo. Naishukuru kwa kushusha bei ya matrekta ili wakulima wengi waweze kuondokana na jembe la mkono ili kukuza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pembejeo ni kubwa, Wizara lazima ishughulikie tatizo hili kwa umakini. Pembejeo ziwashishwe, ikiwezekana zianze kusambazwa mapema kuanzia mwezi Septemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Ruvuma unategemea sana kilimo cha kutumia mbolea. Bila mbolea, kilimo cha mahindi na tumbaku hakiwezekani. Msimu wa mvua unaanza mwezi wa kumi na moja, hivyo mbolea na mbegu zipelekwe mwezi Septemba, wakulima watakuwa wamejiandaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema ikaandaliwa ratiba ya usambazaji wa pembejeo kila Mkoa kutokana na misimu mbalimbali ya mvua katika Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu soko la mazao ya chakula, sasa hivi mazao haya yanauzika nchi jirani. Ni vema Wizara ikajipanga vizuri ili kuwezesha Mikoa wa Ruvuma na Mikoa mingine kuwa na masoko ya uhakika na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Goweko/Nsololo limeongelewa tangu mwaka 2010 kwamba upembuzi yakinifu unafanyika. Mpaka sasa mwaka 2012/13 hakuna maendeleo yoyote.

Mheshimiwa Waziri tunahitaji hili bwawa na mengine Jimboni Igalula kwa ajili ya umwagiliaji, mifugo, maji ya kunywa, ufugaji samaki na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itusaidie Jimboni kuunda ushirika ili vikundi viweze kukopeshwa matrektu na kuongeza uzalishaji katika kilimo na kuongeza thamani kwenye mpunga, mahindi, karanga na alizeti badala ya kuuzwa ghafi na kukuza kipato chao na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pembejeo zifike kwa wakati hasa mbolea ya kupandia na kukuzia. Masoko ya tumbaku yawepo pamoja na vumilia (kijiji) ili cess ibaki Igalula badala ya kwenda Manispaa ya Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuongeze Maafisa Ugani ili wananchi walime kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu za kisasa za miembe Igalula na Mkoa wa Tabora na kuongeza thamani ya zao hilo – *juice* na baadhi yaliyokomaa kusafirishwa nchi za nje kwa bei kubwa. Viwanda hivyo pia viongeze thamani ya zao la asali ambayo iko sehemu zisizolima tumbaku yenye *nicotine*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata taarifa kuwa ile 2% ya *cess* tumegawiwa na Wilaya ya Uyui imepata shilingi 800 milioni. Ninaipongeza Serikali kwa kutupatia pesa hizo ambazo zitatumika kukamilisha miradi ya maendeleo Wilayani. Tunapongeza Mheshimwa Waziri Mkuu Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa jithada hizo na fedha hizo kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha tumbaku Tabora ni muhimu ili ajira pia ipatikane na kujumuisha inayozalishwa Kigoma, Rukwa na Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwe mfuko wa tahadhari ili bei ya zao la tumbaku na mengine ikishuka wakulima waweze kufidiwa kila mwaka kukiwa na m dororo wa uchumi duniani pamoja na kuwa na viwanda vinavyoongeza thamani ya mazao haya na ajira iongezeke pamoja na ongezeko la mzunguko wa fedha kwa wingi wa kodi kupatikana.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali ina lengo la kuondokana na kilimo cha kujikimu (yaani chenye tija ndogo) fedha zilizotengwa kwa miradi ya maendeleo haziwezi kutufikisha huko. Mfano fedha za maendeleo shilingi 67,260,154,000/=, za ndani shilingi 14,937,000,000/=, za nje shilingi 52,323,154,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuangalie fedha tulizozitegemea hapa kutoka kwa wafadhili kwa kiwango kikubwa kama wafadhili wamesitisha misaada kwetu kutokana na vigezo kwamba sisi wenyewe tumesaidia kwa kiasi gani kuleta maendeleo ya Taifa letu na wanachokisaidia mara nyingi zinaishia mikononi mwa wajanja, je, maendeleo tuliyoainisha kwa kuondokana na kilimo duni tutafanikiwa? Ni vema Serikali ikapunguza fedha za kawaida angalau, fedha za maendeleo zikaongezeka kidogo. Lakini utegemezi katika fedha za maendeleo tusiendelee kuweka mategemeo kwamba tunaweza kuvuka lengo tulilokusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla bajeti iliyotengewa Wizara ya Kilimo ni ndogo sana, naiomba Serikali kufikiria kwa kina, kwani pato la Taifa kwa kiasi kikubwa tunategemea sekta ya kilimo. Kama tutaendelea kuitengea fedha kidogo namna hii kilimo nchini hakiwezi kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuandaa mipango mizuri ndani ya sekta hii lakini nailaumu kwa kutotenga fedha ya kutosha kulingana na mipango iliyoinisha. Wengi tunafahamu kwamba bila kilimo uchumi wa Taifa unadidimia, kwa nini Serikali isitenge fedha za kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Benki ya Kilimo, mara nyingi Serikali imekuwa ikitiwa kuhusu utaratibu wa uanzishwaji wa Benki ya Kilimo nchini kwa kuwapatia mikopo wakulima wadogo na wakubwa kuweza kuendeleza kilimo chenye tija. Kwa nini mchakato huu wa

uanzishwaji sasa ni muda mrefu haukamiliki? Imekuwa tukiwapa tamaa wakulima wetu kwa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli dirisha la mikopo kupitia Benki ya Rasilimali linakidhi haja kwa wakulima wetu? Je, Serikali inaweza kutuhakikishia kwamba mchakato unakamilika lini? Je, hili dirisha linaloandaliwa linawaendeleza wakulima walio wengi nchini?

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa kuteuliwa kuwa viongozi Wakuu wa Wizara hii nyeti. Aidha, nawapongeza Katibu Mkuu kwa juhudhi anazofanya kwa kushirikiana na watendaji wote wa taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bei ya pamba, naiomba Serikali ianze mpango wake wa bima kwa mazao ya kilimo ilioutangaza mwaka huu wa fedha kwenye zao la pamba. Kwa vile mpango wa bima uko tayari kuanza, naishauri Serikali iutekeleze kwenye bei ya pamba ili kunusuru adha na hasara wanayopata wakulima 16 milioni wa pamba kutokana na kuyumba kwa bei ya pamba kwenye soko la dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa skimu ya umwagiliaji wa Isole/Kishinda Sengerema. Mradi huu unatajwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri (kiambatisho na. 11), naomba utekelezaji wake uharakishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Katunguru Irrigation Scheme*, mradi huu unatekelezwa kupitia *DIDF/DADP*. Naomba ukamiliishwe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ni ndogo sana ukilinganisha umuhimu wa Wizara hii inayotegemewa na asilimia 75% ya Watanzania. Hivyo Wizara hii iongezewe fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itambue umaarufu wa Bonde la Ziwa Rukwa. Kwa jinsi lilivyo na umuhimu wa kuwa na uwezo mkubwa wa kuweza kutumika katika kilimo cha umwagiliaji. Nasema hivi kwa sababu eneo hili lina mito mingi sana. Bonde zuri lenye rutuba ya kukubali mazao yote. Serikali ina mpango gani wa kuliendeleza Bonde hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utoaji wa pembejeo, naomba Serikali inapotoa pembejeo itoe pembejeo kwa mazao yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya umwagiliaji, naiomba Serikali kutenga fedha kwa ajili ya mradi wa Maleza wenye eneo la hekta elfu saba na mia tano (7500), mradi huu umeombewa mfululizo kwa miaka mitano lakini nashangaa hata katika bajeti hii siajona mahali ambapo panataja mradi huu wa Maleza. Naomba maelezo na ufanuzi wa hoja hii.

Mheshimiwa Spika naomba vituo vifuatavyo vyta kununua mahindi ambavyo ni Sandulula na Kaengesa vipatiwe fedha ili vifanye kazi. Vituo hivi vilifunguliwa toka mwaka jana lakini kutokana na ukosefu wa fedha, vituo hivi mwaka jana havikununua mahindi hadi kusababisha wakulima kushindwa kuuza mahindi yao. Kulima vizuri kutokana na Serikali kushindwa kununua mahindi yao. Naomba maelezo kwa mwaka huu kama vitafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima kutozwa ushuru wa mazao. Naomba mkulima huyu mdogo asitowze ushuru anapopelea mazao yake sokoni kuuza mazao yake kwani kumtoza mkulima huyu mdogo ni kumwongezea umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa Wahandisi wa Kilimo cha Umwagiliaji. Serikali ijithadi kuongeza Wahandisi wa Umwagiliaji ili kuendeleza kilimo cha umwagiliaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupunguza bei ya vifaa vya trekta kama vile *harrow*, Majembe, *Planter* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa pembejeo za kilimo kipindi cha kiangazi. Tumekuwa tukitoa pembejeo kwa kipindi cha mvua tu. Tunaomba Serikali ianze kutoa pembejeo katika kipindi cha kiangazi kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa chakula katika Tarafa ya Kipeta. Tarafa hii itakuwa na upungufu wa chakula kutokana na mazao yao kukauka. Tunaomba Serikali ipeleke chakula.

MHE. MWIGULU L.N. MADELU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naipongeza Serikali kwa jitihada za kuwakomboa wakulima. Nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa jinsi wanavyojituma kuhakikisha llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inatekelezwa na kuendelea kuwaweka wakulima wetu karibu na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iweke kwenye mpango wake ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji katika Kijiji cha Makunda ili bwawa hilo litumike kwenye Kilimo katika mbuga iliyopo kati ya Nguvumali, Usuru, Motomoto, Zinziligi, Mkulu, Simbalungwala, Misuna na Ng'anguli. Pia Wizara ijenge bwawa kati ya Mto na Mtekente kuwezesha umwagiliaji katika vijiji vya Mgunga, Kinkungu, Tyema na Mtoa, hivyo hivyo na kwa Kata ya Mtoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie pembejeo za Kilimo. Serikali ina nia njema sana ya kuwasaidia wakulima mbolea na mbegu kwa ajili ya kuongeza mazao. Naiomba Serikali ijithadi kwa hali na mali ili pembejeo ziweze kuwfafikia wakulima kabla ya msimu kuanza ili kuondoa hujuma hii ya kupeleka pembejeo wakati wakulima tayari wameshaanza kuvuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali itilie mkazo upatikanaji wa kiwanda cha kuchuja/kukamua alizeti (*double refine*) ili kuchochaea kilimo cha alizeti na kutengeneza ajira kwa vijana na wananchi wa Iramba kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuwa na mpango maalumu wa kuinua mazao yenye kuliingizia Taifa fedha. Alizeti ni moja ya zao lenye uwezekano wa kuliingizia Taifa fedha za Kigeni. Kwa sasa mafuta ya alizeti ni asilimia 20 ya mahitaji. Jitihada za Serikali zikiongezwa zitawenza kufikisha asilimia 50 ya mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuitaka Serikali iongeze bajeti ya Kilimo, kwani kila mwaka inaendelea kushuka. Tukitaka nchi iendele, lazima kipaumbele kikubwa tuongeze bajeti ili iweze kukidhi mahitaji ya Sekta ya Kilimo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo cha umwagiliaji ni muhimu sana katika kunusuru Taifa letu lisipate njaa, kwani tukiimarisha kilimo cha umwagiliaji, tutakuwa na uzalishaji mkubwa na kutokomeza njaa katika nchi na kupata chakula cha ziada ambacho Taifa hili lingeweza kuuza nje ya nchi na kuleta fedha za Kigeni katika Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa hili nguvu kazi kubwa iko kwa vijana amba wengi wao hasa wa vijiji wanategemea kilimo. Laiti tungewasaidia kwa kuwajengea uwezo wa vitendea kazi na kuwawezesha vijana wengi wasingekimbilia Mijini. Ni muhimu Serikali sasa ijenge uwezo wa kuwapatia vitendea kazi kupitia vikundi vyao ambavyo wataviunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la masoko kwa mazao ya biashara ambayo yanazalishwa nchini ni lazima Serikali iandae mpango mkakati wa kutafuta masoko nje kwa mazao yanayozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazao haya kama kahawa, pamba, chai, pareto na tumbaku, lazima tuyaongezee thamani kwa kujenga viwanda vya kusindika mazao haya. Kama

Wizara haitaweka mpango mkakati wa kujenga viwanda vyta kusindika kelele za kila siku, zitaendelea kusikika kutoka kwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mbegu, Serikali lazima iandae mfuko wa kuboresha Taasisi za Utafiti wa Mbegu zipewe umuhimu mkubwa wa kuzalisha mbegu bora ambazo zitasambazwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itaziwezesha Taasisi za Utafiti, Serikali haitanunua mbegu kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa soko la zao la tumbaku, naishauri Serikali iwasaidie wakulima hawa zao hili, kwa kuwatafutia soko la nchi ya China ili wapate soko la kudumu kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, kwa zao kahawa, tusiruhusu iuzwe ikiwa mbichi, tutakuwa tumeiua sector hii ya zao la kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iondoe tatizo la migogoro ya wakulima na wafugaji. Tusipotenganisha maeneo ya wakulima na wafugaji, tutaanzisha migogoro mikubwa ambayo itavunja amani katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja endapo tutayafanyia kazi haya.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika - Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, pamoja na Watendaji wote walioandaa bajeti hii yenye mwelekeo mzuri, lakini inakabiliwa na ufinyu wa fedha ukilinganisha na majukumu mengi, mazito ya kuwaletaa maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali waitazame bajeti hii upya ili iongezewe fedha zaidi kurahisisha utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo ikiwemo mikopo ya pembejeo, kilimo cha umwagiliaji, kuimarisha Vyama vya Ushirika na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa busara wa kufufua Vyama vya Ushirika nchini, utaratibu huu utasaidia sana kuboresha Vyama vya Ushirika pamoja na kuwaimarisha wakulima kuweza kupanua kilimo na kuwa na kilimo chenyeh tija kwa kuinua pato la wakulima. Hivyo, naiomba Serikali kutoa Watendaji wa kusaidia usimamizi ili Vyama hivi vya Ushirika visianguke tena. Ninasubiri maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niendelee kupongeza juhudzi za uongozi wa Mkoa wa Singida chini ya Uongozi wa Mkoo wa Mkoa wa Singida Dkt. Parseko Kone kwa kufufua na kuanzisha Vyama vya Ushirika 81 na vyote viko mstari wa mbele kushirikiana na wafanyabiashara wadogo wadogo kununua alizeti kwa kushindikana bei kwenye soko, yaani magilio yatakayofunguliwa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imesaidia sana wananchi kuacha kuuza alizeti kwa hasara na walangazi walivyokuwa wamezoea kuwafuata wakulima mashambani. Sasa wananchi watapata habari kila siku bei iliyoko kwenye soko ni Shilingi ngapi. Watauza bei ambayo itawapa faida na maendeleo makubwa. Pia Serikali ya Mkoa itapata takwimu ya pato la Mwananchi wa Singida kwa mwaka ni Shilingi ngapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanaotokea kwenye Mikoa inayolima pamba, kuwa zao hili bado halijamnuifaisha mkulima kwa sababu ya soko lake kuwa chini kila mwaka kutohana na utaratibu mbovu wa Bodi ya Pamba kununua pamba kwa bei ya hasara, kisha wakulima hukopwa, hawalipwi kwa wakati muafaka, hata mizani zinazotumika zinawaibia wakulima. Ushauri wangu ni kuwa, soko la pamba liwe huria ili kila mkulima achague mahali pa kuuza ama ushirika wa pamba uangaliwe upya. Nasubiri ufanuzi wa Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado utaratibu wa mikopo ya pembejeo haujawa wazi kwa wakulima. Naomba elimu itolewe ili wananchi wengi waelewe wakiwemo wanawake ili waweze kukopa. Hadi sasa wanaonufaika na mikopo hii ni wajanja wachache tu. Ni ukweli usiofichika kuwa hata wanawake wanao uwezo mkubwa sana wa kilimo cha kisasa, tena wana usimamizi wenye tija. Ninaomba wapatiwe mikopo ya pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza juhudzi za Maafisa Ugani katika kutoa elimu kwa wakulima wa kilimo cha kisasa. Ni ukweli usiofichika kuwa Maafisa hawa wanatembea sana vijiji, wengine hata usafiri hawana na kama wanazo pikipiki, fedha za kununulia mafuta ya petroli hawapewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuhakikisha kila Afisa Ugani anao usafiri na fedha za kununulia petroli ili waweze kuwafikia wakulima. Vilevile ninashauri kuwa hadi sasa Maafisa Ugani bado wapo hadi ngazi ya Kata. Naomba sasa ajira zifike ngazi ya Kijiji ili kuwapunguzia Maafisa Ugani hawa ukubwa wa maeneo ya kuhudumia. Hii itasaidia sana Maafisa Ugani hawa kuwafikia wakulima wengi pia hata wao kupata muda wa kulima mashamba darasa ya kufundishia wakulima. Nasubiri maelezo ya Waziri au Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujulisha Serikali kuwa Mkoa wa Singida kuna maeneo zao la mahindi linastawi vizuri sana. Hivyo naomba wakati wa masika, mbegu za mahindi zipelekwe Singida na vile vile wanaolima mahindi, takwimu za zao la mahindi zitambulike ili Serikali iweze kupata takwimu za pato la mwananchi wa Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza sana Serikali kwa kukazania kilimo cha umwagiliaji. Vilevile napongeza juhudzi za wakulima wa mpunga na bustani Singida, kwani wanayatumia vyema mabonde yaliyopo Mkoani Singida. Naomba skimu za umwagiliaji Singida zitengewe bajeti zote ili ziweze kuwasaidia wakulima kuboresha kilimo cha umwagiliaji kwenye mabonde yote yaliyo Singida, mfano, Wilaya ya Manyoni, Kata za Sanza, Nkoko, Iramba Kata ya Shelui, Mto na kadhalika. Nasubiri maelezo ya Mheshimiwa Waziri, kaka yangu *Engineer Chiza* na Naibu Waziri - Mheshimiwa Malima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono nikiwa na mategemeo kuwa mchango wangu utapewa uzito unaostahili pamoja na michango ya Wabunge wenzangu kwa Serikali kukubali kuvunja Bodi na kuongeza bajeti ya Wizara hii ya Kilimo chakula na Ushirika. Nawatakia afya njema na utekelezaji wenye tija.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali katika maeneo yafuatayo: Kwanza, Serikali itawezaje kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo wakati bajeti yake haikidhi mahitaji? Je, uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo, upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kilimo utafanikiwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika katika eneo la masuala mtambuka katika Kilimo, ni kwamba kumekuwa na tatizo kubwa ambalo limejitokeza ambalo hasa linahusu matatizo ya wafugaji na wakulima. Naliongelea hili kwa sababu maeneo haya, wafugaji wamekuwa wakilisha ng'ombe zao katika mashamba na bustani za wakulima, kwa mfano katika Kata ya Mpanda ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 18 Julai, 2012 kumetokea mapigano makali kati ya wafugaji wenye asili ya Kisukuma na wakulima wa Kata hiyo, baada ya wafugaji hao kuingiza ng'ombe katika maeneo ya bustani na mmoja wa wakazi wa eneo hilo ameumizwa vibaya sana na wafugaji hao baada ya kuhoji kwa nini wameingiza ng'ombe zao shambani. Je, Serikali haioni kama hili ni janga la Kitaifa na linapaswa kushughulikiwa ipasavyo? Je kutokana na mikakati ya kupunguza umaskini, kwa staili hii tutaweza? Kwa mtindo huu ulivyo sasa na kwa hali ya baadaye: Je, tutaweza kutatua na kukabiliana na njaa ambayo kwa sasa ni janga la Kitaifa na Kimataifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itoe utaratibu na majibu kwa hali hiyo inayoendelea sasa katika maeneo mbalimbali nchini hasa pia katika Tarafa ya Mpimbwe Mkoani Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa sukari na bei ya sukari: Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuipatia Bodi ya Mazao mchanganyiko ili iweze kuagiza sukari na kuisambaza nchini ili kupunguza pia bei ya sukari ambayo kwa maeneo kama ya Mpanda inafika mpaka Sh. 2,500/= kwa kilo, hivyo kumfanya mlaji kununua sukari kwa kipimo cha kijiko. Je, Mwananchi wa kawaida anaweza kumudu hali hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba yote ambayo yalichukuliwa na wafanyabiashara mbalimbali kwa nia ya kuwekeza na wameshindwa kuyaendeleza, ni vyema wakanyang'anywa na kugawiwa wananchi ili waweze kulima na kuyaendeleza katika mazao ya chakula. Mashamba hayo ni kama yale ya Mkonge Tanga na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuendelea kuvumilia kuangalia wakulima wakiumizwa na wafugaji bila sababu yoyote ya msingi. Hatua za kisera, kinidhamu zinapaswa kuchukuliwa kwa haraka na tatizo hili liangaliwe na kutatuliwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza zao la mahindi lionezwe bei kwa kilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri na yenye kutekelezeka. Hata hivyo ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, usemi uliopo tokea zamani kwamba "Kilimo ndio uti wa mgongo" huo ni ukweli na hasa nchi kama zetu ambazo ni masikini na ardhi ipo ya kutosha. Lakini bado uvivu umetawala kwa baadhi yetu kukimbia kilimo na kwenda Mijini. Serikali kwa kuongeza nguvu, imekuja na "Kilimo kwanza" kwamba Serikali imeona kwamba bila ya kutilia nguvu kilimo na kuzishirikisha sekta binafsi pamoja na kuwashamasisha vijiji ni kuendeleza shughuli za kilimo na Serikali kujikita katika kutoa ruzuku ya pembejeo ili kuongeza tija na uzalishaji na mazao ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri tena kwa hotuba yake katika ukurasa wa 43 hadi ukurasa wa 44 kwa jinsi Wizara ilivyoweza kuwashamasisha wakulima kwa kukubali kutumia zana za kilimo ili kupata tija ya mazao. Vilevile kwa kukubali kuwakopesha Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Umma waweze kukopa na kudhaminiwa na Waajiri wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba anayo dhamira nzuri ya kusaidia kilimo na kumsaidia mkulima, lakini baada ya kupatikana mazao shambani: Je, miundombinu ya kutoa mazao shambani, mbona mibovu? Sasa shirkiana na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu pamoja na Halmashauri kutengeneza barabara zilizo bora kutoka shambani hadi vijiji ili kuweza kufikisha mazao hayo sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli Mheshimiwa Waziri anajitahidi na hata hotuba yake imeweza kujieleza, lakini kuna baadhi ya shughuli zipo nje ya uwezo wake na upatikanaji wa barabara bora kutoka shambani hadi Vijiji. Hata hivyo, hata hilo lisimamiwe ili kumsaidia mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara hii isimamie bei za mazao yetu na pia kutafuta masoko ya mazao yetu ili kupusha kelele za wananchi, ingawa katika ukurasa wa 66 umeelezea hali halisi ya masoko nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa inayolima korosho Tanzania ni Lindi, Mtwara, Pwani, Morogoro, Ruvuma, Tanga na kadhalika. Mikoa hiyo inapata shida sana, kwani pembejeo huchelewa kufika, zao lenyewe halinunuliwi, vilevile Vyama vya Ushirika au Vyama vya Msingi husika vinawakandamiza wakulima. Serikali ifanye uchunguzi wa kina kujua kuna usiri gani ndani ya usambazaji wa pembejeo na ununuzi wa korosho, kupitia Vyama vya Msingi? Upo usiri unaokuwepo ndani yake, naomba majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili naomba Mkoa wa Lindi katika Wilaya zake tupate zana za umwagiliaji maji hasa katika Wilaya ya Ruangwa, kwani wana mito na mabwawa yanayofaa kwa *irrigation*. Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuendelea kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa tumbaku Kibondo wamekuwa wakisumbuliwa kwa kupangiwa bei ya chini na wakati mwingine wanakosa soko kabisa. Napenda kuishauri Serikali na kupata majibu, lini wakulima hawa wa tumbaku wataachwa kusumbuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mbolea ya ruzuku pamoja na mbegu imekuwa haiwafikii wananchi. Kuna utaratibu ambao unafanyika wa kuwalaghai wananchi kwa kuwapatia fedha ndogo ili wasaini vocha na kisha mbolea ile inakwenda kuuzwa Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vikao vya Kamati za Pembejeo Wilayani Kibondo vimeduwa vinafanyika bila Wabunge kujulishwa na hatupewi *documents* za maamuzi yaliyofikiwa. Naomba Serikali ifuatilie jambo hili. Kama Wabunge hatupo, basi Makatibu wetu waitwe na walipwe kama Wajumbe wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa Tarafa ya Mabamba – Kibondo, wamekuwa wakisumbuliwa sana wanapokwenda kuuza mazao yao Burundi kwenye mpaka wa Mkalazi, pia wanatozwa ushuru kinyume na taratibu, mfano mtu anakwenda kuuza mchicha na kadhalika, vitu vidogo vidogo lakini anatozwa ushuru, wakati TAMISEMI wamekuwa wanafafanua jambo hili mara kwa mara Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mawakala wa pembejeo za kilimo *walio-supply* mwaka 2011 Wilaya ya Kibondo, napenda kuishauri Serikali iwalipe Mawakala hawa kwani ni muda mrefu umepita na wanafilisika kwani walitumia fedha nydingi na mitaji mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali na kupewa majibu kwamba mwaka huu pembejeo zitafika kwa wakati kwa kuangalia misimu ya kila eneo la ukanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Serikali ifuatilie mradi wa Skimu ya Umwagiliaji Mugondogondo, kwani fedha zimetolewa na hakuna kinachoendelea. Mugondogondo iko Wilayani Kibondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mbegu bora za alizeti, wananchi wa Muhamwe wanapenda kuwa na zao la alizeti, kwani udongo wa Muhamwe unakubali zao hilo, hivyo Serikali iweke utaratibu ili wapate zao hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Umwagiliaji ya mwaka 2010/2011 na 2011/2012 Kibondo, haikutekelezwa ipasavyo. Naomba Serikali ifuatilie, kwani miradi hii inasuasua. Mfano, mradi wa uchimbaji bwawa la Misezero kwenye vijiji vya Twabagondozi, Bitale na Mradi wa Kahambwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali iweke utaratibu ulio wazi kwa wananchi kukopesha matrekti ya SUMA JKT kupitia Halmashauri, kwani mpaka sasa Halmashauri

hazijafunguka kusaidia jambo hili. Utaratibu wa Mkulima mmoja mmoja hauwezekani, kwani wakulima wengi hawana mitaji wala hati za kuweza kuwawezesha kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Naibu Spika, pole na majukumu. Pia hongera kwa kazi nzuri wewe na timu yako hapo Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, nirudie kukujulisha kama niliviyowahi kukuandikia barua juu ya kiwanda cha alizeti kilichopo kijiji cha Chibelela ambacho madhumuni yake ni kusindika mafuta ya alizeti. Kiwanda hiki kimefadhliliwa na *UNIDO* kwa gharama kubwa takribani miaka minne iliopita, na licha ya wananchi kushirikiana na *UNIDO* kwa kiwango cha hali ya juu, lakini hadi sasa kiwanda hicho hakifanyi kazi kama kilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo hilo, naomba atume mtaalamu akatembelee kiwanda hicho aone matatizo yake na baadaye Wizara ione umuhimu wa kusaidia kutatua matatizo ya kiwanda hicho ili kiweze kufanya kazi ya kuongeza thamani ya zao la Alizeti ambalo linalimwa kwa wingi na wananchi wa Chibelela.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusu Wilaya ya Bahi. Wilaya hii ni kame, lakini yenye fursa muhimu kwa kilimo cha umwagiliaji kama itapata uwezesajji katika suala zima la kilimo cha umwagiliaji hasa katika ujengaji wa mabwawa ya kuhifadhi maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Lakini sijaona mambo muhimu yaliyoandalila kwa Wilaya yangu ya Bahi kuwa sehemu muhimu ya uendelezaji kilimo cha umwagiliaji katika Kanda hii ya Kat. Naomba nipate maelezo ya kuridhisha juu ya jambo hili.

MHE. WILLIAM V. LUKUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 na mwaka 2010/2011 na ya mwaka 2011/2012, Mfereji wa Mlenge Pawaga ulipangwa kuendelezwa na mwaka 2010 Waziri aliwatangazia wananchi kwamba ingepeleka Shilingi bilioni 1.7 na uhamasishaji ukafanya. Mwaka 2011 Wizara ikaahidi itafanya kila linalowezekana ili mfereji huo upewe fedha, lakini hazikupelekwa. Nataka kujua mwaka huu zitapelekwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ipeleke timu ya Watalam kuchunguza mfereji wa Mlambalesi (Mlowa) ambao umewekewa karibu Shilingi milioni 900 lakini mfereji haujakamilika. Mfereji huo ulikuwa ukamilike kwa fedha chini ya Shilingi milioni 500. Kwa nini hizo zote hazijamaliza mfereji? Timu hiyo iainishe mapungufu yote na Wizara iweke mikakati ya kurekebisha ili kutenda haki kwa fedha za Serikali.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuunga mkono hoja na kuchangia baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hali halisi ilivyo ni kwamba, kwa Serikali kutotilia maanani uzalishaji wa mbegu hapa nchini, badala yake kuruhusu pesa ya ruzuku kufaidisha wazalishaji kutoka nje ya nchi kwa asilimia 75. Naiomba Wizara itilie mkazo uzalishaji wa mbegu kwa kutumia Taasisi zetu badala ya kufaidisha wazalishaji kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha pale ambapo kama Taifa, tunaingiza viuatilifu ambavyo ni *substandard* na kazi hii inapokuwa inafanya na Taasisi ya kuaminika kama *TPRI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mkurugenzi Mkuu wa *TPRI* achunguzwe, kwani ye ye kwa kushirikiana na Msajili kwa maslahi yao binafsi wamekuwa wakiingiza viuatilifu ilivyo chini ya kiwango kwa manufaa yao binafsi. Naiomba Wizara ichunguze uongozi wa *TPRI* pamoja na Msajili wa viuatilifu ili Taifa hili lisendelee kupata hasara kwa maslahi ya watu wachache. Menejimenti ya *TPRI* wamelazimika kujuzulu ili wasiwe sehemu ya uozo huu, lakini cha kushangaza Wizara hajashituka na hilo hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *irrigation schemes*, jambo lisilokubalika ni jinsi ambavyo miradi hii imekuwa ikichukuwa muda mrefu mno kabla ya kuanza kupata matunda yanayotokana

na miradi hii. Nimejaribu kupitia kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwa bahati mbaya nimeshindwa kuona miradi iliyoko Jimbo la Kalambo na Wilaya ya Kalambo.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Manaibu wake na Wakurugenzi wote kwa kuwasilisha bajeti nzuri na yenye matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuja na dhana ya Kilimo Kwanza kwa lengo la kuleta mapinduzi ya kijani nchini. Dhana hii ilizinduliwa takribani miaka minne iliyopita (3 Agosti, 2009) lakini utekelezaji wake hauonekani pamoja na nguzo zake kumi kubainishwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nguzo yake ya pili, Serikali iliahidi kugharamia Kilimo Kwanza kwa kutekeleza majukumu yafuatayo pamoja na mambo mengine ambayo ni kuongeza bajeti ya umwagiliaji kufikia hekta zisizopungua milioni saba na kwamba Serikali itaaniszisha mfuko maalumu wa fedha kwa ajili ya Kilimo kwanza. Utekelezaji wa haya yote umefikia wapi? Naomba nipate majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde la Mahenge na Ruaha-Mbuyuni linafaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji katika Wilaya ya Kilolo Mkoani Iringa kwa kutegemea mto usiokauka wa Lukosi. Eneo linalomwagiliwa kwa sasa ni takribani hekta 300 tu wakati eneo linaloweza kumwagiliwa ni takribani hekta 2000. Ombi langu kwa Serikali, naiomba ijenge miundombinu ikiwa ni pamoja na banio la Mgambalenga na Mifereji yake ili eneo kubwa zaidi liweze kulimwa kwa umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu tumesema tuna eneo la hekta milioni 44 zinazofaa kwa Kilimo na hekta milioni 29.4 ambazo zinazofaa kwa Kilimo cha umwagiliaji. Takwimu hizi ni za siku nyingi na kumekuwa na mabadiliko mengi. Hivyo ni vyema Serikali ikafanya tathmini mpya ili kufahamu ni eneo kiasi gani ambalo bado lipo kwa Kilimo cha umwagiliaji?

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia hotuba hii katika eneo la pembejeo, hasa kwa zao la korosho. Zao hili ambalo kwa sasa linazalishwa kwa wingi katika Mkoa wa Pwani na Mikoa mingine ya Kusini mwa Tanzania, kwa muda mrefu zao hili limekuwa kero kwa wakulima, kwani haliwanufaishi na badala yake linaendelea kuadumaza. Naomba Serikali iwasaidie wakulima hawa kwa kununua kurosho zote ama kutoa "guarantee" ili kuhakikisha kuwa wakulima wanalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa sasa imeshindwa kabisa kuwasaidia wakulima hawa kupitia Vyama vyao vya Msingi. Vyama vimekopa pesa katika Benki za *NMB* na *CRDB* kwa *Interest rate* ya asilimia 15 tangu Oktoba mwaka 2011. *Interest rate* hii itaongezeka hadi kufikia asilimia 21 ifikapo Oktoba, 2012. Naiomba Serikali ifanye kila liwezekanalo kuhakikisha kuwa hii *Interest rate* inalipwa na Serikali badala ya Vyama vya Msingi ili wakulima waweze kupewa fedha zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni namna ya kuwasaidia wananchi wa maeneo ya *Delta* kuweza kuwa na zao la biashara badala ya zao la minazi kufa. Zao hili ambalo kwa muda mrefu limekuwa likifanyiwa utafiti, lakini hadi sasa hakuna mafanikio yaliyopatikana. Kwa kuwa eneo hili la *Delta* lilikuwa na minazi mingi ambayo kwa sasa imekufa, wananchi wamehamasika kulima zao la michikichi na wanahitaji mbegu (200,000).

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ikishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ili katika msimu ujao wa mvua za vuli hapo Oktoba/Novemba, 2012 waanze kuotesha vitalu vya miche. Kwa kufanya hivyo, tutawasaidia wananchi kuwa na zao la kudumu.

MHE. DKT. FENELLA E. MUKANGARA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza kabisa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri nafasi ya vijana katika kipaumbele cha Kilimo Kwanza hapa nchini, ni muhimu ionekane wazi kimatendo. Nia hiyo ionekane katika mipango na utekelezaji unaogusa vijana wa aina zote, wasomi na wasio wasomi. Wizara yenye dhamana na vijana ikishirikiana na Wizara ya TAMISEMI, Ardhi na Kazi, Kilimo; kazi hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kutambua vikundi mbalimbali nya vijana upo, unaendelea na unaratibiwa na Idara ya Vijana kuitia Afisa Vijana wa TAMISEMI. Nashauri Wizara ya Kilimo itoe kipaumbele cha makusudi katika kuhakikisha usalama wa chakula wa kupata mtazamo chanya na vijana. Wizara ya habari, vijana utamaduni na michezo tayari inafanya hivyo kuitia Wilaya, Mikoa na TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri *awareness raising* kwa jamii kuhusu umuhimu wa kilimo na hasa nafasi ya vijana katika hili "The National campaign", uwepo ushirikiano wa karibu baina ya vijana (hizi Idara/sekta mbili) pamoja na Idara yenu ya Habari, Kilimo, ione kane wazi kufanya hivyo, hasa kwa nia ya dhati ya kufikisha elimu na kufikisha habari sahihi za kuhamasisha wananchi hasa vijana katika kupenda kilimo na kuhakikisha tunajenga usalama wa chakula nchini, na vijana wanakuwa mstari wa mbele katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kwa dhati kazi nzuri itakayofanywa na Wizara na Watendaji. Mengi niliyoyazungumza na Mheshimiwa Waziri aliyetoka nayaona yanafanyiwa kazi hasa yanayolenga vijana. Ni kuboresha na ku-link vizuri tu kunahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata maelezo ya Serikali kuhusu mafao ya waliokuwa wanachama wa Vyama nya Ushirika, Wilaya sita za Mikoa wa Morogoro ambao mpaka leo hawajalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo na wakulima wadogo na wakubwa wachache Mikoa wa Morogoro hususan Wilaya ya Kilombero, napenda kupata majibu ya Serikali: Je, ni Maafisa ugani wangapi wameajiriwa na kupelekwa Mikoa wa Morogoro na idadi ya waliopolekwa Kilombero? Je, Maafisa ugani wangapi hawajaajiriwa na kwa nini hawajaajiriwa? Ni kwa sababu waliopo kazini wametosha!

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuanzia ukurasa wa 86 hadi 87 na katika ukurasa wa 149 inaelezea, Wilaya ya Kilombero na mwekezaji wa Kampuni ya KPL na uzalishaji wa mpunga. Hotuba inasema ameanza na siyo kwamba ameanza, bali anaendelea, kwani ni miaka mitano sasa tangu mwaka 2008 hadi sasa mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, kama wanaendelea kupata faida, wananchi wa vijiji viliviyotajwa katika hotuba viliambulia kupata elimu na siyo kweli wameongeza uzalishaji kwa kuwa baada ya kupata elimu hawakuwezesewa hata kwa mkopo wa masharti nafuu ili wapate zana za kisasa za Kilimo. Pia wananchi wahapimiwi ardhi yao na kumilikishwa mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilombero pamoja na kutajwa sana katika kilimo, lakini wananchi wa kilombero walio wengi hawajui kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba ufanuzi.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nzungumzie kuhusu zao la kahawa. Mezani kwa Waziri kuna malalamiko makubwa yanayohusu *KCU*. Hoja yangu ni kwamba, kwa nini Serikali haichukui hatua kwa bei ya kahawa; kahawa hainunuliwi kwa wakati na kwa taslimu bali kukopwa; Uwazi katika Menejimenti ya *KCU*; na Waheshimiwa Wabunge kutokukubaliwa kuingia katika Mikutano ya *KCU*. Tunaomba majibu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyetembelea Mikoa wa Kagera na alipofika Missenyi alisema kuwa tutaingia katika Umoja wa kupata ruzuku ya pembejeo. Tunapenda kueleza kuwa bila kupata pembejeo, hatuwezi kuzalisha na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alikiri kuwa tutakuwemo, na Wanamisenyi wanataka majibu.

MHE. RAJAB M. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia kwa mwaka huu wa fedha, bajeti kwa ajili ya matumizi ya kawaida imeongezeka toka Shilingi billioni 152.41 mwaka 2011/2012 hadi Shilingi billioni 170.364 sawa na ongezeko la asilimia 11.78. Wakati matumizi ya kawaida yakiongezeka, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo imepungua toka Shilingi bilioni 105.94 mwaka 2011/2012 hadi Shilingi billioni 67.260 sawa na asilimia 57.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpangilio huu wa kuongeza fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida, huku bajeti na maendeleo ikipungua, tena kwa kiasi kikubwa, ni kuhujumu ufanisi wa kilimo katika Taifa letu ambapo asilimia 80 hutegemewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafikiria nini kuitesa na kuihujumu Sekta ya Kilimo iliyo tegemeo la Watanzania walio wengi? Nafikiri Serikali imeamua kudidimiza kabisa Sekta hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni baya zaidi ni utegemezi wa bajeti ya maendeleo. Kitabu cha Waziri Sh. 14,937,000,000/= ni fedha za ndani na Sh. 52,323,154,000/= ni fedha za nje. Huu ni utegemezi mkubwa sana kwa nchi inayojitahidi kujikwamua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nahitimisha kwa kuitaka Serikali ifikirie upya kuhusiana na nia yake ya kuinua Kilimo. Pia Serikali ione yenye jinsi inavyoweka rehani nchi kwa kupuuza sekta hii inayobeba Watanzania walio wengi.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua uhalali wa viwanda vyote vya Ushirika vya kuchambua pamba ndani ya Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Mara (kwa sasa kimefilisiwa) mali zake kuendelea kuwa chini ya mufilisi zaidi ya miaka 17, ni sera ya namna gani hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MBAROUK SALIM ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikisisitiza ubia kati ya sekta binafsi na wakulima wadogo. Ubia huu mara nyingi sana umekuwa siyo mzuri kwa wakulima wetu wadogo, kwani wanachoambulia mwishoni ni kupoteza mashamba yao. Tusipokuwa makini, tutaendelea kushamirisha ukoloni mamboleo sisi wenyewe na kuendelea kuwa masikini karne hadi karne. Hakuna tofauti yoyote ya ubia wa sasa na ukoloni wa zamani ambaao ulihusisha unyakuaji wa rasilimali za Waafrika ikiwepo ardhi. Wawekezaji wanapokuja na kunyakua ardhi kwa kigezo cha ubia, ni kuza uhuru wetu na utu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima ifike mahali tukatae kudhalilishwa na kunyang'anya ardhi yetu, kwani wakulima wetu wakishapoteza ardhi, kilichobaki ni umasikini kwao na vizazi vyote vinavyofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012 umeacha viporo vingi sana ambavyo havieleweki namna itakavyokamilishwa ikizingatiwa bajeti ya mwaka huu imepungua kwa ujumla wake. Viporo hivi vitaifanya sekta hii na nyingine nyingi kufilia/kudorora na hatimaye kuleta athari mbaya katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Serikali ilione hili na kulifanyia kazi, pia itambue Sekta ya Kilimo ndiyo mhimili mkuu wa Taifa lolote, kwani bila kilimo, hakuna chakula (njaa), hakuna viwanda, hakuna maendeleo, hakuna utulivu/amani na hakuna maisha.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Kilimo haijatengewa fedha za kutosha kwa madhumuni ya kuongeza tija na kipato, na uzalishaji wa chakula na mazao mengine. Mgao wa matumizi ya kisekta unaonyesha kuwa Sekta ya Kilimo ilitengewa asilimia 2.92 mwaka wa fedha 2010/2011 na asilimia 1.65 mwaka 2011/2012. Kwa muda wa zaidi ya miaka 20, sekta hii imekuwa ikitengewa chini ya asilimia tano ya matumizi ya Serikali, wakati makubaliano ya nchi za SADC ni kutenga angalau asilimia 10 ya matumizi kwenye kilimo ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na kupunguza umasikini uliokithiri vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya Kilimo imekuwa kwa asilimia 3.6 wakati ongezeko la watu linakadiriwa kuwa asilimia 2.9. Nafasi muhimu katika kuleta mapinduzi ya kilimo ni katika maeneo ya utafiti wa Mbegu bora, Mbolea inayofaa kwa mazao katika maeneo mbalimbali na madawa, huduma za ugani na elimu kwa wakulima, miundombinu ya umwagiliaji, maji na usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara imetengwa kabisa na mpango wa Kilimo wa SAGCOT, lakini unapotaja Mikoa ya Kusini hutaacha kutaja Mikoa hiyo. Serikali kupitia Wizara hii, ielete wananchi wa Mikoa hii, mpango gani wa maendeleo wa kilimo umetengewa Mikoa hii na pia kwa kuwa Wizara na Serikali imetenga Mikoa hii iwaeleze wananchi kuwa Mikoa hii ipo ukanda gani wa nchi au ni Taifa gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii imelenga Lindi na Mtwara katika kuipa Mikoa ya Kusini kipaumbele katika miundombinu ya umwagiliaji. Ikizingatiwa kuwa kuna mabonde yanayotirisha maji tokea enzi ya Adamu na Hawa kuanzia Bonde la mto Rufiji, Matandi, Mbwemkuru, Lukuledi, Lumesule mpaka Ruvuma. Je, Serikali imepanga Mikoa ya Kusini ijhusishe na Kilimo cha aina gani, ukiangalia kuwa korosho imekuwa ikiwakumbusha wananchi wa Mikoa hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upatikanaji wa pembejeo kwa Mikoa hii, bado ni mdogo. Mpaka tunachangia bajeti hii *Sulphur*, maeneo mengi haijapatikana. Pembejeo hazipatikani kwa wakati. Vocha zimekuwa zikiliwa na wanaopewa majukumu ya kufikisha kwa wakulima, madawa ya kupulizia korosho hubadilishwa kila mwaka. Leo *Sulphur* ya unga, kesho ya maji, keshokutwa Bifidan, mara inakubalika toka Arabuni, mara bora ni ya Tanzania, mara ya Naliendele (Mtwara) na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati kila msimu, hususan *Sulphur*? Serikali imewachukulia hatua gani Watendaji waliohusika na ubadhirifu wa vocha kwa wakulima vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itangaze dawa bora ya upuliziaji mikorosho badala ya kuifanya itoe matoleo mapya kila msimu. Pia Serikali ielete mpango wa Wizara na Serikali kuhusu Mradi wa Kilimo cha Maksai uliopangwa kuanzishwa katika Kata ya Mingoyo (tokea ilipokuwa ndani ya Halmashauri ya Wilaya). Kadhalika, Serikali ielete kupitia mgogoro wa wanakijiji wa Mkwaya na mamiliki wa Kampuni ya *African Blackwood* wametengewa maeneo gani ya Kilimo wakati suala lao linashughulikiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwendelezo wa Kilimo cha ufuta katika Kata ya Mingoyo Kijiji cha Mkwaya, mpaka sasa kuna mpango gani wa kuendeleza zao hilo? Naomba Serikali ielete mamlaka za kisheria zinazovipa Vyama vya Ushirika vya Msingi na Vikuu kulazimisha kuuziwa mazao kutoka kwa wakulima hata kama wakulima hawaoni faida ya Vyama hivyo.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuchangia hapa leo. Napenda kuishauri Serikali kwanza kabisa kwa namna walivyopanga bajeti ya Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika hawajaitendea haki. Kila mwaka badala ya kuongeza bajeti ya Sekta hii, inazidi kushuka. Fedha ya Maendeleo iliyopangwa ni ndogo sana na kuwa sehemu kubwa, asilimia 80 ni bajeti tegemezi kutoka fedha za wafadhili wa nje. Wataalamu wa Wizara hii wana mikakati mizuri sana na inayoweza kuleta mabadiliko na mapinduzi kiuchumi katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ingeangalia namna ya kuongeza fedha ya maendeleo katika bajeti ya kilimo nchini. Fedha hiyo kidogo inayopangwa pia haifiki kwa wakati, kilimo kinategemea msimu, kuchelewesha fedha za maendeleo ni kukwamisha kilimo kwa ujumla. Serikali haiwatendei haki wakulima wa nchi hii ambao ni asilimia 80 ya wananchi wote na pia ndiyo watumiaji wa bidhaa mbalimbali inayozalishwa nchini na inayotoka nje ya nchi (*consumers*). Tunashauri Serikali kutunga Sheria ya VICOBA ili iweze kuwasaldia wakulima wengi nchini. Wakulima wenyewe mitaji midogo wamejunga na VICOBA lakini hawatambuliwi kisheria, inawanyima wakulima walioko katika VICOBA kukopa katika Taasisi za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii bado tunaagiza chakula na bidhaa zinazoweza kuzalishwa hapa nchini, mfano ni matunda ya zabibu, *apples, peaches*, bidhaa nyingine ni *juice* ya matunda, *tomato source, chilli source, tomato paste*, mboga mboga za kwenye makopo, (*canned veg and beans*), hii ni mbali na bidhaa za mifugo. Hata hivyo, viungo vingi leo hii vinatoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tuishauri Serikali itimize ahadi yao ya kuondoa kodi ya vipuri nya matrektta ambayo Bunge hili Tukufu ilishapitisha, lakini Serikali pia iliahidi kuondoa katika bajeti hii ya mwaka 2012/2013 kodi mbalimbali inayogusa vipuri nya umwagiliaji, trela za trekta, tairi ya trekta, sahani za jembe na kadhalika. Pili, Serikali iangalie namna ya kuondoa ushuru wa mazao ambayo umekuwa kero kwa wananchi na wakulima, mwisho wa siku mzigo wa ushuru huo ambao mfanyabiashara anatakiwa kulipa, analipa mkulima sababu bei ya kununua inashushwa kwa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali iangalie namna ya kuhakikisha Mfuko wa Pembejeo na dirisha la kilimo katika Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*) iweze kuwafikia wakulima wa vijijini, wapate hatimiliki na elimu juu ya ujasiriamali. Mifuko hii kwa sehemu kubwa haiwafikii wakulima na vikundi vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru SUMA JKT kwa kuleta matrektta na kukopesha wakulima. Naipongeza Serikali kuteremsha bei na kuongeza muda wa kulipa deni na punguze la malipo ya awali. Aidha, tunaishauri Serikali iteremshe bei ya zana zake, majembe, mabarrow, trela, *powertilla, planter* na pampu za maji. Tunaomba SUMA JKT pia iendelee kuleta matrektta mengine na vipuri kuuzia wakulima pia vifaa au zana nyingine ambazo hawajaleta kama *combine harvesters, planter* za mpunga na nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri Taasisi za Elimu inayotoa elimu ya kilimo na usindikaji wa mazao yake chini ya Wizara husika. Leo hii Wizara ya Elimu haioni umuhimu wa Taasisi hizi. Wanapopanga bajeti ya Taasisi hizi wanatoa kwa usawa na Taasisi hizi hizi kushindwa kufanya vizuri, mfano ni *SUA*. Leo hii hawana zana za kilimo za kufundishia wataalamu wa kilimo, Maabara hazitoshi na pia hawana mafungu katika bajeti ya kufanya masomo kwa vitendo vijijini au kwa wakulima, ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri suala la elimu juu ya ushirika liendelee kutolewa na Serikali. Wananchi bado wanadhania ushirika ni ule ule ambao uliwaflisi huko nyuma. Nchi zilizopiga hatua zimeweza kufanikiwa kwa kutumia ushirika, mfano India, Ushirika wa 'Amul' katika Sekta ya Maziwa umeweza kukomboa wafugaji nchini India, wanaanza katika uzalishaji hadi kufikia masoko *end to end*. Pia wamefanikiwa katika Viwanda nya Sukari nya Ushirika. Wakulima ndio wanamiliki viwanda ambavyo vinaendeshwa na wataalamu kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nielekeze ushauri wangu Manyara na Jimbo la Babati. Tunaishauri Serikali iangalie suala la uzalishaji wa mbegu nchini. Mkoaa wa Manyara ndio unaongoza kuzalisha mbegu mbalimbali Kanda ya Kaskazini na Kati. Tunaweza kuwa wazalishaji namba moja kitaifa, kama Serikali itaweka mkono wake Mkoani Manyara, Wilaya ya Babati. Tunaweza kuwa *seed basket* ya nchi. Tuna Kampuni nne hapo Babati na Makampuni kumi na mbili wanapanda mbegu Babati kwa mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna uzalishaji wa sukari Babati. Kiwanda cha *Manyara Sugar* wanazalisha tani 10 hadi 15 kwa siku kwa miezi minne, wanawenza kuzalisha tani 50 kwa siku kwa miezi minne, kama Serikali itawenza kuweka mazingira bora kwa kuandaa miundombinu ya barabara, umeme na miundombinu ya umwagiliaji, kuna eneo katika Bonde la Kiru ambako kuna uzalishaji wa miwa katika mashamba ya mkataba, wananchi au wakulima wadogo wadogo hawazalishi miwa; wakiwezeshwa basi kiwanda kitawenza kuzalisha sukari kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna uzalishaji wa mpunga katika bonde hilo hilo. Tunaomba Serikali itimize ahadi ya kuchimba visima 15 katika bonde la Kiru pamoja na kujenga vianzio katika eneo la Masware, Shaurimoyo na Kisangaji ambazo zilikuwa katika mpango wa Serikali. Pia bonde hilo lina uwezo mkubwa wa kuzalisha matunda mbalimbali kwa ajili ya soko la

ndani na nje. Ndizi, machungwa, machenza, ndimu, *apples, pears, peaches*, tikitimaji na matunda ya aina mbalimbali. Pia kuna uzalishaji mdogo wa viungo kama binzari, pilipili, tangawizi na maua, pia vitunguu saumu na vitunguu maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishauri Serikali na hasa Wizara ya Kilimo, ije Babati Vijijiini kuangalia fursa zilizopo na hatua tuliyopiga katika kilimo cha kisasa. Tunaweza kufungua fursa na chapter mpya katika Wilaya ya Babati na kwa manufaa ya Taifa katika uzalishaji wa mbegu, sukari, matunda, na mazao ya viungo, na mazao ya biashara ambayo yanasisika Tanzania na duniani, mfano, mbaazi, ngwasa, kahawa, pamba, alizeti, ngano, shayiri, pareto, mpunga na kadhalika. Pia kuna ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na nyama, kuku, mbuzi na mifugo mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, tuna kiwanda cha *Minjingu feltilzer Co.* ya Babati, tunaomba mbolea hiyo ipewe kipaumbele na Serikali. Ni mbolea iliyopimwa na ina ubora wa kutosha sawa na DAP. Tunashauri Serikali iangalie namna bora ya kuanzisha kiwanda cha mbolea ya UREA au Ammonium nitrate. Tukiunganisha mbolea hiyo na ya Minjingu, tuunganishe na madini yaliyopo nchini, tunaweza kuzalisha kila aina ya mbolea na tukawa tuna export mbolea nchi za jirani na nyingine, badala ya kuwa importers. Leo hii ruzuku ya mbolea na mbegu sehemu kubwa inanufaisha nchi za nje na siyo Watanzania, kwa sababu tunaagiza mbegu na mbolea kwa asilimia 70 nje. Tunaomba suala la vipuri vya matrekta, tairi za matrekta, trela na vipuri vya umwagilaji viletwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate majibu.

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuchangia bajeti hii kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni ugonjwa wa migomba, mnyauko. Ugonjwa huu umeathiri sehemu kubwa ya migomba Mkoani Kagera. Ugonjwa huu umesababisha uharibifu mkubwa wa migomba, chanzo kikuu cha chakula na kupelekeea njaa. Mbaya zaidi, ugonjwa huu umeanza kushambulia malando magimbi na hata miti itoayo matunda. Hali hii ni mbaya, ni janga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali na hata watu binafsi kwa juhudhi zao wamejithadi kutambua chanzo cha ugonjwa na namna ya kuukabili. Napenda niieleze Serikali yangu kuwa ugonjwa huu unafahamika kwa marefu na mapana yake. Hoja hapa ni namna ya kuondoa na kuzuia usienee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uzoefu wa nchi, mfano Uganda, ugonjwa huu umedhibitika. Muhimu hapa ni nguvu na ushiriki wa Serikali hapa ni kuwa wagani, watendaji na viongozi wa Vijiji na Serikali wanashirikiana na wananchi kuharibu migomba yote iliyoathirika. Wananchi wanaelekezwa kuzuia kuenea kwa vifaa kuwa *sterilized* kwa moto au *breach*, imo *chemical - JJK*. Vinakuwepo vikundi vya kilimo ambapo kwa kila Kitongoji kuna timu mbili au tatu za vijana wanne. Hawa kazi yao ni kutembelea mashamba na kutambua kama kuna maambukizi mapya baada ya operesheni nilioitaja juu, chini ya taratibu na sheria za Serikali. Timu hizi zina mamlaka ya kumlazimisha mkulima kuharibu maambukizi mapya, hapa ndipo Serikali inapotakiwa kuzingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi yangu ni kwanza iundwe timu ya Serikali Makao Makuu ya Wizara, Sekretarieti ya Mkoa na Wilaya. Timu hii ipate nguvu ya Halmashauri na ya Mkuu wa Wilaya. Pili, kwa kushirikiana na Serikali za Kata na za Vijiji, utaratibu nilioupendekeza hapa ufuatwe. Tatoo, Serikali itoe ruzuku kwa kuwapa JJK bure ili kwa matendo waandae vifaa na kuzuia maambukizi ya ugonjwa huu. Nne, Tarafa tatu za Jimbo langu Izindo, Kamachumu na Nshamba zitumike kama jaribio la mafanikio. Kimsingi, watu wa maeneo yanayolima migomba wamekwishaelewa tatizo hili. Baada ya miezi mitatu ya operesheni kali kwenye Jimbo langu, Wilaya ya Muleba ivamiwe na kwa mafanikio yatakayopatikana, tuokoe Mkoa mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Sekta ya Kahawa, zao hili ni chanzo kikuu cha fedha lakini sasa tumpata tatizo kubwa kutokana na uendeshaji wake. Kahawa ni moja ya mazao yanayoliingizia Taifa fedha za kigeni, hata hivyo ni dhahiri kuwa Serikali na KCU hawana

msaada wa maandalizi katika kuhamasisha kilimo cha kahawa. Serikali imejipiga risasi miguuni kwa kutelekeza zao la kahawa:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kueleza kwamba Bodi ya Kahawa inachelewa kufungua minada hali inayotoa mwanya kwa walanguzi toka Uganda kununua kahawa kwa bei nafuu. Pia Bodi/Serikali inaruhusu Makampuni ambayo yanashiriki kwenye minada ya Shule mpaka kwa wananchi kununua kahawa, hali inayodhoofisha ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, *KCU* kwa mawasiliano na Bodi iliwatangazia wakulima bei ya kahawa, lakini kabla hata ya mnada kufunguliwa, bei imeshuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Serikali kupitia Idara ya maendeleo ya ushirika na hapa chombo cha ukaguzi na Mrajisi wanalea magonjwa katika Chama cha Ushirika Kagera (*KCU*) ilhalilwananchi wakilia kwa mateso. Kwa dalili hizi, *KCU* ikifa sitashangaa na mchana wa saa 6.00 nitasema Serikali imehusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie suala la miradi ya umwagiliaji Mkoani Kagera na hususan Wilayani Muleba. Pamoja na dhamira nzuri ya kuendeleza miradi hii, ipo haja ya kusimamia utekelezaji wake, nakiri kuwa nina mashaka na ufanisi katika utekelezaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe ushauri juu ya kuendeleza kilimo cha biashara kwa Mkoa wa Kagera. Kutokana na jitihada ya mahali tulipo, Serikali itawezesha ili nguvu ya soko, *demand driven incentive* ichangamshe kilimo cha biashara Kagera. Nimelizungumza hili kwenye *RCC* na kwenye bajeti ya Waziri Mkuu. Hata hivyo, msimamo wa Serikali ni sahihi, lazima turuhusu mazao ya Kagera yauzwe nchi jirani ili kupanda kwa bei kuchochee wananchi kuwekeza katika kilimo, mazao kama *ovacardo*, mihogo, ndizi, alizeti, mchele yanaweza kujitafutia soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuiomba Serikali yangu ifikirie ombi langu la kushirikiana nami katika kupambana na ugonjwa wa mnyauko wa migomba.

MHE. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo ni uti wa mgogo. Ni muhimu Serikali kuwa na mikakati na mpango mahsus ikuendeleza kilimo. Wakulima wadogo wadogo ndio hasa wanaozalisha mazao ya chakula, mbolea, madawa na pembejeo nyingine ziwafikie kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji ndiyo mkombozi wa Kilimo nchini. Mageuzi ya Kilimo yatapatikana tukikuza na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Skimu za umwagiliaji za Mwamapuli, Itumba, Buhekela, Choma, Igumbi Wilayani Igunga ziendelezw. Suala la bei ya pamba ni muhimu likashughulikiwa. Madhara ya bei ya Sh. 660/= kwa kilo ni makubwa kwa wakulima na Hamashauri zinazotegemea sesi (*Cess*) ya asilimia tano kutoka kwenye bei ya pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kwa mfano ilikuwa na matokeo ya bei ya Sh. 800/= kwa kilo na kutegemea pato/mapato ya Shilingi bilioni mbili, kwa bei ya Sh. 660/= kwa kilo, Halmashauri itapata chini ya Shilingi bilioni moja. Hii inaathiri sana bajeti ya Halmashauri hiyo. Serikali itoe ruzuku ya bei angalau ifike Sh. 800/= kwa kilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Ginery* ya Chome iliyouzwa kwa mwekezaji iliachwa ikaharibika wananchi wakakosa ajira. Naishauri Serikali ifufue *Ginery* hiyo. Waziri atembelee *Ginery* hii na kujionea uharibifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Igunga ina mahitaji ya tani 8,575 ya nafaka. Naomba Serikali ipeleke chakula katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, na naunga mkono hoja.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Naomba utakapokuwa unafanya majumuisho yako, unijibu ni namna

gani vikundi vya *SACCOS* vya Nzega nilivyovitengeneza na kuviwezesha vitapata mikopo ya matrekta na pia, je, Serikali iko tayari kutuletea mbegu za alizeti kwa wananchi wa Nzega kwa bei ya ruzuku?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mbolea za ruzuku kwa ajili ya mazao ya mpunga, pamba na mahindi, ni kwa nini watu wa Nzega hatupati? Binafsi, nimeanzisha kule Nzega Miradi ya Kilimo cha Kisasa cha Alizeti (*Balimi Revolution Project*) na pamba (*Nzega cotton project*): Je, Serikali ina *complement* vipi jitihada zetu hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, embe zinastawi sana Nzega na Mkoa mzima wa Tabora na takribani kila Kaya inapanda na kutunza miembe miwili mitatu. Lakini bahati mbaya sana wanalima miembe kwa mbegu za kizamani na kwa kuona mbali na uwepo wa soko la uhakika la Kampuni ya Azam na zile za Wakanya, watu wa Nzega na Tabora kwa ujumla tunadhani tukipanda miembe ya kisasa ya *SUA*, tutaleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi kwa wananchi. Je, Serikali ipo tayari kutuletea mbegu za miembe ya kisasa toka *SUA* kwa bei ya ruzuku ili mpango wetu wa kuhamasisha kila kaya kulima miembe ufanikiwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iongeze tofauti ya bei katil ya ile tarajiwa ya wakulima na ile iliyopo sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, mara kwa mara Serikali imejenga desturi ya kuingilia kati bei ya mazao ya wakulima. Kwa upande mmoja, inaweza ikasaidia kudhibiti uholela unaoweza kujitokeza katika biashara ya mazao hasa ya chakula. Kwa upande wa pili wa Shilingi inaweza ikawanyima wakulima uhuru wa kufurahia matunda ya kazi zao. Mfano hai katika hii ni kuwakataza wakulima wasiuze bidhaa zao nje ya nchi kwenye soko/bei nzuri. Serikali kwa kufanya hivi, imeshindwa kuelewa kuwa hatua hii haina manufaa kwake wala kwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa kuhusu suala hili ni kuwaruhusu wakulima kuuza mazao katika nchi za jirani kwenye bei nzuri. Hii itasaidia kuwapa wakulima ari na moyo wa kulima mazao zaidi, lakini pia wainuke kiuchumi na kuondokana na umaskini. Pia Serikali iweke utaratibu mzuri wa kimkakati kuvuna utajiri kutookana na mazao ya chakula kwa kuuza mazao haya nchi za jirani mfano Kenya yenye upungufu mkubwa wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuagiza mbegu kutoka nje tena kwa asilimia zaidi ya 70 ni fedheha, tena kubwa ambayo inatia kinyaa. Kitendo hiki kinawenza kuleta tafsiri kuwa huenda tunawaabudu watu wa nje na kutimiza maslahi yao huku tukiwakandamiza watu wetu wa ndani. Kwa nini tuisitumie fursa ya Vyuo vilivypopo kama *SUA* na vingine pamoja na wataalam walipo kutengeneza mbegu zetu wenywewe? Kila mwaka Serikali inasomesha wataalamu wengi, lakini hawawatumii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isipobadilika, italeta majanga mengi katika Taifa letu.

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu itaendelea tu pale ambapo mapinduzi ya viwanda yatafanikiwa ili tusiwe tegemezi kwa zana muhimu za maendeleo. Nchi yetu imebarikiwa kuwa na ardhi kubwa na nzuri ambayo inaruhusu kilimo cha zao la aina yoyote. Hivyo basi, mapinduzi ya viwanda kwa nchi yetu yanapatikana ndani ya mapinduzi ya kilimo: viwanda vya kutengenezea, kubuni na kuunda nyenzo za kulimia kama matrekta, mbolea na kadhalika; nyenzo ambazo zitalimia mashamba kuzalisha mbegu bora, kuwekea miundombinu ya umwagiliaji ili mazao yapatikane mengi kwa tija kubwa kwa sehemu ndogo ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile viwanda vinahitajika kuyaboresha mazao yapatikanayo mashambani kuwa bidhaa za thamani kama vile pamba kuwa nguo, matunda kuwa *juice*, katani kuwa kamba na kadhalika. Ni dhahiri basi, mapinduzi ya viwanda yamo ndani ya mapinduzi ya kilimo, kabla na baada ya kulima. Hivyo basi, kilimo kinahitaji msukumo mkubwa kitengewe pesa za kutosha katika bajeti na kutekeleza mipango ya kukiendeleza kwa dhati.

Kilimo ni shughuli ya nchi nzima, hivyo msingi uwe kuiwezesha kila Wilaya kuweza kuwa na kiwango cha juu cha kujitosheleza kwa mazao yanayolimwa humo na mazao mengi yanamea katika kila sehemu. Isitoshe tayari kuna mimea ambayo imekubalika tangu zamani kulimwa sehemu mbalimbali kama vile katani, minazi, mihogo, korosho, matunda na kadhalika katika Wilaya ya Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iamue kwa dhati kuwa itashughulikia na pia kujihusisha moja kwa moja kwenye ukulima wa kuiwezesha kila Wilaya kuwa na kiwango cha msingi cha mazao. Baada ya hapo, kuwe na msukumo wa kuzalisha mazao ya ziada katika sehemu maalumu kama vile inavyofanyika kwa mpango wa kukuza kilimo katika ukanda wa kusini mwa Tanzania - SAGCOT. Hili litendeke katika kila Ukanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo ni lazima tuamue na tutende. Mwendo wetu wa kutenda siyo wa kasi ya kuridhisha. Mwaka 2006 tulianzisha programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo lakini yale yaliyomo kwenye programu hiyo ambayo ilitakiwa ihusishe kila Wilaya. Kwenye Wilaya yangu ya Tanga, halionekani linalotendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pembejeo za ruzuku hazipo, faida za utafiti wa mazao hazionekani, huduma za ugani ni za kususua na mashamba darasa hayapo, hayaonekani, zana bora za kilimo na umwagiliaji haziletwi kiasi ambacho hata *powertiller* zilizopangiwa Wilaya hii ni tatu, wakati lengo ni 35 kwa kila Wilaya. Umwagiliaji ni sufuri!

Mheshimiwa Naibu Spika, yote haya yanaonyesha jinsi Wilaya ya Tanga ilivyosahauliwa katika kilimo, wakati Wilaya hii ina kila viashiria vya kulipatia Taifa pato kubwa kutohana na kilimo. Badala yake mwaka 2010 na 2011 Wilaya hii imekuwa na upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyenzo ambazo Wilaya ya Tanga inahitaji kwa sasa ni pamoja na matrekti ambapo kwa bahati, matrekti ya SUMA JKT yapo, hivyo ningeomba tupatiwe matrekti 20 kwa Kata za ukulima kumi ambazo ziko katika Wilaya hii. Mbolea, mashamba darasa pamoja na Maafisa Ugani pia yanahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Tanga ina Kata 14 vijiji na Kata 10 za shambani. Dhana ya kuwa Wilaya ya Tanga ni Jiji la Tanga na kwa hiyo, hakuna ukulima; ni dhana mbovu inayostahili kuondolewa, kwa kuwa na Halmashauri tatu, yaani Tanga Mjini, Tanga Kaskazini na Tanga Kusini ili Kilimo kipate msukumo unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana Halmashauri ya Wilaya yote ni moja, na hata hivyo, moja haina Mkurugenzi tangu Mei, 2010 hadi leo. Sasa tutegemee nini kama hata Uongozi wa Halmashauri hakuna? Kuna kukaimu tu na kutojamini. Haya ni mambo ya msingi ambayo kama hayakurekebishwa, kilimo kitazidi kudorora Wilayani Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkonge ni zao ambalo liliifanya Tanga ishikilie uchumi wa nchi hii miaka ya 50 hadi 70. Leo hii limetekelizwa pamoja na kuwepo juhudzi za kulifufua, bali juhudzi hizo hazitoshi. Kasi zaidi inahitajika. Hata hivyo, naishukuru Serikali kwa kuanza taratibu ya kuyatwaa mashamba ya mkonge ambayo yametekelezwa na wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufufuaji mashamba ya mkonge yaendane sambamba na uongezaji tija katika mashamba hayo kwa kutumia ardhi ndogo kwa uzalishaji mkubwa ili baadhi ya mashamba haya yatumike kwa masuala mengine, kikiwemo kilimo cha mazao mengine. Upanuzi wa Jiji la Tanga tayari unachukuwa sehemu ambazo hapo awali zilikuwa mashamba, hivyo hili linahitaji kupangwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao lingine ni nazi ambalo ni bidhaa muhimu kwa mafuta, nalo pia limesahuliwa kiasi ambacho halikuorodheshwa kabisa kwenye orodha ya mazao ya mafuta. Mashamba ya minazi yanakufa na hakuonekani jitihada zozote za kuyafufua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyenzo zinazohitajika kufufua mkonge na minazi zipo, ardhi ya mashamba hayo yapo, miundombinu kwenye mashamba ya mkonge ipo, kinachohitajiwa ni watendaji imara kwenye Halmashauri na maelekezo chanya ya Serikali.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hoja iliyo mbele yetu kwa kusema machache. Kwanza, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa ambayo inafanya kwa Taifa hili. Pia naomba kwa Serikali kuititia Wizara hii, kuendelea kutoa pesa kwa skimu za umwagiliaji katika Mkoa wa Morogoro ambazo zimeombewa fedha na Mkoa ili kukamilisha adhma ya Mheshimwa Rais kuufanya Mkoa wa Morogoro kuwa ghala la Taifa la chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara kwa kutupatia pesa za umwagiliaji kwa skimu ya Mbalangwe na Kongwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Sh. 250,000,000/- kila skimu fedha ambazo zimefanya kazi kubwa hasa Skimu ya Mbalangwe, kazi imekamilika. Sasa hivi ni kazi inayomaliziwa ili kujenga mifereji midogo midogo ya wakulima. Bado tunaomba katika bajeti ya mwakani tupatiwe fedha katika mradi wa Kongwa tulo, ili nao ukamilike na uanze kufanya kazi ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu lingine kwa Serikali na Wizara ni kuona kwamba pamoja na nia nzuri ya Serikali kuwapatia wakulima mbolea na pembejeo, wakati umefika sasa kwanza kuona ni namna gani tunapata mbegu ambazo zitatengenezwa humu humu ndani badala ya kutoka nje ya nchi. Hii ni pamoja na mbolea. Nadhani wakati umefika kwa Serikali kuimarisha viwanda vya ndani vilivyopo, ili viweze kutoa mbolea kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili la mbolea, nadhani ni wakati muafaka vile vile kutumia Vyama vya Ushirika na *SACCOS* zilizokuwepo tunakotoka, ili ziweze kusambaza mbolea na mbegu kwa wakulima wetu badala ya kuwatumia wafanyabiashara ambaa nia kubwa kwao ni faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo ni Wizara ambayo vile vile inashughulika na Ushirika kwa kutumia Vyama vya Ushirika na *SACCOS* ambazo tunazo, tutakuwa tunaziimarisha *SACCOS* na Ushirika wetu ambaa ndiyo utasaidia kuondoa umasikini kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wake kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais ili waiongoze Wizara hii ambayo ni nyeti sana. Namwomba Mwenyezi Mungu awape busara na hekima tele ili waweze kulinusuru Taifa hili kutokana na umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwapongeza Watendaji wa Wizara hii kwa hotuba nzuri ya bajeti ya mwaka 2012/2013, nawatakia mafanikio mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi, napenda kuchangia machache yafuatayo kwa nia ya kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uboreshaji wa kilimo, nashauri wakulima wakopeshwe matrekta makubwa, kwani yana tija zaidi, *power tiller* zinashindwa kulima katika maeneo mengi kutokana na *nature* ya udongo. *Power tiller* nyingi hususan katika Jimbo langu, zinatumika kama mkokoteni.

Naomba Serikali isaidie wananchi wa Tarafa za Mkunguni na masombo ili waweze kupata masoko kwa ajili ya mazao yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, viungo aina ya karafuu, mdalasini, hiliki na *vanilla*, ni mazao yanayopatikana kwa wingi, lakini hakuna soko la uhakika. Cha kusikitisha, katika hotuba sijaona Wizara hata kutambua uwepo wa mazao haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, matunda hayana soko na kiwanda pekee cha kusindika, kimefungwa na sababu ya kufungwa hajulikani. Naomba Wizara ilieleze Bunge hili, ni kwa nini viwanda vingi vya kusindika matunda vimekufa? Vitafufuliwaje?

Mhesimiwa Naibu Spika, mashamba yasiyoendelezwa hususan yale ya katani na mengineyo, naomba wananchi wapewe kipaumbele katika upangaji wa uendelezaji wa mashamba haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua, ni kiasi gani cha fedha za mradi wa kilimo cha umwagiliaji wa Kiloka umetengewa? Mradi huu umesuasua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba chakula cha njaa katika Tarafa ya Ngerengere na Mikese kutokana na ukame na uharibifu wa mazao uliofanywa na Tembo wa kutoka *Selou*. Tatizo hili ni dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali isaidie kuanzisha kilimo cha tangawizi katika maeneo ya milimani ili kusaidia wananchi kuinua kipato pamoja na kutunza na kulinda vyanzo vya maji. Vijana wengi wako tayari kulima tangawizi ili waachane na uchimbaji holela wa madini pamoja na ukataji wa mbao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali isaidie sana katika kuimarisha kilimo cha mazao ya mbegu za mafuta pamoja na kuwasaidia wananchi kusindika mbegu hizi kwa kuwezesha uanzishwaji wa viwanda vya mafuta. Napenda kurudia tena kusema kwamba kilio cha Wilaya ya Morogoro ni suala la masoko ya matunda, viungo, mbegu za mafuta pamoja na *vanilla*. Aidha, suala la uvamizi wa mashamba yatokanayo na mifugo na wanyamapori, litatatuliwa kwa kiwango kikubwa kwa ushirikiano na Wizara nyininge zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kuunga mkono hoja pamoja na kuwataki utekelezaji wa bajeti wenye mafanikio, ila wasisahau kilio changu na wabarikiwe na Bwana.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa muda mrefu sasa Wilaya ya Rombo imekumbwa na mabadiliko makubwa ya hali ya hewa. Mvua za vuli na masika zimekuwa zinachelewa na/au zinawahi kuliko inavyotabiriwa. Kutokana na hali hiyo, mazao hukauka kabla ya kukomaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inaleta umasikini kwa wananchi amba kwa kweli wanayo bidii sana ya kilimo. Kwa muda mrefu, Halmashauri pamoja na Mbunge tumedhani na kuiomba Serikali kutupatia mradi wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba maji ya ardhi ni kidogo sana katika Wilaya yetu. Utafiti umeonyesha kwamba ni eneo la Masekini ndilo lenye maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi tunaomba kutengenezewa mabwawa kwa kuinga maji ya mito ya misimu ambayo ni mingi ili baadaye tuitumie katika kilimo. Ni kwa msingi huo, mimi naunga mkono hoja yako na kukpongeza wewe na Naibu Waziri wako kwa mwanzo mzuri na usikivu ulio nao nikiwa na matumaini kwamba wananchi wa Rombo watakuwa na matumaini katika majumuisho yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwamba, inaelekea ardhi ya Rombo haina afya nzuri, huenda aina ya mbolea tunayotumia haifai kwa sasa. Nashauri na naomba wataalamu wa Wizara watutembelee ili kufanya utafiti na kutupa ushauri. Inawezekana sana kwamba ipo haja ya kupanda mimea ya asili kama marejea kwa ajili ya kuongeza afya ya ardhi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni ucheleweshaji wa pembejeo kwa wakulima. Hili limezungumzwa na wengi, hivyo sina bababu ya kuliendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, naunga mkono na namtakia Mheshimiwa Waziri kila la kheri katika utendaji wake wa kazi Wizarani, lakin naomba sana hoja au ombi la mabwawa, malambo katika Jimbo langu alisemee hata kwa dakika moja tu.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka 2012/2013, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii ambayo ni muhimu sana kwa mustakabali wa maisha ya Watanzania na uchumi wa nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, umasikini ni jambo kubwa kwa wananchi wa Tanzania. Wananchi wanaitegemea sana Sekta ya Kilimo hususan katika kuwaondolea umasikini na vilevile hii ndiyo sekta wanayoitegemea kuwapatia ajira kwa walio wengi zaidi kuliko sekta nyingine nchini kwa sasa. Licha ya umuhimu wa sekta hii kwa wananchi na Taifa kwa ujumla, bado ukuaji wake haufanani na mahitaji yake kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu za ripoti ya hali ya uchumi wa Taifa, katika mwaka 2011 inaonyesha kuwa ukuaji wa Sekta ya Kilimo uliporomoka kutoka asilimia 4.2 mwaka 2010 hadi asilimia 3.6 mwaka 2011. Aidha, kilimo kilichangia asilimia 23.7 ya pato la Taifa kwa mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 24.1 mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya ongezeko la idadi ya watu la takribani asilimia tatu kwa mwaka, kuporomoka huku kwa ukuaji wa Sekta ya Kilimo siyo jambo jema kwa Taifa, hasa ikizingatiwa kuwa sekta hii ni muhimu sana kwa ukuaji wa kiuchumi wa nchi yetu na katika kujihakikisha usalama wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Sekta ya Kilimo iweze kutoa mchango stahiki kwa uchumi wa nchi yetu, lazima pamoja na mambo mengine kilimo chetu kiondoke katika mfumo wa kutegemea mvua. Lazima kilimo chetu kiwe cha kuaminika, kinachotegemea umwagiliaji. Mwaka 2011 wakati Waziri wa Kilimo alipowasilisha hotuba yake, aliahidi Bunge lako Tukufu juu ya kuundwa kwa Tume ya Taifa ya umwagiliaji itakayosimamia kwa ukamilifu shughuli za umwagiliaji kwa kuandaa mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya kuanzisha Tume hiyo, na halikadhalika kuandaa mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya Umwagiliaji. Tungependa kujuu utekelezaji umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Ushirika imeendelea kukabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinachangia kwa klasi kikubwa Ushirika kutokuwa na mchango mkubwa katika kumwondolea mwananchi wa vijijini umaskini. Wakati ambapo tunashangilia ongezeko kubwa la usajili wa Vyama vya Ushirika, bado ongezeko hili haliendani na wingi wa wanachama wanaaojunga na Vyama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la idadi wanachama kutoka 2,244,727 mwaka 2010/2011 hadi wanachama 2,396,001 ni ushahidi tosha wa kudumaa kwa ukuaji wa Ushirika nchini ikilinganishwa na mahitaji ya huduma za Ushirika. Kwa mfano, wakati ambapo tafiti zinaonesha takribani asilimia 54 ya Watanzania hawapati huduma za kifedha, SACCOS zetu hapa nchini ambazo zinafikia 5,424 zimeweza kuwa na wanachama 1,059,213 tu, idadi ambayo ni chini ya asilimia tano ya Watanzania wanaostahili kupata huduma za kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi na ukaguzi wa Vyama vya Ushirika umeendelea kuwa changamoto kubwa katika nchi yetu. Licha ya jitihada zilizofanyika kuitia programu kabambe ya mageuzi na modenaizesheni ya ushirika, bado tumeshindwa kupata dawa ya katuondolea tatizo la uwezo mdogo wa kiuongozi na uaminifu kwa Viongozi wa Vyama. Aidha, bado tunashuhudia Vyama Vingi vya Ushirika kutofanyiwa ukaguzi wa hesabu kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni hatari kwa uhai wa Vyama, hasa linapokuja suala la usalama wa akiba wa wanachama. Lazima jitihada za makusudi zifanyike kuhakikisha kuwa mazingira ya kufanya kazi katika Idara ya Ushirika ndani ya Halmashauri zetu yanaboreshwa. Uboreshwaji huo uende sambamba na uanzishwaji wa Kamisheni ya Ushirika nchini ambayo

uanzishwaji wake umechukua muda mrefu sana. Licha ya kuwepo kwa ahadi za mara kwa mara, tunapenda kujua nini kinakwamisha uanzishwaji wa kamisheni hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya ushirika inautambua mfumo wa *VICOBA* kuwa asasi za awali zinazoandaliwa kuwa *SACCOS*. Mfumo huu unazidi kupata umaarufu mkubwa hapa nchini kutokana na kuwawezesha wananchi wengi wa Mijini na Vijiji kupata huduma za kifedha. Pamoja na ukweli huo, nimeshtushwa kuona hotuba ya Waziri kutozungumzia mikakati ya Wizara kukabiliana na changamoto kubwa iliyopo kuhusiana na ulindaji wa usalama wa fedha za wananchi ambao wanaweka hisa zao katika vyombo hivi. Ikumbukwe kuwa, pamoja na Sheria ya Ushirika kutambua *VICOBA* kama *pre-SACCOS*, hakuna mwongozo ulio wazi wa jinsi ya kudhibiti na kukagua asasi hizi. Hali hii inahatarisha usalama wa fedha za wananchi. Ni vyema Serikali ikawa makini katika jambo hili ili yasijekutukuta yaliyotokea wakati wa *DECI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mkinga pamoja na Muheza, Korogwe na Lushoto ni miongoni mwa Wilaya zinazozalisha kwa wingi mazao ya viungo hapa nchini, mazao kama karafuu, Hiliki, Pilipili manga, Mdalsini na hata Kahawa yanastawi katika Kata za Kigongoi, Bosha na Mhinduro katika Wilaya ya Mkinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jambo la kusikitisha ni kwamba pamoja na mazao haya ya viungo kuwapatia wananchi kipato kizuri, uzalishaji wa mazao haya hapa nchini unafanyika kiholela mno. Umefikia wakati sasa wa kuwa na *flagship organization* kwa ajili ya kusimamia uzalishaji na uendeleaji wa mazao ya viungo nchini. Tujulize:-

- Nani anasimamia kwa karibu uzalishaji, ubora wa mazao haya na uongezaji wa thamani wa mazao haya hapa nchini.
- Zipo wapi Maabara kwa wakulima na wanaosafirisha nje ya nchi mazao yetu ya viungo ili kuweza kukidhi viwango vya ubora na kuweka madaraja ya bidhaa zetu?
- Nani anawaelekeza wakulima wetu katika suala zima la ubora, umuhimu wa viunganisho na maghala yanayokidhi viwango vinavyotakiwa?
- Tuna utaratibu upi maalum wa kuwahakikishia wakulima wa viungo wanakuwa na *Special purpose fund* kwa ajili ya upandaji upya wa mimea katika mashamba ambayo tayari yamekuwepo muda mrefu, hivyo kupunguza uwezo wake wa kuzalisha? Halikadhalika, tuna mkakati upi wa kuongeza uzalishaji? Wakati umefika sasa wa kuhakikisha mazao haya yanalingizia Taifa mapato makubwa. Ni vyema tukawa na mkakati wa makusudi wa kuanzisha *spices park for processing and value addition of spices and spice products*. Hatua hii itawezesha vilevile ukuaji wa ajira hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuligusia ni kilimo cha muda mrefu cha wananchi wa Mkinga kuhusiana na shamba la uzalishaji wa mbegu la Mwele liliopo Mkinga. Shamba hili limetelekezwa kwa miaka mingi sasa na hii imekuwa kero kubwa kwa uongozi wa Mkinga kutokana na ukweli kwamba wananchi wa Maramba wana tatizo kubwa la ardhi, wanashuhudia shamba hili likiwa pori na wakati huo huo hawaruhusiwi kuitumia ardhi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hotuba yake, awaeleze wananchi wa Maramba, Wizara ina mpango gani na shamba hili? Aidha, ni vyema mipango hiyo ikawahuisha wananchi wa Maramba ili waweze kuzalisha mbegu katika shamba hili. Endapo Serikali imeshindwa kuendeleza shamba la Mwele, ni vyema wananchi wanaozunguka shamba hili wakagawiwa ardhi ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja nikiamini kwamba, Serikali itazifanya kazi changamoto nilizoainisha, na vilevile imesikia kilio cha wananchi wa Mkinga na itayapatia ufumbuzi matatizo yanayowakabili.

NAIBU SPIKA: Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika ili na yeye atoe mchango wake, lakini bahati mbaya Mheshimiwa Naibu Waziri mambo haya hamjapata fursa ya kuweza kujipanga vizuri lakini tunawaaminia.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Kilimo, Chakula na Ushirika!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, *Subuhanah Wataala Aza Wajalla* kwa mapenzi yake na heri zake kwangu. Hapo hapo, naomba niwape pole Watanzania wenzangu kwa msiba mkubwa uliotufika wa ajali hii ya Meli ambapo Watanzania wengi wamepoteza maisha yao na nawatachia uvumilivu na subira wote waliofiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo, naomba niwatakie Watanzania wenzangu pia heri na baraka za Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunitua kuwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa imani yake hiyo na namuahidi yeye na Watanzania wenzangu wote utekelezaji wa majukumu yangu kwa kadri ya uwezo wangu na afya yangu yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu, kwa mwongozo na ushauri anaotupatia kila mara Mawaziri wake. Kwa nafasi hiyo pia naomba nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Seneta, Profesa David Mwakyusa na Wajumbe wenzangu wote wa Kamati ya Kilimo na kwa ujumla wake kusema kweli Waheshimiwa Wabunge wote, nafanya nao kazi kwa ushirikiano. Nawashukuru sana kwa msaada mkubwa mnaonipatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza, ambaye ni rafiki yangu wa siku nydingi na shemeji yangu na sasa ni Waziri wangu. Naomba nimshukuru Mohamed Muya, Sophia Kabuva, Mbogo Futakamba na watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze na kuwashukuru wapiga kura wangu wote wa Wilaya ya Mkuranga. Naomba wanivumilie, lakini tuko wote katika gurudumu la kulisukuma gurudumu la maendeleo ya Mkuranga. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru familia yangu kwa ujumla, wazazi wangu; nianze na almaarufu Profesa Alhaji, Abdallah Kigoma Ali Malima kwa kuniruhusu kuiga mfano wake, japo viatu ni vikubwa sana na mimi miguu yangu ni midogo. Mama yangu mzazi Mariam Venancia Sefivao; mke wangu barafu ya moyo, Naima, Mwapwani Binti Bakari, na watoto wangu Ali, Amina, Asina, Shinshin, Adamu Junior, Amini, Mariam, Hawa, Hanifa, Abdallah, Samiradi, Tamia, Zurkifri, Jibu na Abdurrahim. *Alhamdullah (Kicheko/Makof)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tusikilizane. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muda wangu huo uhesabiwe (nahisi ufidiwe).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika atakapokuja atawatambua Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia. Wabunge ni wengi, waliochangia kwa maandishi ni zaidi ya 100 na hoja zinazidi kuja. Kwa hiyo, wajibu wangu tumekubaliana na nashukuru ameniruhusu kufanya hivyo, kwani ni kuzungumzia masuala maalum (*very specific*).

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya masuala ambayo ninakuja kuzungumzia ni mazao makuu ya biashara. Ni ukweli kwamba mazao yetu haya yanategemea mambo mbalimbali ambayo tutake tusitake mengine tuna uwezo nayo na mengine hatuna uwezo nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja ambalo nataka tuzungumzie ni kwamba, nataka nirejee kwenye mazao yetu makubwa haya ambayo ni tumbaku, korosho, kahawa na pamba. Nataka nizungumzie changamoto tulionayo kwenye masuala ya soko la dunia, ubora wa mazao yetu, wingi wa mazao yetu, lakini kwa kiasi kikubwa matatizo ya soko la ndani kwa maana *internal market imperfections*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi kikubwa Watanzania tumejaliwa ardhi, lakini na uwezo pia wa kuzalisha kwa kiasi kikubwa sana. Hata hivyo, tatizo ambalo tumegundua kwa muda mrefu ambalo linaingia kwenye tatizo la menejementi ya mazao yetu haya makuu, naomba nirejee kauli ya mama Anna alipotumia neno *syndication*. *Syndication* kwa upande wa Tanzania ni tatizo ambalo linaonekana ni kubwa, na ambalo hapo katikati tulipoingia kwenye mfumo wa soko huria hili jambo hatukilitazama vizuri kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Wizara tumekaa na viongozi wakuu tumekubaliana kabisa kabisa kwamba, kwa mwaka huu matatizo yote ambayo yanatokana na *market imperfections* za ndani kama matatizo ya *syndications* ni lazima tuyafanyie kazi. Nikisema matatizo ya *syndications* kwa mfano ni nini? Kwa mfano, nichukulie kwenye tumbaku, kwa asilimia mia moja tumbaku ina wanunuzi wakubwa watatu; mmoja ananunua asilimia sitini, mwingine thelathini na mwingine huyu ambaye amekuja kama miaka miwili iliyopita akabadilisha mfumo wa soko zima ananunua asilimia kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *you can see kwamba it is so easy*. Hata kwenye sukari ni jambo la watu wanne au watano. Kwenye korosho ni jambo la watu wanne au watano kukaa na kusema mwaka huu tunanunua zao kwa kiasi fulani. Sasa tunasema tuna soko huria, lakini katika uchumi wa kweli *in true economics we do not have a liberal market of agricultural products in Tanzania*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ni kikwazo ambacho ni lazima tuambizane ukweli na lazima tukiondoe. Kwa hiyo, tumekubaliana kwamba, pale ambapo tunaweza kujielekeza na kuondoa matatizo ya *market imperfection* kwenye soko lazima tufanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani hotuba yake ilikuwa nzuri, haya mengine ndiyo, lakini kuna mambo mengine ambayo jamani ni lazima tukubaliane, kwamba *in the last six years* (miaka sita ya mwisho) ya nchi hii *agriculture imebadilika hasa katika uzalishaji* kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napitia hizi *statistics* hapa hakuna zao ambalo halijaongezeka mara mbili. Mwaka 2006 tumbaku iliyokuwa inazalishwa ilikuwa ni tani 50,000, leo tunazalisha tani za tumbaku 120,000, tena tumbaku tunayozalisha sisi ni *fruits yards*, siyo tumbaku ya *bale*. Jana kuna mtu alisimama akasema ile tumbaku ya Malawi, tumbaku ya Malawi ni *bale tobacco*, ile ya chini kabisa hata ikienda sokoni ina matumizi madogo sana. Tumbaku ambayo sisi tunataka kushindana nayo ni ile ya Zimbabwe, *that is a serious tobacco*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni lazima tukubaliane kwamba *we have a problem* katika *addressing issues* za soko, lakini *part of the problem* hizi za *market imperfections* za ndani kusema kweli ni *manageable*. Sisi tunakubaliana na naomba niseme tu kwamba, jana tumekubaliana ndani ya Wizara kwamba ni mambo ambayo ni lazima tuyafanye kimkakati kabisa ili tukubaliane nayo. Kwa mfano; nataka nirejee kwenye bei za vyakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubaliana kwamba sukari ya Tanzania inazalishwa Mtibwa, Kilombero, Kagera, lakini ikitoka Mtimbwa kuja Dar es Salaam sukari hiyo inauzwa shilingi 2,000/= kwa kilo. Sukari inayotoka *Sanantonio Brazil* ikitoka huko mpaka kufika bandari ya Dar es Salaam ni shilingi 1,200/=. Sasa *somewhere in this analysis* tunakuta kwamba, *okay* kuna *analysis*, kama wachumi tunasema kuna ruzuku inatolewa kwenye kilimo. Lakini kuna *transaction cost* kutoka Sanantonio mpaka huko. *What is wrong?* Kwa nini sukari inazalishwa Mtibwa, Kilombero na Kagera kwa shilingi 1,200/= halafu ikifika pale Bukoba Mjini inakuwa shilingi 2,000/=?

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu tunasema aah, unajua Serikali isiingilie. *This is not right!* Tumekubaliana kwamba kama Serikali ya Marekani inavyoingilia kati masuala ya *mortgage lending* kwa ajili ya kuokoa masuala ya kiuchumi na sisi uchumi wetu mkubwa unashikwa na kilimo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao yanapoingia kwenye balaa lazima tuingilie kati na hili ni mojawapo. Lazima tuingilie kati tukijua *what is this issue ya price imperfection*, maana tunawenza tukakaa tukasema *okay*, tunakuja na suala la kokinga viwanda vya ndani, lakini viwanda vya ndani visumize Watanzania. *That is the reality of economics!* Maana kama tunataka tufanye uchumi wa haki na wazi ni kwamba, Watanzania wawe huru kuchagua kile kitu wanachotaka kununua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lazima tufike sehemu na tumekubaliana kwamba, baada ya kupitisha bajeti yetu tunakaa na wazalishaji wenyewe wa sukari Tanzania, ni wanne(4).

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tumekubaliana na nashukuru Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza kwa karibu sana ni suala la kuongeza wazalishaji wengine. Sasa hivi inaonekana tuna miwa mingi zaidi kuliko inayotumika viwandani na uwezo wa kuzalisha miwa mingi imebainika kwamba upo na watu wanataka kuzalisha. Sasa tunataka kuondoa vile *vi-protection clauses* vyote ili watu waingie wazalishé miwa na wale wanaotaka kuanzisha viwanda vidogo vidogo waanzishe pia. *That is the only way tutapambana na syndication.* (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wewe kama ni mzalishaji mkubwa upambane na hawa wadogo, lakini usiombe Serikali au Bunge litunge sheria ya kukulinda wewe, halafu wewe unatupiga kwa kuza kilo sh. 2,400/=, *that is wrong.* (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchele unazalishwa pale Pawaga, Iringa kwa mjomba wangu William Lukuvi. Unatoka pale kwa shilingi 1,400/= unafika Dar es Salaam wakati ule wa *crisis* kwa shilingi 2,800/= *What is the issue there?* Pale hakuna *issue ya economics*, pana *issue ya transaction cost* na watu wanafanya udalali tu na nini, sasa *somewhere* Serikali lazima tuingilie kati. Tumekubaliana kwamba, tunaingilia kati na *one way* ya kuingilia kati kwenye mambo haya wanapokuja watu wengine wanaotaka kuleta mchele wa bei nafuu tuwaruhusu walete uingine upambane.

Mheshimiwa Naibu Spika, *problem* ya mchele wa Tanzania lazima tuseme kwamba, siyo *problem*, ni neema kwamba mchele wetu ni bora kuliko aina zote za mchele zinazozalishwa *around us*. Nilikwenda pale Matai kwa Josephat Kandege na Katavi, juzi tulikwenda Shinyanga, watu wanautaka ule mchele wote kwa lengo la kuupeleka Rwanda, Burundi, Congo na kadhalika. Sasa wale wenzetu wa kuja wanautaka kwa *any cost*, matokeo yake wanapandisha bei ya ule mchele kwa kiasi kikubwa sana na Tanzania *we have changed our eating patterns, consumption* ya mchele imeongezeka *gradually* mionganii mwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, *effect* yake ni kwamba, *because we are paying so much more for rice inflation is going so much higher* (mfumuko wa bei). Sasa Serikali lazima tuingilie kati hapo *somewhere* kusema kwamba, jamani eeh, sikiliza, sisi tunaingiza hauwezi kufanana, lakini mchele unaofanana ili kuwapa Watanzania *choice* ya kununua mchele kwa 2,800/= au 1,600/=, *in that way* tunawenza tukapambana na tatizo la mfumuko wa bei ambalo kwa sasa hivi linachangia ...

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani tulipokuwa Wizara ya Nishati na Madini tulikuwa tunasema kwamba, mfumuko wa bei unachangiwa na chakula na mafuta, *oil products, petroleum products and food products*. Ni kweli, lakini ukiangalia pamoja na sasa hivi petroli kusimama hapo kwenye dola 90 kwa *barrel* kwa muda mrefu lakini *inflation yetu is still flying, why? Because the food products are too volatile.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumekubaliana kwamba kwenye hili la namna bei za vyakula zinavyocheza, Serikali lazima iingilie kati kwa makusudi. Sasa tuna bahati mbaya nyininge moja; tunafanya mikakati ya kuwapa watu mahindi kwa bei nafuu, sukari kwa bei nafuu, mchele

waingize bila kodi ili kupunguza bei, lakini wakija hao hao Watanzania wenzetu ambao tunawapa nafuu hiyo, wafanyabiashara lukuki wanakuja hapa wao pamoja na kutengeneza faida wanataka kutengeneza *super profit* na kuna wengine tunao humu humu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ukitoa kibali kwa ajili ya kupunguza bei tunakubaliana na Mheshimiwa Daktari Mgimwa na Gavana wa Benki Kuu kwamba tukitoa kibali cha tani 30,000 za mchele tutapunguza bei kwa kiasi fulani. Ukija uza kwa bei ambayo tumekupangia Serikali. Usianze kusema ooh, sijui unajua soko huria, hakuna! *That is a market intervention* ambayo inakuja inapangiwa bei yake, hutaki acha. Halafu ukichelewa kuagiza usije humu unaleta barua kwamba, aah, unajua mimi sijui naonewa kwa sababu mimi Mtanzania, hakuna!

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *time* ambayo unaambiwa kwamba mchele, mfano sasa hivi tunajua kwamba mwezi wa Kumi na moja, kumi na mbili na wa Kwanza kwa uzalishaji wa mchele na hivi watu wanaupora na nini, tunaweza tukawa na tatizo la mchele mwezi wa kumi na moja. Hatujajiandaa sasa hivi, lakini tukikupa kibali cha kuleta mchele mwezi wa kumi na moja au wa kumi na mbili unaleta mchele mwakani mwezi wa sita, halafu unakuja unataka tuanze..., *this is wrong.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tukubaliane kwamba Serikali tumejipanga ndani ya Wizara, katika suala hili kusema *kweli no go area* kwa sababu Watanzania wa kawaida wanaumia. Tumekubaliana, tumepokea ujumbe wa Waheshimiwa Wabunge kuhusu suala la Bodi za Vyakula: Bodi ya Pamba, sijui Bodi ya Kahawa na nini, humu mote ambamo tumeona Bodi zinachangia moja kwa moja kwenye *market imperfections* tutachukua hatua. Mheshimiwa Waziri amekubali hilo, ni ushauri mzuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mazao inatakiwa kufanya kazi ya kuamsha zao lenyewe, sasa *you know* tunaweza tukawapa Bodi *performance indicators* watwambie katika kazi tuliyowapa wamefanya nini! Wamesukuma zao kwa kiasi gani, tukiona wamekaa mwaka mmoja kama Wabunge wanavyosema, wamekaa tu, wananyoosha miguu kwenye posho na vikao, waondoke waje watu wengine. Lakini baadaye tusije tukashikana mashati, maana Wajumbe wengine wako humu humu. (*Makof!/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwa Wabunge waliozungumzia suala la alizeti, mtama na mahindi. Zao kuu ambalo linapewa ruzuku ni mahindi kwa sababu ndilo ambalo linasimama kama zao kuu la chakula kwa Watanzania walio wengi. Hivi karibuni tumejikuta tuna tatizo kubwa la *ku-move* mahindi yanayozalishwa Sumbawanga, kule chini kule Mbozi, Mbeya, Ruvuma na kadhalika, maana *we are moving almost 100,000 tons*, tunahamisha tani laki moja (100,000) na zaidi kila mwaka kutoka upande mmoja wa Tanzania kwenda upande mwingine, gharama zake ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Martha Mlata anaposimama, naomba nimwambie kwamba, tumekutana na Wakuu wa Mikoa wote tumekubaliana kwamba ni mkakati maalum wa kuangalia kila mkoa utakavyopambana na njaa. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba, Wakuu wa Mikoa ya Singida, Dodoma, Iringa amejielekeza pale kwenye Jimbo la Isimani; Shinyanga ye ye amejielekeza *specifically* kukabiliana na tatizo la Kishapu ambayo kila mwaka inataka chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Kishapu wanasema, sisi badala ya kutuletea mahindi kwa bilioni za fedha, hizo bilioni za fedha ambazo mnazitumia katika kusafirisha mtuletee katika mfumo wa ruzuku mbegu za alizeti, mtama na mbolea. Kwa nini? Kwa sababu ile alizeti inataka kuwa ni zao la biashara, mtama zao la kupambana na njaa kwa maana ya *substitute* ya mahindi, kwa sababu unahimili ukame zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba tarehe 27 Juni, tulikaa na Wakuu wa Mikoa yote na kila mmoja alikuja na *plan* yake. Nikupe mfano tu: mkoa wa Tanga wenywewe unasema unataka alizeti na mtama kwa ajili ya Wilaya mbili tu, Handeni na Kilindi, wengine wote watapata *support* kutoka Wilaya hizi. Kwa hiyo, naomba niseme na nimhakikishie Mheshimiwa

Martha Mlata alilosema, kwamba kweli sisi tumewasiliana na Mkoa wa Singida, wenyewe wametaka alizeti kama zao la biashara na mtama kama zao la chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa anasema mahindi yanazalishwa Singida, *fine*, lakini wanaangalia mabadiliko na matatizo ya hali ya hewa kwamba, mtama una ustahimilivu zaidi. Naomba nilichukue hasa aliposema kwamba, vijana wengi wametaka kujielekeza kwenye mahindi. Lakini nimwambie pia kwenye mtama tuna soko kubwa kweli la Tanzania Breweries, Serengeti na watu wa Kenya wote wanautaka mtama wa Tanzania kwa ajili ya kilaji. Soko lile lipo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri watu wa kule *SOLOS* kwenye kituo chetu cha utafiti wamebuni mbegu ya mtama ambayo inatoa mtama kutoka kwenye tani mbili au tatu kwa heka hadi tani nane kwa heka. Sasa ile mbegu *combination* yake ni kwamba, itumike mbolea ya *phosphate* na mbolea ya samadi ambayo kwa kanda ile iko nyingi sana. Unapopanda ile unapata tani nane kwa heka, Mungu akupe nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumekubaliana kwa kushirikiana na mkoa wa Singida kwamba tuelekee kukabiliana na tatizo hilo. Naomba niseme kwamba, kwenye zao la alizeti, jamani tunacho-*import* Tanzania ni tani 200,000 za mafuta ya kula. *Importation* hiyo iko nyuma ya mafuta ya petroli tu. Sasa mikakati tuliyopanga Wizarani tumekaa na Wakuu wa Mikoa kama tulivyosema na kuangalia ni mkakati gani tunaouhitaji ili tupunguze japo kwa nusu na tani 100,000 zizalishwe ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna namna mbili za kufanya; moja ni kuboresha mfumo wa ruzuku na alizeti. Sasa ruzuku iliyokuwa inakwenda kwenye alizeti ilikuwa ni kama shilingi milioni 100 au 200. sasa tumebadilisha tunapeleka ruzuku ya kama shilingi billioni mbili (2) ili kupata mbegu zaidi kwa mwaka huu kwenye zao la alizeti na zao la mtama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo lake kwa zao la alizeti ni kwamba, baada ya hapo na Taasisi za Fedha zimesema zitatoa mikopo kwa vikundi vidogo vidogo kwa ajili ya *refinement* ya alizeti. Tumekwishaongea na Mheshimiwa William Mgimwa kwamba atatoa kipaumbele, ataangalia namna ya kutoa nafuu ya kodi kwa makampuni ambayo yatazalisha mafuta ya kula kwa kutumia mazao yanayozalishwa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, imo tayari kwenye bajeti, lakini tuangalie namna itavyoboreshwa zaidi ili tuhamasishe uwekezaji. Tayari kuna mwekezaji pale anaitwa *Mount Meru* yupo Singida, lakini tunataka wawekezaji wakubwa wengine. Kuna mashine zipo pale Mpanda, Katavi tunataka ile ambayo inazalisha sasa hivi kwa asilimia 20 iende mpaka asilimia 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niseme kwamba, kwa upande wa mkakati wa alizeti hilo limefanyiwa kazi na Mikoa ambayo ilikuwa imelengwa awali ilikuwa Singida, Iringa, Dodoma, Igunga pale na Nzega, Kishapu na kule Sumve na Kwimba. Sumbawanga kwa maana ya Rukwa na Katavi na maeneo ya Iringa nao wameomba kutumbukizwa na wao wanaomba wanasema wana nafasi kubwa ya kuzalisha alizeti. Kwa hiyo, Sumbawanga kwa maana ya Rukwa, Katavi, Iringa na maeneo ya Tanga, Handeni na Kilindi na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunakabiliwa kidogo na hilo, kwamba bajeti ya kusambaza ruzuku ya mbegu ya alizeti na mtama tulikuwa tumeifinya kidogo, lakini Mheshimiwa William Mgimwa anasema tutafanya kazi. Lengo la kuelekea kwenye alizeti ni kupunguza zile tani 200,000 tunazoleta za mafuta kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekezee kwenye mbolea ya Minjingu. Naomba sana nimshukuru Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe kwa sababu ndio wamekuwa wanalihimiza hili jambo kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme hili jambo nalifahamu vizuri kwa sababu chanzo chake kilikuwa ni kwenye kibali cha eneo la kuchimba *sulphate* ambayo ipo Minjingu ambayo kwanza ilikuwa ndogo, kulikuwa na leseni wababaishaji wamechukua maeneo ya pembeni pale mpaka kule, kuna eneo linaitwa Vilima Vitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi, Mheshimiwa William Ngeleja rafiki yangu mwenzangu wa Simba na Mheshimiwa Peter Dalaly Kafumu, tulitoka tukaenda Vilima Vitatu, tukakagua lile eneo tukakuta kuna leseni za wababaishaji tu wamekalia lile eneo miaka chungu zima halifanyiwi kazi. Kwa makusudi tukatenga lile eneo kama ni eneo ambalo litakuwa limetengwa kwa ajili ya uzalishaji wa *sulphate* basi. Kwa sababu wakati huo kiwanda cha Minjingu kilikuwa kinazalisha tani 5,000 za Minjingu *local sulphate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo sasa lilikuwa kuipeleka *production* hiyo kwenye tani 200,000 au 300,000 kwa sababu mahitaji yetu ya mbolea ni makubwa. Lakini baadaye ikabainika kwamba *local sulphate* kama mbolea ile pekee yake inakidhi katika baadhi ya maeneo. Sasa tukawambia sababu mojawapo ya kuwapa hiyo leseni iliyopanuliwa ya *sulphate* ni wao kufanya uwekezaji wa ziada. Wakakubali kutoa uwekezaji huo kutoka 5,000 wakapeleka kwenye tani 15,000 kwa mwezi kwa maana ya tani 180,000/-. Lakini tukasema *Local sulphate* ina matumizi machache, twende kwenye mbolea ya *NPK*, wakakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Mungu kwamba nipo Wizara ya Kilimo, nimefuatilia kwa miaka mitatu, umefanyika utafiti wa wataalam wetu wakubwa kubaini matumizi ya hiyo *NPK plus* ambayo inatumia *urea*, *sulphate* na *sulphur* na virutubisho vingi vingi tu. Kwa hiyo, hiyo mbolea imeonekana inakwenda sambamba na *DAP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaleta *DAP* nchini ikifika Dar es Salaam mwaka huu ni sh. 80,000 mpaka nikipeleka Ruvuma kwa Mheshimiwa Vita Kawawa inakuwa sh. 95,000 au 100,000. Mbolea ya Minjingu ikifika Ruvuma, ikifika Mbeya, ni sh. 64,000, hivi kweli jamani? Japo tayari kuna watu wanasema sema maneno kwamba aah unajua Serikali inaingilia kati hivi mbolea zinafanana uzalishaji na Wabunge wenyewe mmesema mbolea ya sh. 64,000 kwa nini tunambebesha mkulima wetu mzigo kwa kumwuzia sh. 95,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubaliana kwamba tuta-link fence matumizi ya mbolea kwa baadhi ya maeneo ya Tanzania. Tatizo lillikuwepo ni kwamba matumizi ya *NPK plus* ni zaidi ya tani 100,000 na kitu, lakini uzalishaji wake ule ulitoka tani 5,000 kwenda tani 15,000. Kwa hiyo, sasa hivi katika kipindi hiki kwa sababu ni mbolea ya kupandia na kuna maeneo mengi ya Tanzania yanapanda mwezi Septemba na mwezi Oktoba, mwaka huu tunakubaliana kwamba tutafute *at least equivalent* tani 30,000 za kuanzia mwaka huu, lakini mwakani ili watu wajipange kwa nafasi ni lazima Serikali tutawapa nafasi Minjingu *NPK Plus* ili ijandae kwa muda mrefu zaidi wa kukabiliana na hili tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, jamani tukubaliane tunapotoa ruzuku kwa *DAP* maana yake tunatoa ruzuku kwa mbolea inayozalishwa na mwenzetu. Maana yake kule kwake imetengenezwa inakuja kuletwa kwetu na sisi tunaitolea ruzuku kwa fedha zetu sisi. Kwa nini tusiitolee ruzuku mali yetu wenyewe kwa bei ndogo na ili wakulima iwfafie kwa bei ndogo. Naomba niseme kwamba hilo tumelifanyia kazi Wizarani na tunaamini tutakwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la ubora wa mbolea. Hili ni jambo ambalo haki ya Mungu hao jamaa wanaoshiriki katika hili jambo wanapata dhambi sana. Kuna watu wanachukua mbolea wanaifikisha kwa wakulima wamechanganya na simenti, wamechanganya na vitu vyaa ajabu. Mkulima wa Tanzania ambaye ha-suspect kitu chochote amekwishatoa fedha zake sh. 30,000 na Serikali imetoa ruzuku 50,000 anaweka kwenye ardhi kitu ambacho ni kibovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichofanya, sheria imetuletea kitu kinaitwa *National Fertilizer Regulatory Agency*, huyu anakuwa kama *EWURA* fulani lakini kwenye upande wa mbolea. Lengo lake ni kupambana na uchakachuaji huu, inaongozwa na mama Daktari Susan Ikela, hivi ninavyozungumza amekwishamaliza kufanya fujo sana katika Mkoa wa Ruvuma, anakwenda Rukwa, anakwenda Katavi tunataka aende hapa katikati. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni mwaka wake wa mwanzo amepangiwa bajeti ya milioni 140 haitoshi, amesema jana Mheshimiwa Said Nkumba haitoshi. Tumekubaliana na Mheshimiwa William Mgimwa kwamba tutaangalia hapa katikati, lakini na sisi wenyewe tutafanya

reallocation. Kwa sababu tunapomwezesha huyu mama *actually tunachopata ni saving*, maana akiokoa matumizi ya mbolea mbovu na sisi tunapata uzalishaji bora zaidi katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba hata mkiangalia kwenye vitabu vyenu mtaona ni shilingi milioni 140, lakini kusema kweli tumeji-*commit*, yeye mwenyewe alikuwa anataka kama bilioni 1,000,400,000/= na tumesema kwamba hapo ndani tutaangalia kwenye *reallocation* kwa sababu kuelekea katika hili jambo, ni jambo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la mafunzo na huduma za ugani na utafiti, tumeyapokea maelezo yote yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *Extension Service* ni suala muhimu mno maana ndiyo watu wanaotakiwa kwenda kukabiliana na wakulima wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana kuna Mbunge mwenzetu alizungumzia suala hili kwamba zamani watu hawa wa *Extension Service* walikuwa wanakwenda na sinema zao kwenye magari. Kwa hiyo, wanakwenda pale jioni sinema ya kwanza inapigwa na Mr. Shash Kabul na nani watu wanajaa pale akishamaliza ile sinema ya Shash Kabul inakuwa senema ya *Extension*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niseme kweli siyo vitu vyote, kuna Mbunge mwenzangu amesema kuna mambo ya kizee, sasa siyo mambo yote ya wazee ni mambo yaliyopitwa na wakati hata hili ni jambo nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba katika ushauri huu kurejesha mfumo ule ambaa unaboresha mawasiliano, unaongeza mawasiliano baina ya Serikali na hawa Wagani na wakulima, hili ni jambo nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme lingine la utafiti. Limetajwa kwamba, katika kanda nzima hii, the *Eastern Central Africa* tuna watafiti wazuri sana. Miongoni mwa watafiti hao jana walikuwa wananiambia kwamba kuna watu wanatoka Zimbabwe na wapi wanakuja kumfuata bingwa wetu anaitwa Ndunguru, wapo pale Mikocheni. Wanatoka huko watu wa Zimbabwe kwa ajili ya masuala ya *GMO* na kadhalika na nini. Kwa hiyo, naomba tusiwe na woga, wanasema wazungu *fear of the unknown*, tusiwe na woga kwa kile tusichokielewa. Sisi tuna misingi mikubwa ya wataalam wa sayansi na *Inshallah* tuendelee kuwatumia ili waboreshe sekta yetu ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba nizungumzie maendeleo ya Ushirika. Serikali kwa makusudi imeweka fedha nydingi sana katika mfumo wa Ushirika kwa lengo la kuwafikia wakulima walio wengi. Jamani lazima tukubaliane kwamba kwenye mfumo wa Ushirika tumeangushana. Kama tuisipouangalia huo ukweli na tukakaa, ndugu yangu Abdul Marombwa na Mbunge mwenzangu jirani amezungumzia suala la korosho Mkoa wa Pwani na mimi ni mdaa. Jamani hakuna suala la ajabu kama hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali haikupeleka fedha kwa ajili ya kuokoa zao, ilikuwa ni *guarantee ambayo* zao likiuzwa fedha yote ile inarudishwa. Kwa hiyo, hiyo siyo *stabilization fund*, ile ni *guarantee ambayo* mabenki yametoa na ambayo fedha yote itarudishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha ile imekwenda, kule kuna baadhi ya Vyama vya Msingi ambavyo tumemuagiza Mrajisi na *COASCO* na wengine waende haraka watwambie fedha zimekwenda kule, mimi nikienda Mbunge wao wananifokea wewe unafanya nini huko, upo umekaa tu kama gogo sisi tunaumia na zao letu la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia fedha zimekwenda kwenye Vyama vya Msingi. Lakini ukiangalia pale kwa sababu kuna watu walikuwa wanataraja kwamba itakuwa ile fedha ya majaliwa, walichofanya wakawahi kwanza kutia ndani wao. Sasa unakuta viongozi vya Vyama vya Ushirika wana mapikipiki, kwa mwaka huu wamenunua fuso mbili, wakulima hawajapata hela yao. *That is the case for vyama karibu vyote vya korosho.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakulima wanasema hebu tupeni fedha zetu, hicho sasa ndio kitu kikubwa ambacho tunakumbana nacho. Naomba na hili nipate muda kidogo. Kwanza, suala hili la ushirika *there is a gap between Uongozi wa Vyama vya Ushirika na Wanaushirika wenye we. Kuna tatizo kubwa hapo baina ya wajibu wa kila mmoja.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jambo ambalo tunakusudia kufanya hivi tunavyozungumza Muswada wa Sheria mpya ya Ushirika upo tayari ambao tunatarajia mwezi Novemba, mwaka huu utakuja muupitishe hapa Bungeni. Haiwezekani kwamba wajibu wa viongozi wa Vyama vya Ushirika unaishia kwao. Lazima Serikali na Bunge tuwe na uwezo wa kuwaambia nyie mmekula fedha za wananchi mnawekwa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipofika huko tutasema tuna fedha katika Vyama vya Ushirika, kumbe hakuna. Unajua *format ni hii, wenzetu kule sjui wanafanyakaji?* Viongozi wa Vyama vya Ushirika kwenye nchi zingine wanawajibika kwa watu wao, sisi wananchi wetu wale wanachama wa Vyama vya Ushirika wanaonesha dalili ya kutokuelewa sana. Kwa hiyo, mtu akishakuwa kiongozi pale basi anafanya anavyotaka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba, tunajitahidi kwenye masuala ya Sheria mpya ya Ushirika, sera na uharaka wa kukamilisha Sheria hiyo, lakini pia kuongeza uzalishaji wa Afisa Ushirika kwenye Halmashauri zetu. Pia sheria hii mpya inalenga jambo, maana ushirika ni mambo mawili. Kuna Tume ya Ushirika na Mrajisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka na Mrajisi huyu au mdhibiti wa Vyama vya Ushirika awe pemberni, afanye kazi *independently* kama Wakala na huyu ambaye *CEO* wa Tume ya Ushirika ye ye atakuwa anafanya masuala ya *promotion* na kuhamasisha Ushirika na wanachama. Lakini huyu anayefuatilia hamwezi mkawa ofisi moja. Huyu anafanya uhamasishaji na huyu anafanya udhibiti, ikiwa kama mishahara yenu, kasma zetu zinakwenda pamoja hamwezi kufanya kazi pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulichokubaliana ni kwamba, hawa wawili watengwe ili Mrajisi awe ana uwezo wa kwenda kuangalia kitabu cha Chama cha Ushirika saa yoyote na kwa muda wowote anaotaka na akikuta kuna matatizo anayapeleka *PCCB* na anayapeleka popote ambapo yatashughulikiwa. Ukishakuwa kiongozi wa Chama cha Ushirika ni dhamana, siyo ulaji na hili ninalisema kwa sababu katika Vyama vya Ushirika tuna makusudio maalum *especially* kwa zao la tumbaku la Mheshimiwa Said Nkumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka Vyama vya Ushirika viongeze ushiriki zaidi kwenye kuboresha zao lakini pia amezungumzia suala la Kiwanda cha Tumbaku pale Tabora. *One way* Serikali imeangalia ni kutafuta mifumo *Agro processing* ili kipatikane kiwanda pale Tabora, lakini ambacho kinaweza kikawa na usimamizi wa Vyama vya Ushirika. Isiwe kila jambo lazima awe mwekezaji binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwanza nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuzungumza na Watanzania wenzangu. Pia namshukuru Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kunipatia nafasi hii ya kusema haya ya mwongozo kabla ya ye ye hajaja kuhitimisha hoja yetu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mengine mengi, lakini naangalia pale kwenye saa naona muda wangu umefika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena sana sana na naunga mkono hoja. Nakushukuru sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Mhandisi Chiza, karibu sana Mheshimiwa.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhimitisha hoja hii niliyoitao jana. Lakini kwanza, naomba niseme kwamba, kwa kweli kuanzia jana na leo nimekuwa katika shule moja nyingine tofauti na nimejifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua zamani nilizoea na mimi kuka aha hapa na wakati mwingine kusifiwa sifiwa. Lakini kuanzia jana nikiwa nimekaa nasikia mishale inatoka huko, nageuka Naibu Waziri ananiambia imetoka CCM, nageuka nikigeuka natazama imetoka huko, lakini baadaye nikaona aah kumbe wakati mwingine ndiyo njia ya kufunza na kuelewa. (*(Makof/Kicheko)*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo pia nimefarijika nilipokuwa natazama kipindi cha *TBC* baada ya kusikia wakimzungumzia yule mtu wa ngumi, sijui ni *miss cheka*, yupo ustadhii mmoja akisema kwamba mpaka arudi, atakapokuja akatuomba radhi sisi tutamhesabu kwamba ni mwenzetu. Lakini pia akasema ukiwa kiongozi lazima usemwe na usiposemwa basi ujue wewe hufanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kweli nawashukuru sana sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu mizuri, wote mmechangia kwa nguvu sana mpaka nimejifunza hata na ndugu yangu David Kafulila naye akasema bajeti nyingine ni za kizee na nyingine ni za ujana. Lakini yote naamini ilikuwa ni kwa njia njema tu. Mmenisaidia. (*(Makof)*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji ni wengi, lakini naomba kwa ruksa yako sasa wale waliochangia kuititia hotuba ya bajeti ya Serikali nisiwataje kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwishawatambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda ningependa niende moja kwa moja kwanza niwatambue wale ambao wamechangia katika hotuba kwa siku ya leo. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia ni 137. Waheshimiwa Wabunge 30 wamechangia kwa kauli na Waheshimiwa Wabunge 107 wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuwatambua hawa waliochangia humu ndani kwa kuzungumza. Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji; Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Waziri Kivuli alisema siku nyingine taa itawaka lakini sijui ni lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Mheshimiwa Sulemain Nchambi Suleiman, Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa David Silinde. (*(Makof)*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Zaynabu Matitu, Vullu, Mheshimiwa Daktari Augustine Mrema, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Ismail Aden Rage na Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Daktari Hadji Mponda, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi na Mheshimiwa Martha Moses Mlata.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wapo Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Daktari Henry Shekifu, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Juma Seleman Nkamia, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Daktari Titus Kamani, Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany na Mheshimiwa Adam Kighoma Malima Naibu Waziri. (*(Makof)*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni wengi kweli kweli. Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Abdul Mteketa, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Angella Kairuki, Mheshimiwa Zakia Meghiji, Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa Azzan Zungu, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Abas Zuberi Mtemvu na Mheshimiwa Lucy Philemon Owenya. (*(Makof)*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Daktari Shukuru Kawamba, Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Daktari Mchungaji Getrude Lwakatare, Mheshimiwa Kapteni John Chiligati, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa Daktari Christina Ishengoma na Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Mansoor S. Hiran, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Janet Z. Mbene, Mheshimiwa Silvestry F. Koka, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa AnnaMaryStella J. Mallac, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu, Mheshimiwa Phillipa G. Mturano, Mheshimiwa Selemani J. Zedi, Mheshimiwa Deogratius A. Ntukamazina, Mheshimiwa James F. Mbatia, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mheshimiwa Stephen M. Wasira, Mheshimiwa David Z. Kafulila, Mheshimiwa Dkt. Augustine L. Mrema, Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Meshack J. Opulukwa, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana W. Kikwembe, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Moshi S. Kakoso, Mheshimiwa Mwigulu L. N. Madelu, Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mheshimiwa William M. Ngeleja na Mheshimiwa Maida H. Abdallah. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Eng. Athumani R. Mfutakamba, Mheshimiwa Dkt. Therezya P. L. Huvisa, Mheshimiwa Lolesia J. M. Bukwimba, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, Mheshimiwa Dkt. Hadji H. Mponda, Mheshimiwa Abdulsalaam S. Amer, Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mheshimiwa Zaynab M. Vullu, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Omary A. Badwel, Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Felix F. Mkosamali, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mheshimiwa Zarina S. Madabida, Mheshimiwa Selemani S. Jafo, Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mheshimiwa Esther L. M. Midimu, Mheshimiwa Abia M. Nyabakari, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Mheshimiwa Christina L. Mughwai, Mheshimiwa Moses J. Machali, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Dkt. David M. David, Mheshimiwa Innocent E. Kalogeris, Mheshimiwa Omari R. Nundu, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Dkt. Lucy S. Nkya na Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Dkt. Fenella E. Mukangara, Mheshimiwa Charles J. Mwijage, Mheshimiwa Susan L. A. Kiwanga, Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mheshimiwa Joseph R. Selasini, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Alphaxard K. N. Lugola, Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangalla, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mheshimiwa Salum K. Barwany, Mheshimiwa Assumpter N. Mshama na Mheshimiwa Dkt. Dalaly M. Kafumu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hao ndio waliochangia kwa maandishi. Kama kuna wengine nitaendelea kuwatambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikubaliana na mwenzangu Mheshimiwa Naibu Waziri, na naomba nimpongeze kwa kazi kubwa sana aliyoifanya kabla yangu. Tulikubaliana kwamba yeye afafanue yale mambo ya ujumla ili nipate nafasi angalau niwaguse japo sitawenza kuwafikia Wabunge wote, haiwezekani. Orodha ni kubwa kabisa na ni ndefu, lakini angalau tu ambao nitawenza kuwafikia niweze kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi aliyoifanya, wenyewe ni mashahidi, miezi miwili tu, lakini mmeona jinsi alivyoweza kuimudu Sekta hii ya Kilimo. Nakushukuru sana ndugu yangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuendelea, nzungumze jambo moja ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, nalo ni hili suala la fedha kuwa kidogo. Ni kweli kama mnayvoelewa, tangu siku ya kwanza kabisa, tukiwa hapa tukipitisha bajeti ya Serikali, ilijionyesha kwamba zamu hii fedha inaonekana kuwa kidogo, lakini lengo kubwa la Serikali ilikuwa siyo suala la kuwa kidogo, ilikuwa kwamba kwanza tujielekeze kwenye fedha ambayo tukiitenga,

tuna hakika kwamba fedha hiyo itakuja kuifikia Wizara husika. Haina maana ya kujifurahisha, kutenga mabilioni ya fedha ambayo mwisho wa siku *disbursement* unakuta haifiki fedha ile tuliyokubaliana. Kwa hiyo, tukasema tujaribu kujielekeza kwenye kiwango ambacho tunaweza tukakifika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninachotaka kusema kwa siku ya leo, iko dhana kwamba fedha iliyotengwa kwenye miradi ya maendeleo ni kidogo sana ikillinganishwa na fedha ambayo imetengwa kwenye matumizi ya kawaida. Sasa nilitaka nilifafanue tu kwamba, kuna neno ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri amelitumia, linaitwa *fenced*, kwamba yako maeneo ambayo ni ya matumizi mahsusti katika Wizara yangu. Ukiangalia bajeti hii, utakuta *OC* nimeomba Sh. 170,364,421,000/=. Sasa hizi ukizitazama, unaziona kama ni fedha za matumizi ya kawaida tu, kama kusafiri tu, lakini siyo kweli, maana yake siyo hiyo. Ndani ya fedha hizo, ziko fedha zimetengwa kwa maeneo maalum *ring fenced* ambazo hazitatokea kwenye fedha za maendeleo. Kwa mfano, katika fedha hizo ruzuku ya pembejeo hii ambayo ndiyo tunaizungumza humu ndani, tunaipigia kelele katika Sh. 170,000,000,000/= Shilingi billioni 75.1 tumezitenga kwa ajili ya pembejeo tu na fedha hizo haziguswi. Hazitaguswa kwenye posho, mafuta na kadhalika, zinakwenda kwenye shughuli za pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye ununuzi wa mahindi *NFRA*. Tulinwombwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba tunaanza na fedha kidogo, lakini hebu tuongezee.

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza nikawasahau, samahani, nakumbushwa kwamba Mheshimiwa Rosweeter Kasikila naye alichangia kwa maandishi, naomba nimtambue na Mheshimiwa Luhaga Mpina naomba kumtambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la ununuzi wa mahindi katika fedha hizo za *OC*, lina Shilingi billioni 27.6 na hizi ni za kuanzia tu. Lakini pia katika fedha hizo, kuna ugharamiaji wa Bodi za Mazao pamoja na ile Bodi ambayo tunaizungumza, Bodi ya Mazao ya Nafaka na Mazao mchanganyiko na Bodi nyiningine, Sh. 15,727,000,000/=. Fedha hizi haziguswi, zote zinaonekana kama *OC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Udhibiti wa Milipuko ya Visumbufu Sh. 750,000,000/= na uendeshaji wa Vyuo na chakula cha wanafunzi huwezi kugusa fedha hizi. Hizi fedha zinakwenda mahsusiti kwa ajili ya wanafunzi. Nafikiri nilikuwa namfuatilia Mheshimiwa sikumbuki alikuwa Mheshimiwa nani, lakini alizungumzia suala hili la vyuo vyetu. Tumetenga Sh. 350,000,000,000/= kwa sababu ni lazima wanafunzi wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Pembejeo pamoja na uchache wake tumetenga Shilingi billioni 2.8. Halafu yako Mashirika ambayo tunashirikiana nao, juzi wakati tukiwatambulisha walikuwa wamekaa humu; yako Mashirika kama ya *FAO, IFAD, ASERCA, International Red Locust* na kadhalika, haya ni Mashirika ambayo lazima tuyachangie. Haya tumeyatengea Shilingi billioni 2.2. Ukiujumlisha fedha zote hizi unapata Sh. 127,782,888,400/=. Hizi zote ziko katika fedha zinazoitwa matumizi ya mawaida. Sasa hizi nyiningine ndiyo hayo mambo mengine yaliyobaki. Niliona hili niliweke vizuri ili isije ikaonekana kwamba labda hizi fedha ni za kwenda tu kula au timesahau kabisa mambo ya maendeleo. Nadhani niliyoyataja kwa kweli ni mambo kama ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme lingine la ujumla kabla sijakwenda kujibu hoja za Wabunge wale wachache nitakaoweza kuwafikia, na hili ni jambo la pamba ambalo wengi wetu tumelizingumza sana. Ningombwa niongezee kidogo sasa kwa yale ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri alikwishazungumza. Kwanza naomba ni-*declare interest* kwamba mimi natoka Wilaya ya Kakonko na sisi tunalima pamba na ni mkulima mwenzenu wa pamba. Kilimo hiki cha pamba nakijua na matatizo yanayowapata wakulima wa pamba. Naomba niwahakikishie kwamba nayafahamu. Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka kwenye maeneo yanayolima pamba, akina Mzee Cheyo wote mnaonisikiliza kwa bidii kabisa kwamba, natambua changamoto ambazo zinakipata kilimo hiki cha pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawaomba kwa sababu changamoto hizi tunazjua na kwa sababu ninyi mmekubali kabisa na nilisikia kama mlikuwa mnanipongeza kwa dhati kwamba

hebu mnipe muda huu mfupi na mimi nianze kutafuta namna ninavyoweza kuchangia kuzitatu changamoto hizi za pamba kuliko kuninyima bajeti hii, halafu useme tayari sasa tumeanza kumaliza matatizo haya. Kwa hiyo, nianze kwa kuwaomba kwanza bajeti hii muipitishe ili tuweze kusaidiana kuchanganua changamoto hizi. Naelewa yako matatizo ambayo yanaendana na urasimu katika utoaji wa leseni za pamba, haya nayafahamu. Najua yako makubaliano mabaya kati ya Bodi ya Pamba na baadhi ya wanunuzi na wafanyabiashara. Haya nimeyafahamu kwa sababu tulituma watu kwenda kupeleleza huko na wakayagundua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa pia kwamba baadhi ya wanunuzi inaelekeea wakati mwininge kama vile wanapendeleta. Haya yapo, lakini naelewa pia Bodi ya Pamba mmeilalamikia kwa kiasi kikubwa na nataka niseme tu, siyo Bodi ya Pamba tu, Bodi nyingi zina matatizo ya hapa na pale. Bodi ya Korosho ukienda kwenye Kahawa ni hivyo hivyo, kuna matatizo. Utakuta wengine wanakiuka hata sheria, wengine wanaamua kuuza *cherry*, wakati mwininge tunasema tunataka iuzwe *parchment* wengine wanaauza *cherry*. Kwa hiyo haya matatizo yanayoendana na Bodi yapo, lakini wakati mwininge suala ni kutazama ni kipi kimejitokeza ili tuweze kukirekebisha? Ndiyo maana nasema hebu nipeni muda basi ili angalau na mimi nionyeshe umahiri wangu kama naweza. Miezi miwili tu jamani, hata sijakaa sawasawa, mnasema mambo ni magumu Mheshimiwa Cheyo! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa kwamba Bodi ya Pamba wakati mwininge imekuwa inaingilia maeneo ambayo yalipaswa yatekelezwe, aidha, kwa pamoja au na wadau mmoja mmoja, lakini wakati mwininge imekuwa ikipora. Nimeyapata haya baada ya kutuma watu kwenda kupeleleza huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwininge Bodi imeyapangia Makampuni Kanda za kujinadi na kushauri uanzishaji wa vikundi badala ya Vyama vya Ushirika ambavyo kimsingi ndiyo tunasema vingestahili kuingia mkataba na wakulima. Kwa sababu kilimo cha mkataba hiki ambacho kinaleta matatizo kule katika Kanda ya Ziwa ukikiangalia kwa ndani, kilimo cha mkataba chenyewe kimsingi siyo kibaya, lakini ule utendaji, mikataba ile inavyoingiwa ndiyo dosari zilipo. Kwa mfano, kama ungeniuliza, ningesema watu wa kuingia mikataba na watoa huduma visingekuwa vile vikundi vidogo vidogo sana. Kwa sababu hata katika mbolea tumeeleza mfumo unaokuja tunasema kuwa tutafanya utaratibu wa kuvikopesha vikundi au Vyama vya Ushirika, lakini Mabenki yenye yanatuambia hayatapokea vikundi ambavyo havikusajiliwa ambavyo havina Benki Akaunti, ambavyo havina *Bank Statements*, ambavyo havina kumbukumbu, kwa maneno mengine viwe vikundi ambavyo vinajua kutunza mahesabu yake.

Sasa ningesema chombo ambacho kingekuwa kama Mwakilishi kikakopa kwa niaba ya wakulima, ni ushirika. Sasa ushirika kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, bado kweli una matatizo kila mahali, na ndiyo maana tumefika hapo. Kila mahali kwenye kila zao tunapata matatizo. Lakini vinginevyo kilimo cha mkataba kama tungekipeleka kama tulivyokuwa tunakifikria, basi kisingeingilia matatizo haya, lakini hayo matatizo tumeyaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa pia kwamba liko tatizo la kuendesha mfuko ule wa WAKFU. Hata mimi nimeliona na wakati mwininge nimewambia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba iko mifuko ya WAKFU, hii ya *CDIF* karibu katika kila zao, na mimi nimesema jinsi tunavyoendesa mifuko hii, navutwa kufikiri kwamba tufikie mahali pia tuikague, tufanyie *auditing* tuone kama inafanya kazi yake kama iliyopangiwa. Maana yake kuna mahali pengine inaonekana na yenye labda katika kuitumia inachangia matatizo. Kwanza, tumeambiwa wako wakulima 350,000 waliopo katika kilimo cha mkataba, lakini wakulima wanaolima pamba, siyo hao tu, ni wengi. Kwa hiyo, utakuta wale walioko kwenye kilimo cha mkataba ni wachache kweli ukilinganisha na wale ambaa wanalima pamba. Sasa unapoingiza kilimo cha mkataba ghafla, ujue kwamba lazima kuna kundi fulani ambalo unalinyima haki kwa sababu ni kama vile kwenye Ushirika. Ushirika tunasema ni *voluntary*. Huwezi kulinazimisha kuingia kuwa mwanaushirika kama sijataka; hata Sheria ya Ushirika inasema hivyo. Sasa ukisema kila kitu kiwe hivyo kabla hujanielimisha nikaelewa, utakuwa umeniletea matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, liko tatizo bado, hata wakulima wale ambaa wako huko, kuna wengine tumewaingiza humo lakini hawaja-*qualify* kuingia katika kilimo cha mkataba.

Ninachotaka kusema ni nini hapa? Kwamba, kilimo cha mkataba bado tunayo nafasi ya kukiboresha, kukitafutia namna ya kukiboresha ili kiweze kutoa huduma ambayo ilikuwa *intended*. Lakini kwa wakati huu lazima tukubali kwamba uko upungufu, nakubaliana na wakulima wote wa pamba. Sasa dhana ambayo imekuwa ikitolewa na Waheshimiwa Wabunge wengi hapa ni dhana ya kwamba Serikali iangalie itafanyaje kufidia pale ambapo bei imeanguka.

Mimi nataka niseme hivi, mkokotoo wa bei kwanza sisi kama Serikali hatupangi bei ya zao lolote hata liwe la pamba, kahawa, tumbaku, hatupangi. Wanaopanga bei ya mazao ni wadau. Hata hii ya pamba tunayoizungumza ili ofikia Sh. 660/= mimi nilikaa pembeni nikasubiri waniletee majibu. Wakulima walikaa wakiwakilishwa na TACOGA, vikao vingi tu walikaa na wanunuzi, tena walikaa kule Ofisini kwenye Wizara yangu, walikaa masaa mengi kwenye saa 8.00 usiku wakafika mahali wakasema, hapa tulipofikia sisi tunaona bei hii tuiache sasa ianzé kufanya kazi, ndipo wakaenda kule wakatangaza. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba Serikali ndiyo inayopanga bei hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunachokifanya ni kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira fulani yatakayosaidia bei iwe nzuri ya mkulima na ndiyo maana ukitazama ule mkokotoo wa bei ya pamba, kwanza wanunuzi walikuwa wanataka Sh. 520/= . Sisi tukasema haiwezekani, na wengi wamekwenda mpaka wamemwona Mheshimiwa Rais. Tukasema tutafute jinsi wanavyowenza wakapanda angalau basi wafike hata Sh. 725/=, lakini wakafika mahali wakavutana sisi tukasema tutachangia angalau kwa kupunguza hata ile *crop cess* tukasema tuipunguze kutoka 5% iende 2%. Jambo hilo litafanya ili fedha ile iweze kuchangia kwa mkulima. Yote hayo tukafanya, lakini walipofika kwenye mkokotoo ule wa bei, naambiwa wale wanunuzi wakasema ukigusa bei ya pamba, ile mbegu, hapo ndiyo basi tena, maana wanajua hapo ndiyo wanaposhikia wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kawaida, lazima tuseme ukweli kwamba mara nyinyi wafanyabiashara, tena wanisamehe bure, siku zote katika mkokotoo wa bei wao lazima wanavutia kwao, ni kutaka kumlalia mkulima ndicho hicho kitu tunachokiona siku zote. Lakini sisi tunasema lazima tuvutane wote kwa pamoja tufike mahali mfanyabiashara asimlalie mkulima na mkulima naye angalau afute jasho lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nini ambacho nataka kukisema siku hii ya leo? Naona Mzee Cheyo anatizama kwa bidii sana. Ninachosema ni kwamba, nimejaribu kupitia yale ambayo tulikubaliana katika Mkutano Mkuu tulipokuwa kule Mwanza kwamba ni njia zipi zinaweza kutusaidia kupandisha bei ya mkulima apate chochote pale. Tukijidai kwamba Serikali itafidia, tutakuwa waongo. Kuna wengine wemesema weka hata Sh. 100/= tu; ukiweka, *you are talking of over 30 to 40 billion shillings*.

Mheshimiwa Mpina '*Shwa*', alisema Serikali iweke fidia Shilingi bilioni 102 ukisema uweke hiyo, Mzee Mrema anakuja anasema na mimi kahawa nataka Shilingi bilioni tatu, pareto naye anakuja anasema nataka Shilingi bilioni kadhaa. Kwa kweli hata tungesemaje, tutakuwa hatuitendei haki Serikali kwamba inaweza kujilingiza hapa. Tunachokisema ni kwamba tutafute tufanye nini, ili bei hii ya mkulima angalau ipande.

Sasa ninachotaka kuwaambia wakulima wa pamba ni kwamba, ninachokiona mimi kinaweza kutusaidia, tulikubaliana kuongeza na kupanua wigo kwa njia njia moja au nyininge kwa wanunuzi, ili angalau ushindani uwepo kiasi fulani tuondoe *monopoly* ya wanunuzi. Kwa sababu wanunuzi wanapokuwa watatu, wanne au watano, hao lazima wana-collude na wanapanga bei wanavyotaka. Sisi tunachotaka ni kwamba angalau waongezeka kidogo, lakini nao wakiongezeka wasiende wakaongezeka akina Kangomba wakawa wengi kama ilivyokuwa kwenye korosho. Kwa sababu ukiwaongeza wanunuzi wakawa ma-middlemen wengi badala ya kumpa bei hata ile ya Sh. 660/= watakwenda kuinunua hata kwa *give away price* ya Sh. 300/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunataka angalau tuangalie wakulima wangapi na wanunuzi gani wanaweza wakaongezeka na kuongeza ushindani ili ile bei angalau basi hata ile Sh. 660/= isiende chini ya hapo, badala yake ipande iende juu. Hili mimi naamini linawezekana kwa kuongeza ushindani. Sasa hili la pamba, naomba nilimalizie kwa kusema hivi. Kuna hatari ya kulifanya soko la pamba kwa sasa kuwa kwa asilimia 100% huria kila mtu kupeleka Kangomba

kununua pamba. Kwa sababu inawezekana hata hawa *middle men* wataingia, katika mazingira haya yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwarejeshe kwenye maamuzi ya Mkutano Mkuu wa wadau ambapo tulifanya hivi; mwanzoni sikukubaliana nalo jambo hili, lakini naomba nikubaliane nalo ili liweze kutusaidia kuongeza wigo. Kwamba wenye viwanda vyta kuchambua pamba waliochukua pembejeo na ambaao hawajalipa na wanadaiwa na wakulima fedha za pamba, hao tuwaruhusu wapewe leseni. Lakini Bodi ya Pamba isitoe kibali cha kutoa marobota ya pamba kutoka kiwandani, yaani *release order* mpaka mnunuzi husika awe amelipa deni analodaiwa. Hayo tulikubaliana kwenye mkutano wa wadau, tukasema tukifanya hivi tutakuwa tumeongeza wigo na watu ambaao hawakupata leseni angalau watapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili nimeona nilikubali, najua lina mikingamo yake pale, kwa sababu ukitizama taratibu tulizoziwekea, ilikuwa kwamba hawa wasipewe leseni. Lakini nachelea kusema hawa tuwanyime wote, lakini tayari wana vikundi walivyohudumia na wanadaiwa na wakulima. Mimi ninafikiri tuwape nafasi nao ili waingie sokoni watusaidie kuongeza ushindani halafu bila shaka bei ya pamba inaweza ikaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hilo la pamba niliachie hapo, lakini niwaombe wakulima wa pamba wenzangu, nipeni na mimi nafasi hiyo, nami baada ya shughuli hizi, nitakachokifanya sasa hivi ni kwenda kwenye *ground* kuona nini kinaendelea kule kwenye pamba ili kila inapowezekana tushauriane na vyombo vingine, tushauriane na bosí wangu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, na Mheshimiwa Rais kila kinachotokea tuweze kuona namna ya kusaida. Naomba katika hilo tusaidiane.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ndilo jambo la ujumla ambalo nilitaka niliseme kwa siku ya leo kwa upande wa pamba. Sasa kwa muda uliobakia, haya ya ujumla sitayasema, lakini naomba kwa haraka haraka kama nitaweza kwa wale nitakaowafikia na ambaao sitawafikia, naomba mnisamehe bure, lakini tutaweza kuwaletea majibu kama kawaida kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nipongeze Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo ikiongozwa na Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa kwa kazi kubwa sana waliyoifanya. Ukitizama sana hotuba yangu niliyoitoa jana na ukisoma sana maoni ya Kamati, utakuta kwa sehemu kubwa sana maoni ya Kamati yale yamezingatiwa katika hotuba yangu. Hii ina maana kwamba Kamati ilifanya kazi kubwa sana ya kuchambua mapendekezo yale na yote yalikuwa ya maana na hoja zote walizotuvekea tulizikubali. Kwa haraka haraka, naomba nizitaje kwa sababu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja moja ilikuwa Wizara zote zinazohusika na Sekta ya Kilimo zipewe fungu la kutosha kutekeleza Kilimo Kwanza. Serikali inatekeleza azma ya Kilimo Kwanza kuititia ASDP lakini nataka nizungumzie dhana ile ya Kilimo Kwanza. Kuna mchangiaji mmoja kama sio Prof. Kulikoyela, kuna mmoja alizungumzia hili. Maana watu wengi wanadhani ukisema Kilimo Kwanza ni Matrekta. Kilimo Kwanza ni mabonde yangu ya umwagiliaji. Kule Kalya, Kashaghulu na kwingine ni kweli ni sehemu ya Kilimo kwanza, lakini dhana pana ya Kilimo Kwanza siyo hiyo. Dhana pana ya Kilimo Kwanza maana yake ni kila sekta inayoweza kuchangia kilimo ichangie kilimo, ndiyo maana yake.

Kwa hiyo, unapozungumzia Kilimo Kwanza, hata afya inachangia Kilimo Kwanza. Watu wakiwa wanaumwa Malaria, wakiwa na wadudu tumboni, kama hawaponi, hawawezi kwenda kulima. Kama miundombinu ya barabara haipo inayosafirisha mazao kutoka shambani kwenda sokoni, mazao yale hayawesi kupata soko. Basi kila sekta inatakiwa itoe mchango wake. Ndiyo dhana pana hii ya Kilimo kwanza. *Of course* pamoja na haya mengine ya matrekta, visumbufu vyta mimea, umwagiliaji, vyote ni Kilimo Kwanza. Lakini ukiitizama Kilimo Kwanza kwa dhana pana, maana yake ndiyo hiyo. Ndiyo maana Kamati ikasema Wizara zote zinazohusika na sekta hiyo zifanye hivyo. Naishukuru sana Kamati ya Kilimo na Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kulikuwa na suala kwamba Serikali itoe elimu kwa wakulima na wananchi kwa ujumla kuhusu maana halisi ya Kilimo Kwanza, hilo nimelifafanua. Serikali iendelee kuhusisha sekta binafsi katika utekelezaji wa Kilimo Kwanza. Kwa hili la sekta binafsi

tumeeleza mara nyingi, kwamba sekta binafsi kwa kweli mchango wake umekuwa ni mdogo. Lakini kwanini mchango wake unakuwa mdogo? Ni kwa sababu kilimo kama wengine wanavyoziogopa ni sekta ambayo ni *fragile*. Sekta binafsi kama mnavyoijua wanapenda wakiweka fedha wapate.

Kwa hiyo, mara nyingi wanaogopa sana kuingia kwenye kilimo kwa sababu ya ile *security* ya mazao. Lakini tumeanza kuingiza dhana hii kwa upana ndiyo maana sisi kama Serikali kwa kufuata ile Sheria ya *PPP* pamoja na Kanuni zake, tumeanzisha utaratibu huu wa *SAGCOT*. *SAGCOT*, ni *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania* ambayo inalenga kuwaleta wakulima wakubwa, wakulima wadogo na wa katika wakae pamoja ili wale wakulima wadogo waweze kufaidi teknolojia, mbinu na hata ikiwezekana na mitaji ambayo wakulima wakubwa wanayo.

Sasa wakikaa pamoja, sisi tunafikiri kwamba wanaweza wakasaidiana. Lakini naomba niseme ile dhana ya kwamba kwa kufanya hivi tunachotaka ni kunyang'anya wakulima mashamba yao, siyo kweli. Katika dhana hii, hata mkulima mkubwa akija hawezi kuwa mbadala wa mkulima mdogo wala mashamba ya wakulima wadogo haya ambayo tunayokwenda kuyapima kwa Mheshimiwa Marombwa, zile hekta 105,000 hazina maana ya kunyang'anya wakulima wadogo na kuwapa wakulima wakubwa hata kidogo. Siyo maana yetu hiyo. Ni kwa kutenga tu kwamba huyu mwekezaji au mkulima mkubwa na mwekezaji siyo lazima awe mweupe au Mzungu ni pamoja na wewe mweusi unaweza ukawa mwekezaji vilevile. Hata Prof. Kulikoyela aliniambia anaweza kuwa mwekezaji. Tunataka hata wawekezaji wa namna hiyo waje. Sasa tunataka hawa watu wakae pamoja waweze kusaidiana na ndiyo lengo la kuanzisha utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, hili la *GMO* amelizungumza Mheshimiwa Naibu Waziri, nisingependa nilirudie tena. Lakini nilitaka niondoe dhana ile ya kusema kwamba tusiendelee kufanya *research* katika *GMO*. Mimi kidogo simwelewi Mheshimiwa Zitto, anasema anapingana sana, hataki kusikia *GMO*. *GMO* iko duniani, *GMO* nchi jirani wanayo inatumika, wengine imefika mahali wanaitumia hata kwenye mazao ya biashara tu. Kwamba kwenye chakula tusiitumie. Lakini katika hotuba yangu nimeeleza madhara yanayoweza kutokana na *GMO*, madhara na faida zake. Lakini nikasema hatuwezi kujilingiza kichwa kichwa. Ndiyo maana nikasema matumizi ya Uhandisi Jeni, kwa maana ya *GMO*, bado tutaendelea kuyapa nafasi kwa maana ya kuyafanyia utafiti ili tufike mahali tutakapoamua sasa ama tunaingia jumla au hatuingii tuwe na uhakika. Ndiyo maana nikasema tunaendelea kutenga fedha ili tuweze kufanya utafiti katika suala hili la *GMO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali iongeze bajeti ya Sekta ya Kilimo; hili nadhani sina haja ya kuendelea kulizungumzia kwa sababu wote mmeona malengo yetu kwa kweli ni kufikia huko. Lakini nitoe mifano kwamba tangu mwaka 2003 tumekuwa tukiongeza bajeti, tulikuwa na asilimia 3.81, tukafikia asilimia 6.8 mwaka 2011/2012, mwaka 2012/2013 bajeti ya Sekta ya Kilimo ni asilimia 5.3 ilishuka. Lakini ninachosema hapa ni kwamba, iko dhana pia nyingine potofu. Tunapokokotoa na kusema bajeti ya Sekta ya Kilimo, hatumaanishi kilimo cha mazao kwa bajeti hii tunayoizungumza hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yuko Mheshimiwa pale akasema ni asilimia 1.7 ya bajeti, siyo kweli. Ukiwemo Sekta ya kilimo unazungumza kilimo cha mazao, unazungumza mifugo, unazungumza hata misitu ni sekta hii. Kwa hiyo, tunapokokotoa hii, tunapochukua fedha zilizoko TAMISEMI, zilizoko Mifugo, zilizomo Kilimo yenye *proper* ndipo tunazungumza Sekta ya Kilimo. Sasa ukiichukua hii kama *percent* ya bajeti ya Serikali, ndipo unapopata *value* ile ya mchango wa Serikali kwenye Sekta ya Kilimo. Kwa hiyo, wale wenzangu mnaopigapiga hesabu ile ya kuchukua hii Bajeti ya Wizara unaweka juu ya Bajeti ya Serikali ndiyo unapata *percent* hii, hiyo ni dhana potofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niweke vizuri angalau kila mnapochangia hili muwe mnaelewa tunapozungumzia Sekta ya Kilimo. Waheshimiwa Wabunge sina jinsi kwa kweli ninavyoweza kuyasemea yote haya. Naomba nizungumzie habari ya umwagiliaji, siwezi nikagongewa kengele ya pili bila kusema umwagiliaji.

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili hiyo. Toa hoja tu Mheshimiwa.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(*Makofii*)

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

KAMATI YA MATUMIZI

KUHUSU UTARATIBU

MWENYEKITI: Wamesimama Waheshimiwa Wabunge watatu. Mheshimiwa Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimesimama kuhusu Kanuni ya 112 ya Kanuni hizi za Bunge lako Tukufu. Naomba niisome inasema; "Masharti ya Kanuni ya 77 yatatumika kuhusu Kamati ya Bunge Zima ila tu kama idadi ya Wabunge waliyohudhuria itakuwa bado haifiki nusu ya Wabunge wote baada ya kipindi kilichowekwa na Kanuni ya 77(3), Mwenyekiti ataondoka kwenye Kiti chake Bunge litarudia na Katibu atahesabu idadi ya Wabunge waliohudhuria na kama idadi yao bado itakuwa bado haijafikia nusu ya Wabunge wote, basi Spika ataahirisha Bunge."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimehesabu zaidi ya mara mbili kwenye Ukumbi huu Wabunge walioko ndani ya Ukumbi huu hawazidi 110 na idadi ya Wabunge wote ni 352 na nusu ya Wabunge ni 176. Kwa hiyo ili kutendea haki na hasa ukizingatia hoja iliyoko mbele yetu ni zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania wote na ndiyo walipakodi. Naomba tuhesabu idadi ya Wabunge walioko ili tutende haki na tuweze kutekeleza Kanuni zetu. Naomba kutoa hoja.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru. Nami nasisitiza kuhusu Kanuni ya 77 kufuatwa. Nasimama kwa 77(1) na(2). Nikianza na (1) inasema "Akidi kwa kila kikao cha Bunge wakati wa kufanya maamuzi itakuwa ni nusu ya Wabunge wote kama ilivyofafanuliwa na Ibara ya 99 ya Katiba isipokuwa kwamba idadi hiyo haitahusu uamuzi wa kubadilisha masharti yoyote ya Katiba kwa mujibu wa Ibara ya 98." na ya (2) inasema; "Mbunge yoyote aliyehudhuria anaweza kumjulisha Spika kwamba Wabunge waliopo ni pungufu kwa akidi inayohitajika kwa ajili inayoendelea."

Kwa hiyo, nasisitiza kabisa kwamba na mimi nimehesabu humu ndani Wabunge hatufiki nusu na nusu ya Wabunge ni 176 ukitoa zile nafasi tano ambazo Wabunge hawapo. Kwa hiyo nasema kabisa ufuate Kanuni zetu tuahirishe Bunge hili mpaka tutakapokuwa tumetimia.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilitaka kusimama kwa mujibu wa Kanuni 77 kama Mheshimiwa Felix Mkosamali alivyozungumza. Kwa hiyo, kwa kuwa hoja imeshaeleweka, ninaomba tu Kanuni ziweze kuzingatiwa ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali kwa kuwa umeongea wa mwisho, na umetumia 77 (1) na (2), naomba usome kwa sauti 77 (3).

MHE. MOSES J. MACHALI: Kanuni ya 77 (3) inasema kwamba: "endapo Spika ataridhika kwamba ni kweli idadi ya Wabunge walio ndani ya ukumbi wa Bunge ni pungufu ya akidi inayohitajika, atasimamisha shughuli za Bunge kwa muda atakaoutaja na atamwagiza Katibu kupiga kengele." Mwisho wa kunukuu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa jambo hili linategemea kuridhika kwangu, naomba tuendelee, na nitakuwa naendelea kuangalia, halafu kwa wakati muafaka nitatoa mwongozo wangu kwa uhakika. Lakini vilevile cha pili ni kwamba, naomba tuheshimiane na tupeane nafasi. Kanuni hii ita-*apply* zaidi wakati ule nitakapokuwa ninahoji kwa ajili ya kufanya maamuzi. Tunaendelea, Katibu.

Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika

Kif. 1001 – *Administration and HR Management* Tshs. 1,556,023,000/=

MWENYEKITI: Mnadhimu Mkuu wa Upinzani, nini tena katika hatua hii?

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba samahani sana, tunafanya maamuzi tayari, ukishasema kama kifungu kinaafikiwa ni uamuzi umeshapitishwa wakati hakuna *quorum*.

MWENYEKITI: Ni Kanuni ipi ambayo unaizungumzia?

MHE. TUNDU A. LISSU: Ni Kanuni hiyo ya 112 (1) lakini vilevile Kanuni ya 77 (1) iko wazi sana, inasema kwamba hakuna uamuzi utakaofikiwa.

MWENYEKITI: Unafahamu kuwa nimesimama?

MHE. TUNDU A. LISSU: Nilikuwa sijakuona.

MWENYEKITI: Unajua utaratibu kwamba nikisimama tunapeana nafasi Mheshimiwa Mnadhimu Mkuu wa Upinzani? Unafahamu kabisa kwamba wewe na mimi tunapaswa kusaidiana kuongoza, nikishakuwa nimetolea ufanuzi kuhusu jambo, siyo vizuri sana kuanza kulibishia jambo lile lile tena. Utaratibu wa Kanuni hizi ambazo unazikazia sana kuzisemea zinakataza jambo hili. Kwa hiyo, naomba tuendelee, hilo la kanuni ambalo wenzako wametoa utakapofika wakati wake tutaona jinsi ya kufanya Tuendelee.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*.....Tshs. 37,370,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa hatusikii ni fungu gani, na ni *page* gani?

MWENYEKITI: Tuendelee Katibu.

Kif. 1003 – *Planning Monitoring and*

Evaluation Unit Tshs. 219,730,000/=

Kif. 1005 – *Legal Service Unit*.....Tshs. 21,656,000/=

Kif. 1006 – *Procurement Management Unit*..... Tshs.35,720,000/=

(*Vifungu Viliviyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote*)

Kif . 1007 – *Management Information Unit*.....Tshs 29,350,000/=

MWENYEKITI: Mkisimama katika wakati huu mnaniipa picha kama vile mnataka kusema kitu fulani.

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati*

ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1008 – *Internal Audit Unit* Tshs. 27,930,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 - *Promotion Services Section*..... Tshs. 360,376,000/=

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Leticia Nyerere.

MHE. LETICIA M.NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma ya 221000 - *Travel in country*, ningemba nipaye maelezo kwa nini imetuwa mara mbili kwa mwaka huu wa fedha?

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kifungu 221000 - *Travery in country*, kifungu hiki ni kwa ajili ya kulipia posho za kujikumu na gharama za usafiri kwa watumishi wa kitengo ndani ya nchi. Kifungu kimeongezeka kutokana na kupanuka kwa majukumu ya Tume na ongezeko la watumishi katika Idara zinazohusiana na Tume.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 4002 – *Cooperative Micro*

Finance Section Tshs. 412,410,000/=

Kif. 4003 – *Cooperate Banking and*

Investment Section Tshs. 84,810,000/=

Kif. 4004 – *Cooperate Marketing and*

Information Sect Tshs. 82,970,000/=

Kif. 4005 – *Registration Services Section* Tshs. 196,160,000/=

Kif. 4006 – *Inspection and Supervision*

Services Sect Tshs. 3,039,704,000/=

*(Vifungu Villiyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Fungu 43 - Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

Kif. 1001 – *Administration and HR*

Management Tshs. 3,834,664,410/=

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko katika program ya 10 (1001) sina haja ya kushika mshahara wa Waziri, ni rafiki yangu wa siku nyingi, ila tu nataka ufanuzi. Kwenye hotuba yake ukurasa wa 19 ameeleza vizuri kwamba katika Mikoa yenyewe ukame, Sera ya Serikali ni kupeleka miradi ya umwagiliaji ili kuondokana na njaa za mara kwa mara katika Mikoa hiyo, sasa katika Mkoa wa Singida kwenye utekelezaji kuna baadhi ya *scheme* kule Manyoni, kuna bwawa la umwagiliaji ambalo tulikaa ofisini kwake na wataalam wake tunamwagilia eneo kubwa tu manyoni mpaka Bahi Mkoa wa Dodoma, ni kitu kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajapan walishatoa kidogo kiasi cha Shilingi milioni 200 kwa kuanzia na akaahidi kuwa mwaka huu Serikali pia ingeunga mkono. Ninapekua humu sioni kama imo, watanielekeza, nilitaka ufanuzi. Ahsante.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyo sema Mheshimiwa Mbunge mradi huu siyo mgeni kwangu, ni mradi mzuri sana. Nilichomuahidi ni kwamba tumekwishapata fedha kutoka *Food Aid Counterpart Fund* fedha hizi bado hazitoshii kujenga bwawa. Kinachofanyika sasa ni kwamba fedha zile turuhusu zitumike kufanya sehemu ya kazi tu, kwa mfano, kazi za usanifu ambazo zilikuwa haziruhusiwi, jambo hilo limekubalika na mimi

mwenyewe nimelisimamia. Nataka nimhakikishie kuwa mradi huo utatengewa fedha kupitia mfuko wa maendeleo ya umwagiliaji ili bwawa hilo liweze kujengwa.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasimama kwenye kifungu 101 kwenye mchango wangu wa maandishi nilikuwa ninataku kupata maelezo ya Kisera kuhusu viwanda vya kuchambua pamba ambavyo vilizwa, vilibinafsishwa, lakini waliopewa wakaviacha na wengine wakauza mitambo. Nilikuwa naomba maelezo kwa Mheshimiwa Waziri kuwa Serikali ivifufue viwanda hivi kuwa vitasaidia sana kupandisha bei ya pamba, kwa mfano, jineri ya Choma cha Nkora.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo viwanda vingi vya mazao vya pamba na korosho ambavyo havitumiki kama tulivyokusudia tulichoamua ni kwamba viwanda vile ambavyo vimetelekezwa tutavifanyia mapitio na vingine ambavyo walikiuka tumesema tutawanyang'anya ili tuweze kuvitumia kwa jinsi ilivyokusudiwa.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, program 10, fungu 101, *Sub vote* 210100. Katika mchango wangu wa maandishi nilipenda kujua kama Wizara hii au Serikali inajua mgogoro uliopo kule Kata ya Mugani. Kata ya Mugani inalima sana tumbaku pamoja na Kata ya Mitundu na Kata Mwamagembe na hata Rungwe, lakini msimu uliopita Chama cha Msingi kimoja chenye wananchama 150 ni wanachama 12 tu waliolipwa na waliobakira wote hawakulipwa na wengi wanalamika mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo liliopo ni la bei, kuwa waliambiwa bei nzuri, lakini walipovuna wakati wa kuuza, bei ilianguka na Vyama vya Msingi vilikuwa vimelimbikiza madeni. Katika kukatwa, wengi wakawa hawana kitu kitu. Sasa kama suala hili linajulikana, ningeomba kujua kama Mheshimiwa Waziri yuko tayari kwenda Mugani na siyo mbali sana ili akalione hilo tatizo ili aweze kutoa ufumbuzi.

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyo sema wakati najibu hoja kwa upande wa Vyama vya Ushirika, matatizo yaliyojitekeza ni mapana kidogo. Lakini katika hili la alizeti, tayari tumeanza kulifanyia kazi kupitia Serikali ya Mkoa wa Singida. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Lwanji kuwa, tukimaliza hili Bunge tutatoka wote, mimi na yeye, Mheshimiwa Waziri ameshakubali, ili twende tukaangalie tatizo hili na namna ya kulikabili kwa sababu linaonekana lipo katika mfumo huo na pia tutachukua wasimamizi wa Vyama vya Ushirika ili kumaliza tatizo hili.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema kitu kidogo kwa Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri, ni kweli kabisa umeamua kuikanyagakanya kanuni ambayo ndiyo inayotuongoza katika Bunge hili Tukufu? Mimi nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri kuwa aweze kuiondoa au kuiahirisha hoja hii.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Opulukwa, nilikwisha toa maelekezo, siyo vizuri tena ikajirudia. Tumeshakuwa Wabunge wazoefu hivi sasa, nafikiri ile miaka ya kujifunza tumeivuka na tukishakuwa tumefanya maamuzi, hatu-query tena maamuzi hayo, tunasonga mbele kwa wakati muafaka. *We will pick this matter.* Ninajua na ninaona kuna watu wanahangaika, najua kinachoendelea! Kuna baadhi ya watu wanadhani tuko Shule ya Msingi au Sekondari. Hili jambo siyo sawasawa hata kidogo!

Waheshimiwa Wabunge, tupeane nafasi mambo haya yanakwenda kwa utaratibu, tutaelewana tu, kama huna hoja, nyamaza. Hii habari ya kuvuruga kila kitu siyo nzuri, hivi vitu ni *expensive*, ni gharama kwa Watanzania na sisi wote hapa ni vitu tunavyovisema kila siku kwamba tuangalie matumizi ya nchi hii kuahirisha Bunge siyo jambo dogo lakini nimesema nitalifanyia maamuzi baada ya muda si mrefu na kanuni inanipa nafasi nifani nafasi Mheshimiwa Mshama. (*Makofii*)

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamaliza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mshama.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ninasimama katika *vote* namba 43 *sub vote*.

MWENYEKITI: Tuendelee moja kwa moja bila kupoteza muda kwa sababu tunajua ni mshahara wa Waziri.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeuliza swali kwamba kwa kuwa ruzuku ya pembejeo ni sera ya Kitaifa.

MWENYEKITI: Kabla Mheshimiwa Mshama hujaendelea naomba niwataje Mheshimiwa Machali, Mheshimiwa Kafulila, mnafanya fujo kwa kelele kubwa naomba mtulize sauti zenu pamoja na kampeni mnayoendeleza. Mheshimiwa Mshama endelea.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoanza kwa kuwa ruzuku ya pembejeo ni Sera ya Taifa na wakati Waziri Mkuu alipotembealea Mkoa wa Kagera hususi kwenye Jimbo la Nkenge alituahidi kuwa mwaka huu tutawekwa katika moja ya Wilaya itakayopewa ruzuku ya pembejeo. Mimi ningependa kuuliza na kuelezo je tumewekwa katika hilo kwani nimetafuta kote sijaona naomba maelezo.

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tuliongea suala hili na Mheshimiwa Mshama naomba nirejee tu kumwambia kwamba orodha hatunayo hapa ya maeneo yote yaliyopewa pembejeo kwa mwaka huu lakini tukimaliza hapa nitakutana naye na tutalipatia ufumbuzu suala hilo.

MHE. LOLESEA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa kunipa nafasi, Mimi pia katika mchango wangu wangu wa maandishi nilitaka ufanuzi kutoka kwa Serikali hasa kwa uanzishwaji wa *scheme* za umwagiliaji kandokando ya Ziwa Viktoria katika mikoa ya Geita, Mwanza, Mara, Kagera na Simiyu. Ninhaitaji ufanuzi kwamba Serikali itaanzisha lini *scheme* za umwagiliaji ili kunusuru maisha ya wananchi.

WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi ni kwamba miradi ya umwagiliaji inaanzia huko kwenye maeneo miradi ilipo. Kwa hiyo wao ndiyo watambue kwanza kwamba sisi tunataka kuanza mradi hapa, halafu wakishaitambua wanaiweka katika mipango ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya husika, baada ya hapo ndipo unaletwa kuombewa fedha. Kwa hiyo labda nimshauri Mbunge kwmaba tutakapopata muda wa ziada nimpe utaratibu mzima wa kufuata maana unaanza kwenye Halmashauri yake.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa jana nilizungumzia suala la mizani. Nataka kujua ni upi mizani halali katika hii mitatu, mizani wa rula, mizani wa *spring balance* na *dictor* upi ni mizani halali kwa sababu ipo mizani mitatu inayotumika na mizani yote hiyo inamuibia mkulima.

WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hii mizani, nadhani Mbunge atakumbuka kwamba tuliamua msimu uliopita kwamba mizani yote ya rula itaondolewa sokoni ili tuingize mizani ya *digital*, lakini kwa bahati mbaya mizani ya *digital* iliyoingizwa nchini haitoshi na ndiyo maana nilitoa kauli hapa kwamba katika mazingira hayo hatuwezi kuacha soko lisimame kwa sababu mizani ya *digital* haijatosha, tukasema tutaruhusu mizani yote ya rula, ya *digital* na ile mingine itumike sokoni isipokuwa tutaweka wasimamizi kuhakikisha kwamba wakulima hawaabiwi. Maana tunaambiwa walikuwa wanaabiwa *16 up to 40 percent* kutumia mizani ile. Kwa hiyo yote inatumika lakini inatofautiana, tunachofanya ni kuweka wasimamizi kukagua isitumike kumuibia mkulima.

MHE. MAIDA HAMADI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante snaa. Katika mchango wangu wa maandishi nililiza Serikali kwamba katika taarifa ya hali ya uchumi mwaka huu ilitueleza kwamba pato la Taifa lilihuka kwa kiasi kikubwa na ilichangiwa na kushuka kwa sekta ya kilimo nchini ambayo ilisababishwa na ukosefu wa miundombinu ya umwagiliaji. Katika bajeti hii Serikali imetenga shilingi billioni mia mbili thelathini na saba lakini katika miradi ya maendeleo

imetengwa bilioni 67 tu ambazo kati ya hizo bilioni 14 ndizo ambazo ni fedha za ndani na bilioni 52 ni fedha kutoka kwa wafadhili. Je, Serikali imejipanga vipi kama wafadhili hawakutoa fedha hizi katika kuimarisha kilimo kama kukuza miradi ya maendeleo na kuimarisha umwagiliaji nchini ili tuweze kujikimu na kuongeza pato la Taifa nchini.

WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba fedha za ndani ni kidogo na wengi wamechangia, lakini katika mazingira tuliyonayo, hatuwezi kusema kwamba sasa tuache kufanya miradi ya umwagiliaji kwa sababu fedha ni kidogo. Lakini nakubaliana naye kwamba fedha hizo zinapokuwa kidogo, tunatafuta njia nyingine ambayo inaweza kutusaidia kutekeleza miradi. Nilikuwa najibu swalii la Mheshimiwa Chiligati hapa sasa hivi, nikaelezea fedha ambazo tumepeata kutoka kwenye vyano vingine nje ya Serikali. Nikataja mfuko wa *Food World Counterpart Fund*, wala haupitii ndani ya jengo hili. Tunapokwama kupata fedha, tunaangalia na vyano vingine vya fedha na zamu hii tumeamua kwamba hata sekta binafsi tunataka iingie kuchangia kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, hizo ni njia nyingine ambazo ni kama njia mbadala pale ambapo fedha za Serikali zitakuwa zimepungua.

MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi nimeeleza kwamba karibu mwaka mzima tangu nilipomwandikia barua Waziri wa Kilimo nikimwomba aiveke Wilaya ya Ngara katika orodha ya Wilaya zinazopata ruzuku ya pembejeo, mpaka sasa barua hiyo sijajibiwa. Namwomba Waziri mpya wa Kilimo awaeleeze wananchi wa Ngara ni lini Wilaya yetu itawekwa kwenye orodha hiyo?

NAIBU WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ntukamazina kwamba Wilaya yake itawekwa kwenye orodha ya Wilaya zitakazopokea ruzuku ya pembejeo kwa msimu wa mwaka huu.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeombia Serikali ielete ni jinsi gani itaiwezesha Bodi ya Tumbaku iweze kuajiri ma-classifier wasiopungua 30 kwa ajili ya kutoa huduma katika Wilaya 22 zinazozalisha zao la tumbaku. Naomba maelezo.

NAIBU WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Kakoso kwamba, hata hapa kwenye makaratasi ambayo tunayo, baadaye tunaweza tukaonana na Bodi ya Tumbaku, tumekubaliana, wamesema wanahitaji ma-classifier kama 34 hivi, na tumekubaliana kwamba kwa sababu ya umuhimu wa tatizo lenyewe, Wizara tulifanyie kazi suala hili na tupate ufumbuzi wa ma-classifier hao, japo kwa awamu, lakini tuanze kulishughulikia msimu huu wa fedha.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuelezea kwa kina ni jinsi gani ambavyo Serikali imedhamiria kuwashirkisha vijana kwenye kilimo ili waweze kuondokana na tatizo la ajira. Lakini pia ninapenda kupata ufanuzi, ni utaratibu upi ambao Wizara itautumia ili kuhakikisha programu hii inawanufaisha walengwa? Kwa sababu uzoefu unaonesha kuwa mara nyingi tunakuwa na dhamira ya kuwasaidia wahusika, lakini unakuta programu nzima inakwenda inachakachuliwa na wanaonufaika siyo walengwa.

Je, kama Wizara imejipanga vipi kimkakati kuhakikisha kwamba hawa vijana wananaufaika na hiyo miradi ambayo mmeipanga. Je, mna-/lnk na Halmashauri au mnatumia utaratibu gani?

WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, hawa tunaowazungumzia kuwapa ajira, na nimesisitiza katika hotuba yangu kwamba niwaweke katika makundi mawili. Wapo vijana ambao wapo katika Halmashauri, hao watapitia katika vikundi ambavyo vitatambuliwa chini ya Halmashauri zao; lakini lingine ambalo nimelitaja katika hotuba yangu, nilikuwa nalenga pia vijana ambao wanamaliza masomo katika Vyuo na Vyuo Vikuu. Jambo ambalo mpaka sasa hivi nimekwishalfanya ni kwamba nimepitia katika Vyuo Vikuu, kama Chuo Kikuu cha Sokoine, nimekwenda Chuo cha Arusha Technical Collage, vile vile na vyuo vingine nina mpango wa kuvipitia. Tunachokifanya sasa, tunafanya pamoja na Vyuo Vikuu kuandaa programu maalum kuwatambua wahitimu wenyefani ya kilimo ili wanapotoka tuwe na

utaratibu maalum wa kuweza kuwatafutia ardhi na kuwapa mitaji ili waweze kujajiri watumie elimu yao.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi niliuliza kuwa Serikali itakuwa tayari kuuangalia Mkoa wa Manyara kuwa *seed basket*, wawe wazalishaji wa mbegu katika Mkoa huo kitaifa kama Morogoro ilivyokuwa? Kwa sababu kwa sehemu kubwa, Wilaya ya Babati ndiyo tunaongoza Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Kati kuzalisha mbegu, lakini pia makampuni karibu yote ya mbegu yapo eneo lile la Manyara, wanazalisha mbegu mbalimbali.

Je, Serikali iko tayari kuunga mkono na kuweka miundombinu mbalimbali kuhakikisha kuwa inakuwa namba moja kitaifa na ukizingatia kuwa mbegu inatakiwa izalishwe sehemu moja na kupelekwa maeneo mbalimbali? Watalaan wanashauri mbegu unayopanda sehemu yako uibadilishe upeleke mbegu na uchukue mbegu ya mbali. Je, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba Mkoa huo unakuwa *Seed Basket* kitaifa?

WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni jambo jema kabisa kwa sababu mahitaji ya mbegu nchini bado ni makubwa na uzalishaji bado ni mdogo kama nilivyoeleza katika hotuba yangu. Lakini jambo la maana ni kwamba, nimeongea na Mheshimiwa Jitu Soni na tumekubaliana kwa sababu katika eneo lake na hasa *Kiru Valley* ina *potential* kubwa sana ya kuzalisha mbegu na mazao mengine. Vile vile kuna wazalishaji wa mbegu wapo katika bonde hilo. Tumekubaliana kwamba pamoja na kuzalisha mbegu na mazao mengine, tutatafuta utaratibu tutengeneze *Inception report*, na kwa makusudi kabisa, nataka tuwe na programu ya uendelezaji wa bonde la Kiru ili liweze kutusaidia kuzalisha mbegu.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilielezea namna ambavyo maeneo mengine yanakumbwa na tatizo la njaa kutohana na ukame japokuwa maeneo hayo yamezungukwa na mito mikubwa sana. Nilitoa mfano wa mto Momba Kipeta kwamba wananchi wana tatizo la njaa wakati walishatengeneza mradi wa Skimu ya Mareza na mwaka 2011 nilifuatilia, mwezi wa Nne nimekwenda Ofisi ya Waziri wa Kilimo, nikapeleka mpango wa Halmashauri, lakini nashangaa katika mpango huu sijaona fedha iliyotengwa kwa ajili ya mradi huo wa Mareza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo.

WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba hatukumtengea chochote huku ndani, kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, lakini pia ningependa nimhakikishie Mbunge, maana yake tulilizungumza pia mimi na yeye, na nikamwahidi kwamba asipate taabu kwamba asipoona mradi ndani ya kitabu hiki, basi ndiyo mwanzo na mwisho. Lakini nimeshamwaahidi kabisa kwamba mitafanya utaratibu na Mheshimiwa Naibu Waziri bahati nzuri kumbe na yeye anapajua, ameshakwenda, tutajitahidi tuhakikishe kwamba eneo lake nalo tunaliweka katika mipango yetu.

MHE. MOHAMMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa kuzungumza kuititia hoja ya Waziri Mkuu, nilieleza tatizo sugu la kero kubwa ya ndege waharibifu kwa Jimbo la Singida na Wilaya zote za Mkoa wa Singida, kwamba linafelisha na kuzorotesha sana jitihada za wananchi katika kilimo cha mazao ya chakula na mazao ya biashara, nikaishauri Serikali kwamba iangalie uwezekano wa kununua ndege kwa ajili ya kuangamiza ndege hawa, kwa sababu ndege tunayoitumia sasa hivi ni ndege kuu kuu yenye takribani zaidi ya miaka 35, lakini ndege yenye pia siyo yetu. Ni ndege ambayo inamilikiwa na nchi karibu sita. Wakati wewe unaitafuta hapa, iko sijui Sudan, Somalia; kwa hiyo, nikasema wakati umefika ili kwenda kweli na dhana ya Kilimo Kwanza, nchi yetu au Serikali yetu ifanye utaratibu wa kununua ndege zake au ndege yake angalau moja ya kuanzia ili kuondoa tatizo hili ambalo ni kero ya siku nyingi kwa wananchi wa Jimbo langu na Wilaya zote za Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua, ni hatua gani Serikali imefikia juu ya mpango huo?

WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema Mbunge ni kweli, lakini nilipokuwa najaribu kuelezea, hapo nilitaja mashirika ambayo tunashirikiana nayo, mojawapo ni *Red Locust Organisation* na wapo wenzetu ndani ya ukanda wetu ambao tunashirikiana wakati milipuko ya visumbufu vya mimea inapotokea. Tunawasiliana na tunasaidiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nakumbuka Mheshimiwa Missanga alisha-suggest kabisa kwamba afadhali tuwe na ndege yetu, na sisi katika bajeti hii tumetenga Shilingi bilioni moja na nusu kwa ajili ya kununua ndege. Tumewasiliana na tukaambiwa kwamba kuna uwezekano wa kuipata ndege hiyo kwa Shilingi bilioni moja na nusu. Lakini tunazo ndege zetu za kilimo anga ambazo bado zinatengenezeka, lakini fedha hizi tulizotenga ni kwa ajili ya kununua ndege kwa ajili ya kupambana na kweleakwelea. Namshukuru kwa mawazo yake ambayo yamepelekea sisi kuamua kutenga fedha hizi.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Katika mchango wangu wa kuongea jana, niliongelea juu ya matatizo ya mabwawa katika Mkoa wangu wa Tabora, hususan bwawa la Inara ambalo sasa hivi hakuna maendeleo yoyote yanayofanywa, na kuna bwawa lingine la Goweko katika Kijiji cha Nsololo tangu mwaka 2009 Serikali inaa giza haijatekeleza na haikutoa maelezo yoyote kuhusu mabwawa. Namwomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ambayo yataniridisha, na mimi nina imani na yeye.

WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Rage alizungumzia kuhusu mabwawa haya, na hatukutenga fedha kuto kana na fedha kidogo tulizokuanazo. Lakini vile vile anafahamu kwamba upande huo huo bwawa la Kamhalanga na mabwawa mengine, tumeyatengea fedha na yanaendelea kukamilika. Kwa hiyo, haya mabwawa ya Inala na Goweko hatujayashau. Mimi nimefanyakazi Tabora, naya fahamu yote kwa majina na kwa macho. Nimemwahidi kabisa kwamba tutaweka katika programu kwa sababu katika ukanda wa kati, *solution* ni kuvuna maji ya mvua. Kwa hiyo, na ye ye ni mmojawapo katika Mikoa hii ambayo *solution* ni hiyo. Aendelee tu kunivumilia, naamini tutamfikia.

MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika mchango wangu wa maandishi, nilijadili juu ya uamuzi wa Serikali wa kuimarisha kilimo hasa kwa kutekeleza Kilimo Kwanza na nikasema ni namna gani Serikali imekuwa ikiwaangusha wakulima huku ikihimiza kilimo katika suala la usambazaji wa pembejeo. Pembejeo ambazo zinatolewa kwa wakulima zinawafikia kipindi ambacho hawana pesa, badala ya kuwapelekeea kipindi ambacho wana pesa kama mwezi huu wa Saba. Lakini katika hotuba hii, bado uhakikisho huo sijauona kwamba: Je, tutapata mwarobaini kuititia bajeti hii kwamba sasa pembejeo zitawafikia wakulima katika kipindi muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

NAIBU WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mipata, lakini kwa ujumla na Watanzania wote, kwamba, suala la vocha na pembejeo mwaka huu tumekaa na Wakuu wa Mikoa kama tulivyo sema tarehe 27 Juni, na tumelipangia mikakati ili Mikoa ambayo inaanza kupanda msimu wake wa kupandia mwezi wa Tisa, tumalize tatizo hili la vocha na tatizo la pembejeo kabla ya msimu wa kupandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tulitoa ahadi kwamba tutatoa kauli Bungeni kwa ajili uelewa na ufahamu kwa Watanzania wote, hususan wakulima wa Tanzania pamoja na Wabunge.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ili tuweze kuendelea vizuri, naomba kwa hatua hii Bunge lirjee.

(*Bunge lilitrudia*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge naomba tukae. Katibu naomba kengele igongwe kule nje.

*(Hapa Kengele lligongwa illi walioko nje ya Ukumbi
waingie Ukumbini)*

MBUNGE FULANI: Wewe Mnyaturu, kaa chini.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane ili tuweke sawa baadhi ya mambo. Kama nilivyomwambia Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Machali na Mheshimiwa Mkosamali, unaposoma ile Kanuni ya 77 (3) inasema: "Endapo Spika ataridhia kwamba idadi ya Wabunge haitoshi, ina maana inanitaka inipe nafasi kama mwendesha kikao, njiridhishe kwa namna moja au nyngine kwamba kweli idadi ya Wabunge haikidhi akidi ambayo inatakiwa katika kufanya maamuzi. Nilipokuwa nahitaji muda wa namna hiyo, baadhi yetu wanapiga kelele, baadhi yetu wanafanya fujo, baadhi yetu wametoka shule jana, taabu kweli! Wanataka tuendeshe mambo kisekondari-sekondari! Ni ukweli, kwani ni uwongo? Ni ukweli wengine wametoka shule jana. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyokumbuka, na ni vizuri wananchi waelewe kwamba tuna msiba mkubwa wa kitaifa unaoendelea Zanzibar na kwa hiyo, kuna baadhi ya Wabunge kutoka Vyama vyote hasa kutoka Zanzibar ambao wapo Zanzibar kwa ruhusa ya Spika, kuna Mawaziri na Manaibu Mawaziri ambao wapo Zanzibar na wengine wapo kwa shughuli maalum kwa ruhusa ya Spika. Kuna Wabunge kadhaa ambao nimewaruhusu mimi mwenyewe leo wapo kwenye msiba kwa ajili ya mazishi ya mama yake Mheshimiwa Michael Lekule Laizer kule Longido. Kwa hiyo, hawa wote wameondoka kwa ruhusa.

WABUNGE FULANI: Aaaaah!

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawaombeni ndugu zangu tunapokuwa tunatoa maelezo, tusikilizane kama watu wazima, tupeane nafasi. Mnalolitaka litakuwa, lakini twende kwa utaratibu kwa kuheshimiana na kwa kusikilizana. Inanisikitisha sana tunapovunjiana heshima, tunapokuwa kama watoto wadogo. Mksema ninyi nawapa nafasi, mnasema mpaka mwisho. Nikisimama mimi kusema, kelele moja kwa moja. Mimi sidhani kama inatujengea heshima mahali popote pale katika nchi yetu kwa taratibu za namna hiyo. Kwa sababu hayupo mtu wa kumkandamiza mwenzake hapa, hata kidogo! Tunafanya jambo ambalo ni la msingi, ni jambo la nchi.

Kwa hiyo, katika suala la akidi ilibidi njiridhishe kwanza katika wale waliopo hapa. Je, kuna Kamati zozote ambazo zinakutana au Wabunge wengine wowote ambao hawapo, kwa maana ya kwamba wamesaini asubuhi kwamba wapo, lakini kwa sasa *physically* hatuwaoni humu ndani? Ukichukua hesabu hizo unaanza kupata matatizo kidogo. Ndiyo maana nikachukua muda kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, lakini kwa ajili ya jambo hilo, kwa vile muda pia haupo upande wetu, basi inapaswa kuendesha kikao hiki kwa busara ya Kiti zaidi, naamua kwamba hatua hii ya Kamati ya Bunge zima na upitishwaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2012/2013, zoezi hilo litamaliziwa Jumatatu asubuhi. Itakuwa ni kwa muda mfupi sana na Jumatatu hiyo hiyo, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto itawasilisha, na mjadala wake utamalizika kwa sababu ni wa siku moja hata kama wachangiaji wake watakuwa ni wawili.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi Jumatatu saa tatu Asubuhi.

*(Saa 7.10 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya
Jumatatu, Tarehe 23 Julai, 2012, Saa Tatu Asubuhi)*

